

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 10 Novemba, 2016**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na Mkutano wa Tano, Kikao cha Tisa, kama mlivyoona Waheshimiwa Wabunge Order Paper ilivyo, kile kipindi maarufu hatutakuwa nacho kwa udhuru maalum wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI ,VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevyta nchini ya mwaka 2015.

**MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 94

**Kuipanua Hospitali ya Wilaya ya Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto ina hospitali moja ya Wilaya ndani ya Halmashauri mbili na Majimbo matatu, hospitali hii inategemewa na watu zaidi ya 500,000.

Je, ni lini Serikali itaifanyia upanuzi hospitali hiyo hasa wodi ya akina mama wajawazito?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omar Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imepanga kufanya upanuzi wa miundombinu ya Hospitali ya Wilaya katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo zimetengwa shilingi milioni 50 kwa awamu ya kwanza. Fedha hizo zitatumika kujenga jengo ambalo litakuwa kwa huduma za mama na mtoto, zikiwemo wodi za wajawazito. Hadi kukamilika jengo hilo linatarajiwa kugharimu shilingi milioni 350.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuimarisha vituo vya afya vilivyopo ili viweze kuwa na uwezo wa kufanya upasuaji mdogo wa dharura hasa kwa mama wajawazito ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Kwa kuwa Jimbo la Lushoto lina kituo kimoja tu cha afya, ambacho kinahudumia takribani Kata saba; je, Serikali haioni sasa kuwa umefikia wakati wa kujenga vituo vya afya hasa katika Kata ya Makanya, Ngwelo, Kilole, Gare, Ubiri, Magamba, Malibwi pamoja na Kwai?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Lushoto wamejitolea kujenga zahanati katika vijiji vya Mzalagembe, Bombo, Mavului, Mbwei, Mazumbai, Ilente, Mbelei, Makanka na Kwemachai, lakini zahanati hizi zimebakia kukamilika tu.

Je, Serikali inatoa tamko gani sasa la kumalizia zahanati hizi pamoja na kupeleka watumishi ili wananchi wa Jimbo la Lushoto waondokane na usumbufu wa kutembea umbali mrefu hasa kwa mama zetu na dada zetu?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa sijui kama vijiji hivyo Mheshimiwa Jafo toka Kisarawe mpaka Lushoto huko. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, kwanza katika kumbukumbu yangu Mheshimiwa Shekilindi amekuwa akiuliza maswali mengi sana ya sekta ya afya, ofisi yetu inakiri mchango mkubwa wa Mheshimiwa Shekilindi katika Jimbo lake na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, katika kulifanikisha suala hili, Serikali tumeelekeza mpango wetu wa sasa tunaondoka nao, jinsi gani tutafanya katika mwaka huu wa fedha, kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya. Mheshimiwa Shekilindi kwa sababu jana nilikujibu hapa kwamba nina mpango wa kuanzia katika Mkoa wako wa Tanga, tena ratiba nimeibadilisha nitaanza siku ya tarehe 21, na Mheshimiwa Shangazi, nitakuwa naye hiyo tarehe 21, tutaangalia jinsi gani tutafanya baada ya kuwa kule site, kutembelea hivyo vituo. Katika mpango wa bajeti inaokuja lengo kubwa ni kuimarisha vituo vya afya, katika ujenzi kwenye maeneo yetu, tumelenga kwamba angalau kila Halmashauri katika mwaka wa fedha tunaondoka nao tujenge kituo kimoja cha afya.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika katika suala zima la maboma nimesema, tulifanya assessment katika Halmashauri zote, na hili ni agizo la Kamati ya Bajeti, maboma yote ambayo hayajakamilika, tumepata idadi ya maboma. Ndiyo maana nimesema katika bajeti ya mwaka huu unaokuja sasa, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, tuungane pamoja kwamba jinsi gani tutafanya mpango mkakati wa kibajeti tuweze kumaliza maboma yale ambayo Mheshimiwa Shekilindi umeyazungumza katika maeneo yako, tukimaliza yale tutakuwa tumesogeza kwa ukaribu zaidi huduma za afya kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nakuunga mkono katika hilo na Serikali imesikiliza kilio chako.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Wilaya ya Longido imeanzishwa mwaka 2007, takribani miaka tisa mpaka leo Wilaya ile haina hospitali ya Wilaya, matokeo yake wagonjwa wakipewa

rufaa, wanapelekwa, Mount Meru - Arusha, kiasi cha kilometra 94 na Serikali imekuwa ikiahidi itajenga Hospitali ya Wilaya. Tunataka majibu ya uhakika, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Longido?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Longido haina Hospitali ya Wilaya kama zilivyo Wilaya nyingine nyingi tu hapa nchini. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi ya Halmashauri, inaanzia kwenye mipango ya Halmashauri na baadaye bajeti ya Halmashauri. Kwa hiyo, niwasihii sana Waheshimiwa Wabunge kwamba kule kwenye mipango ya Halmashauri ndiko vitu hivyo vionekane ili baadaye vikija huku Bungeni tuweze kuvitengea bajeti kwa mujibu wa taratibu za kibajeti.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida mimi kupata wageni wanaoomba vitu nje ya bajeti. Uwezo huo sina na hata Waziri wa Fedha, nadhani hana. Bajeti ikishapitishwa ndicho kitakachofanyika. Hivyo, Wilaya ipange mipango yake, mipango hiyo iwemo kwenye bajeti za Halmashuari zao. Jambo kubwa litakalobakia sasa ni kwa Wabunge ku-demand utekelezaji wa bajeti ili tufikie yale malengo hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwasihii Waheshimiwa Wabunge, kwamba kwa sera ya Serikali ni kuweka kituo cha afya kila kata, lakini Serikali tumeamua na tumepanga na Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba kila Halmashauri basi angalau ijenge kituo kimoja. Katika Halmashauri 185 tulizonazo, tukifanya tutapata vituo karibu zaidi ya 400, wakati toka uhuru tuna vituo kama 600 tu.

Mheshimiwa Spika, nadhani hii itatusaidia sana, wa-dedicate maeneo, indication kulingana na maeneo ambako kuna problem kubwa. Jambo lingine ni kwamba kwenye zahanati wananiomba ramani, ramani ile iliyotolewa na Wizara ya Afya tumekubaliana na Waziri wa Afya kwamba ni kubwa mno kwa zahanati kila kijiji na haitekelezeki kwa sababu ya gharama kubwa karibu ya 1.8 billion ili iweze kutekeleza ule mradi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumekubaliana ku-review ile bajeti, kwa sababu tuna zahanati ambazo zilijengwa wakati tulipopata uhuru tu, zilitosha kutuhudumia mpaka leo tupo. Kwa hiyo, tunadhani zisiwe kubwa kiasi cha kushindwa ku-manage uchumi wa kijiji kwa sababu sehemu kubwa ni michango ya wananchi itatumika pamoja na kwamba Serikali itaweka mkono wake, lakini lazima ramani iwe ya kawaida inayoweza kuwa manageable. (Makofi)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi TAMISEMI, kwa majibu yako nisisitize kwamba Wizara iendelee kujandaa kwa ajili ya ile semina kwa Wabunge ambayo itafanyika kwenye kikao kijacho cha Bunge, kwa sababu ni ukweli kabisa usiyopingika kwamba maswali mengi yanayouлизwa kuhusu TAMISEMI, ni maswali ambayo katika mazingira ya kawaida tusingeweza kuyaruhusu hapa. Ni maswali ambayo yanatakiwa wewe mwenyewe kama Diwani uwe umeingiza vitu vyako kwenye bajeti badala ya kuja kuuliza hewa hapa. Kwa hiyo, huko mbele baada ya hiyo semina maswali mengi ya aina hiyo tutakuwa hatuyaweki kwenye Order Paper ya siku hiyo.

Mheshimiwa Hawa ghasia!

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda niulize swalii la nyongeza.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijiini tayari imeshapanua kituo chake cha afya cha Nanguruwe, ambapo pia kinacho chumba cha upasuaji cha kisasa, chenye vifaa na kimeanza kutoa huduma kwa lengo la kuifanya iwe hospitali ya Wilaya, ambapo majengo yote yanayotakiwa yamekamilika.

Je, ni lini Serikali itaibadilishia hadhi kutoka kituo cha afya na kuwa hospitali ya Wilaya baada ya kuwa kila kitu kimekamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mpango wa bajeti tulipokuwa tunajadili na watu wa Mtwara kule Nanguruwe, mwaka huu kwamba wameonesha demand ya kituo hiki, na ni kweli walihakikisha kituo hiki kimekamilisha vitu vyote vya msingi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Hawa Ghasia, tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya kuangalia zile taratibu za kikawaida kuhakikisha kituo hiki sasa kinapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya, tukijua wazi kwamba ikiwa hospitali ya Wilaya hata kasma ya bajeti itabadiili eneo hilo na wananchi wataendelea kupata huduma nzuri baada ya kituo hicho kupanda kuwa Hospitali ya Wilaya. (Makofii)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara inayofuata ambayo ni Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundii, swalii linaulizwa na Mheshimiwa Ester Mmasi.

Na. 95

### **Uteuzi wa Watumishi Taasisi za Elimu ya Juu**

**MHE. ESTER M. MMASI** aliuliza:-

Changamoto nyingi kwa upande wa kada za waendeshaji Vyuo Vikuu unatokana na uteuzi usio na tija katika nafasi za Wakuu wa Vitengo, Rasilimali Watu na uongozi chini ya Mwongozo wa Universities Charter.

Je, nini msimamo wa Serikali kuhakikisha kada za watumishi wa umma, Taasisi za Elimu ya Juu zinaheshimika na nafasi za Wakuu wa Vitengo, Rasilimali Watu, zinatumika kiufasaha kulingana na miongozo ya kiutumishi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa kada za waendeshaji pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo katika vyuo vikuu vya umma hufuata muundo wa utumishi wa wafanyakazi waendeshaji ambao pamoja na mambo mengine, unazingatia miongozo inayotolewa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba tatizo siyo taratibu, sheria au miongozo iliyopo ya uteuzi kama hati idhini za vyuo vikuu (*universities charter*), bali ni ukosefu wa maadili ma ubinafsi kwa baadhi ya wahusika kwenye michakato hiyo. Serikali imeshachukua hatua ya kuchunguza malalamiko kama hayo katika vyuo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sanyansi, na Teknolojia ili kujua ukweli na ikibainika kuwa kuna wahusika walivuruga utaratibu na kipelekea kuteuliwa viongozi wasiostahili watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo kimsingi yamejikita kwenye suala la msingi.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni dhahiri kwamba kupitia miongozo ya Serikali juu ya mishahara na posho za waendeshaji na hata walimu wa vyuo vikuu Tanzania, ni kwamba iko mikondo mathalani PGSS 13, PGSS 14, PGSS 15, hizi ni kada ambazo zinapaswa kuongozwa na waendeshaji kwa maana ya kwamba siyo academicians. Practice iliyopo sasa hivi ni

kwamba viwango hivi vya mishahara havitumiki kwenye kada husika kwa kuwa nafasi hizi za uongozi wa juu ni kwamba unaongozwa na academicians.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafsiri kiwango cha mshahara PGSS 13 ambayo inashikiliwa na Wakurugenzi ambao ni wanataaluma PGSS 14 na PGSS 15 ili viwango hivi viweze kutumika kwa waendeshaji wa vyuo vikuu au taasisi za elimu ya juu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kama ambavyo nimejibu katika swalii msingi niende tu katika ufanuzi wa ziada kwamba baada kuona kwamba kuna malalamiko aina hiyo na mengine kwa kweli katika vyuo vyetu mbalimbali hasa vyuo vikuu, Wizara kwa kuzingatia hilo, mwezi huu wa kumi ulioisha tumeunda vikundi kazi (team) kwa ajili ya kufuatilia hayo mambo yote katika vyuo vyetu vyote vikuu vikiwemo vyuo binafsi ili kuona kwamba kwanza vinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, lakini pili uongozi unapangwa kutokana na taratibu na sifa zinazostahili, vilevile kuangalia miundombinu na maslahi kwa ujumla yanayohusu viongozi wa ngazi hizo kama yapo sahihi au hayapo sahihi. Bila kusahau hata watumishi wengine ambao hawaonekani kama ni watumishi muhimu (*supporting staffs*), kama wapishi, kuona kwamba je, chuo kinawenza kuijendesha kiuhalali au laa!

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nizidi tu kusema haya mapendelekezo yako, unayozungumza nayo yatazingatiwa katika kutafakari masuala hayo. (Makofii)

Na. 96

### **Kilimo cha Umwagiliaji - Mto Rufiji**

**MHE. MARY D. MURO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji katika Mto Rufiji ili kuongeza ajira na chakula?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Rufiji umepita katika maeneo mengi ambayo yanafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji ingawa maeneo mengi huwa yanakumbwa na changamoto ya mafuriko wakati wa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, mpango kabambe wa umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*) wa mwaka 2002 uliahanisha maeneo yanayofaa kujenga skimu za umwagiliaji katika maeneo ya Mto Rufiji yakiwemo maeneo ya Segeni, Nyamweke, Ngorongo na Ruwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaanza kuendeleza scheme ya umwagiliaji ya Segeni, Wilayani Rufiji ambapo hekta 60 zilishaendelezwa na kuna mpango wa kuongeza hekta 60 zaidi. Aidha, Serikali imetuma shilingi milioni 358 kwa ajili ya scheme ya Nyamweke ambayo ina hekta 300 iliyopo Wilayani Rufiji kupitia mradi wa kuendeleza scheme ndogo za umwagiliaji kupitia ufadhili wa Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliainisha pia mashamba ya makubwa ya uwekezaji kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya miwa na mpunga. Baadhi ya mashamba yaliyoainishwa ni pamoja na Lukulilo hekta 8,000 kwa ajili ya kilomo cha mpunga, Mkongo hekta 10,551 kwa ajili ya kilimo cha miwa, Muhoro hekta 10,000 kwa ajili ya kilimo cha miwa, na Tawi/Utunge hekta 15,924 kwa ajili ya kilimo cha miwa. Aidha, taratibu za kuwapa wawekezaji katika maeneo hayo zinaendelea kupitia *Tanzania Investment Centre*

**SPIKA:** Ahsante sana Injinia Kamwelwe. Eeh, swali hili mbona waulizaji wa nyongeza wengi sana? Mheshimiwa Mary Deo Muro swali la nyongeza.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwenye majibu yake ya msingi amesema zimetumwa shilingi milioni 358; je, zimetumwa lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili uendelezaji unaanza lini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer Kamwelwe* kwa maswali hayo mafupi mawili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 358 zilitumwa miezi miwili iliyopita na tulipata fedha kutoka Serikali ya Japan bilioni 29.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba uendelezwaji unaanza lini. Katika hizo fedha sasa hivi kinachofanyika ni kuandaa mikataba, ni maeneo

mengi ambayo yalikuwa bado mikataba hajjaandaliwa. Ni kuandaa mikataba kwa sababu usanifu ulishafanyika ili kuweza kuingia sasa mikataba na wakandarasi na kazi hiyo iendelee kutekelezwa.

**SPIKA:** Hili swali, Mheshimiwa Mwakasaka nilikuona.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mkoa wa Tabora hususani Tabora Mjini tuna mabwawa makubwa mawili, Bwawa la Igombe na Bwawa la Kazima, pia tuna mradi wa bwawa ambalo lipo Kata ya Ndevelwa ambalo limeigharimu Serikali zaidi ya shilingi bilioni moja ambalo mpaka sasa hivi halifanyi kazi kwa sababu linavuja.

Mheshimiwa Spika, sijui Serikali ina mkakati gani wa kufanya mradi huu ambaao kwanza umekwama, lakini pamoja na haya mabwawa mengine yaweze kutumika katika kilimo cha umwagiliaji ili wananchi kwa ujumla waweze kupata ajira pamoja na kuweza kupata mazao kwa ajili ya kujikimu kutohana na hali mbaya ya chakula ambayo inaikabili nchi yetu kwa sasa? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, mabwawa mawili ya Igombe na Kazima yanatumika kwa ajili ya maji ya matumizi ya binadamu na Bwawa la Igombe limeshaboreshwu tayari lina maji ya kutosha, sasa kuangalia uwezekano kwamba yanaweza yakatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji basi tunalichukua tuweze kulifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bwawa hili ambalo limebomoka, hili kwa sasa tayari tumejikita kuhakiksha kwamba mabwawa yote ya zamani yanaboreshwu ili yaweze kufanya kazi zilizotarajiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Vulu nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ZAINAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani hususani Wilaya ya Rufiji naomba nirudi kwenye swali la msingi.

Sote tunafahamu Rufiji ina mto na ina bonde zuri sana la kilimo; tuna Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Rufiji kwa maana ya RUBADA. Je, Serikali itaweza kutuambia nini kazi za hiyo mamlaka? Kwa sababu bonde liko pale, maji yapo pale hakuna kinachoendelea katika uzalishaji wa mazao ya aina mbalimbali.

Je, kuna sababu ya hii mamlaka kuendelea kuwepo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna sababu ya mamlaka kuwepo? Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba ipo haja ya mamlaka hiyo kuwepo. Kilimo cha umwagiliaji katika nchi hii kimeanza mwaka 1940 na kilianzia Rufiji, wakati huo ilikuwa hekta 160 ndio zilianza kutumika kule Rufiji. Baada ya hapo muda uliofufata tuliamhia Mbarali, hiyo ilikuwa ni mwaka 1960. Kutokana na mamlaka hiyo kuwepo uboreshaji kuhusu kilimo cha umwagiliaji umeendelea kutokana na hiyo mamlaka, hatimaye mpaka tumekuja kuwa na Tume ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeipitisha mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na data ambazo ziliwuwa zinaandaliwa na hiyo mamlaka ndiyo imetufikisha hapa tulipo sasa hivi. Tayari Serikali imeshaainisha maeneo mengi kama nilivyojibu katika swalil la msingi kuhakikisha kwamba sasa bonde hili la Mto Rufiji ambalo linatokana na Mto Ruaha na mito mingine ya Kilombero na kutokana na mamlaka hii imemeanishaya maeneo na sasa hivi maeneo mengi yamesanifiwa sasa hivi tunachosubiri ni fedha kuanza utekelezaji. Kwa hiyo, mamlaka hii uwepo wake ni wa muhimu, data zote kuhusu kilimo cha umwagiliaji zina hii mamlaka.

**SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee kwa sababu ya muda na Wizara ya Fedha na Mipango, swalil la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, Mheshimiwa Kafumu tafadhalii.

Na. 97

### **Utunzaji wa dhahabu safi nchini**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Moja kati ya jukumu la Benki Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 51(2)(a) cha Sheria ya Benki Kuu, 2016 ni kutunza dhahabu safi.

Je, kwa nini Serikali imekataa kutunza dhahabu safi katika Benki Kuu wakati Tanzania ni mionganoni mwa nchi zinazozalisha dhahabu safi na kwa wingi Afrika?

## **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Benki Kuu ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuwa na utulivu wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa. Ili kufanikisha azma hii, Benki Kuu inadhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa kutumia nyenzo mbalimbali zikiwemo kuuza dhamana na hati fungani za Serikali na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni kati ya mabenki ambayo ni *Interbank Foreign Exchange Market*.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu lake la msingi, Benki Kuu hutunza hazina ya rasilimali za kigeni zinazotosha kuagiza bidhaa nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Hazina ya rasilimali za kigeni inaweza kuwa dhahabu-fedha yaani *monetary gold* au fedha za kigeni. Uamuzi kuhusu hazina itunzwe vipi unazingatia vigezo mbalimbali vikiwemo vile vya kudumisha thamani, wepesi wa kubadilisha yaani *convertibility* na faida inayopatikana kwa kuwekeza hazina hiyo.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu kwa muda mrefu haijaweka dhahabu kama sehemu ya hazina ya rasilimali za kigeni kutokana na bei ya dhahabu katika soko la dunia kutokuwa tulivu na hivyo kusababisha uwezekano wa kupunguza thamani ya hazina ya rasilimali ya nchi. Mfano, tumeshuhudia bei ya dhahabu ikishuka kutoka dola 1,745 za Kimarekani kwa wakia moja Septemba, 2012 hadi dola za Kimarekani 1,068 Disemba 2015. Aidha, ununuzi na uuzaaji wa dhahabu unahitaji ujuzi maalum ambapo kwa kuzingatia jukumu la msingi la Benki Kuu ambalo tumelieleza hapo juu, Benki Kuu haijajijengea uwezo katika eneo la biashara ya dhahabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafumu umeridhika na majibu?

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yasiyotosheleza sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. (*Makofii*)

Swali la kwanza; kwa kuwa kutunza dhahabu kwenye hazina ya nchi yoyote ni kuashiria utajiri wa nchi hiyo; kwa mfano, nchi ya Marekani ina dhahabu zaidi ya tani 8,100 kwenye hazina yake, lakini nchi ya Ujeruman 3,300 na nchi ya Italia ina tani 2,450. Kwa nini Tanzania tunachelea chelea kutunza dhahabu wakati sisi sasa hivi ni wazalishaji wa dhahabu duniani? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa Tanzania ni nchi inayozalisha dhahabu kama Ghana, ina tani nane kwenye ghala yake, lakini Afrika ya Kusini ina tani 125. Na kwa kuwa kwa kipindi cha muda mrefu dhahabu imekuwa ikipanda thamani. Miaka ya 1900 dhahabu ilikuwa zaidi ya dola 200, miaka ya 2000 ilikuwa zaidi ya 500; sasa hivi ni zaidi ya dola 1000. Kwa nini Serikali inachelea kwamba dhahabu inatelemka bei. Kwa nini sasa Serikali isifanye utafiti ikaangalia nchi zingine zinafanyaje na ikatunza dhahabu kwenye hazina yake kwa ajili ya kupandisha uchumi wa nchi yetu? Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipanga, Mheshimiwa Ashatu Kijaji, majibu! Waziri mwenyewe wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mpango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sababu kubwa ya msingi ya Benki Kuu ya nchi yoyote kuweka akiba yake katika dola ni kuiwekea akiba (*reserves*), hiyo ndiyo sababu ya msingi ya Mataifa yote. Hata katika historia wakati wa vita, dhahabu ilichukuliwa kama mkivamia nchi moja kitu cha kwanza mnachokimbilia kuchukua kwa wale mliowashinda mnachukua ile dhahahu kwa sababu ina hesabika ndiyo inabeba thamani ya vitu. Kwa hiyo, sana siyo kuonesha kiwango cha utajiri katika nchi kama sababu ya msingi ya kuweka akiba yako katika dola. Vilevile tunachelea kuweka akiba yetu katika dola kwa sababu ya msingi....

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa dhahabu bwana!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, tunachelea kuweka akiba yetu katika dhahabu kwa sababu ya tabia ya bei ya dhahabu katika miaka ya karibuni kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, hata huko Ghana ambako ni kweli wana akiba ya dhahabu ya tani 8.4 ambayo siyo sehemu kubwa sana ya akiba yao ya reserves na wamekuwa na akiba hiyo toka mwaka 2000, kiasi hicho hakijabadilika. Hali kadhalika Afrika ya Kusini toka mwaka 2016 wamebakiwa na tani 123.8 tu na kiasi hicho kimeteremka na kufikia tani 183.1, lakini ni wasiwasi huo wa mwenendo wa bei ya dhahabu katika soko la dunia. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali inafanya uchambuzi kuona uwezekano kama tunaweza tukaweka sehemu yetu ya akiba katika Tanzanite badala ya dhahabu lakini hii ni kazi ambayo inaendelea.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Zitto, swali la nyongeza.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo Naibu Waziri ameyajibu amesema kwamba Benki Kuu hajijajengea uwezo katika eneo la biashara ya dhahabu. Nadhani swali la msingi hapa ni kuweka akiba (reserve) kama dhahabu, siyo kufanya biashara ya dhahabu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pili, Waziri atakuwa anakumbuka huko nyuma Tanzania ilikuwa inaweka reserve hii kwenye dhahabu. Kwa hiyo, uzoefu wa kuweka hivyo tunao na swali la msingi hapa ni kwamba kwa nini tusitumie na baadhi ya migodi tunaimiliki wenyewe, tusitumie sehemu ya uzalishaji kutunza kwa sababu bei ya dhahabu hata iwe nini bado huwa ni stable zaidi kuliko bei ya dola au fedha zingine za kigeni ambazo tunawekea akiba zetu. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa Benki Kuu ya Tanzania ni kweli miaka ya 1980 tulikuwa na utaratibu huo lakini tulipigwa kweli, maana wakati ule bei ya dhahabu iliporomoka kutoka dola za Kimarekani 700 kwa ounce zikaporomoka chini mpaka kufikia dola 235 kwa ounce moja. Hiyo ndiyo ilifanya Serikali iamue kuuza hata ile dhahabu iliyobaki baada ya kupata hasara kubwa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Na baadae imepanda.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Baadae imepanda ni sawa.

Lakini sasa uzoefu tunaouzungumzia ni pamoja na uwezo wenyewe wa pale Benki Kuu kusema hii ni dhahabu kweli na hii siyo...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane Mheshimiwa Spika amenipa nafasi.

Kwa hiyo, ni muhimu sana ule uwezo wenyewe uweze kujengwa ndani ya Benki Kuu, siyo tu kuitambua ile dhahabu yenyewe iliyo halali na sivyo, lakini na biashara yenyewe na kufuatilia mwenendo unavyoenenda duniani.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni kwamba Serikali inalifanya kazi ili kuangalia tena uwezekano wa kuweka akiba yetu katika dhahabu au madini mengine ya vito ambayo tunayo hapa nchini. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; swali linaulizwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini.

Na. 98

### **Malipo ya Fidia kwa Wananchi Kupisha Mradi wa EPZA**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Wananchi wengi katika Kijiji cha Guta na Tairo walitoa ardhi yao kwa ajili ya mradi wa EPZA, sasa ni takribani miaka saba tangu kufanyiwa tathmini, pia wananchi hao hawaruhusiwi kuendeleza maeneo hayo.

Je, ni lini wananchi wa vijiji hivyo watalipwa fidia halisi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999 Kifungu cha 3(1)(g)?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za kutwaa eneo la EPZ/SEZ Mara zilianza mwaka 2007 kwa kutambua mipaka ya eneo. Eneo lililopendekezwa ni la Kijiji cha Tairo kilichopo Kata ya Guta, Wilayani Bunda na lilikuwa na ukubwa wa hekta 2,200 likijumisha vitongoji vya Kirumi, Mabatini A & B na Bushigwamala. Uthamini wa eneo la mradi ulikamilika mwezi Julai, 2009 na taarifa yake kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali mwezi Septemba, 2009. Kwa mujibu wa uthamini, fidia iliyo takiwa kulipwa kwa eneo lote ni shilingi bilioni 3.477.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Mamlaka ya EPZ iliamua kupunguza ukubwa wa eneo na hivyo kuendelea na utwaaji wa eneo la kitongoji kimoja cha Kirumi. Aidha, fidia iliyo hitajika kufidia eneo hilo ilikuwa ni shilingi bilioni 2.143 zilizopaswa kulipwa ndani ya miezi sita bila riba. Tayari Mamlaka ya EPZ ilikwisha peleka jumla ya shilingi bilioni 2.358 kwa ajili ya malipo ya fidia ikijumuisha riba ya ucheleweshaji. Fedha hizo zililipwa kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2009 na 2012 kwa wadai wote, isipokuwa wananchi watatu ambao Ndugu Chacha M. Marwa, Ndugu Gati M. Marwa na Ndugu Juma W. Mgoba, ambao bado wanadai jumla ya shilingi milioni 21.943 licha ya EPZ kupeleka fedha zote kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuchelewa kwa malipo hayo, tarehe 20 Mei, 2016 aliye kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara aliagiza TAKUKURU na CAG wafanye uchunguzi wa matumizi ya fedha zilizotolewa na EPZA. Taarifa hiyo inasubiriwa ikamilike na pindi itakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watumishi waliohusika na ubadhilifu wa fedha hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wamemuongopea kabisa. Kwa sababu suala la EPZ nilianza ku-deal nalo tangu nikiwa Mbunge wa Viti Malaam na mpaka Mbunge wa Jimbo, hiyo Kata ndiyo Kata yeye wapiga kura wengi na ndiyo walijonipa kura nyingi kwa sababu ya hiki kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pesa zilizotumika kulipa EPZ ni shilingi 1, 240, 000, 000, hakuna ukaguzi wowote ambao umefanyika, wala uchunguzi wowote mpaka hivi sasa tunavyoongea. Kilichotokea, Mkaguzi wa Ndani alitoa ripoti kwa Mkuu wa Mkoa ambaye naye katumbuliwa kuhusiana na hili na Mkuu wa Wilaya aliyeshiriki na ubadhirifu huu ametumbuliwa kwa ajili ya udanganyifu wa suala hili.

Swali la kwanza, je, uko tayari sasa kuagiza TAKUKURU na CAG kufanya uchunguzi ili watu waliokuwa wakilindwa na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wiliya washughulikiwe?

Swali la pili, nini hatma ya wananchi wa eneo hili ambao waliahidiwa watapelekwa katika eneo mbadala ili kupisha mradi wa EPZ na wala hawana tatizo nalo? (Makofi)

**SPIKA:** Nilikuwa naangalia kumbukumbu zangu hapa Mheshimiwa Ester Bulaya kama bado ni Mbunge wa Bunda Mjini au? Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Charles Mwijage. (Kicheko)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizopewa na watendaji wangu wanasema wamelipa bilioni 2.3, yeye alizopata ni bilioni moja, hapa kuna tatizo na hili ni tatizo la kipolisi. Mimi pamoja na CAG pamoja na TAKUKURU, nitamuomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anisaidie. Hili siyo suala la TAKUKURU siyo suala la Polisi, tofauti ya bilioni moja ni pesa kubwa sana wala haihitaji uchuguzi, ni kupiga foleni watu, aliyelipwa acae huku, ambaye hakulipwa acae huku watu wanakwenda selo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niko tayari na nitaomba Mheshimiwa Mwigulu anisaidie na Mheshimiwa Simbachawene, kwa sababu wanaotuhumiwa ni watu wa TAMISEMI. Hili siyo langu, hivi siyo viwanda hivi, hili siyo eneo langu ni la Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Mwigulu. Wizi siyo viwanda. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Bulaya nashukuru, Serikali itakwenda kulishughulikia tunapokwenda Mawaziri watatu kukamata panya hao, tutahakikisha wananchi wanapewa maeneo mazuri. Zaidi niwaambie watu wa Mara, jambo la muhimu linalonuma ni kuhakikisha watu Mara tunatafuta wawekezaji ili EPZA iweze kutengeneza sehemu ya uwekezaji kwa ajili ya maendeleo ya ukanda ule.

**SPIKA:** Kwa kuwa Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Simbachawene wapo, nadhani ingekuwa vizuri, Mheshimiwa Simbachawene tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, nimesikia na tutalishughulikia! (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana, tunashukuru. Naomba tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rarya na litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwamoto.

Na. 99

#### **Hitaji la Mahakama ya Mwanzo na Watumishi Wilaya ya Rarya**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Wilaya ya Rarya ilianzishwa mwaka 2007, ina ukubwa wa kilometra za mraba 9,345 na idadi ya watu wapatao 400,000, lakini inakabiliwa na tatizo la uhaba wa watumishi katika Mahakama ya Mwanzo ya Kineri, Ryagoro, Obilinju na Shirati. Hadi sasa Wilaya ya Rarya inatumia Mahakama ya Wilaya ya Tarime inayosababisha kesi kuchelewa kusikilizwa kwa wakati.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya kwenye Jimbo la Rarya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rarya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kuna upungufu wa watumishi katika Mahakama za Mwanzo zilizotajwa kwenye swali hili ambapo kuna upungufu wa watumishi takribani tisa wakiwemo Mahakimu na Wasaidizi katika Mahakama hizo. Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017, Mahakama imejipanga kupeleka watumishi hao katika mahakama hizo hususan Mahakama ya Mwanzo ya Nyaburongo ambayo inahitaji Hakimu. Mahakama ya Mwanzo ya Kinesi

ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja kwa sasa haitumiki kutokana na uchakavu wa miundombinu yake ambayo itafanyiwa kazi katika mipango ya ukarabati ya baadae.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Rarya umewekwa katika mpango mkubwa wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, katika mwaka wa fedha huu, Mahakama imepanga kujenga Mahakama ya Wilaya Bunda na Mahakama Kuu - Mara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swalii la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya Wilaya ya Tarime kule Rarya inafahamika, kesi ni nyingi na zinachukua muda mrefu kuamuliwa na hivyo, kuwatia hasira watu wa Rarya, kama ambavyo tunajua.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuongeza watumishi wengi zaidi ili kesi ziende haraka? (Makofii)

Swali la pili, kwa kuwa matatizo yaliyoko Rarya yanafanana kabisa na yaliyoko Kilolo na kwa kuwa Kilolo ni Wilaya ambayo imeanzishwa toka mwaka 2000, lakini haina Mahakama yoyote.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa kuanzisha Mahakama ya Wilaya kwa kuwa kesi nyingi za Wilaya ya Kilolo mnajua hasira zao huwa zinaishia wapi ili waanzishe haraka? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto wanaishia wapi hao? (Kicheko)

Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria nina hakika umemuelewa Mheshimiwa Mbunge, tunaomba majibu ya Serikali. (Kicheko)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu wa kuongeza watumishi katika mahakama zetu mbalimbali ili kesi ziweze kwenda haraka. Pia niweze tu kutoa tahadhali vilevile kwamba hata kama kuna watumishi wapo wa kutosha, bado kesi ambazo zinachukuwa muda mrefu ni kesi za jinai ambazo zinahitaji kwa kweli uangalifu wa kutosha hasa upande wa upelelezi na vilevile katika kuchambua ushahidi ambaa unajitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa upande wa mahakama tutajitahidi kuongeza watumishi kama nilivyosema kwa upende wa Wilaya hiyo ya Rarya na tutajitahidi vilevile kuharakisha usikilizaji wa kesi nchini. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mahakama imejipanga kwamba, baada ya mwezi Disemba mwaka huu, kuanzia mwaka kesho Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu zitahakikisha hazina kesi za zamani zilizozidi umri wa miezi 24 yaani miaka miwili. Vilevile Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi hazitazidi mwaka mmoja na Mahakama za Mwanzo hazitakuwa na kesi za zamani za miezi sita.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba Kilolo haina Mahakama ya Wilaya, namuomba sana Mheshimiwa Mbunge, hizo Wilaya tunazihitaji, lakini ujenge na hoja tuletee kwa maandishi, vilevile tuhakikishie una eneo lenye nyaraka stahili tuweze kuingiza katika mpango wa ujenzi wa mwaka ujao wa fedha. (Makofii)

**SPIKA:** Nimewaona Mheshimiwa Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Musukuma anza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliahidi kuja kufanya ziara katika Mkoa wa Mara na hususan Wilaya ya Rarya, lakini kwa sababu zisizoweza kuzuilia alikomea Musoma.

Je, yuko tayari sasa baada ya Bunge hili kuambana na Mbunge wa Rarya ili kwenda kuona usumbufu wa wale wananchi wa Rarya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, sijawahi kwa kweli kuahidi kwenda Wilaya ya Rarya, lakini ahadi yangu ipo palepale ya kuzuru Mkoa wa Mara mzima. Kutokana na tatizo hili kwamba Rarya kweli ina *special conditions* za kutembelea, naomba tu Mheshimiwa Mbunge ajenge hoja mimi nina muda wa kutosha wa kuweza kufika huko na tukakagua maeneo mbalimbali. Lakini ziara ya Mkoa wa Mara ipo palepale tutafuatana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa sababu lengo letu kubwa ni kukagua vilevile Magereza Mkoani Mara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la mwisho la nyongeza kwenye eneo hili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kiukweli nasikitika kwa majibu ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusiana na umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Rorya. Tangu Bunge la Kumi nakumbuka nikiwa Mbunge wa Viti Maalum nimekuwa nikiongelea suala zima la kupatikana kwa Mahakama ya Wilaya ya Rorya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kukiwa hakuna Mahakama Wilaya ya Rorya, Mahakama ya Wilaya ya Tarime inakuwa na kesi nyingi na ndiyo maana mwisho wa siku tunakuwa na mrundikano wa kesi ambazo hazifanyiwi uamuzi kwa muda muafaka. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Rorya tayari wana ardhi na kwa sababu tumekuwa tukiongea umuhimu kuwa na Mahakama ya Wilaya ya Rorya tangu Bunge la Kumi, ni vegezo vipi ambavyo vilitumika kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 wasipeleke Mahakama ya Wilaya Rorya wakaamua kupeleka sehemu nyingine Tanzania ikizingatiwa jiografia ya Wilaya Rorya ni kubwa, watu wanatoka mbali sana kuja Wilaya ya Tarime. Naomba kujua ni vigezo vipi vimetumika kwa Serikali isiweze kujenga Mahakama ya Wilaya ya Rorya mwaka huu wa fedha hadi waseme ni mwaka ujao wa fedha? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimetamka mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tuna tatizo kubwa la miundombinu ya mahakama, kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama Kuu katika nchi yetu. Nimelieleza wazi hili na tatizo hili haliko Rorya tu!

Mheshimiwa Spika, nilimeshaeleza wakati ninajibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge watatu katika Mikutano iliyopita kwamba ninalishukuru Bunge lako Tukufu limetupitishia shilingi bilioni 46.76 kwenye Mfuko wa Mahakama na hizo shilingi bilioni 46.76, tutatumia shilingi bilioni 36 kujengea mahakama hii haijapata kutokea. Vilevile, tuna fedha ambayo mapema mwaka huu, mnakumbuka Mheshimiwa Rais aliagiza wapewe zote mahakama shilingi bilioni 12.3 jumla ni bilioni 48.3.

Mheshimiwa Spika, tumesema tunaanza kwa ujenzi wa mahakama 40 katika mwaka huu wa fedha, ninaomba utuamini kwa sababu mahakama sasa hivi imeshaanza ujenzi wa kisasa wa mahakama tena nafuu, lakini ujenzi uliyo bora kwa miezi mitatu anapata mahakama ya kisasa kama tulivyofanya mahakama ya Wilaya ya Kibaha.

Namuomba Mheshimiwa Mbunge avumilie tu, tumeipanga Rorya katika mwaka wa fedha 2017/2018, wavumilie kama Wilaya zingine zinavyovumilia kwa sasa.(Makofii)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea baada ya Wizara ya Katiba na Sheria, sasa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Swali linauliza na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbungeni wa Chambani.

Na. 100

### **Kuboresha Chuo cha Misitu Olmotonyi**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN** aliuliza:-

Karibu theluthi moja ya ardhi ya Tanzania ni misitu na kuna uhaba mkubwa wa watalaam wa misitu nchini.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha Chuo cha Misitu cha Olmotonyi?

(b)Je, kila mtalaam wa misitu aliyepo leo anasimamia hekta ngapi za eneo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna upungufu wa watalaam wa misitu nchini. Kwa sasa kila mtalaam wa misitu aliyepo anasimamia jumla ya hekta 25,000 za misitu. Kimsingi uwiano huu ni mara tano zaidi ya uwiano unaokubalika Kimataifa wa mtaalam mmoja kwa hekta 5, 000. Kwa kutambua hali hii, Wizara yangu imeanza kutatua tatizo hili kwa kuboresha miundombinu ya Chuo cha Misitu Olmotonyi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Norway inatekeleza mradi wa kuwezesha jamii kupitia mafunzo ya shughuli za usimamizi shirikishi wa mistu na mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unalenga kukijengea chuo uwezo kwa kukarabati nyumba za watumishi saba, kuimarisha maktaba ya chuo kwa kuweka samani, vitabu vya kiada na vitabu 137 vya mada 22 tofauti, vifaa 62 vya kufundishia, kompyuta 15 na kutoa mafunzo ya kompyuta kwa wakutubi watano; ukarabati wa mtandao wa mawasiliano na kuunganisha chuo na Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia mradi unaendelea na ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wanachuo 100 na ukumbi wa mihadhara wenyewe uwezo wa kuchukua wanachuo 200 kwa wakati mmoja. Vilevile mradi umewajengea uwezo wa kutumia mbinu bora za kufundisha wahadhiri 16 wa chuo hicho. Mradi unatoa mafunzo kwa jamii ya vijiji ni kuhusu kuhifadhi misitu na shughuli mbadala za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kupitia mradi huu, Serikali inatoa ufadhili kwa wanafunzi wa ngazi za cheti na ngazi za diploma ili waweze kukamilisha mafunzo yao katika chuo chetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu, kuanzia mwaka 2013/2014 mpaka 2015/2016, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imegharamia ukarabati wa nyumba tisa za watumishi, kumbi za chakula na mikutano; na ununuzi wa kompyuta mbili na basi aina ya Tata kwa ajili ya usafiri wa wanafunzi wanapokwenda kupata mafunzo nje ya chuo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizi, chuo kumeongeza uwezo wake wa kupokea wanafunzi wengi zaidi na kuwajengea uwezo wawe wataalamu mahiri katika ngazi ya masomo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo anajitetea na kijificha katika msitu wa njugu. Ni-declare interest mimi ni mtaalam wa misitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilichouliiza ninataka kujua Serikali ina mkakati gani mahsus i wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika chuo kile ili kukabiliana na paragraph ya mwanzo ya majibu yako. Ileleweke kwamba tunaposema wataalam wa misitu (*foresters*) hasa ni wale certificate na diploma kwa sababu wale ndiyo field officers na kukosekana kwa wale ndiyo sasa hivi deforestation imeongezeka na afforestation imepungua.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua mkakati upi wa Serikali wa kuongeza idadi ya wanafunzi wa certificate na diploma katika chuo kile ili kukabiliana na hali hii tuliyonayo katika nchi yetu ya uharibifu wa misitu na mazingira? (*Makofii*)

Swali la pili, mheshimiwa Waziri, Chuo cha Misitu cha Olmotonyi katika miaka ya 1980 kilikuwa na hadhi ya Kimataifa, sijui leo; na kilikuwa kinapokea wanafunzi kutoka nje ya nchi. Je, Serikali inasema nini katika kukiboresha chuo hiki kikaendelea kupokea wanafunzi kutoka nje ikawa ni moja kati ya source of income za Serikali hii, kuipatia fedha za kigeni? Nashukuru! (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein. Majibu sasa ya maswali hayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Profesa Jumanne Maghembe.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Yussuf kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni uwezo wa chuo kuongeza wanafunzi na katika jibu la msingi hapa, tumepanua chuo ili kiweze kuwa na *hall* ya mhadhara mmoja ambao unaweza sasa kubebe wanafunzi 200 kwa wakati mmoja. Tumepanua na nafasi nyingine na hasa kuboresha maktaba ili iwe bora zaidi na iweze kuwa na rasilimali za vifaa vya kujifunzia bora zaidi. Kwa kufanya hivyo tunaweza kuongeza wanafunzi wengi zaidi na kufanya chuo kitoe mafunzo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huko nyuma, Chuo cha Olmotonyi kilikuwa kinachukua wanafunzi kutoka nje ya nchi, lakini katika ngazi hii ya cheti na ngazi ya *diploma*, hii ni ngazi ya msingi sana kama elimu ya msingi kwenye mafunzo haya ya misitu.

Mheshimiwa Spika, katika mafunzo haya ya misitu nchi nyingi ambazo ziliikuwa zinaleta wanafunzi kwetu zimejjengea uwezo wake wa kutoa mafunzo ya msingi. Siku hizi wanafunzi wa Kimataifa wanakuja kusoma kwenye chuo chetu cha misitu kilichopo kwenye Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ambacho ndicho chuo bora zaidi kwenye fani ya misitu kuliko vyuo vyote Barani Afrika.

**SPIKA:** Swali liliulizwa na Mheshimiwa Yussuf ambaye ni Afisa Misitu na limejibiwa na Profesa Maghembe ambaye ni Afisa Misitu pia. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba.

Na. 101

### **Fidia kwa Wahanga wa Barabara ya Mwandiga – Manyovu**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni Jimbo la Kigoma Kaskazini aliahidi kuwalipa fidia wahanga wa Barabara ya Mwandiga – Manyovu.

Je, ni lini jambo hilo litatekelezwa?

## **NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mwandiga - Manyovu, yenyeye urefu wa kilometra 56.26 ulianza mwaka 2009 na kukamilika mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii wananchi wa Mwandiga hadi Manyovu walilalamika kwa kuvunja nyumba zao wenyewe bila kulipwa fidia kwa agizo la Serikali. Mwaka 2010 Serikali iliunda tume ya kuchunguza malalamiko hayo na kugundua kuwa wananchi hao walivunja nyumba hizo kwa kuwa zilikuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara kinyume na Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake, hivyo wananchi hao hawakusatahili kulipwa fidia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba umeridhika, hawakustahili fidia?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana nimemshangaa kidogo Naibu Waziri. Kwanza inaonekana historia ya barabara hii haifahamu. Nitaomba kabla sijaauliza maswali mawili madogo, niseme kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi wa barabara hii ya Mwandiga - Manyovu unaanza, kuna watu waliambiwa na Serikali wabomoe wakafuata sheria wakabomoa, wale waliogoma kubomoa wote walilipwa na Serikali hii. Hapa naulizia wale walitii sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize masawli mawili ya nyongeza.

Je, Rais Magufuli ambaye alikuwa Waziri wa Ujenzi, Sheria ya Babaraba hii anaijua vizuri sana, na Waziri Magufuli alipokuja pale kuomba kura eneo la Kalinzi, tarehe 19, mwezi wa Septemba alisema yafuatayo wakati akisema tungependa vitu gani atusaidie atakapokuwa Rais. Moja ya mambo makubwa manne aliyambiwa mojawapo ilikuwa ni suala la fidia ya wale watu amba walitii sheria walipwe. Rais Magufuli alisema maneno yafuatayo, alisema; "Ninajua mgogoro wa barabara hii, wale amba hawakulipwa wameenda mahakamani, ninawaomba mfute kesi tukimaliza uchaguzi na ninyi mtalipwa." Wale wote wamefuta kesi. Sasa nimuulize Naibu Waziri, kesi imefutwa, Rais aliahidi, sasa tujiulize, Rais alitudanganya au wewe ndiye unayetudanganya hapa?

**SPIKA:** Bado napima kama swali hili kweli siyo la uchonganishi. Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una maelezo, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwahakikishie wananchi wale walioathirika wa kati ya Mwandiga na Manyovu, wakati wanaahidiwa na Mheshimiwa Rais kwamba atawalipa fedha kama wahanga wa ile barabara alikuwa hadanganyi, alikuwa anasema kutoka katika sakafu ya moyo wake.

Pili, tunapolijibu swali hili, kwa sababu swali hili eneo lililopewa nguvu ni eneo la fidia, sasa ukitoa nguvu katika swali kwenye eneo la fidia wakati huku unajua kwamba hawa watu hawastahili fidia inakuwa ni tatizo. Kwa sababu hatuwezi tuka-create precedent, maeneo mengi sana tumewataka watu wa mita 30 toka hifadhi ya barabara wabomoe nyumba zao bila fidia, kwa sababu ndivyo sheria inavyosema, lakini tunapoongelea kuwalipa wahanga ni kitu kingine na ahadi ya Rais ni kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wale wahanga kwamba Mheshimiwa Rais atatekeleza ahadi yake ya kuwalipa, anawalipa kama wahanga, hatuwalipi fidia. Fidia hatulipi ndani ya eneo la mita 30 au mita 22.5 kwa kipindi kile cha chini ya mwaka 2007, na kwa sasa hatulipi ndani ya mita 30 kila upande.

Ninaomba tukileta precedent hapa tutaleta matatizo katika nchi hii, kama ahadi ya Rais kwa specific case ya eneo la Mwandiga mpaka Manyovu, itatekelezwa kwa asilimia 100 kama ambavyo ahadi nyingine zote za Rais tutahakikisha zinatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano.(Makofii)

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Suala la fidia katika kupisha ujenzi wa barabara kule Mwandiga linafanana kabisa na barabara ya lami inayojengwa kutoka Nyamswa - Bunda - Kisolya - Nansio ambayo na yenyewe wananchi kule wanastahili kufidiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka nimemsumbuwa sana juu ya jambo hili, nimemsumbuwa sana Mheshimiwa Waziri, lakini wananchi kule wanadhani mimi sifanyi kazi wanadhani siwasilishi matatizo yao.

Naomba kupitia kinywa chake ndani ya Bunge hili, Wanamwibara wanamsikia, atuambie ni lini fidia ya Wanamwibara hawa watafidiwa kwa sababu wamepisha ujenzi wa barabara? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, nimpungeze sana Mheshimiwa Mbunge Kangi Lugola kwa namna anavyofuatilia haki za wananchi wake. Namuomba sana kwamba wale ambao wanastahili kulipwa fidia tulimuahidi kwamba Serikali itahakikisha watu hawa wanalipwa fidia mara tutakapopata fedha. Hapa hatuongelei watu ambao hawastahili kulipwa fidia kwa maana ya wale ambao majengo yao yalikuwa ndani ya eneo la hifadhi. (Makofi)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, swali la Kigoma Kaskazini linafanana kabisa na swali la wananchi wa Segerea na Ukonga. Wananchi wa Kipunguni A, Kipunguni Mashariki, Kipawa na Kigilagila waliambiwa wapishe maeneo yao kwa ajili ya ujenzi au upanuzi wa uwanja wa ndege. Wanachi hawa wamefanyiwa tathmini tangu mwaka 2007, imekuwa ni danadana, sasa Waziri atuambie ni lini wannachi hawa watalipwa fidia baada ya kuwa wanapewa pesa kidogo wanaambiwa watalipwa na siku zinakwenda na wanashindwa kuendeleza maeneo yao.

Je, ni lini, fidia hizo zitalipwa na hawa wananchi waweze kupata maeneo mengine ya kujisitiri? Wananchi hao wanamsikia. Nakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia na wewe unaishi Kipawa pia? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Segerea anafahamu kwamba tulikaa kikao...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea tu, Mheshimiwa Mbunge, halafu endelea.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Naomba nipewe fursa ya kujibu swalii.

Mheshimiwa Mbunge wa Segerea alishafanya kikao na mimi mwenyewe kuniita, katika kikao hicho nilikutana na wahusika wote wanaotakiwa kulipwa fidia katika eneo la Kipunguni. Kwa hiyo, namshukuru sana, kwanza Mheshimiwa Anatropia kwa kumuunga mkono Mbunge mhusika katika eneo hili na Mbunge mhusika katika eneo hili anafahamu kwamba nimeshatoa ahadi ya kuhakikisha suala la kulipa fidia eneo la Kipunguni kwa ajili ya kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege nitalishughulikia na litafikia mwisho katika kipindi hiki cha miaka mitano na anafahamu sababu yake.

Mheshimiwa Spika, sababu yake ni kwamba kuna fedha ilishatolewa, lakini kuna uwezekano fedha zilizotolewa zote hazikuwafikia walengwa. Kwa hiyo, tumeunda Tume inafanya uchunguzi wa suala hili kuhakikisha zile fedha zilizotakiwa kuwafikia walengwa tujue zimeenda wapi na tutafunua kila palipofunikwa kuhakikisha fedha zile zilizokusudia kulipa wahanga wale zinapatikana na hatimaye wahanga walipwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilimhakikishia Mbunge mhusika wa hilo eneo na sasa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Anatropia, suala hili tumelichukua kwa nguvu na tutalishughulikia, tutafukua kila aina ya kaburi kuhakikisha kwamba wahusika wanalipwa fidia iliyostahili. Nilitoa katika mkutano ule wa wadau kwamba ni katika kipindi hiki cha miaka mitano. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Anatropia endelea kumuunga mkono Mbunge wa Segerea. (Makofi)

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma. (Makofi)

Na. 102

### **Huduma ya Afya kwa Makundi Maalum**

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

Huduma za afya bila malipo kwa wamama wajawazito, wazee na watoto chini ya miaka mitano ni Sera ya Afya ya Taifa lakini utekelezaji wake umegubikwa na rushwa na urasimu mkubwa.

(a) Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha utekelezaji wa sera hiyo ili kupunguza vifo kwa makundi hayo mijini na vijijini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za upasuaji wa kupanga na ule wa dharura kwa akina mama wajawazito hasa wa vijijini ili kupunguza vifo vyta mama na mtoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imendelea kutumia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ilioainisha makundi maalum ya watu, (wanawake wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, wazee wanaozidi miaka 60, watu wenye ulemavu na wasiojiweza) kwa kuzingatia sheria zilizopo ili kutekeleza mikakati ya kuleta unafuu kwa huduma za afya kwa watu wote wanaotakiwa kupewa huduma za afya bila malipo. Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya utaratibu ambao utawafanya wananchi wote wawe wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hatua hii ikifikiwa, changamoto nyingi zinazowapata watu walio katika makundi maalum wanaotakiwa kupewa huduma za afya bila malipo zitakuwa historia. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inaendelea na kuimarisha uongozi katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha kuwa watoaji wa huduma kwa makundi haya wanazingatia sera, sheria, mikakati, miongozo na maelekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha huduma za afya kwa wananchi kwa ujumla wake.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi, hasa wanaoishi vijijini, wanapata huduma za upasuaji za kupanga na zile za dharura, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kuvijengea uwezo vituo vya afya, hasa vilivyopo vijijini ili viweze kutoa huduma za upasuaji hasa wa dharura. Vituo hivyo vimeonesha kuwa na uwezo huo na vinaokoa maisha ya wananchi, hasa wanawake wanaohitaji upasuaji wa dharura. Katika kuvijengea uwezo vituo hivyo, Wizara ikishirikiana na wadau mbalimbali inaboresha miundombinu, watumishi, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa akina mama wengi wajawazito hususani vijijini wamekuwa wakipoteza maisha wakati wa kujifungua kwa sababu ya kukosa huduma ya kupangiwa kufanyiwa *operation* kabla ya siku ya kujifungua, hii imekuwa ikitokana na kwamba akina mama hawa hawapati elimu pale wanapokuwa wanakwenda katika vituo vya afya kwa ajili ya kliniki, hawaambiwi kwamba inawezekana kama mtu anakuwa na matatizo basi afanyiwe *operation* ya kupanga. Serikali imekuwa ikisisitiza *operation* za dharura, na hata katika majibu ya Waziri, amesisitiza sana katika huduma za vituo vya afya kutoa upasuaji wa dharura.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutoa mwongozo katika vituo vya afya kwamba wanapotoa elimu kwa akina mama wajawazito wawaelimishe juu ya elimu ya kupata upasuaji wa kupanga ili kuokoa maisha ya mama na mtoto? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwanza, napenda yeye mwenyewe pamoja na Wabunge wote wafahamu kuwa suala la kupunguza vifo vya wanawake wajawazito wakati wa kipindi cha uzazi ni suala *systemic*, hakuna mkakati mmoja unaoweza kulipatia ufumbuzi. Nikisema ni suala la kimfumo ninamaanisha kwamba ni lazima mfumo mzima uweze kufanya kazi ndipo tuweze kushusha vifo vya akina mama wajawazito katika kipindi cha kujifungua. Kwa maana hiyo ni rai yangu kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye Halmashauri zetu tushiriki kwenye vikao vya kufanya maamuzi ili tuweke kipaumbele kwenye kujenga vyumba vya upasuaji, maabara, na Serikali tutatimiza wajibu wetu wa kupeleka watumishi wenyewe ujuzi wa kutoa huduma ambazo zitawezesha vituo vyetu vya afya nchini viweze kutoa huduma za upasuaji wa kupanga kama anavyozungumza Mheshimiwa Kiteto.

Mheshimiwa Spika, kwamba elimu inatolewa ama haitolewi, elimu inatolewa kila siku kwa akina mama wote wanaofika kliniki, pia niwapongeze akina mama wote nchini kwa kuelewa umuhimu wa kuhudhuria kwenye kliniki za uzazi kipindi wanaposhika ujauzito kwa sababu kiwango cha mahudhurio kimeongezeka sana kutoka takribani asilimia 56 miaka kumi iliyopita mpaka kufikia kiwango cha asilimia 86 kwenye miaka ya karibuni. Hivyo ni kwamba uelewa sasa umeongezeka, akina mama wanadai huduma za kliniki ziwepo, sasa kazi ni kwetu kuzitoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulipa taarifa Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania ina vituo vya afya vipatavyo 489 tu, katika hivyo ni 113 tu vinavyotoa huduma za upasuaji na hii ni changamoto ambayo ipo kwenye Halmashauri zenyewe kwamba zikamilishe katika vituo hivi 489 vianze kutoa huduma za upasuaji na ndiyo kazi ninayoifanya kila siku kwenye ziara zangu. (Makofii)

**SPIKA:** Daah! Swali hili lina watu wengi kweli sasa sijui hata tufanyaje?

**WABUNGE FULANI:** Wanawake.

**SPIKA:** Akina mama eeh?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi ataanza Mheshimiwa Gekul, halafu Mheshimiwa Munde, tutamalizia na mmoja mwanaume. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake walijibu kuhusu suala hili la makundi maalum (akina mama wajawazito, watoto na wazee), walisema kwamba sasa wameiagiza Halmashauri zetu waorodheshe wazee ili wapatiwe kadi za bima ya afya. Naomba nifahamu kama Serikali ipo serious huo mwongozo umeshatolewa na TAMISEMI katika Halmashauri zetu ili Madiwani wapange fedha hizo za kuwalipia wazee bima ya afya katika bajeti inayofuata? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu mafupi kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamisi Kigwangalla

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza mwongozo ulikwishatoka na Halmashauri tayari zimeanza kutekeleza mpango huo wa kuwakatia CHF wazee wote waliopo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba Wabunge wote washiriki kwenye vikao vya bajeti vya mwaka huu ili wasimamie suala hili, kwa sababu utekelezaji wake upo kwenye Halmashauri. Pesa za kuwakatia kadi za CHF wazee wa nchi yetu waliotumikia ujana wao kuletea maendeleo Taifa letu zipo kwenye own source, kwenye vyanzo vya ndani vya Halmashauri ambavyo sisi kama Wabunge ni Madiwani tushiriki kwenye vikao hivyo, tuweze kuwakatia kadi za CHF wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, mwongozo ulikwishatoka na kuna baadhi ya Halmashauri zimeanza kutekeleza mfano mzuri ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kwa rafiki yangu Mheshimiwa Allan Kiula, wao wanatekeleza na wazee wengi wamefaidika na mpango huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe swali la nyongeza tutamalizia na upande huu Mheshimiwa Magdalena Sakaya utakuwa wa mwisho.

**MHE. MONDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi kipengele (b) linafanana kabisa na tatizo tulilonalo Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora tulipata mamilioni ya pesa tukajenga chuo cha *nursing* na *theatre* ya kisasa, mpaka sasa tumekamilisha kwa asilimia 90 sasa hivi tuna miaka minne bado asilimia 10 tu jengo lile na *theatre* ya kisasa vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nilikuja hapa Bungeni nikamuuliza Naibu Waziri Mheshimiwa Kigwangalla akaniambia ataleta wataalam na yeye atakuja na atalifuatilia kwa sababu ni kama milioni 40 na kidogo tu ndiyo zinasababisha lile jengo liharibike na lishindwe kufanya kazi na *theatre* ya kisasa ishindwe kufanya kazi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mara ya pili leo, anawaeleza nini wananchi wa Mkoa wa Tabora kuhusu chuo chao *nursing* na *theatre* yao ya kisasa? Na atupe majibu ya ukweli. (Makofii)

**SPIKA:** Watu wa Tabora kama chuo kile bado si mkasome kule Nzega kuna chuo kingine? Mheshimiwa Kigwangalla majibu na ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nimepokea concern yake nitafika pale Tabora wakati natoka kumzika mzee wetu Mzee Sitta, nitapita pale kukagua na kuona progress imekuwa ni nini kwa sababu tayari suala hili nilikwishaanza kulishughulikia na ninaamini kwamba lingekuwa limepatiwa ufumbuzi kufikia sasa. Kwa kuwa anasema bado naomba nitumie fursa hii ya kwenda mazishi ya Mzee Sitta kupita pale ili niweze kuona hali halisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya Kamishna swali la mwisho.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maagizo mbalimbali na matamko mbalimbali yanayotolewa hapa Bungeni na hata nje ya Bunge na Serikali kuhusiana na kutoa huduma bure kwa makundi haya muhimu, bado tumeshuhudia akina mama wanaojifungua hospitali wanazuiliwa na vichanga vyao kwa sababu tu wameshindwa kulipa gharama za kujifungua.

Je, Serikali inasemaje kuhusiana na haya yanayofanywa na uongozi wa hospitali kama Muhimbili, hospitali kubwa kumzuia mwanamke ndani ya hospitali zaidi ya wiki kwa sababu ameshindwa kulipa huduma za kujifungua. Serikali haioni kwamba inakwenda kinyume na sera zake? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa kuna matukio ya baadhi ya vituo vya kutolea huduma nchini kukiuka utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007. Nakiri kuwepo kwa mapungufu hayo, lakini tayari kwa kuwa tulipata taarifa tulikwisha kutoa maelekezo na hapa Bungeni katika Bunge

lililopita nilieleza na kufafanua wazi kwamba Sera ya Afya inaelekeza wakina mama wajawazito wote na watoto wote chini ya miaka mitano watibiwe bure, pamoja na makundi mengine mabayo nilitaja kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Spika, ninaagiza kwa mara nyingine tena, ninaagiza watoa huduma wote wa afya wa Serikali ama wenyewe mikataba na Serikali watoe huduma hizi bure kama Sera ya Afya inavyosema. Nikikuta ama nkipata taarifa kituo chochote kile cha kutolea huduma hakifuati misingi hii inayoagizwa na sera nitachukua hatua kali dhidi ya viongozi wa taasisi husika. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana swali la mwisho kwa siku ya leo la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Viti Maalum Tabora.

Na.103

### **Ugonjwa wa Sickle-Cell**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Ugonjwa wa sickle cell umejitokeza kwa wingi hapa nchini na watu wengi hawajui sababu zinazosababisha ugonjwa huo, huku wengine wakiamini kuwa unasababishwa na kurogwa au imani za kishirikina.

(a) Je, ugonjwa huo unasababishwa na nini?

(b) Je, dalili zake ni zipi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsantem kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kuuhakikishia umma kwamba ugonjwa huu ni wa kibailolojia na hauna mahusiano yoyote na imani za kishirikina. Ugonjwa wa sickle cell ambao kwa lugha ya kiswahili huitwa ugonjwa wa selimundu ni ugonjwa wa kurithi wa kupungukiwa na damu, ambapo mgonjwa huwa hana damu ya kutosha kwa sababu ya seli zake za mwili sio imara kiasi cha kubeba hewa ya oxygen kwenda sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, ili mtoto aweze kupata ugonjwa huu ni lazima wazazi wawe na vimelea vya ugonjwa huo. Chanzo halisi cha ugonjwa huu ni kubadilika kwa mfumo wa mwili wa kutengeneza vimelea vya kutengenezea damu yaani

haemoglobin. Hii husababisha seli zinazotengenezwa kuwa na shape ya seli kujikunja mithili ya mundu ambayo siyo ya kawaida. Mgonjwa hupata vimelea vya ugonjwa huu kutoka kwa wazazi wote yaani baba na mama kitaalamu tunaita carriers. Mama na baba wanaweza kuwa hawana dalili yoyote lakini wamebeba vimelea vya ugonjwa huo kwenye damu zao na kumzaa mtoto ambaye ana ugonjwa huu.

(b) Mheshimiwa Spika, mgonjwa wa selimundu yaani sickle cell haonyeshi dalili yoyote mpaka afikishe miezi minne ya umri tangu kuzaliwa na huanza na dalili zifuatazo; Kuishiwa damu, kuvimba vidole, kuchelewa kukua kwa watoto, kutoona vizuri na kusumbuliwa na mashambulio ya maumivu mara kwa mara sababu ya kukwama kwa seli hizo na kuzuia oxygen kwenda sehemu ya viungo vya mwili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mcemba swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa ugonjwa huu ni wa kitaalam zaidi na kwa kuwa elimu yake hajijatolewa kikamilifu; je, Serikali iko tayari kutoa elimu kwenye vituo vya afya, zahanati na Wilaya wanapohudhuria kliniki wakina mama. Kwa sababu waathirika wakubwa ni wakina mama, je, Serikali inasema nini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa ugonjwa huu dawa zake zina gharama sana, je, Serikali iko tayari kuzitoa dawa hizo bure ili akina mama na wananchi wote waweze kupata huduma hiyo? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu elimu Serikali tayari inatoa elimu kuhusiana na ugonjwa wa sicklecell na magonjwa mengine yote kwa kina mama kwenye kliniki ya uzazi pindi akina mama wanapokwenda kuhudhuria, aidha wao wenyewe kwa mahitaji yao mbalimbali ama watoto wao walio chini ya umri wa miaka mitano, kwa hiyo, elimu inatolewa.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa kwenye kutoa elimu ipo kwenye kutoa elimu kwa vijana ambao wanatarajia kushika mimba siku za usoni. Changamoto hii ni kwamba bado katika nchi yetu hatubajeti sana fedha kwa ajili ya kinga zaidi kwa kweli tunatumia fursa ya kliniki na watu wanaokwenda hospitalini ama fursa ya shule kutoa elimu ya afya kwa umma, kama tungepata fursa ya kibajeti ya kuweza kufanya hivyo tungeweza kufanya.

Sasa tunashirikiana na wadau mbalimbali kama Chama cha Kitaifa cha Sickle Cell ambacho kinatoa elimu nchi nzima kuhusiana na ugonjwa huu, pia kuna taasisi ya utafiti iko pale Muhimbili nayo inatoa elimu kwa umma nchi nzima kuhusiana na ugonjwa huu. Kwa vijana ambao wanatarajia kwenda kujifungua ama wanapata mwenza ni vema wakapima kama wao ni carriers wa sickle cell ama laa. Kwa sababu carrier wa sickle cell akiona na carrier wa sickle cell wakashika mimba maana yake mtoto ana hatari ya asilimia zaidi ya 25 ya kupatwa na ugonjwa huu kama homozygous yaani kuwa na sickle cell ambayo imekomaa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na ghamara za matibabu ya sickle cell hapa nchini, ugonjwa wa sickle cell napenda kumpa taarifa yeye, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba ni miongoni mwa magonjwa ambayo kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka 2007 ugonjwa wa sickle cell unatibiwa bure. Tiba ya sickle cell ni bure kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya, sasa hivi kuna taasisi imetufuata inataka kutekeleza huo mradi wa kutoa elimu kwa umma nchi nzima ili kuwa-screen watu wote wajue hali zao kuhusiana na sickle cell kama wao ni carrier ama siyo carriers.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda naomba sasa tuendelee na shughuli zingine mkiangalia saa yetu mtaona kwamba tunatakiwa tumalize kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na wageni waliopo katika jukwaa la Spika, tuna mgeni wetu ambaye ni Balozi wa Ireland hapa nchini Mheshimiwa Paul Sherlock, *Irish Ambasador to Tanzania*, karibu sana Mheshimiwa Balozi, ameambatana na Maafisa wawili kutoka Ubalozi huo Ndugu Robert Hull na Aran Corrigan ambaye ni Mshauri Mwandamizi wa Masuala ya Utawala Bora kutota kule na Afisa Ubalozi pia, karibuni sana ndugu zetu wawakilishi wa nchi ya Ireland katika nchi yetu ya Tanzania. (Makofii)

Tuna wageni 106 ambao ni wageni wangu mimi mwenyewe, wanafunzi 95 na walimu watano kutoka shule ya msingi ya NARCO Kongwa naomba msimame pale mlipo, wanaongozwa na Diwani wa Viti Maalum Mheshimiwa Asia Halamsa ambaye pia ni Katibu wa Vijana wa Wilaya. Shule hii ya msingi ni shule ya Serikali kule Kongwa, lakini ni shule ambayo kwa miaka kadhaa imekuwa ikifanya vizuri sana, kwa mwaka huu ilikuwa ni shule ya pili Kimkoa katika matokeo ya darasala saba. Kwa hiyo, shule ya kawaida ya Serikali inashindana na shule zile saint nini na nini na yenyewe inakuwa ya pili kwa hiyo naomba endeleeni kujitahidi mwakani muishinde shule ya Martin Luther ambayo ndio ya kwanza. Karibuni sana wanangu. (Makofii)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunae mgeni wa Mheshimiwa Lucy Magereli ambaye ni baba yake mzazi kutoka Mugumu Mkao wa Mara Ndugu Simon Mwita Magereli. Karibu sana Mzee wetu kutoka Mugumu mpaka hapa ni mbali kidogo, karibu Mzee Magereli. (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Halima Mdee ambaao ni wadogo zake kutoka Jimboni kwake Kawe Jijini Dar es Salaam. Ahsante sana karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Halima.

Wapo pia wageni wa nne wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambaao ni wananchi kutoka Wilaya ya Chunya, Mkao wa Mbeya, wale wa kutoka Chunya karibuni sana. (Makofi)

Pia wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Almasi Maige pamoja na Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambaao ni Madiwani wa Halmashauri ya Tabora Uyui, Madiwani wa Uyui karibuni sana Waheshimiwa Madiwani kutoka Uyui karibuni Dodoma, kila Wanyamwezi wakija hapa huwa nawakumbusha Dodoma magari mengi, kwa hiyo muangalie barabarani huko, msishangae shangae barabara huko. (Makofi/Kicheko)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zubeda Sakuru ambaao ni familia yake Ndugu Doris Mgone - mama yake mzazi na Ndugu Sera Mgone - mama yake mdogo karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Kuna wageni tisa wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkao wa Iringa ambaao ni viongozi wa Timu ya Lipuli kutoka Mkao wa Iringa, wakiongozwa na Katibu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkao wa Iringa, Ndugu Ramadhani Mahano karibuni sana. Wako kule Wanyalukolo karibuni sana, hivi Lipuli bado ipo? Nitamuuliza Mheshimiwa Mwamoto baadaye. (Makofi/Kicheko)

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaao ni wanakwaya wa hamasa kutoka Kilumbi Sikonge Mkao wa Tabora wakiongozwa na mwalimu wa kwaya hiyo Ndugu Fidelis Kombola. Karibuni sana ndugu zangu wa Sikonge, kama nilivyowaambia wenzeni wale wa kutoka Uyui magari mengi hapa muwe makini. (Makofi/Kicheko)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mbunge wa Kiteto ambaye ni wapigakura wake kutoka Kiteto, Mkao wa Manyara. Karibuni sana ndugu zangu kutoka Kiteto majirani zangu.

Pia wapo wageni 22 wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaao ni washindi wa Qambalo Cup 2016 ambaao ni timu ya Nyuki FC kutoka Karatu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo ya kawaida Ndugu Neema Kiula kwa niaba ya Katibu wa Bunge anawaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, kwamba mnaombwa ku-sign kitabu cha maombolezo kwa aliyekuwa Spika Mstaafu Marehemu Samuel John Sitta, ambacho kipo katika eneo la mashine za ukaguzi hapo nje karibu na lango kuu, hivyo Wabunge mnaombwa mkipita eneo hilo basi msaini kitabu kile kama ilivyokawaida na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Katibu Mkuu Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG) anawaomba Wabunge wanawake wote mkutane saa saba mchana kwa ajili ya semina maalum katika Ukumbi wa iliyokuwa zahanati ya Bunge (*Bunge old dispensary*).

Waheshimiwa Wabunge mbona maneno mengi mnawasiwasi zahanati kuna vipimo gani? Huo utaratibu wa kawaida tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania anaomba niwatangazieni Wabunge Vijana kwamba kutokana na dharura zilizopo uzinduzi wa umaja huo wa Wabunge Vijana uliokuwa ufanyike leo saa saba mchana umeahirishwa hadi Mkutano wa Bunge Ijalo, wale Wabunge vijana wale zoezi lenu lile limeahirishwa.

Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika anawaomba wanachama na washabiki wa Klabu ya Yanga, mkutane saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa 'D', ila huko waache ile mijadala ya kujadili kuroga roga wenzao maana yake jana Mbeya kule wamefanya sijui mambo gani. Hawa Yanga bwana, hawapendi sana maendeleo ya wenzao. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yameishia hapo nitoe nafasi kama kuna mawili, matatu, kabla sijamwita Katibu tuweze kuendelea.

## **MWONGOZO**

**SPIKA:** Katibu nitajie majina Waitara, washa chombo.

**NDG RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Millya...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Haonga

**NDG RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Bulaya na Mheshimiwa Zitto.

**SPIKA:** Haya tuanze na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru ninaomba mwongozo wako kutokana na Kanuni ya 68(7) na najielekeza kwenye Kanuni ya 46.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swalii namba 101 swalii ambalo lilikuwa linazungumzia habari ya fidia ya watu wa Kigilagila na Kipawa Dar es Salaam, swalii dogo ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest; wakati anajibu swalii alirudia mara kadhaa akionesha kwamba huenda Mheshimiwa Anatropia hakuwa na haki ya kuuliza swalii lile la nyongeza ni lazima amtaje Mbunge mwenye eneo husika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu wakafahamu kwamba eneo hili kwamba eneo hili pia linaathiri Jimbo la Ukonga kwa sababu wale wananchi ambaa waliondolewa Kipawa na Kipunguni wamepelekwa Kata ya Buyuni, Ukonga. Na hivi ninavyozungumza wananchi wale wamezuiliwa hata namna ya kukutana maeneo yale kujadili mambo yao namna ya kupata fidia kwa sababu ni tangu mwaka 2007 mpaka hivi leo niniavyozungumza. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni shida kubwa sana na alivyojibu hapa anasema kwamba alielekeza wadau wale kukutana wote, mpaka baada ya miaka mitano ndio jambo hili linaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu ninaouomba ni kwamba jana wakati swalii linaulizwa Mheshimiwa Mariam Kisangi aliuliza swalii dogo la nyongeza akizungumzia Jimbo la Ukonga, habari ya umeme, Pugu, Chanika, Msongola wala Naibu Waziri wakati anajibu hakuzungumza, hakunitaja Mbunge wa Ukonga kwamba Mbunge nimeshanzungumza naye. Naibu Waziri Nishati na Madini anakaa Pugu kwenye Jimbo langu; tumeongea naye zaidi ya mara 15 katika Bunge hili tangu Bunge limeanza kwamba umeme uende katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, alijibu jana hakutaja kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Ukonga Waitara mimi ninayezungumza nimeongea naye mara nyingi kama alivyofanya leo. Nilikuwa ninaomba mwongozo wako kwamba:-

Je, nikudhalilisha Viti Maalum wasiulize maswali ya nyongeza kwa sababu hawana majimbo au ni nini kinafanyika? Kwa sababu hakuna sababu ya msingi yoyote ya Mheshimiwa Mbunge anasimama kuuliza swalii la maana badala ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri kujielekeza kwenye jibu la msingi anaanza kumtaja mhusika ambaye ni wa chama chake. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba mwongozo wangu...

**SPIKA:** Tumekusikia Mheshimiwa Waitara naomba ukae kwa kweli wala siyo mwongozo ilikuwa ni maelezo tu ambayo wala hayana ukweli...

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**SPIKA:** Hakuna Mbunge yejote ambaye anazuiwa kuuliza swali lolote lile na Wabunge wengi limekuwa likiulizwa swali la mahali fulani, Mbunge wa mahali pengine anaunganisha anauliza swali la nyongeza na yamejibiwa hapa hapa. Kwa hiyo, tunaendelea Mheshimiwa Millya. (Makofii)

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 48 na kwa manufaa ya muda naomba nisiiosome.

**SPIKA:** Naomba usome kwa sababu ni kanuni ambayo hajazooleka.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 48(1) inasomeka hivi; “Masharti ya jumla yafuatayo yatatumika vilevile kuhusu hoja ya kujadili suala la dharura.”

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais, akifungua Bunge hili tarehe 20 Novemba, 2015; pamoja na mambo mengine aliyoyataja ni kwa namna gani nchi na wananchi watanufaika na rasilimali yao hususani ya madini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, kwa uzalendo, kwa ukweli aliyataja madini ya Tanzanite kama ni lazima mkakati wa kipekee uchukuliwe kwa ajili ya kuwanufaisha Watanzania na wananchi kwa ujumla kuhusu madini haya.

Mheshimiwa Spika, nilipoingia Bungeni nimekuwa nikipigia kelele kunufaika kwa wananchi wa Simanjiro, Naisinye na Mererani kuhusu madini ya Tanzanite, jambo ambalo mpaka sasa halijaza matunda. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2013 Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya Tanzanite One, na wazawa wakanunua hisa zile za kampuni ya awali ya wageni. Tangu kampuni hii ikabidhiwe kwa wazawa, wazawa hawa wamekuwa wakiwafukuza wananchi kazi, lakini la pili wananchi wa Simanjiro, Naisinye na Mererani kwa ujumla wake hawajaweza kunufaika na rasilimali yao kuanzia siku ile.

Mheshimiwa Spika, sasa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Millya nakuomba ukae kidogo Kanuni uliyoitumia unapaswa kuisoma yote mpaka mwisho.

Kuhusu jambo la dharura, pamoja na mambo mengine jambo la dharura lazima liwe na sifa ile ya 3(b) yaani liwe ni jambo ambalo linaudharura kwa maana ya kwamba limetokea siku hiyo au siku za karibuni sana.

Sasa hili unalolisema ni jambo ambalo unaweza ukalileta katika taratibu za kawaida nyingine ukaangalia kwenye kanuni, si dharura ya kwamba jana kuamkia leo kuna jambo huko Simanjiro limetokea katika mazingira haya unayojaribu kuyazungumzia.

Kwa jinsi hiyo naomba tu utumie Kanuni vizuri nitakupa nafasi katika fursa nyingine ili uliweke vizuri kama kawaida, kwa sababu siyo tukio hilo ni jambo la ukweli ulilolizungumza lakini linahitaji... hapana hapana hoja yako uliyoijenga bado imekwenda vibaya. Tunaendelea na Mheshimiwa Haonga. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Nilikuwa najenga hoja Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kama haupo ninakufuta mimi.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la leo wananchi wameandamana...

**SPIKA:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, kwa Kanuni ya 68(7) naomba pia niweze kuomba muongozo kuhusu jambo ambalo limetokea leo mapema Bungeni na jambo hili limezoleka, halijatokea leo tu, lakini limekuwa likijirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upendeleo wa dhahiri kabisa unaofanywa na kiti chako wewe pamoja na Naibu Spika, lakini pia na Wenyeviti, wale Wabunge tunaokaa huku nyuma mara nyingi tunaposimama kutaka kuuliza maswali ya nyongeza mara nyingi sana mmekuwa hamtuoni wala hamtukumbuki. Mnaangalia tu maeneo ya mbele hapo.

Mheshimiwa Spika, sijui mmekula maharage gani na suala hili limetuletea usumbufu sana kwa wapiga kura wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala hili limeniletea usumbufu sana kw awapigakura wangu na Wabunge wenzangu tunaokaa hapa limetuletea usumbufu sana, inaonekana kuna Wabunge wengine ambao ni muhimu kuliko wengine. Sasa ninaomba Mwongozo wako kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haonga, nilikuacha tu uendelee kusema kwa sababu bado ni katika Wabunge wageni, kumtuhumu Spika ni kosa kubwa sana. Mimi ni kiongozi mwenye hadhi yangu huwezi kunituhumu kienyejenyeji tu (Makofi)

Kwa kufanya hivyo unadhalilisha chombo hiki na unajidhalilisha wewe mwenyewe. Kwenye mihimili ya wenzetu, hawezi kusimama Ofisa wa Serikali akamtuhumu Rais kama unavyofanya, hawezi kusimama Ofisa wa Mahakama akamtuhumu Jaji Mkuu kama ulivyofanya, lazima tujenge misingi ya kuheshimiana na kupendana, kama kuna jambo si tunaambiana tu mzee huoni kushoto. (Makofi)

Lakini tufanyeupendeleo kwa lipi? Kama ni leo CUF mmeuliza maswali, CHADEMA mmeluliza maswali, CCM wameuliza maswali. Sasa maswali ya nyongeza sharti lake world over uonwe na jicho la Spika, sasa kama jicho la Spika halijakuona Haonga nafanyaje mimi, tena leo umevaa nguo nyeusi nitakuonaje? (Makofi/Kicheko)

Kwa hiyo, ninamalizia kwa kukupa onyo siku nyingine ukirudia hilo kwa hakika sitakuacha salama. (Makofi)

Mheshimiwa Ester Bulaya

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako na hii pia ipo kwenye moja ya Taarifa ya Kamati kuhusiana na taratibu na namna ambavyo baadhi ya Wakurugenzi wetu wanavyoendesha mambo sivyo.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea jimboni kwangu vibanda vimefungwa, wafanyabiashara wamejitatidi kwenda kwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi kutafuta ufumbuzi, imeshindikana. Mkurugenzi ametoa amri ya kupandisha bei ya vibanda kutoka shilingi 12,000 mpaka shilingi 50,000 bila Baraza kukaa kinyume kabisa na taratibu wala Kamati ya Fedha, lakini wafanyabiashara wale wamekuwa wanyenyekemu wamemfuata Mkurugenzi, Mkurugenzi hataki kuwasikiliza.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ninavyoongea vibanda vimefungwa, maduka yamefungwa, wafanyabiashara wamegoma katika Jimbo la Bunda Mjini na hilo pia ni moja ya vitu ambavyo linaikosesha Serikali mapato.

Nilikuwa naomba mwongozo wako nini kifanyike kwa hawa Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya wasiyofuata taratibu na wanaoingilia taratibu za Baraza, ahsante.

**MHE. LIVINSTONE J. LUSINDE:** Kuhusu Utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 64(1) Kuhusu Utaratibu, ningeomba kiti chako kimwelekeza Mheshimiwa Haonga afute maneno ya kwamba sijui mmekula maharage gani, haya ni maneno ya kihuni, yanayotumiwa kuwaambia watu kwamba wamevimbwa.

Kwa hiyo, naomba maneno hayo yafutwe kwenye Hansard, na ni maneno yasiyo ya Kibunge, hata wanaopiga kelele hawajui kwamba hayo maneno ni matusi na hayakubaliki kwenye lugha za Kibunge. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde ninashukuru sana kwa uliyoyasema ndio maana nilipojibu nilijibu vile kwamba lazima tujenge utaratibu wa kuheshimiana tu, hii kuropokaropoka namna hii watu tuna watoto, wajukuu. Eeeh, Mheshimiwa Haonga hatujaja jana sisi hapa. (Makofi/Kicheko)

Nililiacha hili nikijua Mheshimiwa Mboge yupo anajua atakaa naye baadaye atazungumza naye kwamba tabia za namna hii si tabia ambazo zinakubalika katika utaratibu wa Kibunge. Sikutaka kurudia maneno yake lakini ni maneno ya kudhalilisha, ya hovyo, hayana maana hata kidogo. Ndio maana nikasema siku nyingine ukirudia maneno hayo sitakuacha salama. Lazima kama kiongozi uwe kiongozi muda wote, siyo kuropoka tu eti kwa sababu hukuonwa wangapi ambao walismama hapa hawakupata maswali ya nyongeza? (Makofi)

Kwa hiyo, hiki ni kitu cha hovyo kidogo tukiache, turudi kwenye Bunge letu tuwe waungwana tufanye kazi zetu vizuri siyo kwamba kila anayekaa hapa kazi yake ni kubagua watu hilo jambo halipo. Halafu tangu tumeanza Bunge hili mimi nimekaa mara ngapi kwenye maswali hapa, mara ngapi nimekaa? Sasa katika hizi siku ambazo nimekaa ambazo hazizidi hata mbili nimependelea lini? Mheshimiwa Haonga!

Hapana, lazima tukumbushane, tunavuka mipaka kirahisi sana, tunajidhalilisha sisi wenyewe katika tabia hizi. Unamwambia Spika amekula maharage gani nani kakwambia nakula maharage mimi? (Kicheko)

Mheshimiwa Mbwe nakuachia hilo, najua kwa hakika utalishughulikia. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto wa mwisho.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mwongozo ninaouomba unahusiana na majibu ya maswali ambayo Naibu Waziri wa Ujenzi alijibu leo asubuhi kwa mujibu wa Kanuni 45 na 46 zinazohusiana na maswali. Na nitaomba kutumia Kanuni ya 45(3) kutaka majibu yaweze kujibiwa upya.

Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu alieleza kwamba wale wahanga wa ujenzi wa barabara ya Mwandiga - Manyovu hawakuwa wanapaswa kulipwa kutohana swali ambalo Mheshimiwa Serukamba aliliuliza.

Mheshimiwa Spika, Ukweli ni kwamba wananchi wale hawakuwa wamefuata hifadhi ya barabara, barabara ndiyo iliwaifuata na order ilivyotoka ya kubomoa wao wakatii mamlaka wakabomoa. Wale ambao waligoma kubomoa ikaja ikafanywa fidia wakalipwa kwa hiyo waliogoma kutii mamlaka walilipwa fidia, ambao walitii mamlaka kwa kubomoa wenyewe hawajalipwa fidia mpaka leo. Na huu ndio msingi wa swali ambalo Mheshimiwa Serukamba ameliuliza na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyajibu sivyo ambavyo ilivyo hali halisi kule Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba kwa kutumia Kanuni nilioitaja, uiagize Wizara ilifanyie upya kazi upya swali hili ili waweze kuja kujibu kwa mujibu ambavyo Mheshimiwa Serukamba aliuliza, wananchi wale waweze kupata haki yao ya fidia kwa kutii amri ambayo ilitokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mhusika Profesa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, tumeyasikia maelezo ya Mheshimiwa Zitto, tutalichukua na tutalifanyia kazi. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana, huo ndio mwisho wa miongozo kwa siku ya leo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize vizuri, tutakuwa na zoezi la kuaga mwili wa aliyekuwa Spika wa Bunge letu la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Samuel John Sitta hapa Bungeni kesho tarehe 11 Novemba, saa za mchana mara tu baada ya kumaliza shughuli zetu za saa saba.

Kwa hiyo, hiyo kesho tunatarajia kupokea mwili wa mpendwa wetu Marehemu Samuel John Sitta majira ya kwenye saa nane hivi katika uwanja wa ndege wa Dodoma na baadaye kutakuwa na Kikao Maalum cha Bunge saa nane na nusu mchana.

Narudia tena tutakuwa na Kikao Maalum cha Bunge saa nane na nusu mchana. Kwa hiyo nitawaomba by saa nane na nusu Waheshimiwa Wabunge wote tuwe tumekaa kwenye viti vyetu, kwa Kikao hicho Maalum cha Bunge ambacho hakijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu ambapo Wabunge mtapata nafasi ya kutoa salam za rambirambi na baadaye kutakuwa na utaratibu maalum wa kutoa heshima za mwisho. Utaratibu huo utaainishwa katika ratiba itakayotolewa baadaye leo na Order Paper ambayo itatolewa kesho asubuhi.

Baada ya shughuli za kutoa heshima za mwisho mwili utasafirishwa kwenda Urambo kwa mazishi kwa maana ya ndege kuondoka hapa Dodoma uwanja wa ndege saa kumi jioni kesho.

Katika msiba huo Bunge litawakilishwa na Wabunge 10 ambao watakuwa wamechanguliwa na Tume ya Huduma za Bunge kwa kuzingatia uwakilishi wa vyama. Ujumbe huo utaongozwa na Mheshimiwa Spika mwenyewe kuelekea huko Urambo siku ya Jumamosi kwa maana ya kwenda na kurudi.

Niongeze tu kwa kusema kwamba tunampa heshima za kipekee sana Mzee wetu, baadhi yetu tutaupokea mwili kutoka *airport*, tutakujanao hapa na tutauingiza ndani ya ukumbi hapo mbele ya kiti na baada ya hapo kutakuwa na ratiba maalum ambayo itaandaliwa, baadhi yetu watatuwakilisha katika kutoa maneno mafupi ya dakika watakazopewa na kiti kesho. (*Makofi*)

Kwa hiyo, watazungumza kwa niaba yetu na tutafanya hivyo kwa uwiano kama ilivyo kawaida ya Bunge letu na tutaongozwa kipekee na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Upinzani Bungeni katika zoezi hilo, halafu mwili ule tutautoa pale nje ya lango kuu, utawekwa pale kwa muda mfupi, tutaahirisha shughuli za Bunge maana yake wakati zoezi hilo linafanyika itakuwa kwa tunavyokadiria ratiba *tentative* ambayo ipo itakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa hotuba ya kufunga Bunge lakini nitakuwa sijawahoji. Kwa hiyo, kabla sijawahoji ndio zoezi hilo zima litafanyika ili iliingie Kibunge. Maana yake nikifunga Bunge haitakuwa kibunge tena itakuwa kienyeji.

Kwa hiyo, mwili utatolewa pale ili niweze kuwahoji kufunga Bunge mpaka tarehe inayofuata, mkiafiki basi nitafanya hivyo, nitakapokuwa natoka na ninyi tutafuatana kwa pamoja tutakapokuwa kule tutajipanga kwa mbele halafu jeneza lile litakuwa linapita pale na sisi wenyewe kama ni kusaidia kubeba na kadhalika kuelekea kwenye gari lililoandaliwa, tutafanya kazi hiyo kwa pamoja na baada ya pale wachache wetu wataenda *airport* kwa maana ya kusindikiza mwili. Hatutakuwa na zoezi lile tulilozoea la kufungua sanduku na kuanza kupita pale kwa sababu muda tuliopeleka mahali pakwa kwamba tumempa heshima kubwa sana Mzee wetu Marehemu Mzee Samuel John Sitta.

Lakini pia tunajenga msingi ambayo viongozi wetu wa kitaifa wakipatwa na jambo la namna hii watapata heshima hizo, sio tu uwanja wa Taifa Dar es Salaam au mahali pengine popote lakini ni kwa kuletwa Bungeni ambapo ndiyo nyumba ya wananchi wote wa Tanzania ilipo. (Makofii)

Kwa maneno hayo na kwa vile ratiba hiyo ya kesho inahitaji mabadiliko fulani fulani, nitaomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi asimame ili atoe hoja ya kutengua baadhi ya Kanuni za Bunge ili haya niliyoyaeleza yawezekane, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, karibu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa ridhaa yako sasa naomba nitoe maelezo ya hoja ya kutengua kanuni ili utaratibu ulioueleza mbele ya Bunge lako Tukufu kwa siku ya kesho uweze kuendana na matakwa ya Kikanuni.

KWA KUWA nchi yetu imepatwa na msiba wa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Samuel John Sitta ambaao ulitokea tarehe 7 Novemba, 2016 nchini Ujerumani;

NA KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepanga kumuenzi na kumuaga Marehemu Spika Mstaafu kwa kuwa na Kikao Maalum kwa ajili ya shughuli hiyo kesho ijumaa tarehe 11 Novemba, 2016 kuanzia saa nane mchana katika ukumbi huu wa Bunge;

NA KWA KUWA katika kikao hicho maalum familia na baadhi ya ndugu wa karibu wa marehemu wataingia ndani ya ukumbi wa Bunge na pia jeneza lililobeba mwili wa Marehemu Spika Mstaafu litaingizwa ndani ya Ukumbi wa Bunge na kwa kuwa Kanuni ya 139(1) na Kanuni ya 143(e) hadi (f) kinaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni wataketi maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya wageni na sio kuingia ndani ya ukumbi wenyewe wa Bunge;

NA KWA KUWA Kanuni ya 143 inayohusu mpangilio wa ukaaji ndani ya Bunge haihitaji vitu vingine vinavyoruhusiwa kukaa ndani ya ukumbi wa Bunge zaidi ya Wabunge, Watumishi, Mpambe wa Bunge na waandishi wa habari;

NA KWA KUWA vikao vya Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge vilivyoratibu maandalizi ya Bunge kumuaga Marehemu Spika Mstaafu vimeridhia na kuazimia kuliomba Bunge likubali kanuni nilizositaja hapo juu ziweze kutenguliwa;

HIVYO BASI, kwa madhumuni ya uendeshaji wa Kikao Maalum cha Kumuenzi na Kumuaga Spika Mstaafu Mheshimiwa Samuel John Sitta, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 139(1) na Kanuni ya 143(e) mpaka (f) zitenguliwe ili kuruhusu familia na baadhi ya ndugu wa karibu wa Marehemu Spika Mstaafu ambao kwa ujumla wao hawatazidi 12 waruhusiwe kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kushiriki tukio hilo muhimu na maalum.

Aidha, Kanuni ya 143 inayoweka mpangilio wa ukaaji Bungeni itenguliwe ili kuruhusu jeneza lililobeba mwili wa Marehemu Spika Mstaafu Mheshimiwa Samuel John Sitta liingizwe ndani ya Ukumbi wa Bunge na kuwekwa sehemu iliyandalialiwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge wote, lakini kama ilivyo ada naomba niwahoji sasa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Wote kabisa mmeafiki naomba niwashukuruni sana kwa kutupa baraka za kuweza kufanya jambo hili la kesho na kwa vile Mzee wa speed and standards pamoja na mambo mengine alianzisha mambo ya live coverage kesho kutakuwa na live coverage kwenye hilo zoezi. (Makofii)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Iendelee hiyo.

**SPIKA:** Sasa baada ya hoja hii ya kutengua kanuni kuwa imepita naomba nikuite Katibu kuhusu Miswada ya sheria za Serikali, Katibu. (Makofii)

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa mwaka 2016 (The Legal Aid Bill, 2016).

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Endelea Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016*)

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Endelea Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2016 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4)], Bill, 2016*).

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Hizo ndio sheria ambazo zimeshasomwa kwa mara ya kwanza tutazitendea haki katika kikao kijacho cha Januari/Februari mwakani naomba kwa wakati wowote ule zitakuwa zimewekwa kwenye pigeon hole zetu Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe kila mmoja anaondoka nazo ili kuzipitia na pale inapobidi kuwaona wananchi wenu kwa ajili ya maoni yao ili tuweze kuzijadili vizuri na kuzitendea haki katika Mkutano ujao wa Bunge, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Hoja za Kamati za Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya  
Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)**

(Majadiliano yanaendelea)

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea sasa naomba nimuite Mheshimiwa Naibu Spika aje aendelee na majadiliano.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala tulioanza jana, tunaanza na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mijadala hii miwili iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC kwa hiyo, nitajielekeza zaidi na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo kubwa sana wakati tukipitia hesabu za Serikali za Mitaa lililokuwa likijitokeza liliikuwa ni upungufu wa watumishi. Lakini nitajikita zaidi kwenye upungufu wa watumishi kwenye shule za sekondari, shule zetu za sekondari zina shida kubwa sana ya walimu wa sayansi. Katika Halmashauri zote ambazo tuliangalia vitabu vyake kila Halmashauri ilionyesha ina shida kubwa sana ya walimu wa sayansi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke tumetumia nguvu nyingi sana kujenga maabara, lakini sasa lipo tatizo la walimu wa sayansi. Niiombe na niishauri Serikali kwa kadri nionavyo mimi na nguvu tunazozitumia kupata walimu wa sanyansi bado ni kidogo mno, hitaji la walimu wa sanyansi ni kubwa, walimu waliopo ni wachache sana na jitihada tunazoziweka ni ndogo mno ili kupata walimu wa sanyansi. Katika suala la walimu wa sanyansi tatizo kubwa ambalo limetufikisha hapa ni wana sanyansi wenyewe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema wana sayansi wenyewe, ukichukua mwanafunzi anayeingia kidato cha kwanza hajui *chemistry* ni nini hajui *biology* ni nini hajui *physics* ni nini. Lakini mwalimu anayeingia darasani anaanza kumfundisha na kumwambia haya masomo ni magumu sana. Sasa kitendo hicho moja kwa moja kinapelekea mwanafunzi aanze kujenga hisia kwamba masomo haya ni magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana sisi kama Wabunge, niiombe Serikali tutumie muda mwingi kuongea na wanasyansi na waweze kuongea na wanafunzi kwamba sayansi sio ngumu na tangu hapo sayansi wala sio ngumu. Kwa sababu ugumu wa sayansi unakuja pale tu ambapo sayansi haina hadithi nyingi, ikiwa ni suala la *formula* ni *formula*, ikiwa ni *Archimedes Principle* ni *Archimedes Principle*, hakuna maelezo mengi wala nini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana tujitahidi sana na kama Serikali inaona inafaa ni bora ikaanzisha shule maalum za sayansi kwa maana ya kwamba tukianza na shule za sekondari *specially school for science* kwa hiyo pale tutajenga misingi mzuri, wanafunzi wale wataingia pale wakiwa wanajua kwamba wao ni wana sanyansi, huko mbele watatawanyika watapatikana madaktari, ma-engineer, walimu. Kwa hiyo tutakuwa tayari tumejenga msingi mzuri wa sayansi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwendo tunaonenda nao sasa na upungufu wa walimu wa sayansi ambao upo, kwa kweli kuja kukamilisha na kuweza kumudu kuwa na walimu wa sayansi wa kutosha ni kama ni ndoto. Naomba sana Serikali ilione jambo hili ni gumu na ilione kwamba hili linatakiwa

lifanyiwe kazi haraka sana ili tuweze kupata walimu wa kutosha wa sayansi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala la maabara, tulipokuwa tukipitia hesabu hizi na wenzangu wameseme uchochoro mkubwa wa fedha za Halmashauri umekwenda kwenye maabara, kila Halmashauri ilifika pale ikaeleza kwamba fedha imepelekwa kwenye maabara lilikuwa ni agizo la Serikali. Agizo la Serikali ni muhimu, kiongozi mkuu wa Serikali lazima aagize, asipoagiza huyo atakuwa ni kiongozi wa namna gani? Hoja inakuja watendaji hawa wanajua miiko? Kwa sababu pamoja na hayo maagizo wenywewe wamekurupuka tu wametumia mpaka fedha za kununulia dawa, wamechukua mpaka fedha ambazo zilikuwa za miradi ya maendeleo mengine. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana, sasa tufanye zoezi la muhimu la kupitia maabara hizi tujiridhishe kwamba viwango vya fedha vilivyoenda kwenye hizo maabara ni sawa sawa na ubora uliopo kwenye hizo maabara? Kwa sababu fedha yote katika Halmashauri wanasema imeenda kwenye maabara, kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia sasa thamani ya fedha kwenye ujenzi wa hizo maabara. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la uvezeshaji wa vijana na akina mama. Lipo tamko ambalo linasemwa kwamba ni asilimia tano kwa akina mama na asilimia tano kwa vijana kutoka Halmashauri zetu. Lakini kama kweli tunataka kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu na kuwapa akinamama mitaji ya kujiendeleza kibiashara, naona asilimia hizo tunazozitaja hazitoshi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu moja, asilimia hiyo haipo kisheria, lakini pili makusanyo ni kidogo sana. Jambo lingine Halmashauri zina majukumu mengi kweli kweli ambayo yanawabana hawa wanashindwa kuyatekeleza, sasa kuja kumpa kijana ambaye yupo mtaani kumuita kumwambia kuna asilimia tano yako hapa na wewe kama Halmashauri una shida ya fedha inakuwa ngumu sana. Ndio maana tunaona Halmashauri zote hakuna Halmashauri hata moja ambayo imemudu kutoa hizo fedha kwa asilimia 100 kwa miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iangalie utaratibu huu ikiwezekana ubadilishwe, uwekwe utaratibu mwingine ambao utaenda kwa uwiano mzuri na tutahakikisha kwamba vijana wetu na akina mama wanapata hizo fedha kwa utaratibu mzuri, vinginenyo tutakuwa tunatumia nguvu nydingi sana kuelekeza kwamba ni asilimia tano kwa akina mama na asilimia tano kwa vijana wakati kumbe uwezo wa Halmashauri ni chini sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu shughuli za Halmashauri ni nyingi sana sisi kama Wabunge tukija hapa Bungeni tukitoa maombi kwa Serikali kwamba kwenye Halmashauri yangu kuna shida hii, kuna shida hii Serikali inatujibu kwamba lazima iwe kwenye bajeti. Ukienda kwenye bajeti kuongea na watendaji pale Halmashauri jamani tuliiingize hili na wao wanakujibu wanakuambia ukomo wa bajeti. Sasa hebu angalia mkanganyiko huu jinsi ulivyokaa ndio ufkie mahali useme kwamba asilimia kumi ikatolewe kwa vijana na akina mama haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana sasa Serikali ione hilo na ijaribu kuangalia kwamba tunafanya nini ili tuwe na utaratibu unaofanana kwa nchi nzima unaowezesha kutoa fedha kwa ajili ya vijana na kwa ajili ya akina mama, lakini hizi asilimia imeonyesha ni zoezi lilioshindikana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la asilimia 30 ya makusanyo ya ardhi ambayo Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikikusanya na zinapeleka Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi hairudishi zile fedha kule Halmashauri na hairudishi kwa sababu inasema hawajaomba. Hivi jamani kuna sababu ya kuomba kwanini tunaweka bureaucracy katika hili, wewe mwenyewe Wizara ya Ardhi ume-declare kwamba 30 percent itarudi council warudishie wape na maelekezo fedha yenu hii nataka mfanye hiki na hiki, kama kuna utaratibu wa kukagua kakague. Wizara ya Ardhi imerundika fedha zote kwake, hairudishi Halmashauri inasema hawajaomba na tunataka fedha hizi zikirudi zirudi kwenye maendeleo ya ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Wizara ipo serious na inataka fedha zirudi kwenye maendeleo ya ardhi kwa nini isirudishe fedha na ikatoa na maelekezo halafu ikayasimamia maelekezo yake Halmashauri zikapata fedha. Kwa hiyo, unakuja kuona kwamba Halmashauri zinakusanya hii fedha na wakati mwingine Wakurugenzi wanajitua, wanatoa mpaka matangazo lipia kiwanja chako kwa gharama za Halmashauri tukitegemea kwamba 30 percent itarudi lakini ardhi hairudishi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali irekebishe utaratibu huo badala ya kukusanya na kurudisha ibakize ile asilimia 30 kule kwenye Halmashauri ili zibakiwe na ile fedha kwa ajili ya maendeleo ya ardhi. Kama kuna maelekezo wanataka watu wa ardhi wayafanye wayatoe, wawape watu wa Halmashauri ili kusudi watekeleze huo mpango ambao Wizara inaona unatakiwa utekelezwe na Halmashauri kutokana na hilo fungu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la East African Meat. Katika Jiji la Dar es Salaam walanzisha mradi wa kiwanda cha nyama pale Ukonga, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba Halmashauri ya Kinondoni, Ilala na

Temeke walichanga fedha pamoja na Jiji lenyewe kwa ajili ya kuanzisha huu mradi ya *East African Meat*, wakaweka na utaratibu wakaajiri na wataalam mchango ule kama mtaji walianza kulipana mishahara siku ile fedha ilipoisha na kampuni iliishia pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli huu ni utaratibu mbaya sana kwa watumishi wa umma kwamba Halmashauri zimechanga fedha, halafu mmeanzisha kampuni, fedha mliyoichanga kama mtaji mmelipana mshahara na maduhuli, safari na vikao vya bodi na nini halafu fedha imeisha kampuni imeishia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Serikali iangalie suala hili, moja katika suala hili la *East African Meat* kuna suala la kiwanja kilichopo pale Gongo la Mboto. Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam inaanza kuonyesha kwamba kile kiwanja ni mali yake. Ninaishauri Serikali kile kiwanja sio mali ya Jiji kile kiwanja ni cha manispaa zote za Dar es Salaam. Kwa hiyo, Serikali ione na iweze kusaidia kuhakikisha kwamba katika mali kidogo iliyobaki ambayo ni kiwanja kilichopo Gongo la Mboto Halmashauri zote za Dar es Salaam zinanufaika nazo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi tena kwenye suala la elimu naomba niseme jambo moja. Sasa hivi tumehangaika na maabara na madawati, lakini katika nchi yetu kuna kitu kigumu sana kinakuja kinaitwa elimu msingi na hii tumeshaanza kuitekeleza. Elimu msingi hii italeta ugumu zaidi kuliko wa maabara, kuliko wa madawati, kwa sababu itakapofika mwaka 2021 vijana walioko darasa la pili sasa watakuwa wamefikia kuingia kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wataingia kidato cha kwanza wakiwa darasa la sita, watamaliza darasa la sita wataingia kidato cha kwanza. Kwa hiyo na hawa walioko darasa la tatu sasa na wenyewe watakuwa wanaingia kidato cha kwanza. Imani tunayojipa kama nchi ni kwamba tumefikisha zaidi ya asilimia 75 watoto wetu wanaenda sekondari. Lakini tukumbuke kwamba wapo asilimia 75 lakini wana uwezo kiasi gani? Wanatembea umbali gani? Sasa tunataka tupeleke asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali hebu tuunde Kamati za Wilaya za kulisimamia zoezi hili kusudi kila Wilaya iwe na mtazamo wa kuona jambo hili tutalikabili vipi litakapofika kuna shida kubwa ya madarasa, itatokea shida ya nyumba za walimu, itatokea shida ya mahali pa kuishi wanafunzi kwa hiyo lazima tuone. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke watoto hawa ni wa Watanzania wote unapomfikisha mwanangu darasa la sita halafu unamwambia anaenda form one umenielimisha kiasi gani mimi kama mwananchi? Ni vizuri elimu kwa wananchi ikaenda ya kutosha ili kusudi wajue kabisa kwamba vijana walioko

darasa la pili sasa wataishia darasa la sita baada ya hapo wataingia kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo maelezo haya yaende sambamba hata kwenye taasisi zisizo za Serikali zinazotoa elimu, matokeo yake tutakaa kimya itafika siku ya siku wale vijana wameshatekeleza huo mtaala mpya wa elimu wanaingia kidato cha kwanza kila mtu anashangaa. Wote tutakuwa tunashangaa kama vile tulivyokuwa tunashangaa kwamba kwanini shule zetu hazina madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili tunalifahamu na watu wote sisi ni waelewa hebu tulifanyie kazi likae vizuri kusudi fanya maandalizi ya kutosha tukijua kabisa kwamba sasa ifikapo mwaka 2021 vijana wote walioko shule ya msingi watakenda sekondari, lakini watakuwa wanaingia sekondari wakiwa wamekomea darasa la sita. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme nashukuru sana kunipa nafasi na naunga mkono hoja asante. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitawasomea majina kadhaa ya wanaofuata, Mheshimiwa Mbarak Salim Bawazir, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali.

Waheshimiwa Wabunge jana niliwakumbusha kwamba orodha ni ndefu ya wanaotaka kuchangia kwa hiyo kwa ushauri tunaweza kukubaliana kuchangia dakika kumi ili kutoa nafasi kwa sababu kila chama kimeleta orodha ndefu kuliko wale ambao tutaweza kuwapa nafasi leo.

Kwa hiyo, aidha tutoe hizo dakika kumi sasa katika hizo kumi wanaopenda kugawana tano tano watanijulisha. Lakini tukisema 15 hawatafikiwa Wabunge wengi na hapa wote mmeleta orodha ndefu. Kwa hiyo, kama tunakubaliana na hiyo nadhani ni...

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika kumi.

**NAIBU SPIKA:** Dakika kumi eeh!

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Ndiyo. Bwana na wewe utaongea nini dakika 15.

**NAIBU SPIKA:** Sawa hili lilikuwa ni pendekezo na siyo tatizo la kwangu mimi, mimi nitaita tu majina lakini ngoja basi tuhojiane, tuhojiane.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Tunagawana dakika saba saba.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuhojiane ili tusipokubaliana, hatukubaliani ni jambo jepesi tu wala siyo gumu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Ngoja tushauri.

**NAIBU SPIKA:** Au kila mmoja atatoa dakika zake. Niwahoji eeh?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri dakika kumi zimepigiwa kura na wengi, yule ambaye dakika 15 zake anazitaka ataruhusiwa lakini mtu wa chama chake hatochangia kwa kwenda kwa ile idadi. Kwa sababu uwiano tunao na hesabu za dakika pia tunazo hapa hapa, kwa hiyo, kila mtu na upande wake anaposimama atasema *time* hapa wataweka vizuri ili tusigombane kwenye jambo ambalo ni la ushauri.

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Mbarak Bawazir, Mheshimiwa Azza Hillal Hemed.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba niseme ninaitwa Azza Hillal Hamad.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama ndani ya ukumbi wako kuweza kuchangia Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe kwa ruhusa yako, nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki ambao wameondokewa na wapendwa wao katika ajali ya gari ya aina ya Noah iliyotokea tarehe 6 Novemba, siku ya Jumapili katka Mji mdogo wa Tinde poleni sana Mwenyezi Mungu awape subira niko pamoja na ninyi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia katika Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Ukiangalia katika ukurasa wa 40 wa Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa mfuko wa wanawake na vijana asilimia kumi katika Halmashauri ambazo zimekafuliwa, tumekagua Halmashauri 164 katika Halmashauri 164, Halmashauri 112 hazikupeleka fedha ipasavyo katika mfuko wa wanawake na vijana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri 112 halmashauri 6 ziliagizwa na Kamati kuandika barua ya kuji-commit kulipa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Septemba. Cha kusikitisha Halmashauri hizo mpaka hivi ninavyoongea au mpaka Kamati inaleta taarifa ndani ya Bunge hazijaleta barua hizo. Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Halmashauri ya Jiji la Tanga na Halmashauri ya Ruangwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri hizo zilizokaguliwa kuna Halmashauri ambazo hazikuchangia kabisa hata shilingi moja kwa mwaka 2014/2015 ziko ukurasa wa 43. Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Halmashari ya Tunduru, Halmashauri ya Mpanda, Halmashauri ya Tunduma, Halmashauri ya Ludewa, Sengerema na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa wanawake na vijana umekuwa kama ni hisani kwa halmashauri. Watu wanafanya pale ambapo wanaona kwamba inafaa na Wakurugenzi wengi katika Kamati wamekuwa wakijibu kwamba wanatumia fedha hizo kwa sababu ya maagizo yanayotoka juu. Wengi wanasema wanatengeneza madawati, wamejengea maabara. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini fedha hizo zimekuwa kama shamba la bibi? Ni kwa sababu tu hakuna sheria ambayo ipo katika Halmashauri zetu inayowaelekeza Wakurugenzi kupeleka fedha hizo kwa wanawake na vijana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukilisema kwa muda mrefu hili ni tatizo sugu kwa Halmashauri. Wanafanya hivi kwa sababu tu wanawake hawa na vijana hawawezi kwenda kwenye Halmashauri kudai haki yao kwa sababu haipo kisheria. Lakini kama Halmashauri inafikia kupewa maagizo na Kamati, kuandika barua ndani ya Kamati na Halmashauri inakaidi maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Halmashauri hizo haziheshimu wala hazitambui mamlaka zilizopo juu kwa maana ya kwamba waraka huu wa kupeleka mfuko wa akina mama na vijana asilimia kumi ulipelekwa kutoka TAMISEMI. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe na niishauri Serikali kwa kuwa Halmashauri zimekuwa hazi peleki fedha hizo, ni vyema basi Serikali ikaleta Muswada wa Sheria wa Mfuko wa Wanawake na Vijana ili wanawake na vijana hawa ambao wako kule na wanakosa nafasi ya kupata mikopo katika mabenki kwa sababu ya masharti yaliyopo ya mabenki waweze kukopeshwa fedha hizo kama haki yao ya msingi. Vinginevyo tutabaki kulalamika lakini fedha hizo hawatazipata. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaishauri Serikali mlete muswada wa sheria kwa ajili ya mfuko wa wanawake na vijana ili tuweze kuwakomboa wanawake na vijana waliopo kule majimboni kwetu. Katika taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Halmashauri pia ina tatizo sugu. Tatizo hili ni kwamba asilimia 20 ya vyanzo vya mapato zilivyofutwa Halmashauri haipeleki kwenye mitaa na vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 45 wa taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa utaona kuna Halmashauri ambazo tumezitolea mfano hazijapeleka kwa miaka mitatu mfululizo fedha za vijiji na mitaa. Halmashauri hizo ni Halmashuri ya Kilwa, Halmashauri ya Ngara, Halmashauri ya Hai, Halmashauri ya Rombo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwaliza hata fedha hizi kisingizio ni hicho hicho; maagizo kutoka juu. Sasa najiuliza, kwa Halmashauri ambazo wanaweza kupeleka fedha hivi wao wanafanya nini kutengeneza madawati? Kama siyo kwamba ni uongozi mbovu uliopo katika Halmashauri hizi wanashindwa kukaa na kuamua watatengeneza vipi madawati wanakwenda kuchukuwa haki ambayo siyo ya kwao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaondoa tatizo la rushwa katika ofisi za Serikali za Mitaa katika ofisi za vijiji kwa sababu ofisi za Serikali za mitaa na ofisi za vijiji hawana nyenzo za kufanya kazi. Ile haki yao ambayo wanatakiwa kuipata hawaipati; unakuta Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji na Mtaa, hana hata fedha ya kununua karatasi, unategemea nini kwa mwananchi aliyekwenda ana shida yake? Kama siyo kwamba ataombwa fedha ili aweze kukamilishiwa shida iliyompeleka ofisini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali badala ya fedha hizi kuzipeleka kwenye Halmashauri zetu na Halmashauri zinafanya ni shamba la bibi basi fedha hizi zipelekwe moja kwa moja katika vijiji na mitaa ziweze kuwafikia walengwa vinginevyo kila siku tutapiga kelele Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa hawawezi kupata haki yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nikitoka hapo niende, suala la Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu. Halmashauri nyingi zimekuwa zikikaimiwa nafasi hizi lakini cha kusikitisha wengine makuwa wakikaimu kwa muda mrefu na matokeo yake nafasi ile anakuja kupewa mtu mwingine, yeye aliyejaimu hapewi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafutiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Elias Kwandikwa ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kabisa ambacho nilitaka kuongelea ni kuhusiana na watu kukaimu kwenye Halmashauri zilizo nyingi ikiwemo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Geita na mfano kwa sababu niko kwenye Halmashauri tangu miaka mitano iliyopita kwa hiyo ninalewa hali halisi katika Halmashauri pengine na Halmashauri nyingine pia tatizo lipo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sasa niombe tu Serikali suala hili iweze kuwachukulia kwa uzito sana, unakuta kwamba vijiji vingi kwa mfano katika jimbo langu kule wengi yani watendaji wa kata wanakaimu, sasa mtu anapokaimu atawezaje kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi? (Makof)

Kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali ihakikishe iangalie namna kwenye vijiji ambako ndiko ambako tunapeleka shughuli za utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri kwa sababu miradi yote inatekelezwa kwenye vijiji au kwenye kata. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali iangalie utaratibu mzuri kuona kwamba watu wanaokaimu basi waajiri moja kwa moja ili watu waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. Wakifanya hivyo pengine itapunguzwa hata matumizi mabaya ya fedha ya Serikali, maana sasa kama mtu anakaimu anakuwa hana pia hata na uchungu maana hana uhakika na ile ajira yake. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ninaiunga mkono kabisa Kamati ambayo imelizungumzia kwamba watu wengi wanaokaimu katika ngazi ya Halmashauri, lakini vilevile kwenye kata na vijiji hili suala liangaliwe kwa umakini ili Serikali ione kwamba ni jambo la msingi kabisa kwamba watu wanapata, wanapewa fursa kama ni kukaimu basi iwe ni kwa muda mfupi baada ya hapo wapewe ajira za kudumu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni ile asilimia kumi ya mfuko kwa ajili ya wanawake pamoja na vijana. Katika Halmashauri zilizo nyingi jambo hili halitekelezeki, unakuta kwamba Halmashauri hizi zinafanya shughuli mbalimbali za maendeleo lakini wanapopata mapato yao hawawezi kutenga hizi fedha asilimia kumi kwa ajili ya akina mama pamoja na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe kwamba basi suala hili pia litiliwe mkazo kuwepo na usimamizi muhimu ili kuona kwamba sera na taratibu na sheria za nchi zinafanyiwa kazi na zinatekelezwa kulingana na inavyotakiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu udhibiti katika usimamizi wa mambo ya udhibiti wa ndani. Ina maana kwamba kama hatutaimarisha usimamizi wa ndani ina maana kwamba katika Halmashauri miradi mingi itakuwa inatekelezwa pengine chini ya viwango, lakini tukiimarisha udhibiti wa ndani hasa kwenye Halmashauri zetu mimi nina uhakika kwamba hata zile changamoto ndogo ndogo za fedha za miradi pengine kutekelezwa chini ya kiwango tutaweza kupunguza changamoto hii. (Makofii)

Mheshimiwa naibu Spika, kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali iweze kuimarisha kabisa vizuri tuweke wasimamizi ambao watakuwa na maslahi kwa ajili ya wananchi kuweza kuona kwamba kweli wanasimamia na kukagua, lakini pia kuishauri Serikali kuitia Halmashauri kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuweza kufanya shughuli za maendeleo kulingana na fedha ambazo zinatengwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala lingine la ruzuku kutokupelekwa. Ni kweli kwamba kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kulikuwa na changamoto kubwa sana kwamba fedha tulikuwa tunatenga ndani ya Bunge, lakini mwaka unapita zilizokuwa zimepelekwa ni kiasi kidogo pengine chini ya asilimia 100 kwa hiyo zinakuwa chini pengine asilimia 60 au asilimia 50 jambo ambalo lilikuwa linapunguza pia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali iangalie sasa katika mwaka huu, hii ni awamu mpya na nimeona jinsi ambavyo tayari wamekwisha kuanza kufanya utekelezaji katika miradi mbalimbali kwa mfano kupeleka elimu bure kule wanapeleka zile fedha kila mwezi vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe basi hata katika bajeti ya mwaka huu tumetenga asilimia 40 ya bajeti iende kwenye shughuli za maendeleo. Serikali ihakikishe inatekeleza suala hili, hata mwisho wa mwaka tutaweza kuona jinsi ambavyo miradi mbalimbali ya maendeleo imetekelvezeka kule vijijini kwa sababu Serikali imeweza kutekeleza wajibu wake hasa Wizara ya Fedha ambayo inahitajika kuweza kufanya utaratibu huu vizuri zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona jinsi ambavyo kuna mifano ya baadhi ya nchi ambao bajeti ya maendeleo ni zaidi ya asilimia 50, kwa mfano tu hata wenzetu hapa Kenya bajeti ya maendeleo inakuwa ni zaidi ya asilimia 50 na bajeti kubwa wanategemea mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuishauri Serikali pia iangalie namna bora kwamba tuimarishe ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuwezesha angalau asilimia 50 ya fedha za ndani ziwe zinapelekwa kwa ajili ya maendeleo

ya wananchi. Tunashuhudia kabisa kwamba fedha nyingi za makusanyo zinatumika kwa ajili ya kulipa mishahara tu na gherama aina mbalimbali. Lakini kumbe Serikali iangalie utaratibu mzuri angalau yale makusanyo tukiweza yani angalau zaidi ya asilimia 50 zikaenda kwenye maendeleo, wananchi wetu wataweza kunufaika zaidi hasa walioko vijijini ambao wanazo changamoto nyingi sana katika huduma za jamii kwa mfano afya, elimu na masuala mbalimbali. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na changamoto hizi niungane tu pamoja na Kamati ambazo zimewasilisha hoja hii kuona kwamba Serikali lazima katika masuala haya yote iangalie namna ya kuyatafutia ufumbuzi ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali ambazo Mungu ametujalia katika Taifa letu la Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashahidi nchi ya Tanzania tumejaliwa kuwa na rasilimali mbalimbali, madini pamoja na mazingira mazuri ambapo yanaruhusu watalii kuja katika nchi hii. Kusema ukweli tukijipanga katika ukusanyaji wa kodi tayari imekwisha kuanza taunaona *impact* tayari tunaona jinsi ambavyo Serikali inakusanya kodi vizuri kabisa naunga mkono kabisa ukusanyaji wa kodi na niendelee kusitiza kabisa kwamba tujipange zaidi kwa sababu badi kuna watu pia ambao wanaendelea kukwepa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue fursa hii kuiomba Serikali iendelee kuongeza ili makusanyo yawe makubwa zaidi kwa sababu kulingana na rasilimali ambazo Mungu ametujalia katika nchi yetu ya Tanzania. Kupitia mapato hayo nina uhakika nchi yetu sasa tutaweza kupata manufaa makubwa hasa katika wananchi wetu ambao tunahitaji kupeleka huduma kwa wananchi ili wananchi waweze kunufaika na huduma hizi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walio wengi vijijini wana changamoto kubwa ya maisha yao. Vilevile tunashukuru kwa ajili ya TASAF ambayo imeanza kupeleka huduma kwa wananchi. Lakini niombe sasa pia kupitia TASAF tuangalie wale wahitaji kabisa, kwa mfano, wanawake walio wengi vijijini ambao wanalea watoto yatima lakini vilevile wana maisha magumu, kwa hiyo, tuangalie pia hizi fedha zinapokwenda za TASAF tuangalie kweli wale wenye uhitaji hasa walioko katika mazingira magumu zaidi vijijini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nitumie sasa fursa hii kushukuru sana na kuomba Serikali iweze kuyazingatia yale ambayo Kamati imeweza kuyasemea ili kwamba basi wakishayafanya kazi ninauhakika kwamba suala la maendeleo katika Taifa letu yataweza kuonekana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bukwimba. Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi leo kuchangia katika taarifa hii ambayo imewasilishwa na Kamati ya LAAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende ku-declare *interest* ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC. hivyo basi mambo mengi tumeyaona kupitia ukaguzi ambao tumeanya katika muda ambao tuliokuwa tunashiriki hapa Dodoma na Dar es Salaam. Lakini yako mengi tumeyabaini katika Halmashauri zetu nyingi nchini kama siyo asilimia 100 basi asilimia 99 katika usimamizi hazifanyi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu unaweza ukakuta unapata taarifa ya Halmashauri, lakini ukienda kukagua kwa ndani unakuta wamefanya manunuzi yasiyofuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Wanajifanya utaratibu ambao wenyewe wanaona unafaa sasa mwisho wa siku ukikaa ukagundua ukachimba kwa ndani unakuta tayari wana-*interest* labda na yule mtu ambaye anataka kufanya ile kazi ama na mambo mengineyo ambayo yapo katika Halmashauri husika na miradi ambayo wanakuwa wanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii katika *report* hizi za Halmashauri ambazo tumezikagua na tumeziona, tunagundua kabisa kwamba kutokana na Halmashauri nyingi nchini kupata fedha katika robo ya mwisho au robo ya tatu ya kumaliza mwaka, wanapata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hali ambayo inapelekea hata wao wenyewe Halmashauri kushindwa kutimiza ama kutokukamilisha ile miradi ambayo wamejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shida hiyo, unaikuta Halmashauri inaingia kwenye mgogoro aidha na wananchi ama inaingia mgogoro na Serikali ama inapokuja kukaguliwa na CAG wanajikuta wapo kwenye matatizo ya kwamba aidha zile fedha walikuwa nazo wameshindwa kuzitumia na baadaye zinakuwa ni bakaa na wakati mwininge zile fedha wanaambiwa wazirudishe Hazina, kwa hiyo, mwisho wa siku ile miradi iliyokuwepo iliyotengewa zile fedha miradi haifanyiki kwa wakati na zile fedha zimerudi Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hali hii kwa utaratibu huu tukiendelea nao kwa namna moja ama nyingine miradi mingi sana itakwama kwa sababu nachukulia mfano hata pale katika Wilaya yetu ya Igunga katika Jimbo la Manonga, yako majengo ambayo wananchi wametoa fedha zao za kuanzisha mfano ujenzi wa zahanati, ujenzi wa nyumba za walimu, ujenzi wa madarasa ya shule, maabarara lakini unakuta support wanayotakiwa wapate kutoka kwenye

Halmashauri, Halmashauri inaweza ikaandika fedha kuomba kwa ajili ya kumalizia, zile fedha hawapati kwa wakati mwisho wa siku wananchi wanalamika na sisi Wabunge tukija Bungeni tunalamika, hali hii inapelekea miradi mingi kukwama na Serikali inapokuja mwaka mwingine wa fedha tunakuja tunaanzisha miradi mipya na tunaenda kuwaambia tena wananchi waanze kuchangia wakati miradi mingine hajifika mwisho, tunaanza kuwaambia wananchi waanze kuchanga tena. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukianza kumwambia mwananchi achange nyumba ya mwalimu wakati anaona maabara ile pale hajifika mwisho anaanza kukwambia mfano, mbona maabara ile hajjamaliwa na Serikali ilituambia tuchange fedha ili zile fedha wenyewe watamalizia hajjamalizia, leo tujenge nyumba za walimu. Kwa hiyo, hii inaleta mgongano wa kimaslahi kati ya Halmashauri na wananchi lakini pia Halmashauri na Serikali kuu na wakati mwingine hii miradi ambayo inakuwa inaanza haifiki mwisho hivyo basi niiombe sasa na kuishauri Serikali katika suala zima la upelekaji wa fedha, fedha hizi ziende mapema na haraka zaidi ili kuweza kuonyesha kwamba miradi tuliyokuwa tumeipanga katika Halmashauri inatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tumbaini, Halmashauri nyingi zinakusanya fedha kiholela tu hawatumii *EFD machine*. Kwa hiyo, kutokana na kutokutumia hizi mashine za *EFD* inapelekea kukosa mapato makubwa zaidi. Kwa hiyo, niishauri Wizara husika itoe maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kwamba watumie *EFD machine* katika kukusanya mapato yao ya ndani, hiyo yote mpaka katika minada sijui mambo yote wanayofanya vijijini kule. Hii itatupelekea kuongeza mapato yetu katika Halmashauri, lakini itaongeza mapato katika Serikali kuu tukiacha kutumia *EFD machine*, mapato mengi yatapotea. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuombe sasa Wizara ilichukulie hili na itoe maelekezo na isiwe ombi kwamba toeni maelekezo muda fulani kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini mpaka kufikia muda fulani sehemu zote za mapato yenu mtumie *EFD machine*. Hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba Halmashauri zinakuwa na hela, Serikali inakuwa na hela, lakini hata ile miradi tuliyokuwa tumeipangia inaweza kutimizwa kwa wakati. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nipende kuishauri Serikali. Serikali kuu imetenga fedha mwaka huu asilimia 40 za fedha ziende katika miradi ya maendeleo. Sasa hizi fedha zitakwenda ndiyo lakini huku chini usimamizi wake kama ambavyo tumezungumza, wakati mwingine usimamizi mbovu sasa lazima kuwepo na chombo imara ambacho kitakuwa kinasimamia na kufuatialia na chombo hicho ni chombo ambacho tumekiweka wenyewe kisheria ambayo ni

Ofisi ya CAG na kupitia Kamati zetu za LAAC na PAC. Hizi Kamati ndizo jicho la Serikali, lakini ndiyo jicho la Bunge, ndiyo jicho la wananchi kuhakikisha kwamba zile fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu zinafanyakazi lazima ukaguzi uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zikienda na Ofisi ya CAG ikaenda kukagua, Kamati zikaenda kujiridhisha kuangalia maana yake hata tutakaporudisha Serikalini taarifa maana yake Serikali ichukue taarifa yetu sasa ianze kuifanya kazi kwamba sehemu fulani wamefanya madudu, sehemu fulani wamefanya madudu. Sasa zinapokosa Kamati hizi fedha kwa ajili ya kufanya shughuli hii ya ukaguzi ama Ofisi ya CAG inapokosa fedha maana yake hata tukipeleka mabilioni ya shilingi kama hamna anayefuatilia maana yake na yenyewe yatapotea, mwisho wa siku maana yake hata yale malengo tuliyokuwa tumejiwekea tutafika 2020 yale malengo yatakuwa hatujayafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niiombe sana Serikali ihakikishe inawezesha Ofisi ya CAG ipate fedha za kutosha za kukagua. Pia Kamati za PAC na LAAC zipate fedha kwa ajili ya kutembelea miradi, hii itaisadia Serikali ya Magufuli kufikia malengo yake iliyojiwekea kufikia mwaka 2020 kwa sababu itakuwa inajua wapi Halmashauri gani imeharibu, taasisi gani imeharibu na hapo hapo inachukua hatua kuhakikisha kwamba zile fedha wanazozitoa zinafanyiwa kazi ili isiwe kwamba vile maana yake Ofisi ya CAG fedha ilizotengewa ni ndogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha ikiwa ndogo Halmashauri mwaka huu Ofisi ya CAG inafikiria kwamba inaweza isikague hata Manispaa kumi. Sasa kama itashindwa, maana yake taarifa ya mwakani tutakuwa hatuna hapa na kama Ofisi ya CAG ikikosa kufanyakazi maana yake Kamati hizi za PAC, Kamati ya LAAC itakuwa haina cha kufanya, kwa hiyo, mwisho wa siku niishauri Serikali kwamba hizi ofisi zipewe fedha mapema na waharakishe na washirikiane nao bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunafanyakazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa nataka tu kuishauri Serikali hasa kupitia Wizara husika ya TAMISEMI wafuatilie sana hizi Halmashauri. Kuna hizi asilimia kumi ambazo wenzangu wamezungumza za vijana na akina mama. Hizi fedha ni muhimu sana Halmashauri ikatoa, ziko Halmashauri naona zinafanya vizuri, zinatoa fedha kwa ajili ya kutoa kwa vijana na makundi mbalimbali ya kina mama. Hizi fedha zikitoka kwa mfano, kwenye Halmashauri mapato yetu yawe shilingi bilioni mbili maana yake fedha makundi haya iko zaidi ya milioni 200. Milioni 200 ukazichukua milioni 100 ukapeleka vijana, milioni 100 ukapeleka kwa akina mama, hizi fedha zikaenda kwenye makundi haya na kwenye kata husika maana yake mwisho wa siku...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana muda wangu umekwisha napenda kuunga mkono hoja, ahsante. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba, tutamalizia na Mheshimiwa Manase Oran Njeza kwa upande wa CCM.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye taarifa za Kamati ya PAC na LAAC. Nianze kwanza kuishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali ambayo imekuwa ikizichukua ili kuweza kupunguza yale mapungufu mengi ambayo yalikuwepo kipindi cha nyuma. Tumeshuhudia kumekuwa na *reforms* mbalimbali hususani *financial management reforms* zenyе lengo la kuleta udhibiti wa matumizi ya Serikali, lakini pia kuondoa mapungufu mengi ambayo yamekuwa yakijitokeza siku za nyuma. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kumpongeza CAG na wafanyakazi walioko chini ya Ofisi ya CAG kwa sababu taarifa hizi ambazo tumeletewa ni matokeo ya kazi nzuri ya CAG ambayo ameifanya. Wachangiaji wengi wamekuwa wakizungumza juu ya mapungufu yaliyokuwepo, kikubwa yanababishwa na ule udhibiti wa ndani, lakini kama nilivyosema kwamba Serikali imeanzisha pia Ofisi ya *Internal Auditor General* kwa nia hiyo ya kuleta udhibiti madhubuti kwenye taasisi zetu na mashirika yetu na hasa hata kwenye Serikali zetu za Mitaa. Kwa hiyo, naona Serikali imekuwa ikifanya juhudini kubwa na naamini kwamba kadri tutakavyokwenda mambo yataendelea kuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya ukaguzi ni kututhibitishia kwamba rasilimali za umma, zile asset za umma ziko katika hali nzuri, lakini pia tunapata ushauri kutohana na ukaguzi na matokeo yake ndiyo kama hivi kwamba Kamati zetu zimepata *input* ya kuweza sasa kuliletea mapendekezo Bunge ninaunga mkono mapendekezo yote ambayo yapo kwenye Kamati. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite zaidi kwenye mashirika ya umma. Niko kwenye Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Nilitaka nizungumze machache kuhusu ufanisi ambao utatekeleza saa nyingine haya mashirika ya umma kuweza kupunguza matatizo yaliyokuwepo lakini pia kuweza kuongeza mapato, *non-tax revenue* katika Serikali. Kwa sababu ukiangalia bado ule mchango ambao unakwenda kwenye Serikali kwenye mapato bado uko mdogo, ukiangalia kwenye bajeti ya 2016/2017, mchango huu ambao ni *non-tax revenue* ukijumlisha pamoja na Halmashuri uko asilimia 11.3; lakini ukiona kwenye mwaka huu ambao tunakwenda kuzungumzia kipindi kijacho projection iko asilimia 12.35. Kwa hiyo, bado mchango uko mdogo kwa hiyo,

ninaamini kwamba kuna mambo mengi yakishughulikiwa hasa hasa kuboresha mashirika yetu, mchango utakuwa mkubwa katika Pato lile la Taifa.

Mhesimiwa Naibu Spika, nizungumze mambo mawili, jambo la kwanza nilitaka niseme kuhusu kuwezesha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Utakuja kuona kwamba Msajili wa Hazina amekuwa akifanyakazi kubwa kwa upande wa Mashirika ya Umma lakini pia kwenye upande wa PAC naamini kwamba amekuwa kitoa mchango wao kuwezeha kazi za Kamati kufanyika vizuri. Lakini bado liko jambo la kumwezesha huyu Msajili ili aweze kupata uwezo mkubwa wa kufanyakazi na kuweza kusimamia mashirika haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba kazi ya kwake ya kushauri mashirika juu ya uanzishwaji na hata saa nyingine kufutwa baadhi ya mashirika ambayo hayana ufanisi lakini liko jambo pia la kuangalia ule utendaji wenye tija katika mashirika. Kupitia mipango na bajeti za mashirika na hata jana umeshudia tumepitisha mabadiliko ya sheria kwa nia ya maana kusaidia katika mashirika haya ili kuwa na uwiano ule wa matumizi na mapato yanayotoka kwenye mashirika haya hii itaiwezesha Serikali kuweza kupata gawiyo au fedha kutoka kwenye mashirika yetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini anayo majukumu mengi, hii ni pamoja na kuweka viwango vya mashirika yetu kuweza kufanya makusanyo, lakini pia kuweza kuzisimamia hizi Bodi za Mashirika, kusimamia *management* na Kamati zake. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria nipayenda tu kwamba Serikali iitazame hii ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kusaidia kuleta tija na kupunguza mambo ambayo yamejitokeza katika mashirika yetu ambayo yana changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika mashirika yetu ukiingalia sura ya mitaji iliyoko kwenye mashirika yaliyo mengi sura yake siyo nzuri inahitajika ifanyike uchambuzi wa makusudi wa nguvu na kushauri ili tuweze kuona zile *capital structure* kwenye mashirika yetu zinakuwa ni nzuri lakini kunahitaji pia kuweza kuona kwamba kuna mambo ambayo yameonekana kwenye report hii kwamba kuna madeni mengi kwa mashirika ambayo yanakusanya mapato yameshindwa kukusanya mapato vizuri, ipia utakuja kuona kwenye mizania kuna matatizo kwamba kuna rasilimali au asset za mashirika haya hazijafanyiwa evaluation muda mrefu, utaona matatizo yako mengi, iko ile mikakati ya kuweza kudhibiti vihatarishi (*risk management*) katika haya mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria niliseme hili kwamba Serikali iangalie sana hii ofisi. Ofisi inayo majukumu mengi na kama itawezeshwa kwa maana ya kuweza kuhakikisha kwamba wamekuwa na rasilimali za kutosha ili kuweza kushughulikia mashirika haya, tutaona kwamba tutaweza kuongeza ufanisi katika haya mashirika ambayo yapo kwa sababu ukija

kuangalia mashirika yaliyo mengi hawana *investment plan*, mashirika yaliyo mengi utaona hakuna *risk strategy* za kuweza kuondosha hatari ambazo zinafanya mashirika haya yasiwe na ufanisi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya yote haya Msajili wa Hazina anatakiwa kuyatazama na kwa kasi kubwa ili tuweze kuondokana na hayo matatizo ambayo yapo. Utakuja kuona hata kuna taasisi zingine za kifedha ziko chini ya Msajili wa Hazina na zenyewe zimekumbwa na matatizo haya ya kutokupata faida. Kuna mikopo chechefu, lakini pia ule uwekezaji lazima usimamiwe vizuri ili tuone kwamba mashirika haya yanaweza kufanya vizuri. Kumekuwana pia kutokuwa na record nzuri kwenye hesabu, kuna over statement za asset au under statement kwa hiyo haya mambo hayo ni muhimu sana yaweze kutazamwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *internal control*, udhibiti wa ndani ni muhimu sana kutazama katika maeneo yote ili tuweze kupunguza hizi hoja lakini kikubwa tuweze kuwa na ufanisi mzuri katika kusimamia hizi rasilimali. Kwa hiyo, nilitaka nishauri tu kwamba jambo la kwanza Serikali isisitize sana kuhakikisha kwamba kunakuwa na Kamati za Ukaguzi ambazo zinatakiwa ziimarishwe, ziwe na watu wenyewe weledi lakini kama itawezekana pia kwenye mabadiliko ya sheria zetu tuzitazame ili Wajumbe wa Kamati hizi za Ukaguzi waweze kutoka nje ya taasisi husika ili ule ushauri uweze kusaidia kuboresha mashirika yetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la llingine; wakaguzi wa ndani utakuja kuangalia hata katika Halmashauri zetu wakaguzi wa ndani ni wachache. Unakuta wakati mwingine wakipata fursa ya kwenda kwenye mafunzo ofisi zinafungwa zina wakaguzi wawili, zina wakaguzi watatu na hawa wakaguzi wa ndani ni jicho kwenye *management* iweze kusaidia kurekebisha mambo mapema kabla mambo hayajaharibika.

Kwa hiyo, ni muhimu Serikali itazame, imuwezeshe Mkaguzi mkuu wa ndani lakini pia wakaguzi wa ndani walioko kwenye taasisi zetu waweze kupata mafunzo lakini pia waweze kuongezwa ili waweze kutusaidia. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kuangalia pia kuwezesha mashirika yetu yana upungufu wa fedha, Serikali kama inaweza kwa sababu imekuwa ikiongeza makusanyo tuanzishe huu mfuko wa uwekezaji ili uweze kusaidia mashirika na taasisi ambazo ziko chini ya TR ili ziweze kuweza kupata fedha kutoka kwenye mfuko huu. Tuyaimarishe haya mashirika ili mwisho wa siku yaweze kuongeza gawiwo upande wa Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kilio changu kikubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Ofisi ya TR inawezeshwa ili ikiungana na taasisi nyingine zinazoshughulikia masuala ya uadilifu, masuala

haya ya tija, ziweze kufanya vizuri ili mwisho wa siku hoja zipungue lakini kikubwa ziweze kuchangia kwenye maendeleo ya Taifa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tutaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Manase Oran Njeza. Tutaelekea upande wa CHADEMA, Mheshimiwa David Ernest Silinde muda wake anagawana na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyokuwa mbele yetu. La kwanza nijielekeze kwenye ukurasa wa 76 wa kitabu cha PAC. Kwanza nitangaze interest kuwa mimi ni Mjumbe wa PAC hasa kuhusu suala la muamala uliokwama wa shilingi bilioni 100 TAMISEMI. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa sababu ni suala mtambuka, TAMISEMI kama tunavyofahamu ni Wizara mama na inayobeba Halmashauri zetu. Tumewasikiliza Wajumbe waliotangulia wengi tulikuwa tunalalamika pesa haziji kwenye Halmashauri yetu kwa wakati, na tulikuwa tunatafuta mchawi ni nani? Katika hili ni vizuri Serikali ikachukua hatua stahiki kujua liko nini hapo Hazina, kwamba imetoa exchequer ya shilingi milioni 287 kwenda TAMISEMI, halafu wanarudisha nyuma shilingi bilioni 100 bila taarifa ya TAMISEMI wenyewe. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI wanaandika cheque kuwalipa wateja wao wanakwenda benki wanakuta hewa, na hili sio jambo dogo. Katika Bajeti ile ambayo ilikuwa ya shilingi milioni 287 ambayo pesa zilizoletwa hizi ni sawasawa na asilimia 47, maana yake nini? Kama asilimia 47 pesa hazikuja TAMISEMI ukizingatia hata bajeti yetu mpya ya maendeleo ni asilimia 40 hii mpya, hiyo ya zamani ilikuwa chini ya hapo. Ndiyo maana kumbe tunalalamika kwenye Halmashauri zetu pesa haziji tatizo liko huku huku kwa watoa fedha wenyewe. (Makof)

Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano, tuko pamoja kama alivyosema Mheshimiwa Rais alipokuja hapa Bunge tumsaidie na sisi Wabunge tuko tayari kumsaidia katika vita vyake vyaka kifisadi ili kuangalia hizi shilingi bilioni 100 ziko wapi. Kwa sababu bila kuchukua hatua stahiki mchezo huu utaendelea na hali itakuwa kama hivi, kila siku tutagombana, miradi haiendi, pesa haziji baadaye tunaweza kuweka rehani utekelezaji wetu wa llani ya Chama cha Mapinduzi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu NFRA kupata hasara ya shilingi bilioni 6.7. Hasara hii ni kubwa sana. Nakubaliana na sababu zilizotolewa na Kamati lakini kubwa ni kuchanganya biashara na siasa. Kuna watu wamesimamishwa, lakini binafsi nasema wamesimamishwa kiuonevu kwa sababu sio makosa yao. Ilipitishwa hapa kwamba uwezo wa NFRA kuhifadhi ni tani 140,000 kwa ma-godown yao yote, lakini baada ya NFRA kununua mahindi haya viongozi hawa hawa wa juu na sisi viongozi wa kisasa kila mtu anataka mahindi yake yanunuliwe katika eneo lake na kutoa maagizo kwa viongozi wa NFRA wanunue bila kuzingatia uwezo wa kuhifadhi waliokuwa nao.

Leo mahindi yameharibika, tunawatoa kama mbuzi wa kafara wakati kimsingi siyo waliosababisha tatizo hili. Kwa sababu wasingetekeleza maagizo ya wakubwa wao waliyokuwa wanaambiwa kwamba lazima mahindi ya wakulima yanunuliwe bado wangetambuliwa tatizo lingekuwa liko pale pale. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hili naomba Serikali ifanye uchunguzi hasa na kila mtu apate haki yake stahiki kwa sababu uwezo wa kuhifadhi ni tani 140,000 unamuambia mtu anunue tani zaidi ya 200,000, ataziweka wapi? Lazima aziweke nje na akiziweka nje mvua zikija lazima yaharibike. Sasa yakiharibika unakuja kumuadhibu wakati wewe ndiyo uliyemuelekeza kwamba anunue na hela umempelekea. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nataka tu nilizungumze vizuri sana, Serikali siyo mnunuzi wa mahindi. Tunapowazuia wakulima wasiuze mahindi yao nje wakati tunajua uwezo wa kuzalisha mahindi Tanzania ni zaidi ya tani milioni tatu na uwezo wa Serikali kununua ni mdogo, kwenye bajeti mwaka huu tumetenga kununua tani 100,000, wewe utajihesabu ni mnunuzi? Matokeo yake wakulima wanaacha kuuza mahindi yao sehemu zenye wateja baadaye yanakosa soko, kipato cha wakulima kinaenda chini na kudhoofisha uchumi wa wakulima wetu. Kwa hiyo, naomba sana hata mwaka huu mnapokuja tena kununua hifadhi ya chakula tusije kuwazuia wakulima kuuza mahindi yao kwa wateja wengine kwa kusema Serikali itakuja wakati tunajua uwezo huo wa kununua mahindi yote ya wakulima wetu hatuna. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, niungane na maoni ya Kamati yangu hasa kuhusu suala la NSSF kwa sababu huu ni mfuko muhimu sana, ni mfuko wa wapigakura wetu, wastaafu wako huko, ni vizuri Bunge hili likaridhia Kamati hiyo ikaenda kujiridhisha na hali halisi iliyokuwepo huko NSSF. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa hatua stahiki ilizochukua kukabiliana na matatizo na changamoto zilizokuwepo ndani ya NSSF. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe angalizo sana hasa kwenye ule Mradi wa Dege kwa sababu ile ardhi mpaka leo bado ni ya Azimio kwa mujibu wa *title*, lakini pia kuna mkataba ambao NSSF umeingia na mbia wake. Kwa hiyo, suala hili siyo la kukurupuka, ni vizuri kujipa muda wa kutosha kuangalia kwa kina na kujiridhisha mikataba inasemaje ili siku za usoni tusije kuingia kwenye matatizo makubwa zaidi ikiwa tutakurupuka. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wote wanaotuhumiwa bado ni watuhumiwa tu, tusije kuwahukumu kama wakosaji wakati chombo cha kuhukumu ni mahakama. Wote tujipe subira kama Kamati yangu ilivyosema, twende huko tujiridhishe, iletwe taarifa ambayo imekamilika. Kwa sababu jambo hili bado liko kwenye uchunguzi tuviachie vyombo vingine vya uchunguzi viendeee kufanya kazi yake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka kusema kwamba tumefanya kazi yetu katika mazingira ya kutegemea paper work na maelezo tu kutoka kwa *management* na Bodi tulizokutana nazo, lakini kiuhalisia PAC tumeshindwa kwenda kutembelea mradi wowote. Kama unavyofahamu siku hizi kuna watumishi hewa, wanafunzi hewa, tunaamini pia kuna miradi hewa. Kwa hiyo, ombi langu kwako kwa sababu tunakwenda kwenye mchakato wa bajeti ni vizuri bajeti ya Bunge ikaongezwa ili na bajeti ya PAC na LAAC zikaongezwa kuziwezesha kutembelea hii miradi tusije kuuziwa mbuzi kwenye gunia kwa sababu tunaweza kusema mradi fulani upo kumbe haupo. Ni vizuri tukatembelea miradi na mashirika hayo kwenda kujiridhisha zaidi. Pia tupate nafasi ya kutembelea hata makampuni au mashirika mingine ya umma yanayofanana na mifuko hii kwenda kujiridhisha kwa sababu mashirika mengi yanafanya mambo kama hayo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho niombe Serikali ifuatilie hii mifuko. Kwa mfano, NSSF wenyewe kama tunavyofahamu wana majengo mengi lakini cha ajabu majengo yao hawakai, wenyewe wanapanga, ni kitu cha ajabu kabisa. Wana majengo mazuri kwa nini wasikae kwenye majengo yao kuokoa fedha? Kwa hiyo, niishauri Serikali iwape mwongozo kwa sababu hivi vyombo vinasimamiwa na Benki Kuu na Mdhibiti wa Mifuko wawashauri NSSF na mifuko mingine yote warudi kwenye nyumba zao walizojenga wakae huko kuliko tafsiri ya sasa hivi inavyoonekana kwamba wanalazimika kwenda kupanga kwa sababu labda ya 10%. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye miradi ya uwekezaji, mifuko mingi kwa ujumla inawekeza....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Manase Oran Njeza atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Pauline Philip Gekul ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama walivyosema watangulizi wangu, nianze kwanza kwa kuzipongeza hizi Kamati mbili za PAC na LAAC kwa kazi nzuri walizofanya na ripoti zao ni nzuri sana na pia recommendation zao nazo ni nzuri sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianzie pale alipoishia msemajii wa mwisho. Ukiangalia masuala yote haya inaonekana udhibiti wa haya mashirika yetu na hata taasisi zetu kuna mahali pana legalega. Ukijaribu kuangalia kwa mfano mdogo tu kwa ripoti kama ya NSSF achilia mbali hiyo ya Mradi wa Dege lakini wamekopisha mikopo kwa SACCOS mabilioni mengi na wao sio benki, hawana utaalam wa taasisi za kibenki. Kawaida ya SACCOS unategemea kwamba hawa wanafanya *savings and credit* unakuta SACCOS ndiyo zinaanza kukopa, ni kitu cha hatari sana katika uchumi wa nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tungetegemea SACCOS zikusanye *savings* huko na zikopeshe wale members wao. Sasa unakuta shirika kama NSSF ambapo siyo kazi yake inakwenda kukopesha SACCOS na hizo SACCOS kama ripoti inavyosema zingine ni hewa, zaidi ya shilingi bilioni 70 imetolewa kama ilivyoeliza kwenye ripoti humu. Hizo pesa zote ni za umma na zimekwenda sehemu ambayo siyo. Kama ripoti ya PAC ilivyoeliza ufanyike uchunguzi kuangalia namna hiyo mikopo ilivyotolewa na ilikwenda kwa nani na kwa jinsi gani. Sidhani kama wana kitengo maalum kwa ajili ya kukopesha na sidhani kama wana software ya kibenki ambayo inaweza kufanya tracking ya mikopo hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la usimamizi wa mashirika yetu. Kuna mifano imetolewa ya EWURA na SUMATRA kuwa yale makusanyo yao yote wameyatutia katika matumizi ya mishahara na matumizi ya kawaida. Ukiangalia EWURA wametumia zaidi ya 71% na SUMATRA wametumia 82% ya pesa walizokusanya. Sasa unajaribu kuangalia hawa SUMATRA na EWURA ni vyanzo vya mapato ya Serikali, badala ya kutumia hizo pesa kutunisha Mfuko wa Hazina wenyewe wamezitumia kwa matumizi ya kama kujilipa mishahara, posho na matumizi mengine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na PAC kushauri kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina iweze kuimarishwa ili iweze kuyasimamia mashirika haya kwa ukaribu zaidi. La sivyo tutaendelea kutegemea tax revenue na tukaacha hili

eneo ambalo Serikali yetu kama ikilisimamia vizuri litaondoa kabisa kutegemea kodi ambazo zinaongezeka kila siku. Tukisimamia hizi *investments*, haya mashirika tuna uwezo hata wa kupunguza kodi kwa wafanyabiashara wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wenzangu waliongelea kuhusu *Internal Auditor* (Mkaguzi wa Ndani). Nafikiri huu mfumo uliopo sasa hivi kwa Wakaguzi wa Ndani kwenye Halmashauri zetu kuwa chini ya Wakurugenzi siyo sahihi. *Internal Auditor* kama alivyo *External Auditor* wanatakiwa wawe na uhuru wa aina fulani kwa watu wanaowakagua. Sitegemei *Internal Auditor* anayeripoti kwa Mkurugenzi amkague Mkurugenzi atatoa ripoti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikawaida hata *code of ethics* za *Internal Auditors* zinasema *Internal Auditor* awe *independent* anatakiwa aripoti kwa mtu ambaye ni tofauti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nilivyokuwa naangalia governance za hizi Halmashauri zetu nafikiri kuna vitengo ambavyo vinahitaji kuimarishwa kama Audit Committee na Risk Committee. Ukiangalia composition za hivi vitengo nafikiri haziko sawasawa. Kama tungekuwa na *Internal Audit Committee* na *Risk Committee* ambazo zinajitegemea tungeweza vilevile tukaagiza hawa *Internal Auditor* waripoti kwenye hizi committee ambazo ziko nje ya utawala wa DED. Mimi naona kwa vile kuna Director of *Internal Audit* ambaye yuko chini ya Wizara ya Fedha labda angejaribu kuwa karibu zaidi kuwaangalia na kuwasimamia hawa *Internal Auditors* ili waweze kulinda maslahi ya pesa zetu na kusiwe na ufujaji mkubwa wa hizi pesa zetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa David Ernest Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa sababu muda tunagawana, niende moja kwa moja kwenye ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti mbili zimeandikwa vizuri sana na kwa ufasaha na Kamati husika. Hata hivyo, kuna mambo ambayo kwa ujumla tunahitaji sisi kama Bunge kuya-adopt na mengine kutoa ushauri kama Azimio la Bunge kwa Serikali juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mambo mengine katika Halmashauri na taasisi zetu huko mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo yanakwamisha miradi mingi sana katika ngazi za Halmashauri kutokukamilika. Jambo la kwanza ni maagizo ya mara kwa mara yanayotoka kwa viongozi wa juu bila kuwekwa katika bajeti za Halmashauri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa katika Halmashauri zetu kumekuwa na maagizo ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa yaani Mkuu wa Wilaya anaweza kuja katika Halmashauri akatoa agizo ambalo halipo katika bajeti za Halmashauri. Matokeo yake maagizo hayo yamekuwa yakisababisha kuwepo na *reallocation*. Haya ni matumizi mabovu ya fedha kwani fedha ambazo ziliwuwa zimepangwa kufanya kazi nyingine zinaenda kufanya kazi nyingine na matokeo yake anapokuja mkaguzi wa fedha zinaonekana fedha za Halmashauri zimetumika kinyume na vile ambavyo ziliwuwa zimepangiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nilikuwa nashauri ni lazima liingie kama moja ya pendelezo na watu wa Serikali za Mitaa pamoja na taasisi nyingine wajaribu kulichukua na sisi kama Bunge ni lazima sasa tuiambie Serikali, Wakuu wa Wilaya wajue mipaka yao ya kazi, Wakuu wa Mikoa lazima wajue mipaka yao ya kazi na wala siyo kupanga miradi ya maendeleo katika Halmashauri. *Infact* hata kwa ninyi viongozi wa juu kabisa wakiwemo Mawaziri na Mheshimiwa Rais, tuwashauri vizuri tu kwamba wanapotoa maagizo, kwa mfano unasema tunakwenda kwenye *operation* ya madawati, ni jambo jema lakini tuseme hiyo *operation* ya madawati ianze katika mwaka wa fedha ujao siyo katika mwaka wa fedha husika kwa sababu inatuvuruga kabisa katika ngazi ya Halmashauri. Kwa hiyo, hilo naomba tupeleke kama moja ya pendelezo letu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, moja ya jambo ambalo linakwamisha sana utendaji kazi huku chini katika Halmashauri zetu, huu mfumo wa uteuzi sasa hivi umekuwa ni mbovu sana. Nalisema hili kwa sababu moja, nimeshuhudia mwaka huu tumekuwa na idadi kubwa sana ya Wakurugenzi ambao hawakupitia katika utumishi wa umma. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yamekuwa yakisemwa na hili ni vizuri tukalisema vizuri. Watu wetu kule chini wanaanza kazi katika Serikali za Mitaa kwa mfano wanaanza *with an intention*, anaanza kama Afisa Msaidizi Daraja la II, baadaye anapandishwa Daraja la I, baadaye anakuwa Afisa Mwandamizi, siku inayofuatia anakuwa Mkuu wa Idara, *with an intention* siku moja nitakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya fulani ama nitapandishwa na nitakuwa RAS. Huu mwenendo wa sasa hivi ambapo watu wamekuwa wakitolewa *from no where*, mtu alikuwa tu mgombea wa Chama cha Mapinduzi anateuliwa moja kwa moja kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri, imeondoa ile morale na motisha kwa wafanyakazi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii niwaambie kabisa ni moja ya jambo ambao Chama cha Mapinduzi ni lazima mijirekebishe kwenye hili, limeondoa motisha kabisa kule chini. Watu wanalamika na wanunung'unika sana kwamba yaani sisi huku tuliko tumetumikia zaidi ya miaka 30, 20, 18 nategemea siku moja nitapandishwa cheo kumbe pamoja na utumishi wangu wote uliotukuka katika Serikali za Mitaa lakini leo thamani yangu haionekani. Matokeo yake anakuja mtu from no where na mtu yule ambaye humjui uwezo wake wala utendaji wake wa kazi, ile imeondoa sana morale, hata sasa hivi morale imeshuka sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima hili lieleweke kabisa kwamba kwenye masuala ya uteuzi yabaki kama Sheria ya Utumishi inavyosema, lazima mtu atumikie kwa kiwango fulani na akifikia labda miaka saba huyu anaweza kuwa qualified kuwa Mkurugenzi Mtendaji ama kuwa DAS katika Halmashauri husika. Kwa kuendelea na mwenendo huu kitakachotokea ni nini? Wale walioko wanaweza wakawakwamisha hawa wapya ambao wanateuliwa. Wakiwakwamisha hawa wapya wanaoteuliwa zinazoathirika ni Halmashauri na wananchi katika maeneo yetu tunayoongoza. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tunatakiwa kulifanyia kazi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika Serikali zetu za Mitaa moja ya jambo ambalo linakwamisha sana kutokamilika kwa miradi ni Serikali kuchukua vyanzo vya mapato katika ngazi ya Halmashauri. Kwa sekunde mbili ni kwamba tabia ya hii Serikali kujirundikia, sasa hivi tumekuwa tukiona Serikali ikijisifu kuwa na mapato mengi lakini ukweli mapato yako mengi lakini yanatokana na vile vyanzo vya Halmashauri, haijaanzisha vyanzo vyake vipya. Kwa hiyo, tunachotaka waanzishe vyanzo vipya tofauti na kwenda kunyang'anya katika ngazi ya Halmashauri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo dogo la mwisho ni kwamba nimepitia ripoti ya PAC, imeandikwa vizuri lakini watu wa Benki ya TIB walikataa kuleta majina ya wadaiwa sugu ambao wanadaiwa kutokana na kukopa fedha kutoka Benki ya Maendeleo. Matokeo yake ni nini? Kama wameikatalia Kamati ya PAC maana yake wamelikatalia Bunge na hii ni dharau kubwa sana kwenye Bunge lako Tukufu. Hofu hii inatokana na nini? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kwa sababu Mwenyekiti wa sasa wa Bodi hii ni Profesa Palamagamba Kabudi, ni mtu mwenye heshima lakini inapotokea watu wanakataa kuleta majina ya wadaiwa sugu wakati benki ina madeni chechefu ambayo hayalipiki zaidi ya shilingi bilioni 78, kitakachotokea ni kama kilichotokea kwenye Twiga Bancorp. Kwa hiyo, kwa vile hizi benki ni za Serikali na hizi fedha zinatokana na kodi za wananchi, nashauri Kiti chako lazima kichukue hatua dhidi ya taasisi zozote zinazokataa kutekeleza maagizo ya Bunge lako Tukufu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa hayo machache, nafikiri dakika zangu nydingine atamalizia mwingine. Ahsante sana. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, sina taarifa ya Mheshimiwa Mdee ku-share dakika zake lakini baadaye atafuatia Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia ambao wanachangia dakika zao.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Silinde ku-share na mimi dakika chache ili na mimi niweze kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niunge mkono asilimia mia moja hotuba za Kamati zetu zote mbili. Wamezungumza mambo mazuri ya kujenga na naamini Mawaziri wanasikiliza ili wakayafanyie kazi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pale Mheshimiwa Silinde alipoishia kuhusu *TIB* Bank kwamba hawa wadaiwa wanatukwamisha, fedha hizo zisitufikie maeneo mengine. Basi sasa kama Bunge tuazimie kwa nguvu zote kwamba hili litekelezwe na tuwafahamu hawa watu na waweze kulipa hizi fedha ili ziendelee kusaidia maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nilitaka kulizungumzia siku ya leo, ni asilimia tano ya akina mama na vijana. Naungana na maoni ya Kamati kwamba walete marekebisho ya sheria kwa vile ule ni mwongozo umeshashindikana. Nilikuwa kwenye Kamati ya TAMISEMI kipindi kilichopita tulilisimamia hili sana lakini Wakurugenzi hawapeleki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu huo, jambo ambalo nahitaji kuishauri Serikali siku ya leo ni kwamba kwanza ule mwongozo una upungufu. Kwa mfano, wazee wa jinsia ya kiume wao hawapati zile fedha, akina mama wazee wanapata upande wa wanawake na vijana pia wanapata lakini wazee wa jinsia ya kiume (me) hawapati. Nimepita kwenye Jimbo langu na kila nilipopita wazee walilalamika kwamba hawanufaiki kabisa na mfuko huu na wenyewe wanaomba wapate hizo fedha kwa sababu sio wazee wote wenyewe wake na wenyewe watoto. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono mapendekezo ya Kamati kwamba marekebisho yafanyike au ule mwongozo sasa tuuache. TAMISEMI kupitia *miscellaneous amendment* kama ni muswada mzima mtuletee ili na hao wazee wapate fedha hizo tofauti na sasa ambavyo wanahangaika kupata upande wa TASAF wakati TASAF haifiki maeneo yote. Pia mnafahamu TASAF kila baada ya miaka mitatu ndiyo wanabadilisha zile kaya maskini kwa hiyo hawa wazee hawatafikiwa. Kwa hiyo, hili mtuletee na naunga mkono

kabisa mapendekezo ya Kamati ili na wazee wa jinsia ya kiume (me) waingie wapate hizo fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kukazia siku ya leo ni suala la safari za Wakurugenzi. Kwa kweli Wakurugenzi mliotuletea hawakai kwenye Halmashauri zetu, akitoka kwa DC yuko kwa Mkoa wa Mkoa, akitoka kwa Mkuu wa Mkoa yuko kwa RAS. Ametoka kwa RAS anarudi kwa DAS ametoka hapo anaenda kwa OCD, ametoka kwa OCD yuko kwenye safari anasafiri Dar es Salaam au Dodoma, hawakai kabisa kwenye vikao vyetu. Wizara upande wa TAMISEMI muwaandikie basi muwape miongozo kwa sababu hawakai na ndiyo maana baadaye wanapoanza kutumbuliwa wanashangaa kama yale madudu yalifanywa na watu ambao waliwakaimisha wao. Kwa hiyo, niunge mkono maoni ya Wabunge wenzangu ambao jana walizungumza kwamba kuna tatizo kubwa sana kwa Wakurugenzi wetu, muwape mafunzo lakini wakae kwenye vikao vyetu vya Halmashauri waweze kusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuzungumza siku ya leo ni suala la madeni katika Halmashauri zetu. Mlivyotuletea Waraka wa Elimu Bure, kiukweli Serikali hampeleki pesa. Shule ya watoto 300 au 400, mnaapeleka shilingi 200,000, huko huko wanunue mipira kwa ajili ya michezo, huko huko fedha za administration. Niliuliza swali kwa Waziri Mkuu jamani hiki kitu mfanyie review kwa hali ya kawaida shule zetu kuna madeni na Halmasahuri hizi zinadaiwa wakati huo huo mmechukua vyanzo vikubwa vya mapato. Kodi ya ardhi sasa inakusanya kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina hata zile asilimia 30 hamrudishi tena na ndiyo maana juzi nikasema kama ninyi ni waungwana kaeni chini muangalie zile asilimia 30 ambazo mlitakiwa kuzirudisha na mnafahamu zaidi shilingi bilioni 50 hamkuzirudisha, ni shilingi bilioni 4 tu mmerudisha juzi, basi leteni vifaa vya upimaji ardhi katika maeneo yetu kwa sababu huko kwenye Halmashauri zote kwa hali ya kawaida hawana vifaa hivyo.

Mimi niishauri Serikali acheni kuua Halmashauri zetu, kwanza mmepeleka sasa eti bima ya afya wazee tukawalipie kwa fedha gani? Kodi ya majengo mmechukua, TRA mpaka sasa hawakusanyi mnapoteza tu muda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kodi ya majengo ndiyo hiyo tena inakusanya kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Wakati huo kuna madeni, Waraka wa Elimu Bure unataka tulipie madeni ya walinzi, maji katika shule zetu yameshakatwa kwa sababu Halmashauri haina fedha na fedha hampeleki hebu kaeni chini muangalie hizo Halmashauri mnaziweka upande gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nisisitize, kama mnahitaji kujenga hizi Halmashauri mkumbuke mlifanya decentralization kwa sababu wakusanye, walipe na wasimamie. Leo mnapochukua fedha hizo zote, mnatubakisha na ushuru tukimbizane na mama lishe, bodaboda na bajaji, kwa nini? Mtuachie hizo kodi ndiyo zilikuwa zinatusaidia tuendeshe hizo Halmashauri. Muwa-empower hao Wakurugenzi na Madiwani wetu wasimamie hizo fedha muone kama kazi hazitoenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho jamani leteni pesa za maendeleo, hakuna fedha kabisa. Halafu mnategemea hizo barabara tutachonga na nini? Pia kwenye *miscellaneous* mnazotuletea kila siku mtuletee ile ya TANROADS asilimia 70 tuiondoe, asilimia 30 ziende kwenye Halmashauri zetu kuchonga hizo barabara haiwezekani. Nilisema kwenye Bunge hili kwamba TANROADS watusaidie kwenye zile asilimia 70 ili tuchonge hizo barabara lakini ile ni wao wenyewe wapende au wasipende. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani la Jiji. Kwa hiyo, baada ya kuona suala la UDA limeingizwa hapa na mambo yanayohusiana na Jiji yanatajwa ninawajibika kuzungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka niweke rekodi sawa. Jana kuna mtu mmoja alikuwa anazungumza hapa, zamani tulikuwa tunawaita manjuka lakini siku hizi sijui tutawaita jina gani, wakasema kwamba hoja ya kutaka Jiji livunjwe ni kwa sababu ya kashfa ya Kiwanda cha Nyama, lakini anasahau kwamba kashfa hii ya Kiwanda cha Nyama ilitokea wakati Jiji likiwa chini ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Kashfa hii ya UDA tunayozungumza leo imetokea wakati Jiji likiwa chini ya Chama cha Mapinduzi. Wakati sasa Jiji liko chini ya UKAWA tunataka tulisafise ili Halmashauri zile zilizokuwa tatu na sasa hivi zimeongezeka tano ziwe sehemu ya kuboresha lile Jiji. Hawa wezi wanaotajwa kwenye ukurasa wa 31 na 32 wa hii Kampuni ya Nyama na UDA ni makada wao na wanawajua na hatujaona popote walipofikishwa mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, baada ya UKAWA kupata dhamana ya Jiji tumekwenda kubatilisha maamuzi yenye dhuluma yaliyopoka umiliki wa UDA Jiji na nitasema kwa nini?

Niliambie Bunge hili, msije mkathubutu, maana jana nilisikia wanasema kuna ile shilingi bilioni tano aliyolipwa Simon Group tui Pangie matumizi, sisi kama Jiji tunatambua mamlaka yetu. Sasa kama sisi hapa hatujitambui Serikali inatuingilia sisi tunatambua mamlaka yetu. Tulisema hatuwezi kutumia hii shilingi bilioni tano kuhalalisha haramu kuwa kitakatifu. Siyo kwamba haina matumizi, Halmashauri zetu zina changamoto nyingi sana, lakini tulisema hatuwezi kuwa sehemu ya haramu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa bahati mbaya sana TRA baada ya kuona Azimio la Baraza la Madiwani linasema hii shilingi bilioni tano ya Simon Group hatutaitumia kwa sababu kuna ushenzi umefanyika kinyume kinyume kwa kutumia upungufu wa kisheria, wakaenda wakavuta kodi. Kwa hiyo, hayo makusanyo mnayosema yameongezeka mionganoni mwao ni fedha za kifisadi za kuiibbia nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la UDA, nitazungumza kihistoria tu. Hili shirika lilianzishwa mwaka 1974 ambapo Serikali ilikuwa na hisa asilimia 100. Mwaka 1985 Serikali iliamua kugawa hisa zake, asilimia 51 ikaipa Jiji na yenewe ikabakia na asilimia 49. Ni muhimu mkaelewa, hisa kiujumla wake zilikuwa milioni 15 lakini katika hizo hisa milioni 15, hisa milioni 7.1 ndiyo zilikuwa zimelipiwa ama zimekuwa allotted hizo nyingine milioni 7.8 zilikuwa hazijalipiwa. Kwa hiyo, Serikali ilivyogawa hisa, asilimia 51 Jiji na yenewe asilimia 49, Jiji likapata milioni 3.9 na Serikali ikabakia na milioni 3.4. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, figisu lilianzia wapi? Figisu lilianzia mwaka 2011 na wakati nasema haya naomba Serikali ielevi hivi, UDA kama ilivyo mashirika mengine ilikuwa chini ya uangalizi wa PSRC ama ilikuwa specified kwa Tangazo la Serikali Namba 543 la mwaka 1997. Kwa mantiki hiyo, kisingeweza kufanyika chochote mpaka iwe despecified na siyo kwa maneno maneno ila kwa Gazeti la Serikali. Mpaka sasa PSRC ilikuwa hai ikaisha, ikaja CHC ikaisha, haijawahi kuwa despecified. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tafsiri nyingine ni nini? Miamala yote kisheria iliyofanyika kuhusiana na UDA ilikuwa ni batili. Ndiyo maana katika muktadha huo, Jiji baada ya kwenda kwa UKAWA kwa sababu tunasoma na kujlongeza na kwa sababu wengine tulikuwa sehemu ya huu mchakato tukasema hili zoezi ni batili. Nilikuwa naelezea historia nikachanganya kidogo ili kuwaweka kwenye mstari ili mjue kwamba huu mchakato ulikuwa haramu from the beginning. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 kupitia hao hao makada wao, sitaki kuwataja majina maana ni wazee nawaheshimu sana, nimewatajataja sana mpaka wakawa wanani pigia simu Halima vipi? Kwa hiyo, sasa siwataji kwa sababu mnawajua. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 Bodi ya UDA ikaenda kugawa zile share ambazo hazikugawiwa na wala hazikununuliwa milioni 7.8 kwa Simon Group. Kwa aibu wamemuuzia share moja shilingi 145 yaani ile UDA yote walikuwa wanataka kuigawa nusu kwa jumla ya shilingi sijui bilioni 1.5 wakati huo huo ukaguzi ama tathmini iliyofanyika inasema shirika kwa huo unusu wake tu ina thamani zaidi ya shilingi bilioni 18 alikuwa anapewa mtu kwa sababu amehonga honga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mwaka 2011, kwa hiyo Simon Group akawa sehemu ya wanahisa wa UDA kwa kununua zile *unallotted shares* ambayo ni kinyume na *Articles of Associations* za UDA. Nina maandiko hapa ya Serikali, ya Msajili wa Hazina, yako hapa. Kwa hiyo, Waziri wa TAMISEMI tikisa tu kichwa nitakupa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo akapata uhalali kama mwanahisa kwenda kuomba kununua hisa zingine. Serikali ilitaka kuza hisa zake, lakini vilevile Jiji kukawa kuna dhana ya kuza hisa. Serikali ikaachia pembedi lakini Jiji kwa rushwa hizi hizi ikapitisha Baraza la Madiwani, wakapitisha kinyume na utaratibu. Tunajua vilevile hata kama Baraza la Madiwani likipitisha lazima Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ambapo kipindi hicho ni Waziri Mkuu aridhie. Hakuna sehemu hata moja ambayo Waziri wa TAMISEMI ameridhia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na huo ubovu wake sasa Simon Group akatakiwa alipe hiyo hela. Pamoja na ubovu wa mkataba ikakubaliwa mwisho wa kulipa fedha hiyo ni Septemba, 2014 kwa sababu hapa kuna fedha za *unallotted* lakini vilevile kuna fedha za Jiji baada ya Baraza kukaa, bilioni 5.4 hazikulipwa. Tukakaa kama Kamati ya Fedha, ni kwa bahati mbaya sana Kamati ya Fedha ya Jiji na Baraza tukaazimia mkataba ule ukabatilishwe mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa masikitiko na nasema hivi kwa sababu Kamati ya LAAC wakati Baraza lenye mamlaka linasema huu mkataba haramu tunaenda kuubatilisha, LAAC, sitaki kuamini LAAC ilihongwa kipindi kile, ikaja ikasema msibatilishe huu mkataba wakaelekeza Jiji waendelee na makubaliano na Simon Group. Kamati ya LAAC, kuna maelezo hapa na kibaya zaidi, kesho yake baada ya Kamati ya LAAC ilivyokuja kutoa ushauri kwenye Jiji, yale maneno waliyokuwa wanasema LAAC ndiyo hayo hayo maneno ambayo Simon Group aliandika kwenye barua kuhalalisha kwa nini aongezewe muda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, kwanza, fedha za hizo hisa zimekuja UKAWA tumeingia. Fedha iliyotakiwa ilipwe mwaka 2014 imelipwa mwaka 2016, tukasema huu mchakato ulikuwa batili kisheria kuanzia mwanzo. Hata kama

Baraza la Madiwani la kipindi kile chini ya Masaburi na CCM lilipitisha sheria inasema lazima Waziri aridhie, Waziri hakuridhia na hii UDA ilikuwa iko chini ya PSRC, miamala yote ilikuwa ni batili. Kwa mantiki hiyo, ili kuondoa mzizi wa fitina kwa sababu TAKUKURU ilifanya kazi yake, CAG alifanya kazi yake, nitaomba Bunge hili kupitia Kanuni ya Bunge ya 120 tuunde Kamati Teule ili hili suala lifanyiwe uchunguzi, tujue kinagaubaga, tujue mbivu ni zipi, tujue zilizoiva zipi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu eti tunasikia hapa watu wanazungumza, basi zile hisa ambazo Simon Group alikuja kukubali kuzirudisha milioni 7.8 tupewe Halmashauri tugawane. Hivi tunagawanaje wakati hivi tunavyozungumza, Simon Group wamekopa bilioni 50 NMB kwa ajili ya magari haya ya DART. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa eti Serikali inaitetea wakati ripoti ya Msajili wa Hazina hapa analalamika ye ye mwenyewe kama mbia ambaye hakuza hisa zake alikuwa hajui kama kuna kakampuni kingine kadogo cha uendeshaji wa magari ya mwendokasi kalikoundwa na Simon Group. Yaani Msajili ni mbia analalamika hajui halafu anatoka mbele anatetea huo upuuzi. Sisi UKAWA tunaongoza lile Jiji hatutaruhusu. Hatutaki mtuingize kwenye choo cha kike na choo cha kiime kwa kutulazimisha. Eti twende kuwa mwanahisa wakati kuna huyu jamaa kivyakevyake ameenda kukopa shilingi bilioni 50 ambazo zenyewe hatujui kazifanya nini, kuna vibasi pale vya Kichina tu vya kizushi, kwa hiyo tuingie tuwe wanahisa tuwe sehemu ya huo mzigo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi kesho kutwa Baraza la Madiwani tunaenda kukutana kwa sababu hiyo ni mandate yetu, yaani ninyi hapa mnatushauri tu. Kwa hiyo, msije mkajidanganya kwa wingi wenu, hasa ninyi upande wa huku, maana nasikia sijui Jiji linavunjwa, sijui sasa share tupewe, sisi wenyе malii ambao tunaongoza Jiji ndiyo tunaenda kuamua siyo ninyi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo na nitaomba niungwe mkono kwenye kifuncgu cha 120 nitakapokileta hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee suala la Lugumi, nitaomba Mwenyekiti akirudi atuambie Lugumi walienda kufanya nini? Kwa sababu tunajua mliomba mkataba ambao ndiyo unaweza kuainisha haki na wajibu wa kila pande. Tunavyozungumza, na wewe Naibu Spika unajua nawe ulisaidiasaidia kulifunika kuisaidia Serikali, unajua kwamba Bunge linapohitaji mkataba wa aina yoyote linatakiwa kupewa. Kamati yako imeomba mkataba kwa sababu CAG alisema vifaa vimefungwa 14 baada ya hoja ya Mheshimiwa Zitto alipokuwa Mwenyekiti wa PAC, mwezi Mei, 2016 CAG aliitwa tena na hawa kasema vimefungwa 14. Hivi ni miujiza gani imetokea tunaambiwa leo eti vimefungwa 153, ni miujiza gani? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tujibiwe hapa kwa sababu imekuwa ni utamaduni wa nchi hii tunatumia Usalama wa Taifa, tunatumia Polisi, Ulinzi na Usalama excuse kuiibia nchi. Sasa leo Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, malizia sentensi muda wako umekwisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Unajua leo nilikuwa na mizuka sana kwa sababu ya UDA hadi mbavu zinauma. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mwenyekiti wa ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Namalizia Mheshimiwa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu naona humalizi sentensi unaanza kwa kusema leo tena, siyo sentensi hiyo Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Haji. (Makofi/Kicheko)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi kwa sababu ya muda mfupi nikubaliane na kumuunga mkono dada yangu Mheshimiwa Halima kwa hapo alipofika. Nikuhakikishie kwamba na sisi tunajua kama kuna utapeli umefanyika wa kulisadikisha Bunge hili kwamba Lugumi walichokuja nacho mara ya pili ni cha ukweli wakati ukweli halisi unajulikana. Kama alivyosema ni maajabu katika muda wa mwezi mmoja kutoka vituo 14 vikaja 153. Huo ni uongo, ni uongo, ni uongo kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nianze kuchangia kwa kusema kwamba nasikitika sana kwa taarifa hizi nzuri ambazo tumeletewa hapa na wenzetu wa PAC na LAAC lakini kuna upungufu na nataka nianze na hii ripoti ya LAAC.

Kamati hizi ni za Bunge na ni Kamati za mahesabu. Umuhimu wa Kamati hizi hakuna ambaye hawezi kuuona kwa vyovypote vile iwe kwa jicho la karibu au kwa mbali. Hata hivyo, malalamiko makubwa yaliyopo hapa, nataka nisome katika ukurasa wa nne wa taarifa hii ya LAAC, anasema, nanukuu:-

*“Zipo namna kuu tatu za kutekeleza majukumu ya Kamati ambazo ni:-*

3. Kamati kuzuru na kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika baadhi ya Halmashauri ili kujiridhisha na thamani ya fedha katika miradi hiyo (value for money)."

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha sana ni kwamba tunaletewa taarifa hizi, siyo LAAC wala PAC, wote wanasema hakuna aliyepeata fungu la kwenda kujiridhisha na taarifa hizi tulizoletewa hapa. Kwa maana nyine ni kwamba wao wamepelekewa taarifa kwenye meza na wametuletea sisi hapa bila kuthibitisha chochote, hili ni kosa moja kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni mambo ya kimahakama kosa hili linafanana na utakatishaji fedha, uhaini, ugaidi, makosa ambayo hayana dhamana, ndiyo! Kwa sababu tunakotoka tunajua mambo yaliyokuwa yanaletwa kwenye makaratasi na wanapokwenda field kwenye ukaguzi kulikuwa kunakuja manyago makubwa sana. Kulikuwa kunakuja mambo ya hatari, mtu anaoneshwa hapa imejengwa shule wakifika hata kiwanja hakuna. Leo Bunge mmeridhia tuletewe haya kwenye makaratasi badala yake tunakuja kulishwa humu na tunapiga makofi tunakubaliana nayo. Hili ni kosa moja kubwa sana ambalo Serikali haihitaji kupewa dhamana juu ya kosa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najua tunabana na kubana mimi najua kuna utamu wake, lakini na kubanua kuna raha zake. Huwezi kubana moja kwa moja ukadhani mambo yataenda, haiwezekani. Lazima sehemu nyine ubanue kidogo ndiyo raha ipatikane. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ninukuu usemi... (Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, hicho ni Kiswahili cha Kizanzibari, unataka kufanua kidogo? (Kicheko)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ni Kiswahili cha mwambao. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ninukuu usemi wa hekima aliosema Rais Mstaafu kipenzi cha nyoyo, Jakaya Mrisho Kikwete. Hivi karibuni alisema hivi, unapokuwa mpya watu wanataka mambo mapya, lakini yawe mapya ya kimaendeleo siyo mapya ya kuharibu kule tulikotoka. Huu ni usemi mmoja wenyе hekima sana kwa Rais wetu yule mpewa mstaafu, Mungu amjalie akae kwa amani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi taarifa za CAG ndizo zilizosaidia kuonesha madudu makubwa sana yaliyofanyika ndani ya nchi hii lakini leo hata CAG amelalamika kushindwa kwenda kufanya verification kwa sababu hakupewa bajeti ya kutosha. Mnataka kuficha nini ikiwa CAG sasa hapewi uwezo wa

kwenda *field* kuangalia uhalsia wa mambo yanayofanyika? Mmeanza kubana Bunge lisionekane *live*, mmeanza kubana mikutano ya vyama vyasiasa, mmeanza kumbana mpaka CAG asiende kwenye kazi zake? Tunawatendeaje haki Watanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari na kama huko tunakokwenda mwendo wenyewe ndiyo huu jiangalieni upya. Mliwaambia Watanzania mnaleta ajira, mnaleta maisha mazuri, mnaleta afya, Watanzania wakawaamini na kuwapa kura zao sasa fanyeni yale mliyowaahidi Watanzania msiende kinyume chake. Siku ya hukumu inakuja na haiko mbali, siku zinakwenda kweli kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangazwa na jambo lingine na mimi nataka niliseme kwamba Kamati ya PAC wamelalamika hapa na mchangiaji mmoja amelalamika anasema wametaka taarifa ya madeni ya *TIB* wamenyimwa. Hili ni kosa lingine la uhaini kabisa kwa Kamati ya Bunge kunyimwa taarifa ili wafanye kazi zao. Hili Bunge linaonekanaje sasa? Hili siyo Bunge tulilotokanalo sasa tunataka kuchezewa na sisi tumekubali kuweka videvu vichezewe, haiwezekani! Ni lazima tuoneshe wajibu wetu kama wawakilishi wa wananchi ni vipi tumeisimamia Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati yangu hatukukubaliana na hili na *TIB* walileta orodha yote ya waliokopa *Community Import Support* tukawa nayo. Kwa hiyo, haiwezekani ni lazima wakubaliane na matakwa ya Kamati za Bunge, hakuna namna nydingine, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maulid Said Mtulia.

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa na kuchangia jambo hili. Pili, nikushukuru kwa kunipa fursa hii.

Kwanza, nianze kusema naunga mkono taarifa zetu hizi nzuri kabisa zilioandaliwa na Kamati zetu hizi kubwa mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuweka rekodi sawa lakini kubwa kuliko yote kuonesha kwamba sisi watu wa Kinondoni tuliwahi kuonja matunda ya UKAWA. Matunda yale tuliyaonja katika gogoro kubwa linaloonekana kwamba Manispaa na Halmashauri hazichangii 10% za vijana na wanawake. Chini ya aliyekuwa Meya wetu wa UKAWA, Ndugu Boniface Jacob, Manispaa yetu ya Kinondoni ambayo imeitwa manispaa sugu imefanikiwa kutoa pesa shilingi bilioni 2.4. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie wenzangu kama sisi Wabunge tukishirikiana na Madiwani wetu na Wenyeviti wetu wa Halmashauri au Mameya tukawa na nia ya dhati, hizi pesa zinatoka na sisi kwetu Kinondoni zimetoka. Niwaahidi wananchi wa Kinondoni vyovyote itakavyokuwa bila kujali mabadiliko yoyote yaliyotokea tutahakikisha mwaka huu wa fedha 2016/2017 tutatoa pesa shilingi bilioni 6.4 kwa sababu makusanya yetu ya ndani ni takribani shilingi bilioni 64. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masikitiko hapa, tulikuwa tumekadiria kukusanya *property tax* shilingi bilioni 10 kwa Manispaa yetu ya Kinondoni. Leo Mheshimiwa Waziri ameondoa kodi hii kutoka manispaa ameipeleka TRA na mpaka sasa ndio kwanza wamepeleka vibarua vya kuwataarifu watu kwamba wanadaiwa, tuna masikitiko makubwa sana. Kwa kuondoa hii shilingi bilioni 10 maana yake wananchi wa Kinondoni, vijana na wanawake mmewakosesa shilingi bilioni moja ambayo kama wangegaiwa shilingi milioni hamsini, hamsini, ni wananchi 20,000 mmewakosesa pesa hizi. Ni hasara kubwa sana kwetu sisi watu wa Kinondoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri kama atashindwa kurejesha hii *property tax* kukusanya katika Halmashauri basi walau arejeshe katika Manispaa. Kwa sababu kwenye Manispaa pesa nydingi zitapotea, kwa sababu Majiji yana majengo makubwa yenyе thamani kubwa tofauti wakati mwingine na Halmashauri yenyе majengo madogo. Kwa hiyo, tusije tukaipoteza hii fursa kwa kupoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili napenda niishauri Serikali kama wajibu wetu wa msingi, imeelezwa hapa katika ripoti ya PAC tuna Shirika letu la NSSF. Katika mashirika yetu ya hifadhi hili ni shirika kubwa sana. Hili shirika lina utajiri wa shilingi trilioni 3.8. Shirika hili lina miradi 40 ambayo tayari iko kwenye utekelezaji. Shirika hili limepata mabadiliko, limepata Mkurugenzi mpya na ni mtu mwenye uwezo, Profesa, lakini kwa masikitiko makubwa Wakurugenzi nane ambao walikuwa wanafanya kazi na Mkurugenzi huyu wamesimamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yawezekana kuna mambo yamesemwa na nashukuru ripoti imeeleza vizuri, lakini imekuja kueleza vizuri suala la Dege Eco Village na imeeleza kwamba si kweli ardhi imenunuliwa kwa milioni 800 kama inavyoandikwa kwenye magazeti wakati mwingine, kilichotokea pale ni kwamba ardhi ile heka 300 imeingizwa kama capital na yule mwekezaji Azimio amepata 20% ya mradi kwa kutoa viwanja 300; siyo kapewa pesa milioni 800 kwa heka, siyo kweli. Kwa thamani ya mradi share atakayopata 20% wameigawanya kwa viwanja ikaonekana milioni 800 wakati siyo utaratibu. Utaratibu na huu sio mgeni, hata National Housing wamewahi kuingia mkataba na TPDC na wamepata 25% katika jengo lile kubwa pale la Mkapa Tower na

kiwanja cha heka moja ni sawasawa na bilioni 4.5. Sasa huu ni utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini masikitiko yangu au ushauri wangu naotaka kumpa dada yangu pale Mheshimiwa Waziri mhusika ni kwamba shirika kubwa kama hili akapewa Director mgeni, Wakurugenzi wake nane ambao walikuwa wanasaidiana na Mkurugenzi aliyeondoka, wandojua uendeshaji wa shirika hili wakakaa pembedi akawa Mkurugenzi mpya anachukua na Wakurugenzi wake wengine wapya, tunapoteza pesa zetu, yaani shilingi trillioni 3.8 tunaziweka rehani. Hawa watu wanatakiwa wawepo wamsaidie, kuna kaka yangu Magoli, kaka yangu Kidula, Wakurugenzi wapo pale waende wakamsaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwininge tunapata hasara kwenye mashirika yetu ni kwa sababu hatujali thamani ya kile kitu tulichonacho. Hii inatuletea matatizo sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Ndiyo muda umeisha huo?

**MBUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afanye kila hali Wakurugenzi hawa wamsaidie Mkurugenzi wetu Mkuu ili uchumi wetu usiyumbe.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana umesikia. Tunaendelea na Mheshimiwa Aeshi Hilaly kwa muda uliobaki.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na kwa kunipa dakika tano zilizobaki na naomba kuchangia maeneo machache sana. Kubwa napenda kuchangia suala la kilimo na Wizara ya Kilimo kwa ujumla pale ambapo Serikali tumepoteza zaidi ya shilingi bilioni sita kwa mahindi yaliyoharibika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia taarifa hii, kimsingi timesikitishwa sana na hatua zilizochukuliwa kwa Wakurugenzi wa Idara ile. Mwaka 2013/2014 Serikali ilitoa maagizo kwamba wananchi wasiuze mazao yao nje ya nchi na Serikali itanunua mahindi yote. Kwa bahati nzuri wananchi walilima mahindi mengi sana na kwa bahati nzuri Serikali ilianza kununua mahindi yale, lakini kwa bahati mbaya mahindi mengi yalirundikana Serikali ikawa haina uwezo wa kuyanunua. Icafikia mwezi wa Novemba mvua zikaanza kunyesha, mahindi yakaharibika yakiwa nje hayajapokelewa na NFRA. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Bungeni Serikali ilitoa tamko kwamba mahindi yote yaliyoko nje yanunuliwe na Serikali. Hapo ndipo kilipotokea kituko kwamba wananchi waliiuzia mahindi NFRA kwa mkopo, hatukuwa na uwezo wa kulipa mahindi yale. Mwaka 2014 kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa sehemu nyingi tulipoteza nafasi zile kwa sababu wanachi walisema tumewakopa mahindi hatujawalipa. Cha kushangaza mahindi haya yaliviyotunzwa yakiwa yameloana na mvua yaliharibika, lakini juzi miezi mitano iliyopita Serikali iliamua kuyauza mahindi yale mabovu. Tukapoteza takribani shilingi bilioni sita na pesa za ziada. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nachangia jambo hili? Waziri wa Kilimo aliyekuwa wakati huo, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba aliidhinisha mahindi yale mabovu yauzwe. Baadaye Waziri wa Kilimo akahamishwa akachaguliwa Waziri mwingine mpya, Mheshimiwa Tizeba, haikuchukua siku mbili akawafukuza kazi Wakurugenzi wote bila makosa. Sasa nataka aje Waziri atueleze ni njia ipi aliyotumia au ni utafiti upi aliofanya na kuwasimamisha kazi Wakurugenzi wale bila kosa lolote kwa sababu mahindi yale yaliharibika kutokana na idhini ya Serikali tununue mahindi yaliyoloana na mvua. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, inauma mtu ambaye amefanya kazi kwa muda mrefu, mtu ambaye amelitumikia Taifa hili kwa uaminifu na kwa kazi ya kutukuka lakini anakuja mtu kumtumbua jipu bila kosa lolote. Nataka niseme tunamuomba Waziri wa Kilimo aje atutolee sababu ipi aliyotumia kuwasimamisha kazi Wakurugenzi wa Idara ile ya NFRA? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa ambalo ni la kushangaza, tuna Meneja anatokea Mkoa wa Rukwa, amekaa Mkoa wa Rukwa takribani miaka 15, hana kosa lolote, kahamishwa kwenda Mkoa wa Songea ndani ya wiki mbili lakini kosa lile la kununua mahindi mabovu linamkuta yeye na yeye anasimamishwa kazi. Haki iko wapi? Mtu afanye nini ili alitumikie Taifa kwa uaminifu mkubwa? Kwa hiyo, sisi kama Kamati tunamuomba Mheshimiwa Waziri aje atujibu hatua zipy alichukua yeye kwenda kuwasimamisha kazi watu bila kuwa na kosa? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kila mtu anataka aonekane anafanya kazi ndani ya Serikali. Kila mtu anataka aonekane anachukua jukumu lake kusimamia watu wengine, lakini hili sisi kama Kamati tunamtaka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aje atujibu kwa nini aliwachukulia hatua wale bila kuwa na kosa lolote wakati kosa lilitokea tukiwa hapa Bungeni mwaka 2014. Tumuulize Waziri wa Kilimo aliyejita kwa nini aliruhusu mahindi yale yauzwe mabovu? Mbona yeye hakuwasimamisha kazi? Yeye hakuliona hili? Aliliona lakini wale walishindwa kwa sababu walikuwa wanasubiri ripoti...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Malizia sentensi Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kuongea kwa sababu muda wa dakika tano ni mfupi, naamini jioni nitakuja hapa kuongea tena dakika 15 zingine lakini namuomba Mheshimiwa Waziri aje atujibu katika hili. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi chetu cha asubuhi. Kabla sijaleta matangazo niliyonayo hapa mezani, mchana kutakuwa na muda mfupi wa kuchangia na majina niliyonayo hapa kama nilivyosema tangu asubuhi bado ni mengi. Watu watakaopata fursa hiyo upande wa CCM watakuwa na dakika 30, upande wa CHADEMA watakuwa na dakika 10 na kwa sababu anayefuata kwenye orodha ni Mheshimiwa Cecilia Paresso, alisema dakika zake atachangia na Mheshimiwa Heche. Kwa hiyo, maana yake dakika 10 za CHADEMA zitagawiwa kati ya hao Wabunge wawili. Upande wa Chama cha Wananchi – CUF watakuwa na dakika tano na anayefuata kwenye orodha niliyonayo ni Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk.

Kwa upande wa CCM tutakuwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Vedastus Mathayo, Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Wametajwa wanne lakini watachangia hizo dakika zao 30 walizopewa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninayo matangazo mawili. Tangazo moja ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hii kuwa leo tarehe 10 Novemba, 2016, saa 7.00 mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi namba 227, Jengo la Utawala. Wajumbe wa Kamati hii mnaombwa kuhudhuria.

Tangazo lingine ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hii kuwa leo tarehe 10 Novemba, 2016, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao na wanafunzi wa Chuo cha Madini Dodoma kujadili kuhusu uhalsia na usimamizi wa mazingira katika maeneo ya migodi. Kuhusu ukumbi, mtajulishwa, nadhani mna utaratibu wenu wa kuwasiliana, mtawasiliana. Mwenyekiti anaomba mhudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 leo jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA KAMATI

#### **Hoja za Kamati za Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)**

(Majadiliano yanaendelea)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa taarifa za Kamati mbili, Mheshimiwa Mussa Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa John Heche cajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kukutana ili tuzungumze masuala ya nchi yetu. Vilevile nichukue fursa hii nikiungana na wenzangu waliotangulia kuchangia Kamati ya LAAC na PAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukumbusha tu kwamba Serikali za Mitaa zipo kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni. Hata hivyo, taarifa ya Kamati pamoja na kuandikwa vizuri kuna baadhi ya maeneo kuna upungufu. Labda nisema katika Halmashauri zetu kumekuwa matatizo ya matumizi mabaya, lakini Kamati imetupa taarifa ya baadhi ya maeneo yaliyochambuliwa kwa mfano katika uchambuzi wa taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 na 2014/2015 na kuonesha hesabu zake zina matatizo katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano, katika matumizi yasiyozingatia Sheria za Manunuzi, hapa kuna upungufu mkubwa kwa sababu Sheria za Manunuzi hazifuatwi na matokeo yake baadhi ya bidhaa au huduma zinazotolewa katika Halmashauri zinakuwa chini ya kiwango au nyingine haziridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, mfumo uliopo sasa hivi katika Halmashauri zetu ambapo Madiwani wametolewa katika ile Tender Board na kuachwa watendaji peke yao ndiyo wanaofanya shughuli za manunuzi, naona huu ni upungufu, naishauri Serikali iliangalie upya suala hili kwa sababu watendaji wanapobaki peke yao huku tukiambiwa kwamba Madiwani ndiyo jicho la Serikali katika Halmashauri, wao wanafanya wanavyotaka, wanatoa zabuni kwa watu wanaowataka, matokeo yake sasa ama bidhaa au huduma zinazotolewa zinakuwa chini ya kiwango. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna upungufu katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati kwa kipindi kilichopita na pia kutojibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lingine kuna usimamizi mbovu katika kupeleka au kutokukamilika kwa miradi au miradi inakuwa chini ya kiwango. Vilevile katika Halmashauri kuna taratibu zilizofanyika za kuzinyang'anya Halmashauri makusanyo ya *property tax*.

Kwa maoni yangu naona hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu Halmashauri ziliwa zikitegemea sana *property tax* kama chanzo chake kikubwa cha mapato. Leo Halmashauri zimenyang'anya kukusanya *property tax* imepelekwa Mamlaka ya Mapato (TRA). Kwa mfano, hata Halmashauri yetu ya Jiji la Tanga ilikuwa na nyumba za kupangisha (*quarters*) pia zimeingizwa katika ukusanyaji wa TRA. Mimi nalionna hili ni tatizo au Serikali itueleze kama imeamua kuziua Halmashauri kwa kifo cha kimya kimya (*silent killing*). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Leo Halmashauri zinahudimia wananchi ikiwa ni moja ya majukumu yake, kuna zahanati, shule, barabara, mifereji na usafi wa miji, unapozinyang'anya vyanzo vya mapato shughuli hizo zitafanyikaje bila fedha?

Mimi nashauri ikibidi Halmashauri zirudishiwe kufanya mapato au kama Serikali imeona *property tax* ni chanzo ambacho inastahili kupata Serikali Kuu basi irudishe vyanzo vingine ambavyo ilizinyang'anya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye suala la Serikali za Mitaa, Serikali nayo inahusika moja kwa moja kuziwezesha Halmashauri ili ziweze kutenda shughuli zake vizuri lakini Halmashauri zimenyang'anya uwezo wake. Hata katika kitabu chetu hiki kuna miradi ambayo imefanywa chini ya kiwango au haijatekelezwa. Kwa mfano, mradi wa maji katika Kijiji cha Kayanze, Jijini Mwanza wenge thamani ya shilingi 618,704,554 haujatekelezwa. Pia kuna mradi wa maji wenge thamani ya shilingi 5,049,000,000 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji nao pia haujatekelezwa. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema miradi ya maji itekelezwe. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresto atafuatiwa na Mheshimiwa John Wegesa Heche na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hizi taarifa zilizowasilishwa mbele yetu, taarifa ya Kamati ya PAC na LAAC. Mchango wangu wa kwanza utajielekeza katika suala zima la Deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Juni, 2016 Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 9.76 maana yake linakimbilia shilingi trilioni 40. Madeni haya kwa mujibu wa taarifa ya CAG ameeleza kabisa hakuna mkakati wa namna gani yanaweza kwenda kulipika. Kulikuwa kuna rasimu ya mkakati huu ya mwaka 2002, ikatengenezwa rasimu nyingine ya mwaka 2004, ikatengenezwa nyingine ya 2014 lakini zote ni rasimu bado haijakamilika kuwa mkakati wa kuona namna *tuta-control* Deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia, itafikia mahali fedha zote za makusanyo ya nchi hii zinaenda kulipa madeni. Kama ambavyo ilivyo leo kila kinachokusanya karibu shilingi bilioni 900 inaenda kulipa madeni. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ifike mahali iandee mkakati. Ripoti ya CAG imesema kabisa hii rasimu ambayo ipo tena imeandaliwa kizamani haiendani na hali halisi ya uchumi wa nchi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaona umuhimu wa kuwa na mkakati huu ambao utaendana na hali halisi ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Tuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo kwa kiwango kikubwa fedha zake zinakopwa na zinaenda kuwekezwa katika miradi mikubwa. Hatukatai kufanya shughuli hizo, lakini unapoenda kukopa halafu hurejeshi inakuwa ni tatizo. Mfuko mmojawapo tu kwa mujibu wa taarifa ya CAG ni PSPF una hali mbaya ambapo unakaribia kafilisika kabisa kwa sababu Serikali hairejeshi fedha ilizozikopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima ifike mahali muache kabisa kukopa hizi fedha za wanachama. Ni fedha za wanachama wanaweka kule wakijua wanajiwekea akiba lakini Serikali mnaenda kuzichukua na ku-invest kwenye miradi mikubwa ambayo tunaona kabisa siyo rahisi muweze kurudisha kwa sababu mmejaa madeni, mnadaiwa ndani na nje, mnakopa tena kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, mnadaiwa kila kona, mwisho wa siku mtaenda kuua hii akiba ya wafanyakazi ambao wanatarajia waipate siku wakistaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaongelea sana suala la kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tumesema sana kwenye Bunge la Kumi. Leo mnajiita wazee wa hapa kazi tu, wazee wa kubana matumizi, si ndivyo mnavyojiita? Kama kweli mnataka kubana matumizi ni lazima muangalie suala la kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iko takribani tano au sita yote ina Wakurugenzi, ofisi, inaendeshwa kwa gharama na kwa fedha za wanachama. Kama mnasema mnabana matumizi muende

muunganishe hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwepo na ama mifuko miwili au mitatu ili hicho mnachokiita cha kubana matumizi mkifanye kwa vitendo siyo mnatuambia tu halafu hakuna mnachokifanya. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya mwisho nitajielekeza katika Serikali za Mitaa. Katika Awamu hii ya Tano mnaenda kuua kabisa Serikali za Mitaa. Mnaenda kuzimaliza wakati Serikali za Mitaa zipo kwa mjibu wa Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uteuzi tu mlio fanya, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa hawa ma-DC, ma-DED, ma-DAS, kwa kweli ni watu ambao hawajapitia kwenye mifumo ya *local government*, wengine wametolewa mnakojua, wamepewa nafasi ambazo hawana *experience* hata nukta moja. Hivi wanaendaje kufanya kazi? Ma-DED wengine hawajui hata vote ni nini, anauliza vote ni nini? Wanauliza hawajui. Hivi mnategemea kutakuwa na ufanisi? Ndiyo maana tunawaambia mnaenda kuua Serikali za Mitaa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali miaka yote imeonesha suala la Serikali Kuu kutokupeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri za Wilaya. Hivi tunavyoongea leo, fedha zilizoenda katika *local government* ni fedha za mishahara tu. Mfano mzuri ni Halmashauri yangu ya Karatu. Fedha kidogo tu ilioienda ni ya barabara shilingi milioni 50 lakini hakuna fedha za miradi ya maendeleo zilizoenda yaani mpaka leo tunaingia robo ya pili ya bajeti ya Serikali fedha hazijaenda katika Serikali za Mitaa. Mnatarajia nini si mnaenda kuzua Serikali za Mitaa.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Wegesa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii na namshukuru sana Mheshimiwa Paresso kwa kunipa muda wake nitumie kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme mambo machache na niseme pale Wabunge wenzangu walipoishia. Tatizo kubwa ninaloliona mimi hasa kwenye uendeshaji wa Serikali za Mitaa ambazo kimsingi ni Serikali kamili, zimepewa mamlaka yake Kikatiba. Leo kila mtu aliyesimama hapa analalamika, aidha, kwa Wakuu wa Wilaya au Wakuu wa Mikoa kuingilia mamlaka za Halmashauri. Hii inafanyika kwa sababu kila mtu anafukuzia kumfurahisha bosi, Mtukufu Rais. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani watu wanafanya madudu pale na imekuwa utaratibu kwamba watu waliofanya madudu wanapandishwa cheo. Sasa na wengine kule Wilayani anatafuta na yeye nitoke vipi. Mkuu wa Wilaya anatembea nyuma kuna kamera utafikiri anaenda sijui kufanya shooting? Mkuu wa Mkoa naye akitembea nyuma kuna kamera, nionekane huko, Mtukufu anione jioni kwenye taarifa, matokeo yake ni kwamba tunaua Serikali za Mitaa. Tunaendesha nchi hii kama duka. Unajua ukiwa na duka asubuhi unasema ile paketi ya sigara iliyokuwa hapa iko wapi, inatafutwa. Ndiyo hayo yanayotuletea matatizo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Diwani, leo Madiwani wote wazuri wanakataa kugombea na hili Mheshimiwa Simbachawene unalijua, watu wazuri wanakataa kugombea kwa sababu hawalipwi mshahara, wandalipwa posho. Leo hata ile posho ambayo wanalipwa, Mkuu wa Mkoa anaona ni shida anaenda kuwaondolea posho Madiwani wakati yeye mwisho wa mwezi analipwa mshahara. Kama yeye ni mzalendo kiasi hicho kwa nini asiache mshahara wake? Sasa hii ndiyo *level* ya unafiki ambayo tunaiwea hapa kwamba Mkuu wa Mkoa anataka kuondoa posho ya Madiwani wakati yeye analipwa mshahara, wao hawana mshahara na mnataka wasimamie fedha ambazo mnapeleka Halmashauri, haitawezekana. Ni lazima tuweke heshima kwa Madiwani, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili fedha zote zinazopelekwa Halmashauri zinakwenda kwenye vijiji, vitongoji, kule ndiyo kuna watu. Serikali hii ya CCM tumeimba miaka yote kwa nini hamtaki kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji fedha kama malipo? Hakuna anayetoa majibu. Wenyeviti hawa wa Vijiji ambao wanafanya kazi kwa hisani kila siku utasikia Mkuu wa Mkoa nimekufukuza kazi, nimewaweka ndani, unawekaje mtu ndani kwa vitisho ambaye humlipi hata senti tano? Kwa hiyo, mimi nafikiri tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za CAG kufanya ukaguzi. Nyie wenyewe mnasema mnataka kutumbua majipu, kumbe ni unafiki mnataka kujificha madudu yenu myafichie ndani humo. Kheri Mheshimiwa Kikwete aliyweweka wazi watu wakajua, ninyi mnaficha hamtaki kujulikana maovu yanayofanywa, mnamnyima CAG fedha. Wananchi wa nchi hii wajue kwamba Serikali hii ni Serikali isiyotaka kukosolewa ndiyo maana haimpi hata CAG fedha ili aende akakague aone hawa Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya mliyopeleka, walioshindwa kura za maoni za CCM madudu watakayofanya kwa miaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote mliyopeleka ni wale walioshindwa kura za maoni za CCM yaani bora wangewachukua ninyi mlioshinda wakawapeleka kuwa Wakurugenzi kuliko kuchukua mtu aliyeshindwa, amekataliwa na wanachama wenzake kwamba wewe huwezi kuongoza, halafu unamchukua

unampeleka eti kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri matokeo yake hajui chochote anayochotakiwa kufanya. (Makofi/Kicheko)

## TAARIFA

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi za Jamii ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kaa kidogo tafadhali.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Naomba tafadhali ulinde muda wangu ni mdogo sana.

**NAIBU SPIKA:** Sawa naomba ukae.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Heche rafiki yangu kwamba hii kutoa nafasi ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi na wengineo katika uteuzi ni nafasi ya Kikatiba ya Mheshimiwa Rais anaruhusiwa kumpa amtakaye, kwa hivyo asione choyo. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitatumia muda wangu kuharibu kwa kumjibu yule najua anachofukuzia nitaharibu sana. Naomba niendelee. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi za Jamii watu wameweka fedha zao, wewe unakatwa mshahara wako unaenda pale. Leo inasemekana fedha hizi zilipopelekwa Benki Kuu mmechukua mmeenda kununulia Bombardier, mnawakataza watu kuchukua fedha zao ambazo wamehifadhi. Yaani kijana amefanya kazi mgodini, ameteseka maisha yake amehifadhi kule, anataka kujitoa au amefukuzwa kazi achukue fedha ajengee watoto wake, mnambwambia mpaka miaka 60. Mnamkataba na maisha? Akifia hapa katikati huko mtampa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa matokeo haya ya kuchukua fedha ambapo tunaendesa nchi kama duka, kila kitu mnataka kiwe centralized, Halmashauri mnaua, Mifuko ya Hifadhi za Jamii mnaingilia, kila kitu na fedha mpaka za wananchi wa kawaida mnataka muwe mnachukua kwenye mifuko yao, ni lazima ikome. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde thelathini malizia.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakusukuru kwa sababu hata nikianza hii hoja hautanivulimia, ahsante. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Heche. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae. Hawa wote wanaotajwa ni dakika tano tano.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru wa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache ambayo ninayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kuzipongeza Kamati zote mbili kwa taarifa nzuri ambazo zimetolewa. Kwa kweli ni nzuri sana na naamini kama Serikali itazifanyia kazi basi hali itakuwa ni nzuri. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo napenda kuchangia ni kuhusu taarifa za Mkaguzi Mkuu (CAG). Kwanza CAG ndiyo mwakilishi wa Bunge hili, ndiyo jicho la kwenda kuangalia kukoje huko katika taasisi zetu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda haraka haraka kwa sababu ya muda, chukulia ripoti ya Serikali Kuu ya mwaka huu. Katika ripoti ya mwaka 2014/2015, katika Serikali Kuu taasisi 18 zilipata hati yenyé mashaka na taasisi moja ilipata hati isiyoridhisha kwenye Serikali za Mitaa ndiyo inatisha. Ukiangalia kwenye Serikali za Mitaa mwaka 2011/2012 hati zenye mashaka zilikuwa 29, hati isiyoridhisha ilikuwa moja na hati chafu ilikuwa moja. Mwaka 2014/2015 kwenye Serikali za Mitaa ndiyo kunatisha, hati zenye mashaka 113, hati zisizoridhisha tatu na hati chafu moja, hii maana yake nini? Maana yake hali siyo nzuri katika taasisi zetu katika kusimamia fedha za umma na hapo lazima Serikali ichukue hatua stahiki kuhakikisha kwamba tunazuia hii hali ambayo ipo. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hati yenyé mashaka maana yake ni kwamba vitabu na hesabu zilizopo hazioneishi sura halisi ya taasisi. Sasa kama hivyo ndivyo ilivyo tusipochukua hatua hali itaendelea kuwa mbaya katika taasisi zetu. Naishauri Serikali yangu tuendelee kuchukua hatua stahiki ili tuhakikishe mambo yanakuwa mazuri katika miaka inayokuja. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu taasisi chache ambazo zinafanya kazi kama TRA. Zipo taasisi ambazo zenyewe zinazalisha, zinafanya biashara, zinanunua raw material, zina-process goods halafu zinaenda kuzalisha zinauza kama TANESCO na zinginezo. Hata hivyo, zipo taasisi zinazofanya kazi kama TRA kwa mfano EWURA na TCRA hawana gharama zingine za uzalishaji zaidi ya tozo, zile tozo ni mali ya Serikali, lazima Serikali iweke mkono wake kuhakikisha kwamba zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hiyo ndio itakayoongeza mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, kwa sababu ya muda nakwenda haraka haraka lakini nzungumzie matatizo ambayo yamejitokeza. Labda niweke taarifa vizuri, nimesikia watu wameliongelea suala la Lugumi labda pengine niweke taarifa vizuri. Kwanza niseme mimi ndiyo nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Lugumi iliyokuwa inashughulikia huo mkataba. Katika mkataba ule hadidu za rejea ilikuwa ni moja kwenda kuangalia kama ile mitambo ilinunuliwa na kufungwa, ndiyo ilikuwa kazi yetu. Hatukuwa na kazi nyingine zaidi ya hiyo na tulizunguka nchi nzima, Mikoa yote, Wilaya zote tukathibitishe kama zilinunuliwa na kufungwa. Naomba niweke rekodi sawa kwamba tulikuta kwa asilimia karibu 99 vilinunuliwa na kufungwa. Kilichokuwepo kwenye taarifa ya CAG alisema katika vituo vyote vile ni vituo 14 tu ndiyo mitambo ilikuwa inafanya kazi zake sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako hili hata Kamati Ndogo ilipoenda ilikuta ni vituo 15 ndiyo vilikuwa vinafanya kazi yake sawasawa. Hiyo ndiyo iliyokuwepo kwenye ripoti ya Kamati yetu. Kama vituo 15 vinafanya kazi yake sawasawa kulikuwa na tatizo gani? Ile mitambo ina kazi tatu, kazi ya kwanza ilikuwa ni kuchukua picha na maelezo ya wahalifu; kazi ya pili ilikuwa ni kuhifadhi kumbukumbu zile kwenye njia ya electronic na kazi ya tatu ilikuwa ni kutuma sasa zile taarifa kwenye mitandao ili kuweza ku-share na vituo vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niliambie Bunge lako vizuri kwamba katika kazi ya kwanza na ya pili ilikuwa haihitaji kabisa mtandao wa *internet*. Hapa ndipo Kamati ilikuwa inauliza kama vifaa vyote hivi vilinunuliwa ni kwa nini sasa vilikuwa havitumiki kufanya kazi ya kwanza na ya pili, ndiyo swali lililokuwepo. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia sentensi muda umekwisha.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilichotaka kusema ni kwamba mitambo yote ilinunuliwa, imewekwa lakini ilikuwa haijaanza kutumika. Hiyo ndiyo hoja ambayo tunayo kwenye Kamati na naomba ieleweke hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa muda huu. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Tunaendelea na Mheshimiwa Doto Biteko atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Vedastus Mathayo ajiandae.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii lakini vilevile niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya LAAC pamoja na PAC kwa taarifa yao nzuri ambao kwa kweli wamefanya kwa niaba yetu sisi Bunge zima. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya LAAC imekuja na mapendekezo tisa kwa mujibu wa tarifa hii. Mimi naomba nitangulie kusema nayaunga mkono mapendekezo yote hayo ambayo imeyataoa. Kwa kweli ukisoma taarifa hii utaona Kamati hii imechukua muda mwangi sana kufanya kazi. Sisi kama Wabunge kwa sababu kazi hii wamefanya Wabunge wenzetu tunawajibika kuwapongeza sana Wajumbe na uongozi wote wa Kamati hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza lililozungumzwa kwenye Kamati hii na mimi nataka nichangie kidogo kwenye maeneo hayo ni upelekaji wa fedha kwenye Halmashauri zetu. Kila Mbunge aliyesimama hapa amezungumza kwa namna tofauti tofauti namna ambavyo kutokelewa kwa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri kunavyoathiri miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu. Wewe unafahamu na Bunge linafahamu shughuli nydingi tunazofanya sisi Wabunge zinatekelezwa kwenye ngazi ya Halmashauri, kama Halmashauri hizi hazipatiwi pesa bila shaka mwisho wa siku hatutakuwa na jambo la maana la kujivunia kwamba tumefanya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye Wilaya yetu ya Bukombe tumepeleka maombi mbalimbali ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Barabara nydingi zilizopo kule kwa muda mrefu hazipitiki kwa sababu maeneo mengi ya Wilaya yetu ya Bukombe yapo kwenye milima, barabara zile zimekatika, hazipitiki. Barabara kama za Maghorofani, Mchangani, Imalanguzu, Nifa, Rulembela na Kelezia hizi zote hazipitiki kwa sababu hazijawahi kufanyiwa matengenezo mwaka uliopita na mwaka huu vilevile hatujawahi kupata fedha. Kwa hiyo, naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya kwamba sasa Serikali iharakishe kuzipeleka pesa kwenye Halmashauri ili tuweze kupata maendeleo haya na ukarabati wa miradi hii uweze kukamilika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine limesemwa hapa, yapo madeni mengine ya watumishi. Hivi mwali mu aliyesimamia mitihani wa kidato cha nne mwaka jana unamkopa kahela kake kidogo hako, jamani hata mbingu haziwezi kufurahi. Wilaya ya Bukombe na Wilaya nyingine kwenye Mkao wa Geita na hili nimeliuliza humu Bungeni, nimekwenda TAMISEMI nimewauliza fedha za walimu waliosimamia mitihani wa kidato cha nne mwaka jana ziko wapi? Wengine wakaniambia uende kwa watu wa Wizara ya Elimu, wengine wanasema hapana nenda TAMISEMI, shilingi milioni 35 walimu wa Bukombe kila tukikutana ndiyo jambo wanaloniuiliza. Kila tukionana wananiambia Mheshimiwa pamoja na maneno mazuri uliyonayo kahela ketu kako wapi? Naomba hapa kahela haka kapatikane, watu hawa wapewe chao, watu hawa wajijue na kahela kao haka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesimamisha kupandisha vyeo vya walimu kwa sababu tulikuwa tunashughulikia watumishi hewa, tumesimamisha mishahara iliyokuwa imepandishwa ikarudi ili tumalize jambo la watumishi hewa, hata haka ka kusimamia mitihani na kenyewe kanasimama, hapana! Naomba sana walimu hawa walipwe fedha zao ili waweze kufanya kazi yao kwa juhudhi wakiwa wanajua kwamba Serikali inawapenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ya mwaka jana iliandikwa barua TAMISEMI kwenda kwenye Halmashauri zote walimu wapya walioajiriwa fedha zao zile Halmashauri zichukue kwenye akaunti yoyote pesa zilipe nauli. Wilaya ya Bukombe shilingi milioni 58 zilichukuliwa ni fedha za wakandarasi zikalipa nauli walimu wapya waliokuwa wameajiriwa, zikalipa subsistence allowance kwa ajili ya walimu wale wapya, fedha hizo hazijalipwa, wakandarasi wanatafuta hela, Halmashauri inahaha ipate wapi pesa ya kuweza kuwalipa wakandarasi hawa. Halmashauri hii ikitakiwa na ambavyo hatuna fedha imani yangu ni kwamba hatuwezi kutoboa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba TAMISEMI kwa barua ile mliyoandika ya kwamba wachukue fedha kwenye akaunti yoyote mtarudisha, rudisheni hizi fedha sasa hivi Halmashauri kule hali ni mbaya. DT hata kukaa kwenye kitinana shida, Mkurugenzi kukaa kwenye kitinana shida kwa sababu wakandarasi hajui watakuja kwa wakati gani. Naomba Wizara ya TAMISEMI tuhakikishe kwamba madai haya tunayashughulikia haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo lililosemwa hapa na watu kwenye Waraka tmezungumzia asilimia kumi ya vijana na akina mama, naomba hili jambo tuanze...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa Mheshimiwa Vedastus Mathayo, Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hizi dakika tano japo ni chache sana nitajitahidi kwenda katika *point form*. Kwanza kabisa niseme kwamba naunga mkono taarifa zote mbili za Kamati ya PAC na LAAC. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa nichangie kwanza kabisa kwenye misamaha ya kodi. Tumekuwa tukiongea kama Bunge na kuishauri Serikali kwamba walau misamaha ya kodi iwe angalau chini ya asilimia moja ya Pato la Taifa. Ujisoma taarifa ya PAC utaona kabisa wameainisha misamaha ya kodi isiyokuwa na tija kwenye Taifa letu na mbaya zaidi inatolewa kwenye makampuni mengine ambayo hayana leseni, mengine wanasema yameghushi. Sasa swali hapa ambalo tungetaka tujue hawa watu ambaao wamepewa hizi fedha, Serikali imechukua hatua gani, wameshazirudisha na kwa wale watendaji ambaao waliidhinisha hii misamaha ya kodi ilhali watu wameghushi nyaraka, leseni zime-expire na mambo mengine wamechukuliwa hatua gani? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni suala zima la madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Siku Mheshimiwa Rais anaongea na wanahabari alisema kabisa kwamba mifuko hii inafilisika kikubwa ni kwa sababu wanasiassa na mbaya zaidi akasema Wabunge sisi ndiyo tunafilisi mifuko hii kwa sababu tumekopa. Kwenye ripoti hii ya PAC imeanisha kabisa zaidi ya shilingi trilioni 1.5 Serikali inadaiwa na Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea kuna wafanyakazi fedha zao hazijapelekwa kwenye mifuko husika, kwa mfano, Askari Magereza na Polisi na wafanyakazi wengine tangu mwezi wa nne mpaka sasa hivi makato yao hayajaenda kwenye mifuko husika. Sasa tunauliza ni kwa nini Hazina wasipeleke hizi fedha za michango kwenye mifuko husika? Yaani mnakopa kwenye michango ya wafanyakazi bado mnakopa kwenye uwekezaji halafu Rais anauambia umma kwamba Wabunge ndiyo wamefilisi mifuko ya jamii, *is he serious?* (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, tumekuwa tukilalamika kuhusu kukaimishwa kwa watendaji kwenye mashirika ya umma lakini pia imekithiri kwenye Halmashauri zetu. Ni wakati sasa Serikali ione umuhimu wa either kuwajiri watu wenye uwezo kwenye vitengo mbalimbali, kwa mfano kwenye

Halmashauri yangu ya Mji wa Tarime mara nyingi nimekuwa nikimfuata Waziri husika, kuna watendaaji wanakaimu kule, ufanisi ni zero, Halmashauri inakuwa haiwezi ikafanya vizuri. Naomba kabisa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ufanye juhudhi na wale wengine ambao wanasimamia mashirika mbalimbali tusiwe tunakaimisha hizi nafasi inapunguza ufanisi wa kufanya kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 20 za ruzuku ambazo zinatakiwa kwenda kwa Serikali za Mitaa na Vijiji. Tumekuwa hata tukiuliza maswali humu ndani, wale Wenyeviti wa Mitaa hawalipwi posho, unakuta hata hawana stationary kwa hiyo wanashindwa hata kufanya kazi. Fedha ambazo mnapeleka kule kwenye Halmashauri haziwafikii Serikali za Mitaa au za Vijiji. Tunaomba sasa Wizara husika muweze kuwa na ufuatiliaji kama ni ripoti inakuwa inatolewa kuhakikisha kwamba hizi asilimia 20 kweli zinatengwa au hazitengwi na kama hazitengwi ni kwa nini zisiende kule chini na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kinahuzunisha zaidi ni zile asilimia kumi kwa ajili ya vijana na wanawake. Kikubwa hapa kinakuja unakuta Halmashauri haina mapato, fedha wanazokusanya wanapeleka sehemu zingine. Kwa hiyo, hii ipo tu kwenye makaratsi kwamba wanawake wanapewa asilimia tano na vijana wanapewa vijana asilimia tano lakini kiuhalisia hakuna. Mfano kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Tarime hiyo kitu haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kwamba vyanzo vya mapato ni vichache, lakini kingine mnaelekeza kwamba fanya kitu fulani kwanza, kwa hiyo, priority ya kutoa fedha kwa ajili ya Mfuko huu kwa ajili ya vijana na wanawake haipo na hii inakuwa inayumbisha. Tunaomba sasa utiliwe mkazo kama nilivyopendekeza kwenye ruzuku ya asilimia 20 na kwenye hii ruzuku ya asilimia kumi ya vijana na wanawake napo Serikali kuititia Wizara husika wahakikishe wanawake na vijana wanaenda kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka nizungumzie...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Esther. Sasa zamu ya Mheshimiwa Vedastus Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hizi hoja zote mbili za Kamati. Nijikite zaidi katika taarifa hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Na mimi nakubaliana kabisa na Kamati ya LAAC kwa changamoto ilizoziona mojawapo ikiwa ni pamoa na baadhi ya Halmashauri kutochangia kabisa ule mfuko wa

vijana na akina mama. Pia Halmashauri kutopeleka fedha kwenye kata na vijiji na uzembe wa ukusanyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tutambue tu jambo moja kwamba mwaka jana ndiyo tulikuwa na uchaguzi na zaidi ya asilimia 70 ya Madiwani ni wapya lakini na hawa Wakurugenzi ni kweli kwamba zaidi ya asilimia 50 ni wapya, kwa hiyo, hata ile namna ya usimamizi wa fedha ni tafizo.

Kwa hiyo, nadhani cha kwanza kinachopaswa kufanyaika hawa Madiwani pamoja na Wakurugenzi wanahitaji kupata mafunzo ambayo yatawasaidia au litawawezesha kuwa na udhibiti na usimamizi mzuri wa hizi fedha zao. Pia hii itasaidia kuondoa ile migongano iliyopo kati ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwa sababu hawa Madiwani wanajua majukumu yao lakini na Mkurugenzi naye atakuwa anajua majukumu yake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka hata sisi Wabunge tulipokuja humu Bungeni bado tulipata orientation. Sasa leo inakuwaje hawa Wakurugenzi wapya wanachaguliwa wengine kutoka maeneo ambayo hawajawahi kuhusika kabisa na masuala ya uongozi halafu wanafika wanapewa majukumu na tunategemea kwamba wanaweza ku-perform. Kwa hiyo, nadhani hiyo ni dosari ya kwanza pamoja na kwamba Serikali inabana matumizi lakini ione uwezekano wa kuendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya Madiwani na hawa Wakurugenzi ambao ni wapya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la makusanyo kuchukuliwa na Serikali, ukiangalia kwenye ile Sheria Na. 7 na Na. 8 zilizounda Halmashauri za Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya ilikuwa inasema wazi kwamba lengo la Serikali ni kuzijengea Halmashauri uwezo ili ziweze kuijendesha.

Sasa mimi naijuliza kama tunafika mahali tunachukua vyanzo vya Halmashauri tunavirudisha Serikali Kuu huko ndiko kujengenya ile Halmashauri uwezo? Kwa hiyo, tunadhani kwamba huu utaratibu wa Serikali Kuu kuona kwamba kuna chanzo hapa ambacho inaweza ikakusanya zaidi ikachukua halafu tukaiacha Halmashauri, halafu tunarudi kuilaumu kwamba haikusanyi wakati huo hata zile fedha ambazo tumeahidi tunapeleka hatuwapelekei mimi sidhani kama tunatenda haki hata kidogo. Kwa hiyo, nadhani tuna kila aina ya sababu ya kuendelea kuzijengea uwezo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mapato yote au kodi zote ambazo zinadaiwa na Serikali Kuu ni za lazima yaani ukiletewa barua na Serikali Kuu kwamba kodi hii unapaswa ulipe, unapewa siku tofauti na hapo ni kwamba hatua kali zitachukuliwa. Ndiyo maana ukiangalia TRA wanapoenda kukusanya mapato yao wanaandamana na polisi, lakini ukiangalia hawa Halmashauri

ambao tunategemea wakusanye siku zote mapato yao ni ya ku-negotiate yaani ni majadiliano na sana akiwa na askari atumie askari mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo ni dhahiri kwamba haya mapato tunayotegemea kutoka kwenye Halmashauri haziwezi ku-perform kwa asilimia tunayotegemea kwa sababu mapato ya Halmashauri inaonekana ni hiari lakini mapato ya Serikali Kuu hayo ni lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo nalo lazima tuliangalie na tuone kwamba ni kwa kiasi gani tunaweza kuzijengea uwezo hizi Halmashauri au Serikali za Mitaa ili ziweze kuijendesha zenyewe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni maslahi ya Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Madiwani. Nadhani hilo tunatakiwa kuliangalia zaidi ili nao waweze kujisikia kama viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuatiwa sasa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Subira Mgali ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kupata nafasi walau dakika tano hizi niseme machache ambayo nadhani yanaweza kutusaidia kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuungana na mapendekezo ya Kamati zote mbili nikiamini kwamba ni moja ya maeneo muhimu sana ambayo kama Serikali itayafanya kazi tunaweza kupiga hatua ambayo tunitarajia. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninavyofahamu mimi suala la ukaguzi, katika Halmashauri zetu, Taasisi zetu na maeneo mbalimbali ambayo kwa kweli CAG anapaswa kufanya kazi huko zinasaidia kuimarisha utendaji bora na matumizi bora ya fedha za Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na uimarishaji huo, kama Kamati hizi mbili kama ambavyo zote zimesema haziwezi kupewa nguvu ya kufanya kazi ya kwenda *field* na kukagua kilichopo itakuwa bado ni sawa na kupiga *mark time*. Sababu moja kubwa ya msingi, kupata Hati Safi hakumaanishi yale yote yaliyofanyika yana ubora wa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunaamini kupata Hati Safi ni uandishi mzuri wa vitabu, lakini Kamati zinapokwenda field zinakutana na vitu tofauti; toka asubuhi Wabunge wameongea hapa. Sasa tunafikiri upo umuhimu, tunaamini kwamba, mambo haya yakifanyika vizuri sina shaka tutakuwa tumefikia malengo ambayo yametarajiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi, limezungumzwa suala la miradi kutokamiliika kwa wakati. Naamini katika Halmashauri zote nchini miradi mingi sana ilianza. Hapa imetajwa miradi ya maabara, ikaja ya miradi ya vituo vya afya, zahanati, madarasa na kadha wa kadha. Vyote hivi, kama haviwezi kupelekewa fedha kwa wakati ni lazima tutakuwa tunakutana na hoja za ukaguzi mara kwa mara na hatuwezi kufikia malengo kwa kweli ambayo wananchi wanatazamia kuyaona sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Fedha za Mfuko wa Vijana na Wanawake; liko tatizo na mimi sina shaka Mheshimiwa Simbachawene atakuwa analifanyia kazi suala hili vizuri akishirikiana na Mheshimiwa Jenista kwa sababu moja tu ya msingi kwamba, fedha hizi imekuwa ni tabia, fedha hizi imekuwa ni mazoea, hazitoki kadri sheria inavyosema na Wakurugenzi wamefanya kama fedha hizi ni za miradi ya kwao pekee yao, si fedha za Serikali kwa mujibu wa sheria. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ningeomba uwekwe utaratibu tena ikiwezekana kwa maandishi kuvisitiza sheria hii kwamba ikiwezekana kila mapato ya mwezi yanayopatikana hata kama vitakuwa vinapata vikundi vitano mpaka 10, lakini mwisho wa mwaka watakuwa wana kiasi kikubwa ambacho wameshakitoa na itakuwa inaonesha uhalsia wa kile tunachokizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa ambao sisi tunaotokana na Chama cha Mapinduzi tumetoa ahadi nyingi na ahadi hizi kwa vikundi mbalimbali ambavyo vimeshaundwa kama haziwezi kutekelezeka bado tutakuwa hatuna maneno mazuri ya kuwardhisha wananchi hawa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye Kamati ya PAC yapo mambo mengi hapa yamezungumzwa na muda uliopita huko nyuma tulisema hapa, kwamba pamoja na CAG kupisha bajeti ambayo tumeipitisha kwenye Bunge hili, lakini ipo miradi, kwa mfano ipo mikataba mikubwa, mikataba ambayo kipato chake tunaamini ni mgawanyo wa Taifa hili. Kwa hiyo kama hatutaweza, kwa mfano, mikataba ya gesi, CAG asipoweza kwenda kukagua huko na haya tunayoyaona bado hatuwezi kuona kile ambacho tunakitarajia miaka 10, miaka mitano ijayo katika kuhakikisha tunamsaidia Tanzania huyu ambaye ni maskini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni juu ya Kamati kushindwa kufanya kazi. Kamati hizi haziwezi kufanikiwa, Kamati hizi haziwezi kuleta matunda chanya kwa sababu kama nilivyosema, upatikanaji wa Hati Safi ni uandishi bora wa vitabu. Wako wahasibu mabingwa wa kuandika vitabu vizuri. Tutaendelea kusifia Hati Safi lakini miradi kule nyuma ni hewa, miradi haitekelezeki, miradi imekufa. Ni lazima tuhakikishe Kamati hizi zinakwenda kukagua miradi ambayo tunadhani imetumia fedha nyingi za Serikali na kodi ya wananchi pia katika kuhakikisha tunamsaidia Mtanzania huyu ambaye ni maskini na mnyonge. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa sababu ya muda; suala la PSPF, fedha nyingi bado hazijalipwa, tunafahamu Serikali imejiwekea mkakati wa kulipa zaidi ya bilioni 150...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha!

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru na naunga hoja mkono. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalo, Mheshimiwa Seleman Jafo ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia hii nafasi. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapa hongera Kamati zote mbili kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuchangia juu ya asilimia 10 ya fedha za akinamama pamoja na vijana. Ni kweli Halmashauri nyingi hawapeleki fedha hizi kwa kina mama. Ningeshauri kuwa hizi asilimia ziwe zinapelekwa kwa akinamama kusudi waweze kufanyia biashara zao na vijana pia waweze kufanyia kazi zao kwa sababu hizi fedha zinasaidia katika ajira. Watanzania wote tunafahamu kuwa ajira ni matatizo sasa hivi, kwa hiyo, hizi fedha zingesaidia kwenye ajira ya akinamama pamoja na vijana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwa Serikali kuwa walismamie kusudi hizi fedha ziweze kupelekwa kwa walengwa ambao ni akinamama pamoja na vijana. Pia na mimi naongelea kuhusu hii asilimia 20 ya ruzuku ya Serikali Kuu kutopelekwa kwenye vijiji pamoja na mitaa. Naungana pamoja na Kamati kama inawezekana zipelekwe moja kwa moja kwenye vijiji pamoja na mitaa yetu, kwa sababu hazipeclekwi kwenye Halmashauri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea kuhusu fedha za maendeleo ambazo kusema ukweli zinachelewa kupelekwa na wakati mwingine hazipeclekwi kabisa. Tunawalaumu kweli Wakurugenzi, lakini unakuta kuwa hizi fedha wakati mwingine hazipeclekwi kiasi kuwa miradi inasimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama bado wanateka maji kwa sababu miradi ya maji bado haijaendelezwa. Barabara zimesimama huko kwenye Halmashauri zetu kwa sababu fedha hazipo, vituo vya afya pia vimesimama; kiasi vingeweza kuboresha na kupunguza vifo vya akinamama pamoja na watoto; lakini kwa sababu fedha za maendeleo hazipeclekwi na wakati mwingine hazipeclekwi kwa wakati na wakati mwingine hazipeclekwi kabisa. Nashauri Serikali iliangalie jambo hili la kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu Mfumo wa EPICOR. Ni kweli Halmashauri nyingine bado hawajajua vizuri kutumia mfumo huu wa EPICOR kiasi kwamba inaleta hoja kwenye mahesabu. Kwa hiyo, Halmashauri hizi ambazo bado hawajajua kutumia mfumo huu wa EPICOR, naomba sana waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani. Mapato ya ndani naomba Halmashauri waweze kusimamia. Imegundulika kwenye Halmashauri nyingi kuwa mapato ya ndani hayakusanywi kama inavyokusudiwa. Kwa hiyo, vyanzo vilivyopo pamoja na vyanzo vipyta, Halmashauri waweze kusimamia kusudi iweze kukusanya kama inavyokusudiwa; kusudi miradi ya maendeleo iweze kutimilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mafunzo kwa Wakurugenzi. Ni kweli Wakurugenzi wengi wapya kweli hawajajua vizuri kazi zao. Nami naungana na Kamati kuwa waweze kupewa semina ya jinsi ya kufanya kazi zao ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukaimu; nimekaa huko kwenye mikoa na kweli kukaimu kwa muda hakuna tija. Naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI iliangalie hili, kama mtu ameshakaimu kwa muda mrefu aweze kupitishwa kusudi aweze kushika Idara moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameshaongeleta, kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema kuhusu Walimu wa sayansi. Imeonekana kuwa Walimu wa sayansi ni tatizo kubwa, hivyo naomba sana liangaliwe, Mheshimiwa Waziri wa Elimu naomba iliangalie suala la Walimu wa sayansi liweze kushughulikiwa kusudi tuweze kupata Walimu hao, no science, no development. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Subira Mgali atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo; Mheshimiwa Olenasha ajiandae. Mheshimiwa Selemani Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa upande wangu kwanza, nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha leo hii tunajadili hoja muhimu sana za Kamati, lakini kubwa zaidi nipende kuzipongeza Kamati zote mbili.

Kamati hizi mbili zote zilizowasilisha hotuba zake hapa zimetuonesha kwamba, ni jukumu gani tunatakiwa tulifanye katika kipindi hiki cha sasa baada ya kupata ripoti hizi zilizofanyika mwaka 2014 na 2015. Tukiwa mwaka 2016 sasa, kama Wabunge na kwa ujumla kama Serikali tujue tutafanyaje ili wananchi waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika Kamati ya LAAC. Naomba nimpongeze Mwenyekiti na timu yao yote ambayo katika njia moja au nyingine, wao wanatusimamia zaidi kwa karibu katika ofisi yetu. Naomba nikiri wazi kwamba, maelekezo waliyoyatoa kwetu sisi na kaka yangu Boniface Simbachawene tumepata viongozi ambao wanatushauri ili kazi yetu iweze kufanyika vizuri katika kipindi cha sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja mbalimbali lakini zote zina mashiko. Hoja ya kwanza ilikuwa ni suala zima la Sheria ya Manunuzi na kweli ukifuahtilia ripoti ya Mkaguzi na hali kadhalika Kamati ilivyofanya uchambuzi mbalimbali ilibainika kwamba kuna changamoto kubwa sana na kutoa maelekezo nini tukifanye. Katika hili, ofisi yetu imeshaanza kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza tumetoa maelekezo katika Halmashauri zote; kwa vile tuna watendaji katika ngazi mbalimbali wengine wakiwa wapya, wahakikishe katika utiifu wa utendaji wa kazi zao, jambo la kwanza wanazingatia Sheria ya Manunuzi ili kuleta tija katika Halmashauri zetu. Hata hivyo, ukifuahtilia ile ripoti imeonesha maeneo mbalimbali ambayo watu walifanya mambo ya hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikwambie na nilijulishe Bunge lako kwamba, katika eneo hili tumechukua hatua mbalimbali. Katika Halmashauri mbalimbali baadhi ya Wakurugenzi wamepoteza nafasi zao, lakini baadhi ya Wakuu wa Idara waliobainika, wameweza kuchukuliwa hatua mbalimbali na hivi sasa wengine wamepelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili katika ofisi yetu hatutavumilia kabisa, wale wote ambao wameonekana ni kikwazo ambao kwa njia moja au nyingine wamehujumu fedha za Serikali na sisi tukiwa tumepeewa dhamana

katika eneo hilo; naomba tulihakikishie Bunge lako kwamba, ofisi yetu imejipanga hivi sasa tutafanya marekebisho makubwa sana na ndiyo maana nimesema kwamba, Kamati imeibua jambo hili ambalo ni jema, ni maelekezo na sisi tunakwenda kulifanyia kazi.

Suala lingine ni Udhafu Katika Usimamizi na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Ni kweli, Kamati ilibaini kulikuwa na udhaifu mkubwa sana katika maeneo mbalimbali, lakini katika eneo hili kulikuwa na marekebisho ya kimuundo kidogo baada ya kupitia hizi hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ofisi yetu hivi sasa kuna Kitengo Maalum cha Ufutiliaji ambacho kinafuatilia maeneo mbalimbali katika jitihada za kuhakikisha kwamba miradi hii iweze kutekelezeka vizuri, hasa kwa fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, jukumu lake kubwa vilevile ni kuhakikisha kwamba inatoa ushirikiano wa karibu zaidi na Ofisi ya CAG na Kamati ya LAAC. Ndiyo maana katika kipindi chote cha mijadala baadhi ya wawakilishi wa kitengo hiki walikuwepo katika mijadala hii kwa ajili ya kutoa ufanuzi wa jinsi ya kufanya katika maeneo mbalimbali ili yaweze kuleta tija katika eneo letu la kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika suala zima la ufuatiliaji, Waziri wangu hapa alitoa maelekezo mbalimbali hata kule Kigoma na Kasulu na baadhi ya watu katika maeneo mbalimbali walichukuliwa hatua za kinidhamu mara baada ya kubainika kwamba baadhi yao walishindwa kutimiza wajibu wao wa kikazi waliopewa. Katika taarifa mbalimbali hivi sasa, ukisoma racket news, ukiangalia kule Kinondoni, Kondoa, Kahama, Kigoma-Ujiji na maeneo mengine mbalimbali baadhi ya watu wamechukuliwa hatua. Hii ni kwa sababu tunatekeleza lile ambalo limeonekana kwamba lilikuwa ni changamoto kubwa sana katika ofisi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu kulinda rasilimali hizi za wananchi ili ziweze kuleta tija katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja inayohusu uzembe katika kusimamia Mifumo ya Makusanyo ya Mapato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja umalize.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika hilo na ndiyo maana tumefanya kazi kubwa sana. Wakati tunaingia pale na kaka yangu Boniface Simbachawene Halmashauri zilizokuwa zinakusanya kwa kutumia mifumo ya kielekitroniki zilikuwa chini ya asilimia 30; leo hii tumefikisha karibuni asilimia 92. Hata hivyo, tumetoa maelekezo mbalimbali katika zile Halmashauri mpya ambazo hazina *network* hasa za umeme na tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha tunafikia lengo la asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini, maelekezo haya ya Kamati tuna kazi kubwa tunayoifanya katika ofisi yetu hapa na tutafika mahali pazuri na ndiyo maana leo hii Halmashauri mbalimbali zimeweza kukusanya karibuni mara mbili ya ukusanyaji wa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikushukuru sana, na kwa vile nina ufinyu wa muda, nipende kushukuru. Kubwa zaidi ni Kamati iliyotusaidia na naomba tukiri katika Kamati hii kwamba, ofisi yetu itajitahidi kutekeleza maelekezo yote kwa mustakabali wa nchi yetu ambao tunajua ndiyo tija wanayoitarajia wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa William Olenasha, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage halafu Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza sana Kamati za PAC na LAAC kwa kazi waliyofanya kwa sababu kimsingi kupitia kwao Bunge limeendelea kufanya kazi yake ya Kikatiba ya kuvisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya PAC ilijadili na kutoa ushauri kuhusu upotevu wa fedha katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula NFRA kutohana na mahindi yaliyoharibika. Kimsingi walishauri kwamba, namna mojawapo ya kuhakikisha kwamba hilo tatizo halijirudii tena ni kutoa fursa kwa wakulima kuza mahindi nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na Wizara imelichukua pendekezo hili na kimsingi kwa sasa hatuzuii wafanyabiashara kipeleka mahindi nje, lakini napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, tunaruhusu chakula kipelekwe nje kulingana na ziada au hali halisi ya chakula ndani ya nchi. Kwa hiyo kuna wakati tunalazimika kupunguza kiwango kinachoenda nje si kwa sababu hatutaki wakulima wetu wanufaikie na biashara ya chakula, lakini ni kwa sababu tunatanguliza maslahi mapana ya nchi ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miezi ya hivi karibuni mnafahamu kwamba, tumekuwa tukichukua hatua kadhaa ili kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usalama wa chakula kwa sababu majirani zetu hali yao si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge pale unapoona kwamba, kuna kidogo kupunguza kasi ya kupeleka nje, mfahamu si kwa sababu hatutaki wakulima wetu wauze chakula nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendeleko na ushauri mwingine ambao Serikali imeupokea ni kwamba, Wakala (NFRA) wajenge maghala kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika bajeti ambayo tunaitekeleza Wakala una mpango wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kutoka tani 246,000 hadi kufikia tani 496,000 kwa sababu tuna mpango wa kujenga vihenge vyenye uwezo wa tani 190,000, lakini vilevile maghala yenye uwezo wa tani 60, 000. Vihenge na maghala hayo yatajengwa Babati, Dodoma, Shinyanga, Makambako, Mbozi, Songea, Sumbawanga na Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja ya Kamati ya PAC, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa vilevile ya kuzungumza baadhi ya masuala ambayo ningependa kuyatolea ufanuzi. Mheshimiwa Omary Mgumba pamoja na Mheshimiwa Aeshi Hilaly walizungumzia sana kuhusu wafanyakazi wa NFRA waliosimamishwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutumia fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, ni kweli kuna wafanyakazi wanne wa ngazi ya juu wa NFRA ambao wamesimamishwa kazi. Nisingependa kuzungumzia kwa undani kuhusu suala hilo kwa sababu tayari Wizara imeunda tume ili kuchunguza tuhuma ambazo zinawakabili na kimsingi itakuwa prejudicial, hatutawatendea haki tukianza kulijadili Bungeni na hata wale wanaofanya uchunguzi nao vilevile, si vizuri wakaingiliwa wakati bado wanaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maelezo kidogo tu ni kwamba, wafanyakazi waliosimamishwa, tuhuma yao si hiyo tu inayosemekana na Waheshimiwa Wabunge, kuhusu uharibifu wa mahindi. Uharibifu wa mahindi ni moja tu kati ya masuala mengi ambayo tume ya Wizara iliyoundwa inachunguza. Kuna masuala kuhusu uuzaji wa mahindi; kuna malalamiko ambayo yanachunguzwa katika mchakato mzima wa kuuza mahindi, lakini vilevile kuhusu fedha zinazotokana na uuzwaji wa mahindi yenyewe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachosema tu ni kwamba, tuvute subira, taarifa ikiwa tayari Waheshimiwa Wabunge mtataarifiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha; atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nizipongeze Kamati zote na Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili taarifa hizi. Kuhusu Wizara yangu katika kitabu cha PAC ukurasa wa 63 mpaka 68 imezungumziwa NDC.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo machache ya kuzungumzia kuhusu NDC; niwakumbushe kwamba hili ni shirika la kimkakati lilioanzishwa na Mwalimu mwaka 1965, na katika ujenzi wa uchumi wa viwanda NDC tumeipanga kwamba ile miradi ya kimkakati ndiyo itashughulikiwa na NDC. Kumbe wakati tunahamasisha sekta binafsi kujenga viwanda, miradi ya kimkakati itakuwa inashughulikiwa na NDC.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba hatujaweka mtaji wa kutosha ndani ya NDC kama ilivyokuwa mwaka 2015, lakini mipango inapangwa kulingana na kila mradi. Kwa mfano, unapozungumzia mradi wa Engaruka, unautambua mradi, lakini huwezi kuwekea pesa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri, tunayo miradi mingi kwa sababu NDC kazi yake ni kutambua fursa, kutambua maeneo ambayo wafanyabiashara wa kawaida hawawezi kwenda. Kwa mfano tunapozungumzia Mtwara Corridor, ni kazi yake kuitambua na kuitangaza. Tunapozungumzia TAZARA Corridor, ni kazi ya NDC kuitambua na kuitangaza ili hiyo sekta binafsi, iwe ya ndani au ya nje iweze kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee limezungumzwa suala la Mchuchuma na Liganga. Nirudie tena, kila mtu anapenda Mchuchuma na Liganga ifanye kazi na Kamati imezungumza maneno mazuri, kwamba hatufanyi maamuzi, wakati wa maamuzi ni sasa na dhamana hiyo iko chini yangu mimi. Nimeagizwa niandike andiko nipeleke kwenye mamlaka na mamlaka itaamua, nillisema mara ya kwanza na Mheshimiwa Deo alinifuata hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema, Mheshimiwa Deo na Waheshimiwa Wabunge, Mchuchuma na Liganga maamuzi yake yanatoka sasa, nitapeleka andiko kwenye mamlaka na mamlaka itaamua na mamlaka inataka Mchuchuma na Liganga iweze kuanza. Kwa sababu Mchuchuma na Liganga ikianza ni kwamba ndiko ile reli ya Mtwara unaweza kuijenga kwa sababu kutakuwa na mzigo mkubwa wa kusomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tuna potential ya watu 5,000, lakini tuna potential ya kutengeneza megawatt 600 za umeme ambazo haziathiriwi na tabia nchi. Nina uhakika bila kuwa-preempt wanaofanya maamuzi kwamba nitakapokwenda mbele yao na sababu hizo, Mchuchuma na Liganga tutafanya maamuzi na kuondoa mambo mawili, matatu ambayo yamekuwa yakiwafanya watu wasifanye maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala la General Tyre na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge mmezungumza maneno mazuri, mmezungumza maneno mazuri kuhusu UDA.

Mheshimiwa Naibu Spika, General Tyre ninayo mimi; zimeelezwa pesa zilizotumika, mimi ndiye niliyezua kwamba General Tyre hatuwezi kuendelea kuipa bilioni mbili, mnieleze tunahitaji kiasi gani kuweza kuifufua na kuiendesha. Nimelishikilia mimi, nimeweka timu inafanya survey, watanieleza twende vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa na uhakika na kitu ambacho nitakifanya General Tyre tutaiendeza. Tunataka kutengeneza kiwanda cha matairi kwa sababu ndiyo kitakuwa sifa ya nchi hii, tunataka kutengeneza shirika kubwa litakalolipa ushuru mwingi, tunataka kutengeneza shirika kubwa litakalowaajiri watu wengi, lakini tunataka kutengeneza shirika kubwa litakalochochea wakulima wa mpira ili watu wanaolima mpira waweze kupata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, yametajwa mashamba ya mpira yaliyopo Muheza na Morogoro; mvute subira. Kwa sababu tutakuwa na uhakika wa soko la mpira tutakuwa na uhakika sasa wa kuwaambia wananchi waweze kulima zaidi, na mpango wetu sisi ni kuyatumia yale mashamba ya NDC kama *nucleus farm* na kama *road base*, lakini tutawahamasisha wananchi watumie *outgrowers* kuweza kuzalisha mpira zaidi kwa ajili ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vilevile kwa mradi wa Engaruka, nimetengewa bilioni 1.7, lakini ninachopigana nacho ni kuangalia nani atakwenda kuwekeza pale. Pia imeelezwa kwamba NDC anashindwa kufanya *feasibility study*, anawategemea wawekezaji. Jambo la muhimu tunafanya ni kutafuta vijana wazuri wanaoweza kwenda sambamba na wale wawekezaji ili kufanya *feasibility study*. Si jambo la ajabu, hata kwenye petroleum industry tunafanya hivyo, jambo la muhimu ni kuwa-monitor wanafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, ushauri wao ni mzuri na tutauzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Boniface Simbachawene ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami niwapongeze Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati zote mbili kwa kazi nzuri, kwa kweli kazi yao ni kwa ajili ya kuimarisha uwajibikaji na matumizi adili ya rasilimali za umma na hili halina budi kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kwa upelekaji wa fedha, niseme tu kwamba nafikiri hili ni tatizo la kimfumo kwa sababu kwa sasa kwa kweli chanzo kimoja tu cha fedha (upande wa kodi) ndicho kinachofanya vizuri wakati vyanzo vingine havifanyi vizuri na kama havifanyi vizuri tunapo-disburse kwa kutegemea kilichokusanywa huwezi ukazipeleka kama inavyotakiwa kama vyanzo vingine havifanyi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji wa fedha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa hasa zile za maendeleo; niruhusu tu niseme kwamba, Serikali kuanzia mwezi Julai mpaka Oktoba tuliweza kutoa Shilingi bilioni 177.3 ambayo ni asilimia 14.3 ya bajeti iliyoidhinishwa. Naomba niliambie tu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia mwezi huu wa Novemba Waheshimiwa Wabunge wategemee mtiririko ambaao ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulipa deni la PSPF na madeni mengine ya ndani; naomba niseme tu kwamba Serikali inaendelea na uhakiki wa madeni haya. Tulishakamilisha uhakiki wa deni la PSPF na sasa tunaendelea kuweka utaratibu wa kukamilisha uhakiki wa Mifuko mingine yote ili tuweze sasa kutoa ile hati fungani ya Serikali na kuweza kuyalipa na mtakumbuka kwamba tumetenga bilioni 150 katika bajeti hii kwa ajili ya kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madeni ya ndani, niseme tu kwamba tumeanza kulipa na nilishaeleza Bunge lako Tukufu kwamba hadi sasa katika quarter hii tumeshalipa shilingi bilioni 187.5 kwa ajili ya madeni ya wakandarasi mbalimbali, wazabuni na madeni ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukusanyaji wa property tax; naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba hadi sasa TRA haijaanza kukusanya property tax kwa sababu ilikuwa ni lazima kufanya maandalizi ya msingi ya kisheria. Kwa hiyo, kwa mfano kutoa tangazo la Serikali, kazi hiyo imekamilika tarehe 30 Septemba, kuna kuandaa kanuni ambazo zinakamilishwa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kulikuwa na kuoanisha mifumo mbalimbali ya Serikali – Local Government Revenue Collection Information System na Property Rate Management System na kazi hii imekamilika mwezi Oktoba na sasa TRA imeanza kutoa zile ankara kwa ajili ya kudai property tax

kwa kipindi ambacho hakijalipwa. Kwa zile halmashauri ambazo hazitaanza kwenye mfumo huu zilishaelekezwa kuendelea kukusanya property tax kwa utaratibu wa kawaida mpaka hapo zitakapofikiwa na utaratibu wa kukusanya na Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kushughulikia kesi mbalimbali, TRA imefanya hivyo na hadi sasa Ofisi ya DPP imeshawateua Wanasheria 24 wa TRA kwa ajili ya kuendesha kesi hizo. Pia kufikia Aprili mwaka huu, kulikuwa na kesi 117 ambazo zilikuwa na kodi kubwa tu – bilioni 116 na hizi zimeshughulikiwa. Kati ya Aprili na Septemba kesi 63 zilitolewa uamuzi na kati ya kesi 66 tuliweza kushinda kesi 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TIB*; niruhusu tu niseme kwamba, hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu *TIB* ilikwishatoa notice kwa wateja wake 26 ambaao wana mikopo ya karibu bilioni 66, ila kati ya hao wateja watatu ambaao wana mikopo ya bilioni 24.7 wamekimbilia mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, yalikuwepo pia madai hapa kwamba *TIB* walikataa kutoa taarifa za wateja. Nafikiri sio kwamba viongozi wa *TIB* ni kiburi, lakini sheria inawazuia kufanya hivyo. Kifungu cha *Banking and Financial Institutions Act* ya Mwaka 2006, section ya 48 under the fidelity and secrecy section, inamzuia mtu ye yote kutoa siri za wateja na kufanya hivyo ni kosa, ukifanya hivyo unatakiwa ulipe faini ya si zaidi ya Shilingi milioni 20 au kufungwa kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote. Kwa hiyo, nadhani hiyo ndiyo sababu ya msingi na si kwamba ni ukaidi wameinyima Kamati hiyo taarifa za wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilisemwa pia kuhusu mfumo wa *IPSAS Accrual Basis*; niseme tu kwamba, Serikali inaendelea kujitahidi kutekeleza mpango kazi ambaao una-cover miaka mitano ili kuweza kuhakikisha kwamba Mfuko huu unatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi; ni ushauri mzuri na TRA imekwishaanza kuchukua hatua na niseme tu kwamba udhibiti wa misamaha ya kodi umeongezeka na Mameneja wa Mikoa wa TRA wamepewa maelekezo mahususi kuweka kipaumbele katika kudhibiti misamaha hii. Zile kampuni ambazo zilitumia misamaha vibaya, kampuni hizo zilizotajwa kwenye taarifa ya CAG zimeanza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kuhusu zile bilioni takribani 99 ambazo zinasemwa zilirudishwa Benki Kuu; hizo zilikuwa ni exchequer issues na sio fedha taslimu ambazo zilirudishwa Benki Kuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mpango, dakika moja umalize.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nimeeleweka, nakushukuru. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jenista atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hizi, lakini kwa namna ya pekee niwapongeze Wajumbe wa Kamati zote mbili kwa ushauri wao kwa Serikali. Niendelee tu kusema kwamba Serikali hii sikivu itaendelea kusikia na hakuna shaka lolote na wale wenye wasiwasi naomba waondoe tu wasiwasi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwanza na la Mheshimiwa Paresso kuhusu kuunganisha Mifuko. Ningependa tu kusema suala hili Mheshimiwa Paresso wala asifikiri kwamba yeye ndio analianzisha leo hapa Bungeni. Kama alikuwa anasikia vizuri Mheshimiwa Paresso tukubaliane kwamba Mheshimiwa Rais alishatuagiza siku ya Mei Mosi akatuambia ni lazima tufikirie sasa kuunganisha hii Mifuko, kwa hiyo ushauri wake ni mzuri sana unaendana pia na agizo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Paresso tuko pamoja na Mheshimiwa Rais alishaagiza suala hili, kwa hiyo, tutalitekeleza tu na tunaendelea na mchakato huo wa kutekeleza agizo hili la Rais pia la kuunganisha Mifuko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kukopesha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo. Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme hivi, Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inaongozwa na sheria. Kwanza Mifuko yenyewe ina sheria zake, lakini pia inasimamiwa na Mdhibiti wa Sekta hii ya Hifadhi ya Jamii, na mdhibiti anaongozwa na sheria ambayo tulitunga mwaka 2008, tukaifanyia marekebisho mwaka 2012 na tukaifanyia marekebisho mwaka 2013. Kifungu cha 9 cha miongozo ya uwekezaji kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kinaruhusu Mifuko hii kukopesha Vyama vya Akiba na Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama miongozo inaruhusu, kwa hiyo, Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inapokopesha SACCOS haifanyi makosa, labda makosa yawe mengine, lakini haifanyi makosa. Naomba Waheshimiwa Wabunge muelewe kwamba mahali pekee ambapo wanachama wanaweza kufaidika na Mifuko hii kupata mikopo yenyewe riba nafuu ni kupitia kwenye vyama vyao vya akiba na mikopo na watakapokopa fedha kwenye vyama hivi vya akiba na mikopo ndipo wanachama wanaweza kwenda kufanya shughuli

nyingine za uzalishaji na uchumi na kuwafanya waendelee kuwa wanachama sustainable kwenye Mifuko hiyo ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba suala la Mifuko kukopesha Vyama vya Akiba na Mikopo tusilipotoshe. Tuzungumze sekta nyingine kama walivyozungumza kwenye Kamati, lakini Mifuko hii inaruhusiwa kufanya hivyo. Tumeona kwamba sasa hivi tunataka kupanua wigo wa wanachama, hivi tunapopanua wigo wa wanachama kwenda kwenye sekta binafsi, vijana wetu waliopo katika sekta isiyo rasmi watafaidikaje na hifadhi ya jamii kama hawatapatiwa airisha la kukopa kwenye Mifuko hii? Kwa hiyo, naomba tuunge mkono juhudzi za mifuko kukopesha wanachama wake wakajenge nyumba, wakafanye nini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme, kama kuna tatizo katika utekelezaji wa jambo hili, hilo ndilo suala ambalo sasa Serikali ni lazima ikasimamie kuhakikisha kwamba vigezo vinafuatwa, lakini kuikataza Mifuko hapana, mwongozo uko hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista tafadhali, Mheshimiwa Ester Bulaya naona umesimama.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri Kivuli na dada yangu namheshimu sana. Hatuna tatizo na hii mifuko kukopesha...

**NAIBU SPIKA:** Tueleze kwanza unataka kufanya nini, ni utaratibu, ni taarifa, ni kitu gani?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa kwa sababu yeye anachangia na yeye hahitimishi hoja.

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu; tunachosisitiza kama Bunge, mionganii mwa SACCOS zilizokopeshwa, kwanza zilikopeshwa fedha nyingi kuliko mtaji walionao na hizo taarifa sisi tulipewa kwenye Kamati. Hata hivyo, mambo mengine ambayo yanaendelea katika mifuko ni aibu! PSPF kuna mtu anaitwa Manji, lile jengo la Quality Plaza Serikali mmeshindwa kumdati, anadaiwa bilioni saba, huu Mfuko unakwenda kufilisika, wewe Waziri ambaye unahusika na hii Wizara husika bado unaendelea kutetea haya!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka, fedha za...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester, naomba utoe taarifa yako; naona umemaliza, haya, Mheshimiwa Jenista Mhagama unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana mdogo wangu Mheshimiwa Ester, lakini angefuatilia ninachotaka kusema ni kitu gani na naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Esther, akifuatilia *Hansard* leo wapo baadhi ya Wabunge wachangiaji wamesema Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii isikopeshe fedha kwa wanachama kupitia mfumo wa akiba na mikopo. Sasa nataka kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba Mifuko ile haifanyi nje ya utaratibu na mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeendelea kusema hapa na naomba Mheshimiwa Esther anisikilize vizuri; kinachotakiwa kufanyika ni kuhakikisha kwamba mikopo hiyo sasa itolewe kwa kufuata taratibu na sheria zilizowekwa na zisigeuze utaratibu wowote. Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Esther, asichukulie udhaifu wa mtu mmoja kuwakosisha haki wanachama wengine wa mifuko, haitakubalika, sisi tutasimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Manji liko mahakamani, Serikali kupitia mfumo tumeshaanza kuchukua hatua na ni lazima tutaendelea kuchukua hatua hata kwa wakopaji wengine. Ninyi Waheshimiwa Wabunge mnajua, hata Mheshimiwa Ester anajua, mimi nina taarifa za NSSF hapa, kuna viongozi, hata kiongozi mmoja mkubwa wa chama fulani hapa ndani na yeye amekopa mkopo chechefu, hajarudisha! Kwa hiyo, tunapozungumza haya tuyaweke yote wazi, bayana, tusifichefiche vitu vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi, kifungu cha tisa (9) kama nilivyosema, kinaweka mfumo wa kukopesha Vyama vya Akiba na Ushirika lakini tunasema hivi, asilimia 10 ya rasilimali za uwekezaji kwenye Mifuko ndicho kigezo kinachowapa ruhusa ya kukopesha Vyama vya Akiba na Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa vyama hivyo vimeshakopesha kwenye vyama hivyo vya akiba na mikopo, mikopo isiyozidi hiyo asilimia 10 ya assets zilizopo. Sisi kama Serikali tutaendelea kusimamia na nina kuhakikishia watu wote waliokopa ni lazima warudishe hela kwenye Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, menejimenti zote ambazo zinafanya kazi kwenye Mifuko hii bila kufuata utaratibu Waheshimiwa Wabunge nawahakikishia Serikali tutaendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge sisi kama Serikali tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri mliotupa, tutafanya kazi na Bunge, lakini tutahakikisha kwamba sekta ya hifadhi ya jamii haitaweza kuhujumiwa na mtu yoyote na tutakuwa makini katika jambo hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu vizuri Mheshimiwa Waziri nadhani kwa sababu ulikuwa unajibu kwa hisia, huyu ni Mheshimiwa Ester Bulaya naona, sawa alisahau neno Mheshimiwa Mwanzoni, kwa hiyo nataka hansard ziweke sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili PAC na LAAC na Makamu Wenyeviti wao pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya na kwa namna tunavyoshirikiana katika kufanya kazi ya maendeleo ya Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, zimezungumzwa hoja nydingi sana, lakini kwa sababu ya muda pengine sio rahisi sana kuweza kuzijibu zote vizuri na nyiningine ni mambo yanayoanza upya. Hata hivyo, nataka niseme jambo moja tu ili Bunge na sisi wote kwa faida ya maslahi ya Watanzania tuweze kuwa makini nalo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapojadili Taarifa za Kamati ni lazima mambo tuliyoyachukulia hatua na kuyamaliza kwenye Kamati kule hayapaswi tena kuja huku na yanapokuja huku yanataka mjadala mpana sana ambao haupo. Kwa hiyo, tunapata shida kwa sababu baadhi mambo hapa tulikuwa tumekwishayazungumza na pengine ilipaswa kuwekwa vizuri ili yasirudi nyuma tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukulie mfano tu suala la UDA. Suala la UDA ni la muda mrefu, lakini nizungumze kifupi tu sitaki kwenda kwenye historia, ikuwaje na ikawaje. Nina muda mrefu lakini nikumbushe tu kwamba tarehe 13 hadi 15 Januari, 2015 Kamati ya LAAC ilitembelea Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kupokea taarifa kuhusu uuzaji na wakati huo Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na msimamo wa kutokuahirisha uuzaji wa hisa zile. Maoni haya yalitolewa na Kamati ya PAC iliyopita ilikuwa chini ya akina Zitto Kabwe, lakini

Kamati ya LAAC ikaagiza kwamba Jiji liondoe shauri liliolofunguliwa Mahakama Kuu kitengo cha biashara ili Simon Group Limited aweze kulipa hisa hizo.

La pili, Simon Group Limited iruhusiwe kulipia hisa hizo haraka na ya tatu Jiji litoe account ya Benki kwa Simon Group Limited ili Simon Group Limited alipie hisa hizo kupitia account hiyo. Hapa yanensemwa mambo kama vile mjadala huu unaanza leo na wakati Jiji lenyewe limekwishardhia. Tarehe 21 na 22 Januari, 2015, Kamati ya Fedha ya Uongozi ya Jiji la Dar es Salaam iliridhia kutekelezwa kwa maagizo haya ya LAAC. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza hapa, Serikali hii ni mpya, Waziri mimi ni mpya, mambo haya yalikwishapita, kinachosemwa hapa maana yake ni kwamba maamuzi yaliyofanywa na Baraza liliopita la Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam yanataka kuvunjwa na Baraza hili liliokuja leo. Sina hakika kisheria inakaaje lakini naanza kuona tatizo na mgogoro kama Bunge hili linaweza likaanza kufuta maamuzi ya Bunge liliopita, kama Serikali inaweza ikafuta maamuzi ya Serikali iliyopita, naanza kuona tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema lakini tumekwenda vizuri na Kamati yako, tumekwenda hatua kwa hatua na mpaka sasa tuna maagizo ya Kamati ya LAAC juu ya jambo hilo na kuna taarifa wanazozihitaji zaidi ili tuweze kufahamu tunalimalizaje jambo hili. Kwa hiyo, Kamati hii tunafanya nayo kazi vizuri, Waheshimiwa Wabunge wasubiri tutakapomaliza na Kamati hii italeta mambo haya hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala la Madaraka ya Rais kuteua. Ukituza Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 35(1), (2), (3) na (4) Rais anaweza ku-establish madaraka yoyote na anaweza kuteua mtu yoyote kushika nafasi yoyote kwa namna atakavyoona inafaa, hawezi kuhojiwa. Sisi wengine wote kama Mawaziri tunafanya kwa niaba yake kwa sababu ndio Mkuu wa Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, haya mambo tunapoyazungumza tujue kwamba yana Misingi ya Kikatiba na Ikulu haiwezi ikakosea kwa sababu iko equipped. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge vizuri sana kwa asilimia mia moja kwamba wateule hawa ni vizuri wakafundishwa, wakapewa semina kama mlivyoshauri, ingawa tumefanya hivyo kwa kiasi kwa kanda, tumetoa semina kwa Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, Ma-DAS, lakini tutaongeza jithhada ya kutoa semina zaidi ili wajue mamlaka yao na mipaka yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Serikali inataka kuzivunja Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hapana! Serikali nia yake ni kuziimarisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu zipo Kikatiba. Sura ya Nane, Ibara ya 145 na 146 zinatamka

uwepo wa Mamlaka hizi, kama zilivyo Serikali nyingine. Kwa hiyo Mamlaka hizi zinapaswa kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, sisi katika llani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika Ibara ya 147, tumesema waziwazi kabisa kwamba tutajitahidi sana kuziboresha na kuzipa uwezo Mamlaka hizi. Tumesema hapa kuendelea kuzifanyia mapitio Sheria zote zinazohusiana na Serikali za Mitaa na Mamlaka za Tawala za Mikoa ili kuharakisha mchakato wa Kugatua madaraka na lengo la kuziwezesha kutoa huduma bora zaidi kutoka ngazi za Vitongoji, Vijiji hadi kwenye Kata.

Pia tumesema (b) kuendelea kuzijengea uwezo Serikali za Vijiji kwa kuzipatia rasilimali watu na fedha ili ziweze kupanga na kusimamia kwa ukamilifu miradi yao. Lakini pia tumesema kuendelea kuongeza kiwango cha ruzuku katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, pia tunasema kuimarisha ubora wa upatikanaji wa huduma za jamii katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pia tumesema kuendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu, za kisheria kwa watendaji wabovu na wanaofanya ubadhirifu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hii tumeisema katika llani yetu ya Uchaguzi na hatuvezi kwenda kinyume na llani hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, niseme tu, kwamba ingekuwa sasa unataka kuchukua hatua hizi tunazozichukua sasa kwa falsafa ya kutumbuana kwa maana ya kuchukua hatua za haraka kunapotokea ubadhirifu au matumzi mabaya ya madaraka, ukalinganisha kinachofanyika leo na kinachosemwa na Wabunge, ukafanya *flashback*, ukaangalia Bunge lililopita na kilichokuwa kinasemwa juu ya Serikali kutokuchukua hatua, unaiona *contradiction*. Kwa hiyo, utawala wa nchi yetu hii unaweza ukawa mgumu sana kuutengenezea *ideology* kwa sababu kila mtu anataka kutengeneza *ideology* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tufike hatua tuamue, na watu wote waliopiga kura kwenye uchaguzi uliopita walipigia kura mabadiliko, nataka niwahakikishie Watanzania wanayataka mabadiliko kwa sababu walipigia kura mabadiliko, whether wao walipigia CHADEMA, whether walipigia CUF, whether walipigia CCM lakini wote wengine walifanya hivi, wengine walifanya hivi, lakini walikuwa wana lugha ya mabadiliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana gani? Ina maana kwamba Watanzania wamechoka kuishi vile ilivyokuwa, wanataka kitu kipyta na ndicho hiki ambacho Rais Magufuli anakiletu, si kama tulivyozoea. Hapa hatuna uwezo wa kukubaliana na kila jambo, tunaweza tukakubaliana kwamba yanahitajika mabadiliko wote tunakubaliana. Yafanyikeje haliwezi likawa jambo la kukubaliana, kwa sababu yanaweza yakawa kwa namna moja hayo yanayotaka kufanyika yanakugusa, kwa hiyo, hatuvezi kukubaliana, tuache

walioshinda na anayeiongoza nchi atupeleke kwa mwendo unaotakiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mengi lakini kama nilivyosema kwamba sisi tutaendelea kushirikiana na Kamati hizi lakini lilizungumzwa suala lingine la suala la Oysterbay Villa. Oysterbay Villa ulikuwa ni mradi wa kujenga nyumba kwa ajili ya kupangisha, mradi huu kusema ukweli ulikuwa ni mbovu, haufai na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshawasilisha Mahakama ya Rufani maombi namba 299 ya mwaka 2016 kupinga uamuzi wa Jaji wa Mahakama ya Kitengo cha Biashara na Sheria uliofanyika ili ufanyiwe mapitio. Kwa hiyo, maana yake sisi Serikali haturidhiki na kinachofanyika pale katika lile, kwa sababu ya muda siwezi kwenda *into details*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *East Africa Meat Company* zilitengwa fedha kiasi kikubwa tu, Dar es Salaam ilitoa Dola milioni moja, llala ikatoa Dola laki nne na themanini, Temeke Dola laki mbili na thelathini na mbili, Kinondoni Dola laki moja na themanini kampuni ya NICO ikatoa Dola laki moja na kumi na moja. Pia kulikuwepo na mwekezaji mwengine anaitwa *Rheinhold and Mahla* wa Malaysia ambaye alitakiwa kutoa mitambo yenye thamani kubwa tu kama sehemu yake ya umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile bodi ya *East African Meat Company* ilipoanzishwa, ilipopata ile fedha ikaanza kuzitumia fedha zile kwenda kutafuta mitaji badala ya kutumia fedha zile kufanya uwekezaji. Serikali hii haifumbii macho ujisadi. Haturidhiki na hili tunaendelea kuchukua hatua na tumeshaanza kuchukua hatua, lakini tumewaomba wanahisa hawa wakutane waone wanaweza kufanya nini? Wakishindwa kukubaliana na wanahisa, basi waseme na ikibidi wa *wind up* ili wagawane kilichopo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Jiji wasikae peke yao lazima wajue kwamba kuna Mamlaka hizi zinatakiwa na zenyewe kushiriki kuona kama wanakwenda mbele au wanakwenda wapi, wakishindwa Serikali itachukua hatua juu ya hao waliofanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile imezungumzwa asilimia 10 ya mikopo ya akinamama na vijana na hapo hapo ikazungumzwa asilimia 20 kwa ajili ya fedha kupelekwa kwenye mitaa na vijiji kama fidia ya vyanzo vilivyofutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, own source inayozungumzwa hapa na kwa maana ya asilimia 10 iko huko huko Halmashauri ambako ninyi Wabunge mpo na ni Madiwani. Wakurugenzi ambao wanashindwa kupeleka fedha hizo mko nao huko na mnashiriki vikao. Mamlaka ya kuwawajibisha mnayo, kuwafukuza hata kuwasimamisha kazi Wakuu wa Idara mnayo, lakini hawapeleki pesa mnawangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana napenda nimuunge mkono Mbunge wa Kinondoni nafikiri, alichangia, rafiki yangu pale, amesema wao wamepeleka mpaka bilioni mbili, lakini pia kuna Mbunge wa Nyamagana amesema na wao wanapeleka kwa sababu wamemsimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hayo mnatakiwa mkawasimamie nyie kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda kwa wapiga kura wetu. Ingawa kuna mgongano mkubwa sasa katika fedha hii ya gawio hili, hasa unapozungumza kuna maagizo ya Kamati hapa ambayo hayakupitishwa kama *parliamentary resolution*, yakaagizwa kwa Serikali kwamba 60 percent ya own source ifanyiwe development.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo inasemwa 20 percent ipelekwe kwenye vijiji, 10 percent igawiwe kwa vijana na akinamama mikopo, 20 percent ibakie utawala, 10 percent ipelekwe kwa ajili ya kukatia bima ya wazee. Yaani there is a contradiction. Nadhani kwa sababu Serikali ndiyo inayotengeneza sera na hili jambo ni jambo la kisera, acha tukakae tutashirikishana tuone namna gani mgawanyo huu unaweza. Kwa sababu formula hii ya 60 percent development ilifanywa wakati Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla akiwa Mwenyekiti wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, si Halmashauri zote zenye uwezo wa kuwa na fedha ya kutoa 60 percent na zikabaki zinaweza kufanya shughuli zake. Itabidi tuzifanyie cluster ili tuone zipi zinaweza zikatoa hiyo pesa kwa development na zikaweza kuijendesha na zipi ziko maskini ambazo zina hela kidogo, hizo hazitaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la fedha limezungumzwa na Waziri wa Fedha. Tatizo la Wakuu wa Idara kukaimu, tumefanya upembusi, Wakuu wa Idara 802 wanakaimu, kati ya hao 583 hawana sifa. Hata hivyo, nani anayepandisha mtu kuwa Mkuu wa Idara? Ni Mkurugenzi, ambaye mnaye pale, moja ya majukumu ya Mkurugenzi ni kuwaambia, wewe kama unaona wanafaa mbona huwapandishi tuwathibitishe? Kazi yenyewe ni nyepesi tu, kuwaleta kwetu na tuwapeleke for vetting, wakirudi wanathibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi hawafanyi hivyo muwahoji huko kwenye vikao na muwachukulie hatua endapo hawataki kuwathibitisha wenzao. Tusaidiane ingawa tunatafakari kwa sababu upungufu ni mkubwa tufanye mass promotion. Tufanye vetting kwa pamoja, tuwatafute watu wenye uwezo wenye sifa, halafu tufanye mass promotion tunadhani pengine inaweza ikasaidia kwa sababu hawa kila siku wanatoka na kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo ya RC na DED yanayoharibu Mipango ya Halmashuri na kuvuruga bajeti, lakini mengine yanaingilia Mamlaka ya Halmashauri zenyewe. Nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge, kwamba hii haikubaliki na kwa sababu jambo lenyewe limekaa kitaaluma unajua masuala ya utawala hayana *principle* yaani yana namna fulani hivi, masuala ya utawala huwezi kuyatengenezea kanuni kama hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani bado kupitia semina hizi tunahitaji kutoa elimu kwa wenzetu ambao wako huko, kuanzia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Ma-DED, lakini pia na Ma-DAS. Nimeambiwa na najua kuna Wakuu wa Wilaya wengine hana raha mpaka aitishe Kamati ya Ulinzi na Usalama kila asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kamati ya Ulinzi na Usalama ikiitishwa kila siku asubuhi watu watafanya kazi saa ngapi? Polisi, OCD anakuwepo pale, mwisho nchi itakuja kuvamiwa pale hawana hata habari wako kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo hili halikubaliki na nachukua nafasi hii kusema waziwazi kawmba waache, Kamati za Ulinzi na Usalama ni vikao muhimu na vinatakiwa kufanyika kwa jambo mahususi au maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yako maamuzi mengine yanafanya *interference*. Kinachoruhusiwa na hawa Viongozi wa Serikali Kuu ni kufanya *intervention* pale ambapo mambo hayaendi sawa, kwa mfano sheria inavunjwa, kuna mipango na mikakati ya kupiga hela, hapo ndipo wanapoweza kufanya *intervention*, lakini haiwezi kuwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa imetoe maamuzi kwa kufuata sheria, utaratibu wote, halafu wewe unasema hii sikubaliani, hapana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inaitwa *interference*, kwa hiyo haikubaliki, tutaendelea kuelezana, lakini wanajitahidi wanafanya kazi vizuri, tunahitaji kueleweshana, tunahitaji kuelimishana na hao walioteuliwa ndugu zangu ni Watanzania wenzetu. Tusiwe na sense ya kuwabagua, wana elimu, wana sifa, wamesoma hata sisi tulipokuwa Wabunge hapa hatukuja na uzoefu huu. Kwa hiyo, tukubaliane kwamba ni wenzetu, ni ndugu zetu, wanatakiwa kupata fursa na wao kujifunza. Ukisoma, Mheshimiwa Zitto alikuwa ameni-consult hapa nikamwambia viko vifungu ambavyo vinawapa Mamlaka lakini kwa sababu ya muda acha niliache. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie vikao vya Mabaraza ya Madiwani na Kamati za Uongozi vinapoitishwa wakati Bunge linaendelea. Tumetoa maelekezo kwamba wasiitishé vikao hivyo wakati Bunge linaendelea. Tumetoa na kuelekeza ma-RAS, nadhani ujumbe labda haujkwenda, pengine tupeleke nguvu zaidi ya kuwaeleza wao wenywewe kwamba, lazima wahakikishe

wanaitisha vikao hivyo wakati Bunge halipo kwenye session ili Wabunge wapate fursa ya kuhuduria. (Makofi)

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa nampa kidogo Mheshimiwa Simbachawene. Inawezekana kwamba kuna...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto ukishasema taarifa, si lazima nikuruhusu kwanza, naona unaendelea tayari...

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Naomba niruhusu dada.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto taarifa.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Inawezekana kuna vitu ambavyo tunapenda sana kuvisikia lakini practical haviwezekani. Kamati za Fedha na Uongozi Mheshimiwa Waziri zinakutana kila mwezi. Kuna nyakati tuko Bungeni miezi miwili mfululizo; Halmashauri, naomba munisikilize kidogo. Halmashauri haziwezi kusimama kusubiri Wabunge warudi majimboni ili kuendelea na kazi. Lazima tukiwataka wao wawajibike na sisi tuwajibike. Haiwezekani hata kidogo tuzisimamishe Halmashauri kufanya kazi kwa sababu sisi tuko Bungeni. Kikao hiki ni cha siku moja. Unakuta kwa mfano natolea mfano wa rafiki yangu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto kwa kuwa ulikuwa unatoa taarifa nadhani ameipata, kwamba vikao huwa vinakaa kwa mwezi, kwa hivyo haiwezekani Wabunge kushiriki. Sasa aipokee hiyo taarifa, haiwezekani Wabunge kushiriki kila wakati. Mheshimiwa Simbachawene, taarifa hiyo unaikubali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali lakini itabidi tu-harmonize haya mawazo na yale mawazo mengine, tupate utaratibu fulani mzuri unaoweza ku-accommodate situations zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie. Kinachokosekana kwenye mamlaka zetu zilizoundwa na Serikali ya Awamu ya Tano ni ari na kasi ya watu kutaka kutekeleza majukumu yao. Niwasih sana Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni Viongozi wale walio kule ma-DC, Wakurugenzi ni Viongozi wenzetu. Tukiwa na tabia ya ku-interact, unafika pale usisikilize Madiwani tu wamekwambia kitu, basi unabeba, huyu hafai, amefanya hivi, sikiliza na upande wa pili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufahamu kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama; na hivyo vyombo vya Ulinzi na Usalama viko chini yao wana taarifa ambazo wakati mwingine sisi hatuna. Kunaweza kukawa kuna mpango wa kufanya hujuma fulani na yeye anayo taarifa halisi, ya kweli, wewe huna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wanafika pale wanakukamata wanakwambia huyu hivi hivi na hivi na wewe unaamini. Unakwenda kuanza kusema, hapana, huyu anaingilia anafanya nini; tuwe na tabia ya ku-interact na hawa viongozi wenzetu itatusaidia. Itatusaidia sana kuyajua yaliyo ndani, kujua taarifa za siri, nani anafanya nini na wakati mwingine ningetamani kama ninavyoyajua mimi na nyie mngeyajua kwenye maeneo yenu yangesaidia kuondoa hii migongano. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa tutawasikiliza watoa hoja. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. (Makofii)

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wachangiaji wote wa hoja hii tulioileta mbele yenu, Taarifa hii ya PAC, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliota maoni yenu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaambiwa napewa muda gani!

**NAIBU SPIKA:** Una nusu saa Mheshimiwa lakini ukitumia muda pungufu ya huo utakuwa umefanya vyema zaidi.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Muda niliopewa nusu saa na wachangiaji walikuwa zaidi ya thelathini, nikienda kwa kila mmoja, nadhani hatutamaliza leo, kwa hiyo, nitayaweka kwa mafungu kutokana na jinsi wachangiaji walivyochanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wachangiaji wote walitupongeza Kamati zetu zote mbili za PAC na LAAC, tunawashukuru sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wachangiaji wote niliowasikia wamekubali kwamba PAC bila kuvezeshwa hatutaweza kufanya kazi yetu kikamilifu. Kwanza kwa sababu tukifanya ripoti tu kama tunavyoletewa bila kuwa na muda wa kwenda kuhakiki tutakuwa hatuwatendei haki waliotutuma kazi hii.

Kwa hiyo, ni wazi kwamba PAC lazima tukiletewa taarifa tuweze pia kwenda kuhakiki. Kwa hiyo tunaomba kama Bunge lako likaridhia kama kweli PAC inahitaji kuongezewa pesa ili ziweze kufanya kazi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wachangiaji wengi walisema kwa msisitizo tena kwa masikitiko, kuhusu jicho letu Wabunge, CAG ambaye bajeti yake ni ndogo sana kiasi kwamba hawezi kwenda kutembelea ile miradi mbalimbali maana ukisema tu sisi tufanye kazi, PAC kazi zetu zinategemea CAG analeta nini. Kama CAG hawezi kwenda kufanya audit ina maana PAC hatuna kazi. Kwa hiyo tungeomba sana CAG bajeti yake iongezwe, vinginevyo tutajidanganya Wabunge hapa na kazi hazitakwenda. (Makof)

Mifuko hii ya jamii imeongelewa sana kwa uchungu na wachangiaji, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na Waziri amejaribu kujibu. Hata hivyo, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri na kusema kwamba walikuwa wanahakiki wafanyakazi hewa na amesema PSPF wameshamaliza, swali langu ni kwamba kama wamemaliza kwa nini hawapeleki, hawarudishi yale madeni ya PSPF ili waendelee kulipa mafao ya wastaifu?

Wastaifu wengi wamelalamikia sana sehemu hii kwamba mafao yao hawalipwi. Wabunge wengi wanapigiwa simu, mimi mwenyewe napigiwa simu kutoka Jimboni kwangu. Kwa hiyo tungeomba, sana kama wamemaliza na wanaendelea na Mifuko mingine, basi angalau Mfuko huu wawape pesa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kuna sehemu nyingine ambazo zinahitaji msisitizo kidogo. Suala la Lugumi ni suala ambalo limetuletea matatizo sana kwenye Kamati, maswali yamekuwa mengi kabla hata haijaundwa Kamati Ndogo na bahati mbaya Kamati yetu hadidu ya rejea yetu ilikuwa inatufunga sana kwenda kuhakiki kama vile vyombo vilinunuliwa na kufungwa ndiyo tulitumwa hivyo.

Bahati mbaya hatukuwa na mkataba kwa hiyo hata kama tumekuta upungufu mengine hatuwezi kuyaingilia, lakini kibaya zaidi tulikuta vifaa vingi kweli vimelundikwa, havikufungwa sasa je, ni vya mradi huu au ni vya mradi mwingine ili tukipita vinaondolewa vinapelekwa kunakohusika? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vilinunuliwa kwa nini havikufungwa? Kwa nini kazi haikuanza? Miaka yote hiyo tangu 2011 mpaka leo miezi mitatu vifungwe? ndiyo kazi kubwa tuliyokuwa nayo. Kamati yetu wameshindwa kujibu maswali mengine tunayokutana nayo, ni sawa na mtu amefungwa miguu na mikono halafu anaambiwa kimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, maswali ambayo bado Kamati ilijuliza baada ya kupata ile Taarifa ya Afisa Masuhuli 28/10; ni je, vifaa vilivyoharibika kabla havijatumika ilikuwa ni wajibu wa nani avitengeneze ndipo vifungwe? Iweje Serikali inasema inasubiri ipate hela za bajeti za mwaka 2016/2017 ndipo ivitengeneze. Hilo ni jibu ambalo hatujalipata bado. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tulikuta vyumba ni vichafu sana, sehemu nyingi vilipowekwa hivi vyombo, je, ilikuwa ni jukumu la nani kutengeneza? Hatujui. Kwa hiyo Kamati yetu ilifanya kazi katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ninywe maji maana hili ni tatizo kubwa sana. Hili tatizo limeninyima usingizi, tunapigiwa simu kwamba ooh tumekatiwa chochote au tumetiwa mifukoni. Ninachotaka kusema Waheshimiwa Wabunge, kama kazi kubwa ya vifaa vile ilikuwa kuchukua picha za wahalifu pale kituoni, kuhifadhi taarifa, kwa nini hizo kazi kubwa mbili hazikufanyika miaka yote hiyo? Je, hivi vifaa vilikuwa vinafanya kazi kweli? Maana hii kazi ya kusema Mkongo wa Taifa ulikuwa haujafungwa ili kuwa na mawasiliano, hii ilikuwa stage ya mwisho, lakini ultakiwa ukifika kituoni ukute picha, taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utusaidie sisi ambao si Wajumbe wa hiyo Kamati, haya maswali unayoyaauliza saa hizi anayepaswa kujibu ni nani, kwa sababu maswali ya Wabunge wote hawa ni wewe Mwenyekiti ndiye unatoa ufanuzi ndio waliyekuuliza. Sasa na wewe ukiuliza mimi sina majibu, mimi siyo mjumbe wa Kamati, kwa hiyo nataka kujua. Kwa sababu Serikali haitapewa tena nafasi tutaelekea kwenye mapendekezo mliyoleta kwenye hii ripoti yenu.

Kwa hiyo utusaidie vizuri ili baadaye Bunge hili litakapokuwa linafanya maamuzi kwenye yale mliyopendeleza humu liwe na taarifa za kutosha. Utusaidie tu hicho Mwenyekiti kwa sababu Bunge hili linawategemea ninyi. Sasa ukiuliza maswali na sisi hatuwezi tena kujib; inabidi utujibu wewe mwenyewe.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nilikuwa nihitimishe hivyo, kwamba ndiyo maana tumesemi! Umeniwhi tu. Ndiyo maana tumesemi hatuwezi kutoa majibu yoyote hapa kwa taarifa tulioletewa tarehe 28 mwezi Oktoba; wakati tunafunga taarifa yetu mpaka tutakapoweza kuhakiki kama kiti chako kilivyo tuambia kwamba, tuhakiki hivi vifaa kama vimefungwa.

Kwa hiyo, ndiyo maana nilitaka kwamba hii ajenda hajafungwa, huu mjadala haujafungwa, tutakwenda kipindi kinachofuata kuhakiki, kwa hiyo tutaweza kuleta taarifa kamili; hivyo ndivyo ilikuwa nihitimishe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *TIB*. Labda niseme tu kwa ujumla kwamba majibu ya Mawaziri nimeyapata mengine yameniridhisha kiasi, maana kasema hizi hoja tutakutana nazo wakati CAG atakapopitia yatakuja. Hata hivyo, mahali ambapo bado pamenipa utata ni ukiangalia jibu ambalo alilitoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kwamba kuna sheria ambayo inakataza mabenki kutoa taarifa za wateja wao.

Nikajiliza kama hivi ndivyo, hivi hii taarifa ya *TIB* tuliletewa kwenye Kamati ili iweje? Imeletwa kwa minajili gani? Kupewa taarifa watu wamepewa hela, watu hawalipi, leo nahoji tujue zile kampuni ambazo zimepewa hela hizi, miaka hawalipi tunaambiwa hapana, hamuwezi kufanya hivyo, hawawezi kutoa siri za wateja. Hizi pesa kwanza ni za nani? *TIB* inawajibika kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Spika amefanya makosa kutojua hiki kifungu kwa vile ameshawaandikia *TIB* kwamba watuletee hizo taarifa za yale mashirika sugu yanayodaiwa ambao hawajataka kuleta hizo taarifa tukazonia ili Bunge lako likatoa maagizo kwamba wachukuliwe hatua gani. Je...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umemtaja Spika, hapo kwamba pengine hakukijua hicho kifungu; kifungu anakijua, maagizo aliyotoa haimaanishi ninyi mtaletewa hiyo taarifa moja kwa moja ndio utaratibu ambao tunautumia siku zote. Kwa hiyo si kwamba kifungu hakikujulikana ama hakukiona, anakifahamu kifungu na ametumia sheria nydingine kuitisha ile taarifa. Itakapomfikia yeye ataangalia namna bora ya kuileta kwenu kama ni taarifa ambayo inapasa kutolewa basi atawaletea. Kama ni ile ambayo haipaswi kutolewa basi hatoileta; tuendelee.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini naomba uniache kwa vile Kamati... (Makofsi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaniwia ngumu kwa sababu kwa maelezo yako wewe ndio unatusaidia tufanye maamuzi na maamuzi lazima tufanye leo. Sasa nikisema nitapata muda wa kujibu baadaye sina na wewe ndio unayetusaidia ili tufanye maamuzi baadaye, Bunge zima hili linakutegemea wewe tu ndiyo mwenye hoja hii.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sitaki kubishana na kiti, lakini nimeshapata taarifa, lakini pia nilikaa nikajiliza ambalo labda litaingia huko. Hivi wateja sugu wanapotolewa kwenye magazeti kwamba hawalipi maana yake nini? Nafikiri Waheshimiwa Wabunge, hiyo hoja tuiache, tusubiri Spika atakapotuletea ile barua na majibu yake tutajua tufanye nini? (Makofsi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kuhusu suala la na SACCOS. Mheshimiwa Mhagama amelijibu, nafikiri alikuwa anawajibu wale Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba NSSF isitoe mikopo kwa SACCOS; amelijibu vizuri. Kamati yetu tatizo lake lilikuwa si hilo, Kamati yetu tumesema tatizo hapa ni kwamba NSSF imeweka utaratibu wake kwamba, mkopaji au atakayekopeshwa atumie vigezo hivi. Kwanza imeweka ceiling kwamba kukopa ni kuanzia *minimum* ni milioni 50, *maximum* ni bilioni moja. Pia wakasema *collateral* lazima ioneokane kwamba iwe ni 50% ya ile *amount* unayotaka kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tatizo letu lilikuwa je, wale waliopewa zaidi ya bilioni moja mpaka bilioni mbili na laki tano, ni sawa sawa hiyo? Si sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa wale ambaao wamepewa mikopo ambaao hesabu zao zilikuwa hazijakaguliwa, lakini wakapewa mikopo, tukasema si sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tukasema wale ambaao hawajarejesha mikopo ile, maana pesa hizi ni za kulipa mafao ya wastaifu, hivyo si sahihi na ndiyo maana sisi tumesema, tunaomba CAG aende akahakiki akafanye ile kazi ili atuletee taarifa kamili. Nani wamelipa na nani hawajalipa, nani wamefanya kinyume ili iletwe katika Bunge lako au katika Kamati tuweze kuleta katika Bunge ili lichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kuzungumza ni mengi nimerukia kwa Manaibu, ndiyo nilikuwa nakwenda nikiangalia hizi responses zilizotoka kwa wenzangu mbalimbali ambaao wamechangia. Sasa naweza nikarudi nyuma kidogo kuzungumzia mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema; ili kwamba hata muda ukiisha tutakuwa angalau zile *important areas* tumezipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengine wamezungumzia kuhusu tatizo la bandarini kuhusu zile meli, kweli wamesema kama sisi tulivyosema kwamba inakuwaje meli iingie mpaka itoke miezi 18 taarifa zake hazijajulikana, hawajalipa. Hilo limezungumzwa na sisi tuliliweka katika taarifa yetu. Kwa hiyo tumesema kwamba bandari yetu inatakiwa iangaliwe kwa ukaribu sana ili iweze kufanya kazi zake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la TRA na misamaha ile ya kodi, pia tumeleta katika Bunge lako ili ijulikane kwamba TRA wapewe maagizo ili wafanye kazi zao. Kuhusu ile misamaha hewa watuambie wale ambaao wana misamaha hewa wamechukuliwa hatua gani? Ndiyo maana tumeleta hilo ili nalo kama Kamati yetu ilivyopendekeza tupewe majibu kwamba

wamechukuliwa hatua gani kwenye misamaha ile ambayo hawakukidhi, wengine ni misamaha hewa, ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine kwa kweli *in general* yamezungumzwa sana hayo ya kuhusu *TR* na kuelezea jinsi ambavyo Kamati yetu imependekeza kwamba *TR* awezeshwe ili na yeye aweze kufanya kazi yake vizuri. Tunampongeza sana kwa kweli ameisaidia sana Kamati yetu na hivyo tunaamini kwamba atakavyozidi kupewa nguvu ataweza kuendelea kufanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haya Mashirika yetu ya *EWURA, SUMATRA* kwa kweli tumesitisiza na Waheshimiwa Wabunge wameliongelea kwamba zile tozo wanazoleta kule Serikalini hazikubaliki, kwamba wapunguze administrative expenses zao ili waweze kutoa tozo linalokubalika Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine samahani kidogo mnisamehe, maana yameingiliana na ya wenzetu, ya *LAAC* lakini *at the end of the day* tunakubali kwamba, pesa za maendeleo kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni vizuri ziende kama zinavyopitishwa na Bunge, otherwise nchi yetu tutapiga kelele hapa, lakini hatutapiga hatua, zipelekwe kwa wakati. Ili zile bajeti zinazopitishwa hapa zihakikishwe kwamba zinafika kule zinakotakiwa ziende.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Kilimo amejitahidi sana kuelezea aliyoayelezea na kuhusu ile ya wafanyakazi kwamba wanaangalia sababu nydingine na kwamba hawakusimamishwa tu kutokana na yale mahindi mabovu, kwa hiyo, tunajua kwamba tutapata taarifa kamili katika ukaguzi ujao ili tuweze kujua hatma yao imekuwa ni nini. Hayo maghala aliyoahidi naamini yatajengwa ili yafanye kazi vizuri na nguvu ya wakulima isipotee bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nimejitahidi ku-cover maeneo mbalimbali na naamini kwamba eneo kubwa la hii taarifa yetu masuala yake yalikuwa yamewekwa katika mafungu hayo niliyoyataja ndiyo maana nimeya-sum up.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tumemsikia Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka akitoa maelezo mbalimbali, lakini tunayo maazimio mbalimbali ambayo Kamati pamoja na mambo mengine imependekeza ili Bunge liweze kuazimia juu ya hayo mapendekezo ya maazimio ya Kamati. Natarajia kwamba wote tunavyo hivi vitabu.

Katika utaratibu uliozoleka kila azimio linapaswa kuhojiwa peke yake, lakini hapa nilipo sijapokea marekebisho ambapo kwa mujibu wa kanuni, kama kuna mtu angekuwa na mapendekezo ya kurekebisha mapendekezo ya Kamati angekuwa ameyaleta.

Kwa hiyo, taarifa ya Kamati imeshajadiliwa, sasa ni wakati wa Bunge kufanya uamuzi. Sasa kwa kuwa hatujapata marekebisho ya Mbunge ye yeyote kwa mujibu wa kanuni zetu, napendekeza kwamba haya maazimio yaliyopo kwenye hii Taarifa ya Kamati niweze kuyahoji yote kwa pamoja kama tunakubaliana hivyo, kwa sababu hakuna marekebisho ambayo yameletwa juu ya mapendekezo haya. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo yapo kwenye Taarifa ya Kamati kuanzia ukurasa wa 88 mpaka ukurasa wa 100 na haya mapendekezo ya maazimio yapo kwenye masuala 14 ambayo Kamati inalitaka Bunge liazimie. Sasa nachukua fursa hii ili kulisaidia Bunge litoe maamuzi, nitawahoji kwa mujibu wa kanuni zetu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali pamoja na Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyomo katika Taarifa hiyo ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Bunge zima kwa pamoja limeafiki nami naamini wameshinda wale walioafiki. Kwa hiyo, mapendekezo ya Kamati yameafikiwa na Bunge zima. Kwa hiyo, haya ni maazimio ya Bunge. Vile vile nachukua nafasi hii kuitaka Serikali ifuatilie maazimio yote haya na utekelezaji wake tutausikia Kamati itakapoleta taarifa kwamba maazimio haya mmefika nayo wapi.

Kwa hiyo, myafuatilie yapo kwenye mambo 14 kama nilivyosema na ni karibu kila jambo moja lina maazimio kama mawili au matatu hivi. Yote myafuatilie, yapo humu na Bunge kwa umoja wake imepitisha mapendekezo yote ya Kamati. Kwa hiyo, Bunge limeazimia yote yale ambayo Kamati imependekeza. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, nawapongeze sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kuitendea haki Kamati, lakini pia kuitendea haki taarifa ya Kamati ilioletwa hapa ambayo Kamati hii ilifanya kwa niaba yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Wajumbe wa Kamati na Bunge zima hongereni sana kwa kuamua kwa pamoja.

Sasa tutaendelea na ratiba yetu. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. (Makofij)

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala wa Taarifa ya Kamati yangu kwa mwaka 2016. Michango mbalimbali mizuri imetolewa na naitaka Serikali sasa kujipanga na kuona namna bora ya kurekebisha kasoro nyingi zilizoainishwa na Waheshimiwa Wabunge ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma na kuongeza ari ya uwajibikaji katika Halmashauri nchini. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na jumla ya wachangiaji 46 ambao wamechangia kwa hoja mbalimbali za Kamati yangu; kati yao 39 wakichangia kwa maneno na saba wakichangia kwa maandishi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika maeneo yaliyogusia matumizi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma, upelekaji usioridhisha wa fedha kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, asilimia kumi ya mapato kutochangiwa katika Mfuko wa Wanawake na Vijana, Halmashauri kutopeleka asilimia 20 ya ruzuku kutoka Serikali Kuu katika Serikali za Mitaa na Vijiji na Marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuwa sheria hii inakinzana na hali halisi ya bei za bidhaa katika soko na mwisho uwezo mdogo wa kuitendaji wa baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kutumia chuo cha mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo kutoa mafunzo kwa Wakurugenzi wapya wa Halmashauri kama ilivyoshauriwa na Mheshimiwa Issa Mangungu, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota. Pia Ndugu yangu Mheshimiwa Silinde alisema na kupendekeza kwamba ni vizuri sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuwatumia watumishi wanaotokana na Watumishi wa Serikali ili iwe motisha chanya kwa wale Wakuu wa Idara katika utendaji wa kazi, maana kwa hali iliyopo sasa watumishi wengi katika Halmashauri ile ari ya kufanya kazi imeshuka sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa inaitaka Serikali itenye bajeti ya kutosha kwa Bunge ili Wabunge waweze kutekeleza majukumu yao kwa ku simamia Serikali hususan kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo badala ya kufanya vikao na mahojiano ya ana kwa ana na Menejimenti za Halmashauri hapa Dodoma. Kimsingi ukaguzi ni moja kati ya shughuli muhimu katika kuhakikisha kuwa kuna nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia hoja ya ufinyu wa bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi unaosababisha ofisi hii muhimu kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Hili limezungumzwa na ndugu yangu Mheshimiwa Khatibu na kusema kwamba Serikali inazibana Kamati za usimamizi wa fedha za Serikali, lakini inaibana Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kwa hiyo, mimi situmii ile *terminology* nyingine aliyotumia Mheshimiwa Khatibu, ila niseme tu kwamba Serikali ilegeze kubana ili basi mambo yaweze kwenda sawasawa. (Makofij/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za usimamizi wa fedha zinatekeleza majukumu yake kwa kutumia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, mwaka huu CAG ameshindwa kutembelea baadhi ya Halmashauri kufanya ukaguzi na uthibitisho wa majibu ya hoja mbalimbali za ukaguzi. Ufinyu huu wa bajeti usipotatuliwa katika bajeti zinazokuja, kuna hatari ya CAG kushindwa kufanya ukaguzi kabisa na hivyo Kamati hazitawenza kuendelea na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na michango mizuri inayohusu usimamizi mbaya wa mikataba na utekelezaji wa miradi ya maendeleo uliobainishwa na Kamati. Naamini kwamba Serikali imeliona hilo na italifanyia kazi hasa kuboresha usimamizi wa mikataba kwa kuwa miradi mingi ya maji katika mwaka wa fedha 2013/2014 na mwaka wa fedha 2014/2015 haikutekelezwa kikamilifu kwa sababu mikataba mingi ilivunjika kabla ya miradi kukamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Martin Msuha, Mheshimiwa Richard Mbogo kwa kutoa maelezo mazuri juu ya mfumo wa fedha wa EPICOR. Mfumo huu niseme wazi umegharimu Serikali fedha nyingi katika kuzunganisha Halmashauri nchini, lakini utendaji kazi wake hauna tija. Baadhi ya taarifa kwa mfano, taarifa za mali za Halmashauri zinaandalisha nje ya mfumo. Ifikie wakati Serikali ione kuwa mfumo huu una changamoto nyingi na hivyo haufai kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa kupata taarifa za Halmashauri ni mgumu kwa kuwa vitabu vinavyowasilishwa huwa vikubwa mno na mapitio yake huwa magumu mno. Dunia ya sasa inaelekea katika mfumo

wa nyaraka laini (*electronic filing system*). Hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza kwamba Kamati inakutana na malundo ya vitabu ambavyo kuvifanya upembuzi inakuwa ngumu sana. Hivyo Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo huu kwa Halmashauri nchini. Hii itapunguza hatari ya gharama za kudurufu vitabu hivi ambavyo ni vikubwa na mzigo mkubwa kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishauri Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuwa huru na kuwa kipangiwe bajeti ya kutosha ili kiweze kusimamia mwenendo wa fedha za Halmashauri. Wazo hili ni zuri kwa kuwa hata Kamati yangu ilibaini tatizo hili. Serikali iendelee kusisitiza kuangalia namna bora ya utendaji kazi wa kitengo hiki ili kulinda fedha za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pauline Gekul alifafanua kwa undani namna bora ya Mfuko wa Wanawake na Vijana ambavyo unawabagua wazee ambaao nao kimsingi wanayo mahitaji ya fedha kwa ajili ya mahitaji ya biashara ndogo ndogo na shughuli nyingine. Kamati iliona hilo na nichukue tena fursa hii kusisitiza uundwaji wa Sheria ya Mfuko huu ili kuongeza tija, ikiwa ni pamoja na kuangalia changamoto ambazo Kamati imeziainisha katika taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea pia mchango wa Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe kwa maandishi kuhusu suala la Mfuko wa Wanawake na Vijana. Nakubaliana na wazo lake la kuangalia uwezekano wa Serikali kutumia mfumo wa hifadhi ya jamii ili kuhakikisha usalama wa fedha za umma. Kimsingi ushauri wake ni mzuri kwa kuwa una faida za ziada kwa wanavikundi; kama vile utaratibu wa kuijwekea akiba, kupata fao la Bima ya Afya na kupata fursa ya huduma ya SACCOS ili kupanua wigo wa biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwepo suala la Serikali kuchukua vyanzo vya mapato vya Halmashauri kama vile ushuru wa ardhi na ushuru wa nyumba. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wamelalamikia suala hili la Serikali kukusanya ushuru wa ardhi na kutopeleka asilimia 30 katika Halmashauri kama ilivyokubaliwa. Niseme wazi, ushuru huu umefikia wakati kwamba Serikali lazima irudishe katika Halmashauri ili kuongeza wigo wa mapato na kuzipunguzia utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi waliochangia taarifa yetu, wameshauri Halmashauri kufuata utaratibu katika kutekeleza maagizo kutoka Serikalini. Suala la ujenzi wa maabarla limegharimu miradi mingi na Kamati ilibaini kuwa ni moja kati ya sehemu zenye walakini mkubwa katika matumizi ya fedha za Serikali. Sasa lipo suala la utengenezaji wa madawati ambalo pia ni

agizo kutoka Serikali Kuu. Naendelea kusisitiza kuwa Halmashauri zifuate sheria, kanuni na taratibu za fedha katika kutekeleza maagizo yao. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika taarifa yetu na Kamati inataka Serikali kuleta majibu kwa maandishi juu ya utekelezaji wa yale yote ambayo Kamati tumeyaazimia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho basi niombe sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na mapendekezo yote yaliyomo katika taarifa hiyo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofij)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ngombale, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kuhitimisha hoja.

Waheshimiwa Wabunge, napendekeza tuchukue utaratibu tuliochukua wakati tukihitimisha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Mapendekezo ya Kamati yapo kuanzia ukurasa wa 66 mpaka ukurasa wa 75 na wamependekeza mambo mengi, kwa idadi yanafika tisa. Kwa hiyo, maazimio yapo kadhaa kwenye mambo haya tisa. Sasa nitawahoji ili Bunge liweze kufanya maamuzi juu ya mapendekezo haya ambayo yameletwa na Kamati.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Za Mitaa pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo yalipitishwa na Bunge)

**NAIBU SPIKA:** Bunge zima limeafiki, kwa hivyo hakuna ambao hawajaafiki.

**MHE. HALIMA MDEE:** Hoja ya kuunda Kamati Teule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima naomba ukae. Kwa hiyo, walioafiki wameshinda. Nachukua fursa hii kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya

na Mwenyekiti wao na pia Bunge zima kwa ushiriki katika yale ambayo Kamati ilifanya kwa niaba yetu. Kwa hiyo, niitake Serikali kuyafuatilia maazimio ya Bunge ambayo limeazimia leo katika mambo haya tisa. Maazimio yapo kadhaa kwa sababu kila jambo moja lina maazimio kadhaa.

Kama Mwenyekiti alivyosema, ni matarajio yetu kwamba mtapeleka kwenye Kamati hiyo majibu ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kwa mujibu wa ratiba yetu tuliyonayo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hoja ya kuunda Kamati Teule.

**NAIBU SPIKA:** Naomba Mheshimiwa Halima ukae, nimepata ujumbe wako, nitakupa fursa baadaye. Mheshimiwa...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara naomba ukae. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu pia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto kuhusu utaratibu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Zitto amepewa nafasi; huwezi kuendelea kusimama na kuwasha *microphone*. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kwa mujibu wa kanuni ni hoja ambayo inakuja mara baada ya jambo kuamuliwa. Kwa hiyo, iwapo atakwenda kuzungumza baada ya hoja nyingine, hoja yake itakuwa imekufa kwa mujibu wa kanuni. Kwa hiyo, naomba tuweze kufuata kanuni. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kanuni inayompa Mheshimiwa Halima haki ya kuomba kuhusu kuundwa kwa Kamati Teule ni 120(1), ambayo inasema, "Kamati teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa.?

Waheshimiwa Wabunge, sijapaona mahali ambapo inasema hicho unachosema Mheshimiwa Zitto na ndiyo maana nimesema, tutakapomaliza nitampa nafasi kwa sababu ameshanipa taarifa kwamba ana jambo analotaka kulileta na kanuni hii haisemi mimi nimruhusu wakati gani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo. (Makofii)

**MHE. WILLIAM A. NGELEJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE**

**YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa nikiwa katikati ya Watanzania nikifahamu kwamba Taifa letu sasa hivi liko katika kipindi kigumu, linaendelea kuwapoteza baadhi ya Watanzania, nami naungana nao kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema kuelezea masikitiko yetu na salamu zetu za pole kwa kuondokewa na wapendwa wetu; Mheshimiwa Mungai na Spika Mstaafu, Mheshimiwa Samuel Sitta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria ndogo, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mtemi, Andrew John Chenge, namshukuru sana Mheshimiwa Spika, lakini pia nakushukuru wewe binafsi kwa mamlaka yenu kwa namna ambayo mmetukubalia kwa mujibu wa Kanuni ya 117(17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili Kamati yangu iweze kuwasilisha Taarifa ya Kwanza ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa mezani Bungeni na Serikali katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yote ya Kamati yetu iliyowasilishwa mezani leo asubuhi pamoja na viambatisho vyake, iingie katika taarifa rasmi za Bunge lako Tukufu kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini kuwa Waheshimiwa Wabunge wataitumia taarifa hii kutoa ushauri zaidi kuhusu sheria ndogo zilizochambuliwa na Kamati yetu pamoja na sheria ndogo nyingine ambazo zitatumika. Aidha, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanya kazi mapendekizo yaliyomo katika taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu chenye mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania Bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao utafuatwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa kuzingatia kuwa Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa sheria, Ibara ya 97(5) inalipa Bunge mamlaka ya kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga sheria ni kuvipa vyombo hivyo fursa ya kuweka masharti ambayo ni mahususi kwa utekelezaji wa masharti ambayo ni ya ujumla yaliyowekwa katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dhana ya udhibiti wa kibunge wa utungaji wa sheria ndogo, (*parliamentary control over subsidiary legislation*) siyo dhana mpya katika mgawanyo wa madaraka ya dola katika Nchi za Jumuiya ya Madola. Udhibiti huu una lengo la kuhakikisha kwamba Bunge linajiridhisha kikamilifu kwamba madaraka ya kutunga sheria iliyokasimu kwa mamlaka nyingine yanatekezwa ipasavyo kwa kuzingatia masharti ya sheria mama iliyoruhusu utungwaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwandishi maarufu wa vitabu vya sheria, C. Takwani aliandika yafuatayo:

*"it is open for the Parliament to confer power upon anyone it likes. If the Parliament delegates its legislative powers to any other authority such as executive, it also has the obligation to see if those powers are properly exercised by the administration."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyokuwa rasmi kwa Kiswahili, tunaweza kusema kuwa mtunzi huyu alikuwa anamaanisha "Bunge limeachwa liweze kutoa sehemu ya madaraka yake ya kutunga sheria kwa yeyote ambaye Bunge litapenda. Bunge likikasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine yoyote kama vile Serikali, litakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa madaraka hayo yanatekelezwa ipasavyo."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni ya Mwandishi huyo, ni wazi kuwa Bunge lisipokuwa na utaratibu wa kudhibiti au kujiridhisha kuhusu utungaji wa sheria ndogo, litakuwa halijajipanga vizuri kutekeleza wajibu wake wa msingi. Dhana ya udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo imeelezwa kwa kiasi cha kutosha kueleweka katika machapisho mbalimbali ya fani ya sheria na masuala ya Bunge. Kwa mfano, katika sheria ilioandikwa na Bharat Raj, mwandishi huyu aliandika maneno yafuatayo kubainisha umuhimu wa uwepo na mfumo wa utungaji wa sheria ndogo nje ya Bunge na ulazima wa Bunge kusimamia na kudhibiti utungaji wa sheria ndogo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitanukuu kama ilivyoandikwa.

*"Delegated legislation is often criticized as an excuse for the legislators, a shield for the administrators and a provocation for the Constitutional purists. However, the very mechanism of delegated legislation cannot and should not be reduced to an evil because it is at the end of the day, a necessity. In the modern world where social, economic, technological, and administrative speed outstrips the placid traditional legislative processes, delegated legislation is an essential means of survival. Thus, since it is the legislature which delegates power, it is primarily for it to supervise and control the exercise of this power, and ensure against its objectionable, abusive and unwarranted use."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi nukuu hiyo inaweza kutafsirika kama ifuatavyo: "sheria Ndogo zinalalamikiwa kutumiwa kama udhuru wa watunga sheria, ingawa kwa watawala na jambo linalowaudhi wanaufasaha wa kikatiba. Hata hivyo utaratibu wenyewe wa sheria ndogo hauwezi na hautastahili kushushwa kiasi cha kuwa ubaya kwa sababu mwingine ni jambo la lazima. Katika ulimwengu wa leo ambapo kasi ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na kiutawala inazidi mchakato wa kawaida wa utungaji sheria, sheria ndogo ni njia ya lazima kuwepo, hivyo kwa kuwa ni Bunge linalokasimu madaraka yake ya kutunga sheria, kimsingi linapaswa kusimamia na kudhibiti matumizi ya madaraka hayo na kuwa na uhakika kwamba, madaraka hayo hayatumiki isivyofaa, vibaya na wala isivyokubalika."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria ya Sura ya Kwanza, imeweka masharti maalum ambayo yanalipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa sheria ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Udhibiti huo siyo wa moja kwa moja kwa sheria ndogo yoyote mpaka itakapotangazwa katika gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria mama inapotungwa na Bunge, inaweza kuweka masharti kwamba sheria ndogo yoyote inaweza kutungwa kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa sheria mama. Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka masharti ya jumla ya kuzingatiwa wakati wa utungaji wa sheria ndogo na moja kati ya masharti hayo ni kwamba sheria ndogo haipaswi kuwa kinyume na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sheria ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika gazeti la Serikali, kwa mujibu wa Kifungu cha 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, sheria ndogo hiyo inapaswa kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge (*sitting days*) kwa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38(1) katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona umuhimu wa kufanya udhibiti wa utungaji wa sheria ndogo, Bunge la Tanzania kama ilivyo katika Mabunge mangine katika Nchi za Jumuiya ya Madola imeunda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo inatekeleza majukumu hayo kwa niaba ya Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari mwaka huu 2016, majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kuchambua sheria ndogo zilizotungwa ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo itabainika kwamba sheria ndogo yoyote ipo kinyume na masharti ya kikatiba, sheria mama au sheria nyingine yoyote, sheria ndogo hiyo itahesabika kuwa ni batili kwa kiwango ambacho imekiuka Katiba, Sheria mama au sheria nyingine yoyote ya nchi kwa mujibu wa Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria za Nchi, Sura ya Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati yetu umejengwa katika dhana ya udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa sheria ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo huweka taratibu, kanuni, masharti na adhabu mbalimbali kwa lengo la kuratibu mwenendo, ustawi wa jamii na ukusanyaji wa mapato. Sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa muundo wa uchumi wa Tanzania unahuisha kwa kiasi kikubwa shughuli za kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, gesi, uvuvi na biashara kama inavyothibitishwa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyeitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge hili la Kumi na Moja, aliposema, na naomba ninukuu:

“Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa kiasi kikubwa ni nchi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii inatokana na ukweli kwamba, sehemu kubwa ya watu wetu wapatao 75% wanaishi vijijini na wanategemea kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya maisha yao.”

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa shughuli hizo huwekewa taratibu mbalimbali ili kuzistawisha na kuziwezesha kuwa na manufaa kwa kutungiwa sheria ndogo. Hata hivyo, utungaji wa sheria hizo katika maeneo mengine umekuwa ukilalamikiwa, mathalan, katika Sekta ya Kilimo wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo wamekuwa wakilalamika mara kwa

mara kwamba sheria nyingi ndogo zinaweka tozo na kodi mbalimbali ambazo badala ya kuwapa unaifuu, zinawaongezea gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba bila ya kuwepo kwa udhibiti madhubuti wa Kibunge wa sheria ndogo ambazo zinagusa jamii na shughuli za kiuchumi za wananchi walio wengi, uwepo wa Bunge kama chombo cha uwakilishi hautakuwa na tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kwamba Bunge la Kumi na Moja lina malengo ya kuhakikisha kuwa jithada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuondoa kero mbalimbali zinaungwa mkono kwa vitendo. Hivyo basi, Kamati ya Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge itahakikisha kuwa inazishughulikia sheria ndogo ambazo ni kero bila kuathiri nia njema ya uwepo wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, kama ambavyo zimeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa sheria ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, ya Sheria Mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo hutungwa mara kwa mara kwa ajili ya utekelezaji wa sheria mama katika masuala mbalimbali. Baada ya kusainiwa na mamlaka inayohusika, sheria ndogo hutangazwa katika gazeti la Serikali ambalo huchapishwa kila wiki kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha (4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, sheria ndogo zinajumuisha yafuatayo: Orders (Amri), Proclamations (Matamko), Rules (Kanuni), Rules Of Court (Kanuni Za Mahakama), Regulations (Kanuni za Kawaida), Notices (Taarifa), By-Laws (Sheria Ndogo za Halmashauri) na Instruments (Hati).

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo zilizotungwa ni nyingi na kwa hali yoyote ile, Kamati yetu haiwezi kuzichambua zote na kwa ukamilifu katika Bunge la Kumi na Moja. Kwa sababu hiyo, basi kwa mamlaka inayopatikana katika Kanuni ya 117(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo: kufanya uchambuzi wa sheria ndogo zote zilizowasilishwa katika Mkutano wa Bunge uliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka sharti kwamba sheria ndogo yoyote iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge ni lazima iwasilishwe Bungeni kama nilivyosema ndani ya siku sita kuanzia Bunge lilipoanza kukaa na baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge kupokea sheria ndogo hiyo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadaye kutoa maoni na ushauri wake kuhusu yaliyomo katika sheria ndogo husika na hatua ambazo Bunge linaweza kuchukua. Hatua hizo ambazo Bunge linaweza kuzichukua ni pamoja na zifuatazo kwa mujibu wa sheria:-

Kwanza, kutoa azimio la kuzuia kutumika kwa sheria ndogo husika kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kikamilifu kutokana na maoni ya Kamati kwamba sheria ndogo fulani haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, ya sheria mama na sheria nyingine ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii hutokea endapo Waziri mwenye dhamana na sheria ndogo husika atakataa kufanya marekebisho ambayo Kamati imependelekeza kabla ya kusomwa kwa taarifa ya azimio hilo Bungeni. Aidha, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kuwa sheria ndogo fulani haikuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali kinyume na Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

Pili, kufanya marekebisho au kuibadilisha sheria ndogo yoyote kufuatia azimio la kuzuia kutumika kuitishwa na Bunge kwa mujibu wa Kifungu cha 38(4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Bunge linaweza kuitisha azimio muda wowote ili kuirekebisha au kuibadili sheria ndogo yoyote iliyoziwa kutumika kwa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ambayo Bunge linaweza kuchukua ni kufanya uchambuzi wa sheria ndogo yoyote ambayo inatumika. Kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa sheria ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiwekea, uchambuzi huu huzingatia maoni ya Wajumbe na wadau wengine kuhusiana na utekelezaji wa sheria ndogo hizo katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ni kufanya mikutano ya wazi kwa lengo la kusikiliza maoni ya wadau kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo zinazowagusa. Kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hualika wadau mbalimbali kwa madhumuni ya kusikiliza maoni yao kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo zinazofanyiwa uchambuzi au sheria ndogo nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano hii ni nyenzo muhimu kwa Kamati wakati wa uchambuzi katika kujiridhisha iwapo sheria ndogo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha uchambuzi wake, Kamati huibua hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufanuzi katika maeneo ya sheria ndogo yenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Wizara inayoguswa, hoja zinazoibuliwa na Kamati huwajibika kutoa majibu kuhusiana na sheria ndogo ambayo inaisimamia. Aidha, kwa kuzingatia utekelezaji bora wa masharti ya Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kifungu cha (8) cha Sheria ya *The Office of the Attorney General (Discharge of Duties)* ya mwaka 2005, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hushirikishwa katika mchakato wa uchambuzi unaofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo, kama ambavyo imefafanuliwa hapo awali, Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kikisomwa pamoja na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kinaweka masharti ambapo Serikali inawajibika kuwasilisha Bungeni sheria ndogo zote ambazo zimetangazwa katika gazeti la Serikali tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliotangulia. Hivyo, Kamati imefanya uchambuzi wa sheria ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge ifuatavyo: Mkutano wa Pili wa Bunge, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati unahusisha sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa (bylaws) pamoja na kanuni za Wizara na taasisi mbalimbali (*rules and regulations*). Maelezo ya ufanuzi kuhusu uchambuzi wa kila sheria ndogo uliofanywa na Kamati yanapatikana katika jedwali la uchambuzi ambalo naamini kwamba wasaidizi wa Kamati wataendelea kusambaza kwa Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo limeambatanishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kisheria wa kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa madaraka ya kutunga sheria ndogo chini ya Kifungu cha 153 cha Sheria za Serikali za Mitaa, yaani Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287. Kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji, Sura ya 288 pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, ni kwa malengo yafuatayo:-

- (i) Kuweka misingi thabiti ya utawala bora katika mipaka ya Halmashauri;

- (ii) Kuimarisha ustawi wa jamii, afya na ulinzi wa wakazi wa Halmashauri husika; na
- (iii) Kuweka masharti ya utekelezaji bora wa sheria mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo zinazotungwa na Halmashauri zinatarajiwa kukidhi matakwa ya Katiba ya nchi, sheria za Serikali za Mitaa, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na sheria nyingine yoyote ya nchi ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na amani, utii wa sheria na ustawi bora wa wananchi wa maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi uliofanywa, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya sheria ndogo zilizotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zina dosari zifuatazo: Kwanza, sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama. Katika hili, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka masharti kwamba, sheria ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya sheria ya Bunge...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba usubiri kidogo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) naongeza nusu saa ili tuweze kumaliza shughuli zetu za leo. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM A. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Narudia. Katika uchambuzi uliofanywa na Kamati tulibaini kuwa baadhi ya sheria ndogo zilizotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (*bylaws*) zina dosari zifuatazo: Kwanza, kuhusu sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka masharti kwamba, sheria ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka au sheria nyingine yoyote. Kamati ilibaini kuwa baadhi ya sheria ndogo za Halmashauri zinakwenda kinyume na masharti hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika sheria ndogo za ushuru wa mazao ya misitu za Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge ya mwaka 2015 ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kifungu cha Sheria ndogo hiyo kinaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi 100,000/= kutokana na makosa yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu ya faini iliyotolewa na kifungu cha sheria ndogo hii, iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 67 cha sheria mama, yaani Sura ya 290 ambacho kinazitaka Halmashauri kuweka

adhabu ya faini isiyozidi sh. 50,000/=. Aidha, adhabu hii haiwezi kutekelezeka kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 74(3) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza kinachosema, naomba ninukuu:

*“Where in a written law a maximum penalty and a minimum penalty are specified in respect of an offence, the offence is punishable by a penalty not less than that minimum nor greater than that maximum.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi ya kifungu hicho cha sheria, iwapo sheria yoyote iliyotungwa imeweka ukomo wa chini au ukomo wa juu wa adhabu katika kosa, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu isiyopungua au kuzidi ukomo uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI ifanye marekebisho katika sheria ndogo zote za Halmashauri ambazo ziko kinyume na sheria mama kwa kuvifuta na kuviandika upya vifungu vyote ambavyo vinaweka adhabu ya faini kubwa kuliko kiwango kilichowekwa na sheria mama. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri hazizingatii misingi ya utungaji wa sheria ndogo kwa kuweka masharti na adhabu ambazo zinakiuka masharti ya sheria mama. Hali hii inatokana na hisia kwamba sheria za Serikali za Mitaa zilizotungwa na Bunge zinaweka kiwango kidogo cha adhabu ya faini ukilinganisha na ukubwa wa baadhi ya makosa yanayoweza kutendwa na kushughulikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati yetu inashauri kwamba hisia hizi kama hazipaswi kuhalalisha Halmashauri hizo kutunga sheria ndogo zinazoweka adhabu kubwa kinyume na masharti yaliyomo katika sheria mama. Hivyo basi, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kufanya marekebisho ya viwango vya faini na adhabu vilivyopitwa na wakati kwa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mama husika, iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba na sheria za Bunge, Kamati imebaini kuwepo kwa sheria ndogo za baadhi ya Halmashauri ambazo zina vifungu ambavyo vinaweza kutafsiriwa kuwa vinakiuka misingi ya haki za binadamu. Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za Kilimo Kwanza na Usalama wa Chakula za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za Mwaka 2015, Kifungu cha 16(d) cha Sheria Ndogo hiyo kinamlazimisha mfugaji kuijunga na Vyama vya Wafugaji na Wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri dhamira ya kifungu hicho, kitendo cha kumlazimisha mfugaji kujunga na kikundi chochote ni kinyume na Ibara ya 20(1) ya Katiba ambayo inampa kila mtu haki na uhuru wa kushirikiana na watu wengine kwa hiari yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wetu ni kuishauri Ofisi ya Rais, TAMISEMI ifanye marekebisho ili kifungu hiki kibainishe masharti ya kuhamasisha wafugaji kujunga na Vyama vya Wafugaji na Wajasiriamali au kuweka sharti linalompa mfugaji uhuru wa kujunga na vyama hivyo kwa kutumia maneno ya "kila mfugaji anaweza kujunga" badala ya kulazimisha kila mtu awe mwanachama wa kikundi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelekee uchambuzi wa kanuni zilizotungwa na Wizara na Taasisi mbalimbali, yaani *rules and regulations*. Kanuni zinazotungwa na Wizara mbalimbali hutungwa kwa utaalam na mara nyingi uandishi wake unalenga kufafanua kwa kina masharti yanayopatikana katika Sheria mama iliyotungwa na Bunge. Hata hivyo, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Kanuni mbalimbali zilizowasilishwa Bungeni, baadhi zilibainika kuwa na dosari ambazo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama ambavyo inaonekana katika jedwali la uchambuzi lililoambatishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya Kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni inayohusu uagizaji wa mafuta kwa pamoja (*The Petroleum Bulk Procurement regulations*) ya mwaka 2015: Sheria ndogo hii imetungwa chini ya vifungu vya 168 na 258 vya sheria ya *The Petroleum Act*. Na. 21 ya mwaka 2015 kwa lengo la kuanzisha mfumo wa uagizaji wa pamoja wa bidhaa za petrol. Mfumo huu una malengo ya kuhakikisha kuwa bidhaa za petrol zinakuwepo katika soko kwa wakati na kwa kiwango stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwepo kwa mambo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ukamilifu ili kuiboresha sheria ndogo hii ili iweze kukidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyingine za nchi. Kwa mfano, Kanuni ya 15 (7) ya sheria ndogo hii inaweka masharti kwamba Waziri anaweza kuzuia bidhaa za petrol zinazosafirishwa nje ya nchi (*on transit petroleum products*) ili zitumike ndani ya nchi katika mazingira ya dharura yatakayobainishwa na Waziri (*localization of transit petroleum products under emergency conditions declared by the Minister*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni ya Kamati, Kanuni hii inampa mamlaka makubwa Waziri na endapo yasipotumika vyema, yanaweza kuhtarisha mahusiano ya kibashara na nchi za jirani. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni ya Kamati, masharti yanayopatikana katika Sheria mama yako wazi kuhusu mazingira ambayo Waziri anaweza kuagiza mafuta yauzwe nchini endapo kutatokea upungufu wa bidhaa za *petrol*. Mazingira hayo ni pamoja na vita au hali yoyote ambayo inasababisha upungufu wa bidhaa za *petrol* kwa mujibu wa Kifungu cha 253(2) cha sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kanuni ya 15(7) ya sheria ndogo hii inampa Waziri Mamlaka ya kuamuru mafuta ambayo yako njiani kwenda nchi za nje kutumika nchini katika mazingira ya tahadhari atakayotangaza Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri masharti ambayo yanapatikana katika Sheria mama, Kamati inashauri kwamba Kanuni ya 15(7) ya Sheria ndogo hii ifanyiwe marekebisho kufafanua haya masharti na maana halisi inayopatikana katika Kifungu cha 253 cha Sheria mama ili kuendana na dhamira ya Bunge wakati inatunga Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 14(4) ya sheria ndogo hii inazitaja bidhaa za *petrol* ambazo zitakuwa zinaagizwa kwa kutumia mfumo wa uagizaji kwa pamoja (*Bulk procurement system*). Bidhaa hizo ni pamoja na mafuta ya taa, mafuta ya magari, mafuta mazito ya kuendeshea mitambo, mafuta ya ndege na gesi inayotumika majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba, Wizara ikamilishe haraka maandalizi ya utaratibu utakaowezesha bidhaa zote za mafuta ambazo Kanuni ya 14(4) ya sheria ndogo hiyo inaagiza ziingizwe nchini kwa mfumo wa *Bulk Procurement System*. Hatua hii itawezesha kushuka kwa bei za bidhaa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo wetu hapa ni kwamba tunafahamu ziko baadhi ya bidhaa ambazo sasa hivi zinaagizwa kupitia utaratibu huu. Sasa ushauri wa Kamati ni kwamba tukamilishe zoezi kwa bidhaa nyingine ambazo hazijaingia katika mfumo wa uagizaji wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *the petroleum retail operations in townships and villages rules* ya mwaka 2016: Kanuni hizi zimetungwa kwa malengo ya kuratibu shughuli zinazohusiana na biashara ya bidhaa za petroli katika miji na vijiji ndani ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo hii inatokana na Sheria ya Petrol ya Mwaka 2015 iliyotungwa na Bunge. Uchambuzi wa Kamati katika sheria ndogo hii ulibaini dosari nyingi ambazo zinaweza kusababisha uhalali wa matumizi ya sheria ndogo hiyo kuhojiwa. Kwa mfano, sheria ndogo imerejea Kifungu cha 5(3) cha Sheria ya Petrol kwamba ndicho kinachotoa Mamlaka ya kutungwa kwake badala ya Kifungu cha 259(1) ambacho ndicho kinampa Mamlaka Waziri kutunga Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 11(3) inaweka adhabu ya faini ya shilingi milioni tano kwa kosa la kuendesha shughuli bila kibali. Adhabu hiyo iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 131(4) cha Sheria mama ambacho kimeweka adhabu ya faini ya kiasi cha fedha kisichopungua shilingi milioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake mbele ya Kamati, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, alisema kuwa, Sheria ndogo iliyochambuliwa na Kamati ilitungwa kimakosa kutokana na sheria ya Petrol ya mwaka 2008 ambayo kwa sasa imefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo na kwa kuzingatia dosari zilizobainika katika sheria ndogo iliyochambuliwa, Kamati inaishauri Wizara ya Nishati na Madini kuifuta mara moja sheria ndogo hii ili isiendelee kutumika na badala yake Wizara itunge Kanuni mpya haraka iwezekanavyo ambazo zitaendana na masharti ya Sheria ya Petrol ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako tu, ni bahati njema kwamba katika ushauri huu Serikali ilielewa ushauri wa Kamati na ikasema itazingatia kupitia maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *the Drugs Control and Enforcement General Regulations* za mwaka 2016: Kanuni hizi zimetungwa chini ya Kifungu cha 67 cha sheria inayoitwa *The Drugs Control and Enforcement Act, chapter ya 95* ambayo imetungwa na Bunge kwa malengo ya kuweka masharti ya kudhibiti madawa ya kulevyta, kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Matumizi ya Madawa hayo na Usafirishaji Wake pamoja na masuala mengine yanayohusiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 14 inaweka masharti yanayoratibu zoezi la kuharibu madawa ya kulevyta yaliyokamatwa. Kanuni ya 14(1) imewataja watu ambao ni lazima wawepo katika zoezi hilo litakaloteklezwa. Watu hao ni pamoja na Jaji au Hakimu, Mwakilishi wa Kamishna wa Madawa ya Kulevyta, Inspekte Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkemia Mkuu,

Mwakilishi kutoka Baraza la Mazingira la Taifa na Usalama wa Taifa na mtu mwingine yeyote ambaye Kamishna wa Madawa ya Kulevyta atamteua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kanuni ya 14(2) inaweza masharti kwamba, Kamishna wa Madawa ya Kulevyta au Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru madawa ya kulevyta yaliyokamatwa yaharibiwe bila kuwashirikisha watu wanaotajwa katika kifungu cha 14(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, matakwa ya kanuni ya 14(2) yanakinzana na kanuni ya 14 (3) inayotaka wakati wa kuharibu madawa kuzingatiwe ulinzi wa afya, usalama na halikadhalika ulinzi wa mazingira. Hivyo basi, kukosekana kwa watu waliotajwa katika kanuni ya 14, yaani ile orodha ya watu wale, kanuni ndogo ya (1), kunaweza kuchangia ukiukwaji wa kanuni ya 14(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kanuni ya 14(5) na 14(7) zinaweza masharti kwa Jaji au Hakimu aliyeshudhia kuharibiwa kwa madawa yaliyokamatwa kujiridhisha kwamba yote yameharibiwa na hatimaye kujaza fomu ya kuthibitisha hilo. Hivyo basi, kutokuwepo kwa Jaji au Hakimu kwa mujibu wa kanuni ya 14(2) kunaweza kusababisha zoezi hilo kutokamilika kisheria. Kamati inashauri kuwa kanuni ya 14 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa mazingira yenye utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kanuni za uasili wa watoto za mwaka 2012: Kanuni hizi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngeleja, nakupa dakika mbili umalizie.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA SHERIA**  
**NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilidhani kwamba kwa muda ulioongezwa, bado kama dakika tano tu hivi, ningeweza kumalizia. Sasa kwa sababu nilishasema taarifa hii itaingia kwenye Hansard kama kawaida, nihitimishe tu kwa kuwashukuru sana viongozi wa Bunge wakiongozwa na Mheshimiwa Spika pamoja na Kamati ya Uongozi kwa mara ya kwanza kwa kuridhia taarifa hii iwasilishwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba tunafungua ukurasa mpya wa utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu sana wa kuwaondolea kero wananchi wetu ambao wanaguswa na mkanganyiko wa sheria ndogo ambazo zimetungwa na Mamlaka ambazo zimekasimiwa na Bunge letu Tukufu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mawaziri wote waliojitekeza kwenye Kamati kutoa ufanuzi wa maeneo mbalimbali ambapo Kamati yetu iliomba ufanuzi wa ziada, Wajumbe wa Kamati kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge amba walipata nafasi ya kushiriki nje ya Kamati yetu, wadau wote waliotoka sehemu mbalimbali za nchi yetu kushirikiana na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utendaji, tunamshukuru sana Dkt. Kashillilah kama Katibu wa Bunge pamoja na wasaidizi wake. Katika Kamati yetu tuna Makatibu Wasaidizi wa Bunge akiwemo Yona Kirumbi, tuna Mkuta Masoli pale, Angela Shekifu, tuna Bwana Stanslaus Kagisa na Paul Chima. Kwa pamoja, tunawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii isingekamilika kama isingekuwa jahazi hili linaongozwa vyema kabisa na Mwenyekiti wetu mahiri wa Kamati ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge ambaye sisi tunamwita encyclopaedia katika masuala haya ya sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja, kulipa Bunge lako litafsiri na kuazimia endapo itawezekana ili haya tuliyoyapendekeza na kuyapitia kwa sababu tumeshaelewana na Serikali, Bunge liwe sehemu ya maazimio yake na hatimaye utekelezaji wake uendelee. Nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, sasa itabidi urudie kutoa hoja kwa sababu hayo maneno mengine yote uliyoongeza, sina uhakika Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa kuunga mkono hoja *at what point*.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

## TAARIFA YA KWANZA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 MAELEZO YA AWALI

1.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa mamlaka uliyo nayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge<sup>1</sup> ili Kamati yangu iweze kuwasilisha **Taarifa ya Kwanza ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo** uliofanywa Kamati. Taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Moja.

1.1.2 **Mheshimiwa Spika**, natumaini kuwa Waheshimiwa Wabunge wataitumia Taarifa hii kutoa ushauri zaidi kuhusu Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumika. Aidha, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanya kazi mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wabunge.

### 1.2 MADARAKA YA KUTUNGA SHERIA

1.2.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu chenye mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambaao utafuatwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

1.2.2 Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga Sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa Sheria, Ibara ya 97 (5) inalipa Bunge mamlaka ya kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yejote au idara yoyote ya Serikali. Malengo ya Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria ni kuvipa vyombo hivyo fursa ya kuweka masharti ambayo ni mahsus (*specific*) kwa utekelezaji wa masharti ambayo ni ya jumla yaliyowekwa kupitia Sheria mbalimbali (*Principal Acts*) zilizotungwa na Bunge.

---

<sup>1</sup> Toleo la Januari, 2016

1.2.3 **Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge huitwa Sheria Ndogo (*subsidiary legislation/delegated legislation*) na hujumuisha Kanuni mbalimbali (*rules and regulations*) pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*).

### 1.3 DHANA YA UDHIBITI WA KIBUNGE WA SHERIA NDOGO

1.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Udhibiti wa Kibunge wa Utungaji wa Sheria Ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) siyo dhana mpya katika mgawanyo wa madaraka ya dola katika nchi za Jumuiya ya Madola. Udhibiti huu una lengo la kuhakikisha kwamba, Bunge linajiridhisha kikamilifu kwamba madaraka ya kutunga sheria liliyokasimu kwa mamlaka nyingine yanatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia masharti ya Sheria Mama iliyoruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo. Mwandishi maarufu wa vitabu vya sheria C. K. Takwani<sup>2</sup> aliandika yafuatayo:-

*"...it is open for the Parliament to confer power upon anyone it likes. If the Parliament delegates its legislative powers to any other authority such as executive, it also has the obligation to see if those powers are properly exercised by the administration..."*

Kwa tafsiri isiyo rasmi kwa Kiswahili, tunaweza kusema kuwa:- "...Bunge limeachwa liweze kutoa sehemu ya madaraka yake ya kutunga sheria kwa yejote ambaye Bunge litapenda. Bunge likikasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine yoyote kama vile Serikali, litakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa madaraka hayo yanatekelezwa ipasavyo." Kwa maoni ya mwandishi huyo, ni wazi kuwa Bunge lisipokuwa na utaratibu wa kudhibiti/kujiridhisha kuhusu utungaji wa Sheria Ndogo, litakuwa halijajipanga kutekeleza wajibu wake wa msingi.

1.3.2 **Mheshimiwa Spika**, dhana ya Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo imeelezwa kwa kiasi cha kutosha kueleweka katika machapisho mbalimbali ya fani ya Sheria na masuala ya Bunge. Kwa mfano, katika insha ya kisheria iliyandikwa na Bharat Raj, mwandishi huyo aliandika maneno yafuatayo kubainisha umuhimu wa uwepo wa mfumo wa utungaji wa Sheria Ndogo nje ya Bunge na ulazima wa Bunge kusimamia na kudhibiti utungaji wa Sheria Ndogo hizo:-

---

<sup>2</sup> Takwani C.K, (2008) Lectures on Administrative Law, 4th edition, Lucknow: Eastern Book Company.

"Delegated legislation is often criticized as an excuse for the legislators, a shield for the administrators and a provocation for the Constitutional purists. However, the very mechanism of delegated legislation cannot and should not be reduced to an evil because it is at the end of the day a necessity. In the modern world where social, economic, technological, and administrative speed outstrips the placid traditional legislative processes, delegated legislation is an essential means of survival. Thus, since it is the legislature which delegates power, it is primarily for it to supervise and control the exercise of this power, and ensure against its objectionable, abusive & unwarranted use.<sup>3</sup>"

### 1.3.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi, nukuu hiyo inasema:-

"Sheria Ndogo zinalalamikiwa kutumiwa kama udhuru wa Watunga Sheria, ngao kwa watawala na jambo linalowaudhi wanaufasaha wa Kikatiba. Hata hivyo, utaratibu wenyewe wa Sheria Ndogo hauwezi na haustahili kushushwa kiasi cha kuwa ubaya kwa sababu mwishowe ni jambo la lazima. Katika ulimwengu wa leo, ambapo kasi ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na kiutawala inazidi mchakato wa kawaida wa utungaji Sheria, Sheria Ndogo ni njia ya lazima kuwepo. Hivyo, kwa kuwa ni Bunge linalokasimu madaraka yake ya kutunga Sheria, kimsingi linapaswa kusimamia na kudhibiti matumizi ya madaraka hayo na kuwa na uhakika kwamba madaraka hayo, hayatumiki isivyofaa, vibaya na wala isivyo kubalika."

1.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) imeweka masharti maalum ambayo yanalipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Udhibiti huo sio wa moja kwa moja kwa sababu Bunge halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa Sheria Ndogo yoyote mpaka itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni.

1.3.5 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Mama inapotungwa na Bunge inaweza kuweka masharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote inaweza kutungwa kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mama. Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria<sup>4</sup> kinaweka masharti ya jumla ya kuzingatiwa wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo na moja kati ya masharti hayo ni kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kuwa kinyume na Sheria Mama.

---

<sup>3</sup> Bharat Raj (2016) Parliamentary Control of Delegated Legislation with Reference to Consultation of Affected Interest: Hidayatullah National Law University, Chhattisgarh

<sup>4</sup>Sura ya 1, Toleo la 2002

1.3.6 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria<sup>5</sup>, Sheria Ndogo hiyo inapaswa kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao vya Bunge (*six sitting days*) kwa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (1).

1.3.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuona umuhimu wa kufanya Udhhibit wa Utungaji wa Sheria Ndogo, Bunge la Tanzania kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola, limeunda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo inatekeleza majukumu hayo kwa niaba ya Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 majukumu ya Kamati hii ni kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.3.8 **Mheshimiwa Spika**, endapo itabainika kwamba, Sheria Ndogo yoyote iko kinyume na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote, Sheria Ndogo hiyo itahesabika kuwa ni batili kwa kiwango ambacho imekiuka Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote ya nchi (*void to the extent of inconsistency*) kwa mujibu wa Kifungu cha 36 (1) ca Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

#### 1.4 MSINGI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

1.4.1 **Mheshimiwa Spika**, msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati umejengwa katika Dhana ya Udhhibit wa Kibunge wa Sheria Ndogo. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoismamia Serikali.

1.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo huweka taratibu, kanuni, masharti na adhabu mbalimbali kwa lengo la kuratibu mwenendo, ustawi wa jamii na ukusanyaji wa mapato. Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania.

1.4.3 **Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa Muundo wa Uchumi wa Tanzania (*Structure of Tanzania Economy*) unahuisha shughuli za kilimo, ufgajji, uchimbaji madini, gesi, uvuvi na biashara kama inavyothibitishwa katika Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli aliyoitua wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja aliposema:-

---

<sup>5</sup> ibid

"Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kiasi kikubwa ni nchi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii inatokana na ukweli kwamba, sehemu kubwa ya watu wetu wapatao asilimia sabini na tano (75%) wanaishi vijiji na wanategemea kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya maisha yao."

1.4.4 **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa shughuli hizo huwekewa taratibu mbalimbali ili kuzistawisha na kuziwezesha kuwa na manaufaa kwa watu kwa kutungiwa Sheria Ndogo. Hata hivyo, utungaji wa Sheria hizo katika maeneo mengine umekuwa ukilalamikiwa. Mathalani, katika Sekta ya Kilimo, wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo wamekuwa wakilalamika mara kwa mara kwamba Sheria Ndogo nyingi zinaweka tozo na kodi mbalimbali ambazo badala ya kuwapa unafuu, zinawaongezea gharama. Ni dhahiri kabisa, bila kuwepo kwa udhibiti madhubuti wa Kibunge wa Sheria Ndogo ambazo zinagusa jamii na shughuli za kiuchumi za wananchi walio wengi, uwepo wa Bunge kama chombo cha uwakilishi hautakuwa na tija inayokusudiwa.

1.4.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba, Bunge la Kumi na Moja lina malengo ya kuhakikisha kuwa, jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuondosha kero mbalimbali, zinaungwa mkono kwa vitendo. Hivyo basi, Kamati ya Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge, itahakikisha kuwa inazishughulikia Sheria Ndogo ambazo ni kero bila kuathiri nia njema ya uwepo wa Sheria hizo.

## 1.5 NAMNA AMBAVYO KAMATI INATEKELEZA MAJUKUMU YAKE

1.5.1 **Mheshimiwa Spika**, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.5.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hutungwa mara kwa mara kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Baada ya kusainiwa na Mamlaka inayohusika, Sheria Ndogo hutangazwa katika Gazeti la Serikali ambalo huchapishwa kila Ijumaa kwa mwaka mzima. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria<sup>6</sup>, Sheria Ndogo zinajumuisha yafuatayo:-

- a) Orders (Amri)
- b) Proclamations (Matamko)
- c) Rules (Kanuni)
- d) Rules of Court (Kanuni za Mahakama)
- e) Regulations (Kanuni)

<sup>6</sup>Toleo la 2002

- f) Notices (Taarifa)
- g) By - Laws (Sheria Ndogo za Halmashauri)
- h) Instruments (Hati)

1.5.3 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zilizotungwa ni nyingi na kwa hali yoyote, Kamati haiwezi kuzichambua zote na kwa ukamilifu katika Bunge la Kumi na Moja. Kwa sababu hiyo basi, kwa mamlaka inayopatikana katika Kanuni ya 117 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

**a) Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika Mkutano wa Bunge uliotangulia**

Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka sharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge ni lazima iwasilishwe Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao (*six sitting days*) baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Baada ya Bunge kupokea Sheria Ndogo hiyo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri wake kuhusu yaliyomo katika Sheria Ndogo husika na hatua ambazo Bunge linaweza kuchukua. Hatua hizo kwa mujibu wa Sheria ni pamoja na zifuatazo:-

i) **Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo husika (disallowance resolution)** - Kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kikamilifu kutohana na maoni ya Kamati, kwamba Sheria Ndogo fulani haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine ya nchi.

**Hatua hii hutokea endapo Waziri mwenye dhamana na Sheria Ndogo husika atakataa kufanya marekebisho ambayo Kamati imependekeza kabla ya kusomwa kwa Taarifa ya Azimio hilo Bungeni.**

Aidha, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kuwa Sheria Ndogo fulani haikuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao (*six sitting days*) baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kinyume na Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

ii) **Kufanya marekebisho au kuibadili Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Bunge (amendment and substitution)** - Kwa mujibu wa kifungu cha cha 38 (4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Bunge linaweza kupitisha Azimio muda wowote ili kuirekebisha au kuibadili Sheria

Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika kwa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

b) **Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote ambayo inatumika**

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojojiwekea. Uchambuzi huu huzingatia maoni ya Wajumbe na wadau wengine kuhusiana na utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo katika Sekta mbalimbali.

c) **Kufanya mikutano ya wazi kwa lengo la kusikiliza maoni ya wadau kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo zinazowagusa.**

Kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hualika wadau mbalimbali kwa madhumuni ya kusikiliza maoni yao (*public hearing*) kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo zinazofanyiwa uchambuzi au Sheria Ndogo nyingine yoyote.

Mikutano hii ni nyenzo muhimu kwa Kamati wakati wa uchambuzi katika kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.5.4 **Mheshimiwa Spika**, ni vyema Bunge lako tukufu likafahamu kwamba, wakati wa Uchambuzi wa Sheria Ndogo, Kamati huzingatia masuala mbalimbali ili kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo hizo zimekidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Mambo ambayo huzingatiwa ni pamoja na yafuatayo:-

a) Iwapo Sheria Ndogo husika inavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Iwapo Sheria Ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting issues*);

d) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo Sheria Ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

f) Maudhui ya jumla ya Sheria Ndogo husika.1.5.5

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha uchambuzi wake, Kamati huibua hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufanuzi katika maeneo ya Sheria Ndogo yenye dosari.

Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kutoa majibu kuhusiana na Sheria Ndogo ambayo inaisimamia.

**1.5.6 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia utekelezaj bora wa masharti ya Ibara ya 59 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kifungu cha 8 cha Sheria ya *The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, 2005*, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hushirikishwa katika mchakato wa uchambuzi unaofanywa na Kamati.

## 2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO

### 2.1 SHERIA NDOGO ZILIZOCHAMBULIWA

2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo imefafanuliwa hapo awali, Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria<sup>7</sup> kikisomwa pamoja na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kinaweka masharti ambapo Serikali inawaijibika kuwasilisha Bungeni Sheria Ndogo zote ambazo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliotangulia. Hivyo, Kamati imefanya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge ifuatayo:-

- a) Mkutano wa Pili wa Bunge
- b) Mkutano wa Tatu wa Bunge
- c) Mkutano wa Nne wa Bunge

---

<sup>7</sup>Op Cit

2.1.2 **Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati unahusisha Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa (By – Laws) pamoja na Kanuni za Wizara na Taasisi mbalimbali (Rules and Regulations). Maelezo ya ufanuzi kuhusu uchambuzi wa kila Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati yanapatikana katika Jedwali la Uchambuzi ambalo limeambatishwa pamoja na Taarifa hii.

## 2.2 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOTUNGWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (BY – LAWS)

2.2.1 **Mheshimiwa Spika**, msingi wa kisheria wa kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni lbara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo chini ya Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, Kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kwa malengo yafuatayo:-

- a) Kuweka misingi thabiti ya utawala bora katika mipaka ya halmashauri;
- b) Kuimarisha ustawi wa jamii, afya na ulinzi wa wakazi wa halmashauri husika; na
- c) Kuweka masharti ya utekelezaji bora wa Sheria mbalimbali za nchi.

2.2.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri zinatarajiwa kukidhi matakwa ya katiba ya nchi, Sheria za Serikali za Mitaa, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Sheria nyingine yoyote ya nchi ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na amani, utii wa Sheria na ustawi bora wa Wananchi wa maeneo husika.<sup>8</sup>

<sup>8</sup> Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, Toleo la 2002

2.2.3 **Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi uliofanywa, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (By – Laws) zina dosari zifuatazo:-

a) **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka masharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka au Sheria nyingine yoyote.<sup>9</sup> Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) zinakwenda kinyume na masharti hayo.

Kwa mfano, katika **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ya Mwaka, 2015<sup>10</sup>** ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (**Sura ya 290**), Kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kinaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki moja (100,000/=) kutokana na makosa yaliyoainishwa. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

**“6. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;–**

- (a) atavuna na kusafirisha mazao ya misitu bila kibali;
- (b) atakiuka masharti ya kibali;
- (c) atachoma au kusababisha moto;
- (d) atakataa au kukwepa kulipa Ushuru;
- (e) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe Ushuru;
- (f) Kuchungia mifugo kwenye misitu ya Hifadhi.

atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki moja (100,000/=) au adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo na kulipa ushuru huo.”

**Mheshimiwa Spika**, adhabu ya faini iliyotolewa na kifungu cha Sheria Ndogo hii iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 67 cha Sheria Mama (Sura ya 290) ambacho kinazitaka Halmashauri kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=). Aidha, adhabu hii haiwezi kutekelezeka kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 74 (3) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinachosema:-

---

<sup>9</sup> Sura ya 1 Toleo la 2002

<sup>10</sup> GN No. 578 ya tarehe 18 Desemba, 2015

**"74 (3) Where in a written law a maximum penalty and a minimum penalty are specified in respect of an offence, the offence is punishable by a penalty not less than that minimum nor greater than that maximum."**

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya kifungu hicho cha Sheria, iwapo Sheria yoyote iliyotungwa imeweka ukomo wa chini au ukomo wa juu wa adhabu katika kosa, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu isiyopungua au kuzidi ukomo uliowekwa.

Kwa kuwa Kifungu hicho hakiweki ukomo wa juu wa adhabu, hakuna kizuizi kwa Mahakama kutoa adhabu ya faini ya shilingi laki tano (500,000/=) kwa sababu shilingi laki tano inazidi shilingi laki moja (100,000/=). Kamati inaamini kuwa, hilo sio lengo lilikusudiwa katika masharti ya Kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwagine ni Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi na Chumvi) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015 iliyotungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)<sup>11</sup>. Kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kinaweka ukomo wa faini ya shilingi laki tatu (300,000/=) kwa makosa mbalimbali yatokanayo na Sheria Ndogo hiyo. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

**"6. Mtu atakayekiuka au kwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini **isiyozidi shilingi 300,000/=** au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo, pamoja na kulipa ushuru anaodaiwa na gharama za usumbufu aliosababisha."**

Adhabu ya faini iliyotolewa na kifungu cha Sheria Ndogo hii pia iko kinyume na masharti ya Sheria Mama (Sura ya 290) ambayo inazitaka Halmashauri kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ifanye marekebisho katika Sheria Ndogo zote za Halmashauri ambazo ziko kinyume na Sheria Mama kwa kuvifuta na kuviandika upya vifungu vyote ambavyo vinaweka adhabu ya faini kubwa kuliko kiwango kilichowekwa na Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Halmashauri hazizingatii kabisa misingi ya utungaji wa Sheria Ndogo kwa kuweka masharti na adhabu ambazo zinakiuka masharti ya Sheria Mama.

---

11 GN No. 520 ya tarehe 20 Novemba, 2015

Hali hii inatokana na hisia kwamba, Sheria za Serikali za Mitaa zilizotungwa na Bunge zinaweka kiwango kidogo cha adhabu ya faini ukilinganisha na ukubwa wa baadhi ya makosa yanayoweza kutendwa na kushughulikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, hisia hizi kamwe hazipaswi kuhalalisha Halmashauri hizo kutunga Sheria Ndogo zinazoweka adhabu kubwa kinyume na masharti yaliyomo katika Sheria Mama. **Hivyo basi, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kufanya marekebisho ya viwango vya faini na adhabu vilivyopitwa na wakati kwa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mama husika, iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.**

b) **Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (unreasonable provisions)**

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya sifa za Sheria Ndogo nzuri ni ile ambayo inaweka masharti ambayo yanaendana na uhalisia, masharti yanayotekelzeza, yasiyo kandamizi na ambayo hayana utata. Kifungu cha 157 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 kinasema kwamba, kila Sheria Ndogo itakayotungwa na Halmashauri inatakiwa kuweka viwango vya ada na tozo ambazo zinaendana na uhalisia (*reasonable fees, charges and tariffs*).

**Mheshimiwa Spika**, katika Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, 2015<sup>12</sup>, kifungu cha 8 (1) kinaweka wajibu kwa kila mmiliki wa nyumba kuweka sehemu ya waenda kwa miguu yaani “pavement” mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.

Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo hii kinatoa tafsiri ya maneno mbalimbali na neno “pavement” maana yake ni sakafu imara ya mawe au matofali ya saruji au udongo yaliyochomwa na kujengewa kutoka katika nyumba hadi katika mfereji au barabara, kwa waendao kwa miguu au watazamaji wa vitu madukani.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri maudhui mema ya kuimarisha usafi wa mazingira wa Halmashauri hii, sharti hili la kisheria haliendani na uhalisia wa mambo kwa kuzingatia kuwa uamuzi wa kujenga “pavement” unabaki kwa mmiliki wa nyumba. Aidha, sharti hili linawezza kutafsiriwa kuwa linaingilia haki za kiuchumi za wananchi wa eneo hilo kwa kutaka kuwabebesha mzigo wa gharama za ujenzi zilizo nje ya uwezo wao.

---

<sup>12</sup> GN No. 15 ya tarehe 1 Januari, 2016

Kamati inashauri kuwa kifungu hiki kifutwe na ikibidi kiandikwe tena kwa kuweka sharti la uhamasishaji kwa wamiliki wa nyumba kujenga “pavements” na sio kuwalazimisha.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwagine ni Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015<sup>13</sup> ambayo imetungwa chini ya Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287. Kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hii kinaweka adhabu ya juu kabisa kwa mujibu wa Sheria (maximum fine) ya kulipa faini ya Shilingi 300,000/= kwa kosa la kutupa takataka ya aina yoyote katika eneo la barabara. Kifungu hiki kinasomeka kama ifuatavyo:-

“11. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa **takataka ya aina yoyote** kwenye eneo la barabara. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atalipa faini ya shilingi 300,000/= au kifungo kisichozi mwezi mmoja au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.” Msitizo ni wetu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sheria Ndogo hii, hakuna tafsiri ya neno “takataka” na hivyo Kamati ilishindwa kujua takataka hizo zinahusisha nini na ni kwa kiwango gani. Kwa maoni ya Kamati, kiwango cha faini iliyowekwa na Sheria Ndogo hii ni kikubwa ukilinganisha na kosa linalotajwa la kutupa takataka ya aina yoyote kwenye eneo la barabara. Aidha, kifungu hicho hakijatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu kwa kuzingatia ukubwa wa kosa kwa kuwa kimeweka adhabu ya juu kabisa (maximum fine).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Kifungu cha 43 (2) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinaweka masharti kwamba Sheria Ndogo inaweza kuweka faini ya juu kabisa au ya chini, Kamati inazishauri Halmashauri kuweka masharti yenye urahisi wa kubadilika (flexible) kwa adhabu katika baadhi ya makosa ili Mahakama iweze kutoa adhabu mbalimbali kulingana na ukubwa wa kosa.

c) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiuandishi na kiuchapaji**

**Mheshimiwa Spika**, makosa ya kiuandishi na kiuchapaji katika Sheria Ndogo yoyote yanaweza kusababisha athari hasi kwa watumiaji endapo masharti yatakayoandikwa au kuchapwa yatakuwa si yale yaliyokusudiwa. Aidha, dosari hizo zinaweza kusababisha mkanganyiko wa maana endapo Sheria fulani itahitaji kutafsiriwa na vyombo vya utoaji haki.

---

13 GN. No. 521 ya tarehe 20 Novemba, 2015

Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Uanzishajji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, 2015<sup>14</sup> ilibainika kuwa na makosa mengi ya uchapaji ambayo yanaweza kuharibu maana halisi iliyokusudiwa na kuleta mkanganyiko wa tafsiri. Makosa hayo yalibainika katika vifungu vya 7 (2), 21 (1), 26 (1) na 30 (1) kwa kukosekana kwa silabi mbalimbali. Kwa mfano, kifungu cha 26 (1) kinasomeka kama ifuatavyo:-

**“26. (1)** Fedha na vyanzo vya mapato ya kituo cha afya vitakuwa vifuatavyo:-

- (a) ichango ya jamii;
- (b) afadhili au michango ya washirika;
- (c) uzuku kutoka serikalini;
- (d) uzuku kutoka Halmashauari;
- (e) hanzo chochote halali.”

Aidha, dosari zilizobainika katika baadhi ya Sheria Ndogo, endapo zitabaki kama zilivyo, utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo unaweza ukawa na changamoto. Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015<sup>15</sup> kifungu cha 4 kinaweka sharti na kuainisha makosa kwa “mkazi” tu na kutoa mwanya kwa mtu mwingine yeyote ambaye si “mkazi” wa Babati kufanya makosa bila kubanwa na Sheria Ndogo hiyo. Sehemu ya kifungu hicho inasomeka kama ifuatavyo:-

**“4.- (1)** Ni wajibu wa kila mkazi wa eneo la Halmashauri kutunza na kuhifadhi barabara iliyoko katika eneo lake na iwe katika hali endelevu ya matumizi na kwamba hataruhusu kwa njia yoyote ile uharibifu wa barabara.” Msisitizo ni wetu.

d) **Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba na Mikataba ya Kimataifa iliyordhiwa. Bunge la Jamhuri ya Muungano lina wajibu wa kutunga Sheria ambazo zinazingatia misingi hiyo ili kuhakikisha kuwa, haki za binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa. Kila mamlaka ambayo imekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge, nayo inawajibika kuhakikisha kuwa inatunga Sheria Ndogo ambazo zinalinda na kuhifadhi haki hizo.

---

14 GN No. 599 ya tarehe 25 Desemba, 2015

15 GN No. 521 ya tarehe 20 Novemba, 2015

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Bunge, Kamati imebaini kuwepo kwa Sheria Ndogo za Halmashauri ambazo zina vifungu ambavyo vinaweza kutafsiriwa kuwa vinakiuka misingi ya haki za binadamu.

Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Kilimo Kwanza na Usalama wa Chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za Mwaka, 2015<sup>16</sup> kifungu cha 16 (d) cha Sheria Ndogo hiyo kinamlazimisha mfugaji kuijunga na vyama vya wafugaji na wajasiriamali. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

**“16. Kila Mfugaji..**

*(d) Atalazimika kuijunga na vyama vya wafugaji  
wajasiriamali...”*

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri dhamira ya kifungu hicho, kitendo cha kumlazimisha mfugaji kuijunga na kikundi chochote ni kinyume na Ibara ya 20 (1) ya Katiba<sup>17</sup> ambayo inampa kila mtu haki na uhuru wa kushirikiana na watu wengine kwa hiyari yake mwenyewe.

Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ifanye marekebisho ili kifungu hiki kibainishe masharti ya kuhamasisha wafugaji kuijunga na vyama vya wafugaji na wajasiriamali au kuweka sharti linalompa mfugaji uhuru wa kuijunga na vyama hivyo kwa kutumia maneno “kila mfugaji anaweza kuijunga”.

## **2.3 UCHAMBUZI WA KANUNI ZILIZOTUNGWA NA WIZARA NA TAASISI MBALIMBALI (RULES AND REGULATIONS)**

2.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni zinazotungwa na Wizara mbalimbali hutungwa kwa utaalim na mara nyingi uandishi wake unalenga kufafanua kwa kina masharti yanayopatikana katika Sheria Mama iliyotungwa na Bunge. Hata hivyo, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Kanuni mbalimbali zilizowasilishwa Bungeni, baadhi zilibainika kuwa na dosari ambazo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama ambavyo inaonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya Kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

---

16 GN No. 585 ya tarehe 18 Desemba, 2015

17 Sura ya 2 Toleo la 2002

**THE PETROLEUM (RETAIL OPERATIONS IN TOWNSHIPS AND VILLAGES) RULES, 2016  
(GN No. 174 ya tarehe 13 Mei, 2016)**

---

2.3.2 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa kwa malengo ya kuratibu shughuli zinazohusiana na biashara ya bidhaa za petroli katika miji na vijiji katika Tanzania Bara. Sheria Ndogo hii inatokana na Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 iliyotungwa na Bunge.

2.3.3 Uchambuzi wa Kamati katika Sheria Ndogo hii ulibaini dosari nyingi ambazo zinaweza kusababisha uhalali wa matumizi ya Sheria Ndogo hiyo kuhojiwa. Kwa mfano, Sheria Ndogo imerejea Kifungu cha 5 (3) cha Sheria ya Petroli kwamba ndicho kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwake badala ya Kifungu cha 259 (1) ambacho ndicho kinampa mamlaka Waziri kutunga Kanuni.

2.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 11 (3) inaweka adhabu ya faini ya shilingi milioni tano (5) kwa kosa la kuendesha shughuli bila kibali (*offence of conducting a regulated activity without a licence*). Adhabu hiyo iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 131 (4) cha Sheria Mama ambacho kimeweka adhabu ya faini ya kiasi cha fedha kisichopungua shilingi milioni ishirini (20).

2.3.5 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 45 na 46 katika Sheria Ndogo hii zinazungumzia utaratibu ambapo mwenye leseni atalipa gharama za decommission na site restoration. Kifungu cha 197 cha Sheria Mama kimeweka utaratibu tofauti ambapo kutaanzishwa Mfuko Maalum (*Decommissioning Fund*) ambapo wenyе leseni watatakiwa kuchangia katika kipindi cha leseni zao ili mwenye leseni atakayehitajika kufanya decommission na site restoration asiingie gharama kubwa wakati wa kufunga biashara husika.

2.3.6 Katika maelezo yake mbele ya Kamati, Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Mb) alisema kuwa, Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati ilitungwa kutokana na Sheria ya Petroli ya Mwaka 2008 ambayo ilifutwa. Kifungu cha 260 (2) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 kinaipa uhalali Sheria Ndogo hiyo kuendelea kutumika pamoja na kufutwa kwa Sheria iliyotoa mamlaka awali.

2.3.7 Hata hivyo, masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 260 (2) katika Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 yakisomwa pamoja na masharti ya Kifungu cha 33 (1) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria Ndogo hii itakuwa na uhalali wa kutumika chini ya Sheria iliyofutwa endapo tu, haitakuwa na masharti

yanayokinzana na Sheria mpya inayotumika. Kifungu cha 33 (1) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinasema:-

**"33 (1) (b)** Where an Act repeals and re-enacts an Act, with or without modification, any subsidiary legislation made under the repealed Act and in operation immediately before the commencement of the repealing Act shall, so far as it is consistent with the repealing Act, continue in operation and have effect for all purposes as if made under the repealing Act."

2.3.8 **Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hiyo, na kwa kuzingatia dosari zilizobainika Katika Sheria Ndogo iliyochambuliwa, **Kamati inaishauri Wizara ya Nishati na Madini kuifuta mara moja Sheria Ndogo hii ili isiendelee kutumika na badala yake Wizara itunge Kanuni mpya haraka iwezekanavyo ambazo zitaendana na masharti ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.**

---

**THE PETROLEUM (BULK PROCUREMENT REGULATIONS, 2015 (GN. No. 508 ya tarehe 6 Novemba, 2015)**

2.3.9 **Mheshimwa Spika**, Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya vifungu vya 168 na 258 vya Sheria ya The Petroleum Act No. 21 Of 2015 kwa lengo la kuanzisha Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja wa bidhaa za petroli (*Bulk Procurement System*). Mfumo huu una malengo ya kuhakikisha kuwa bidhaa za petroli zinakuwepo katika soko kwa wakati na kwa kiwango stahiki.

2.3.10 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa mambo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ukamilifu ili kuiboresha Sheria Ndogo hii ili iweze kukidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kwa mfano, Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo hii inaweka masharti kwamba, Waziri anaweza kuzuia bidhaa za petroli zinazosafirishwa nje ya nchi (*on transit petroleum products*) ili zitumike ndani ya nchi katika mazingira ya dharura yatakayobainishwa na Waziri (*localization of transit petroleum products under emergency conditions declared by the Minister*). Kwa maoni ya Kamati, Kanuni hii inampa mamlaka makubwa Waziri na endapo yasipotumika vyema yanaweza kuhatarisha mahusiano ya kibiashara na nchi za jirani.

2.3.11 **Mheshimiwa Spika**, katika maelezo yake mbele ya Kamati, Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (Mb), alisema kwamba, Sheria ya Petroli imempa dhamana ya kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mafuta nchini ili kulinda uchumi na usalama wa nchi. Aidha alisema kuwa, katika Kifungu cha 5 (2) na Kifungu cha 253 (1) cha Sheria Mama, Waziri ana mamlaka ya kuamuru shehena ya mafuta inayokwenda nchi jirani (*transit*

petroleum products) iuzwe nchini endapo kutatokea upungufu wa mafuta. Kifungu cha 253 (1) kinasomeka kama ifuatavyo:-

**"253.- (1) Where there is shortfall in domestic gas commodities or petroleum products supplies or delivery, the Minister may direct a licensee to make supplies or deliveries from a licensee's facility to cover for such shortfall of gas commodities or petroleum products and may further direct on whom such gas commodities or petroleum products shall be delivered."**

2.3.12 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti yanayopatikana katika Sheria Mama yako wazi kuhusu mazingira ambayo Waziri anaweza kuagiza mafuta yauzwe nchini endapo kutatokea upungufu wa bidhaa za petroli. Mazingira hayo ni pamoja na vita au hali yoyote ambayo inasababisha upungufu wa bidhaa za petroli kwa mujibu wa kifungu cha 253 (2) cha Sheria Mama. Hata hivyo, ukisoma Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati, Kanuni inasema:-

**"15 (7) Under emergency conditions declared by the Minister, the transit petroleum products may be localized."**

2.3.13 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hii inampa Waziri mamlaka ya kuamuru mafuta ambayo yako njiani kwenda nchi za nje (*transit petroleum products*) kutumika nchini katika mazingira ya tahadhari atakayotangaza Waziri (*emergency conditions declared by the Minister*). **Bila kuathiri masharti ambayo yanapatikana katika Sheria Mama, Kamati inashauri kwamba, Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo hii ifanyiwe marekebisho kufafanua masharti na maana halisi inayopatikana katika kifungu cha 253 cha Sheria Mama ili kuendana na dhamira ya Bunge wakati inatunga Sheria hiyo.**

2.3.14 **Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yana malengo ya kuhakikisha kuwa misingi ya uandishi wa Kanuni zinazotungwa na Wizara na Taasisi mbalimbali zinazingatia kikamilifu masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ambayo yanaitaka Sheria Ndogo yoyote kuwa na maudhui ambayo yanaendana na Sheria inayota madaraka. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

**"39.-(1) Words and expressions used in subsidiary legislation shall have the same respective meaning as in the written law under which the Subsidiary legislation is made."**

2.3.15 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 14 (4) ya Sheria Ndogo hii inazitaja bidhaa za petroli ambazo zitakuwa zinaagizwa kwa kutumia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja (*Bulk Procurement System*). Bidhaa hizo ni pamoja na mafuta ya taa (*illuminating kerosene*), mafuta ya magari (*automotive gasoline*), mafuta mazito ya kuendeshea mitambo (*heavy fuel oil*), mafuta ya ndege (*jet-A1*) na gesi inayotumika majumbani (*liquefied petroleum gas*).

2.3.16 **Kamati inashauri kwamba, Wizara ikamilishe haraka maandalizi ya utaratibu utakaowezesha bidhaa zote za mafuta ambazo Kanuni ya 14 (4) ya Sheria Ndogo hiyo inaagiza ziingizwe nchini kwa mfumo wa Bulk Procurement System.** Hatua hii itawezesha kushuka kwa bei za bidhaa husika.

**THE DRUGS CONTROL AND ENFORCEMENT (GENERAL) REGULATIONS, 2016 (GN No. 173 ya tarehe 10 Mei, 2016)**

---

2.3.17 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa chini ya Kifungu cha 67 cha Sheria inayoitwa *The Drugs Control and Enforcement Act, CAP. 95* ambayo imetungwa na Bunge kwa malengo ya kuweka masharti ya kudhibiti madawa ya kulevyta, kuanzisha mamlaka ya kuzuia na kudhibiti matumizi ya madawa hayo na usafirishaji wake pamoja na masuala mengine yanayohusiana.

2.3.18 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 5 (5) inatoa katazo kwa mmiliki wa mali inayopigwa mnada pamoja na ndugu zake kununua mali iliyotaifishwa na Kamishna kutokana na biashara ya dawa za kulevyta. Hata hivyo, Kanuni haijaweka katazo la kuizua Kampuni ambayo mwenye mali ni mmiliki au mbia, kununua mali iliyotaifishwa kiasi ambacho inaweza kutoa mwanya kwa mali hiyo kurudi kwa mmiliki.

2.3.19 **Kamati inashauri kuwa Kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho ili kuzuia mazingira ambayo mali iliyotaifishwa kutokana na biashara ya dawa za kulevyta inaweza kurejeshwa kwa mmiliki.**

2.3.20 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 14 inaweka masharti yanayoratibu zoezi la kuharibu madawa ya kulevyta yaliyokamatwa (*destruction of seized drugs*). Kanuni ya 14 (1) imewataja watu ambao ni lazima wawepo wakati zoezi hilo linatekelezwa. Watu hao ni wafuatao:-

- a) Jaji au hakimu;
- b) Mwakilishi wa Kamishna wa Madawa ya Kulevyta, Inspekte Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkemia Mkuu wa Serikali;

c) Mwakilishi kutoka Baraza la Mazingira la Taifa na Usalama wa Taifa; na

d) Mtu mwingine yeyote ambaye Kamisha wa Madawa ya Kulevyatamatua.

2.3.21 Hata hivyo, Kanuni ya 14 (2) inaweka masharti kwamba, Kamishna wa Madawa ya Kulevyau Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru madawa ya kulevyayaliyokamatwa yaharibiwe bila kuwashirikisha watu wanaotajwa katika Kanuni ya 14 (1).

2.3.22 **Mheshimiwa Spika**, masharti ya Kanuni hii yanakiuka misingi ya uandishi kwa kuwa yanakinzana kwa sababu Kanuni ya 14 (1) imetumia neno "shall" kuonesha ulazima wa kuwepo kwa watu walio tajwa wakati huo huo, Kanuni ya 14 (2) inatumia neno "may" kuonesha utashi anaoweza kutumia Kamishna kuamuru kuharibiwa kwa madawa ya kulevyabila kuwepo watu walio tajwa katika Kanuni ya 14 (1).

2.3.23 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine matakwa ya Kanuni ya 14 (2) yanakinzana na Kanuni ya 14 (3) inayotaka wakati wa kuharibu madawa kuzingatiwe ulinzi wa afya, usalama hali kadhalika ulinzi wa mazingira; hivyo basi kukosekana kwa watu walio tajwa katika Kanuni ya 14 (1) kunaweza kuchangia ukiukwaji wa Kanuni ya 14 (3).

2.3.24 Aidha, Kanuni ya 14 (5) na 14 (7) zinaweka sharti kwa Jaji au Hakimu aliyeshudia kuharibiwa kwa madawa yaliyokamatwa kujiridhisha kwamba yote yameharibiwa na hatimaye kujaza fomu ya kuthibitisha hilo. Hivyo basi, kutokuwepo kwa Jaji au Hakimu kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (2) kunaweza kusababisha zoezi hilo kutokamilika kisheria. **Kamati inashauri kuwa Kanuni ya 14 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa mazingira yenye utata.**

**KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA ZA WATOTO ZA MWAKA 2014 (GN Na. 170 ya tarehe 13 Mei, 2016)**

---

2.3.25 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi ni mionganini mwa Sheria Ndogo nydingizilizochambuliwa na Kamati zinazotokana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009. Kanuni Ndogo hizi zimetungwa chini ya Kifungu cha 99 (1) cha Sheria hiyo. Lengo la Kanuni hizi ni kuanzisha mfumo wa Utendaji na mwenendo unaowiana na Mahakama za Watoto za Tanzania Bara na kuhakikisha kuwa haki za mtoto chini ya sheria zinalindwa.

2.3.26 **Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 21 (3)** inahusu hati ya wito shaurini kwa mtoto (*summons*) bila kutaja mazingira ambayo mtoto anaweza kuhudhuria Mahakamani akiwa au akisindikizwa na mtu mzima. Kifungu cha 99 (1) (f) cha Sheria Mama kinatoa haki kwa mtoto kuwa na ndugu wa karibu au wakili katika taratibu za kimahakama. Kamati inashauri kuwa Kanuni hii iweke sharti la kuwepo mtu wa kumsindikiza mtoto anapoitikia wito wa mahakama (*summons*).

2.3.27 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 25 (1) inaipa Mahakama uhuru wa kutoa hati ya wito kwa mzazi/mlezi/mwangalizi kuhudhuria shauri la jinai linalomhusu mtoto pale ambapo ameshindwa kuhudhuria shauri la mtoto huyo kwa kutumia neno “may” (kwamba Mahakama yaweza). Katika hatua hii ya mwenendo wa shauri, Kamati inapendekeza kuwa Kanuni iweke masharti ambayo yatamlazimisha mzazi/mlezi/mwangalizi kuhudhuria shauri la jinai linalomhusu mtoto huyo kwa kutumia neno (*shall*) (kwamba Mahakama itamtaka).

2.3.28 Kanuni ya 54 (5) inaweka utaratibu wa kufuatwa pale ambapo mtoto aliyewekwa kizuzini kwa muda mrefu zaidi ya kipindi alichopangiwa kuwasilisha maombi ya kuachiwa huru kwa mamlaka husika. Hata hivyo kanuni haijaweka masharti ambayo yanamuwezesha mtoto kupata msaada wa kuwasilisha maombi hayo kutoka kwa mzazi/mlezi/mwangalizi/afisa ustawi wa jamii au mtu mwingine yeyote. **Kamati inashauri kuwa Kanuni hizi ziweke masharti ambayo yanamuwezesha mtoto kupata msaada wa kuwasilisha maombi kuachiwa huru kwa mamlaka husika.**

#### **KANUNI ZA AJIRA ZA WATOTO ZA MWAKA 2012 (GN Na. 168 ya tarehe 13 Mei, 2016)**

---

2.3.29 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009. Sehemu ya Saba ya Sheria Mama inaweka masharti kuhusu haki ya mtoto kufanya kazi, makatazo na mazingira ambayo mtoto hapaswi kufanya kazi, haki za mtoto anayefanya kazi pamoja na taratibu za ufuatiliaji ustawi wa mtoto ambaye anafanya kazi.

2.3.30 **Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini dosari kadhaa katika Sheria Ndogo hii. Moja kati ya dosari hizo ni kwamba, Kanuni hazijataja kifungu cha Sheria Mama inachotoa madaraka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hii.

2.3.31 Katika Kanuni ya 3 ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali, Kamati imebaini dosari kadhaa. Kwa mfano, Kanuni zinatoa tafsiri ya neno “majengo” kwa kujumuisha magari, ndege na maeneo mengine ambayo yangeweza kutolewa tafsiri zinazojitegemea.

2.3.32 Aidha, Kanuni inatoa tafsiri ya maneno “kazi za hatari” ikimaanisha “**kazi yoyote ambayo inamuweka mtoto katika hatari ya magonjwa ya kimwili au majeraha ya kiakili**” wakati Sheria Mama inatoa tafsiri ya maneno “kazi hatarishi” kuwa ni “**kazi yoyote inayomuweka mtoto katika hatari ya kupata madhara ya kimwili au kiakili**”. Tafsiri hizi mbili zinazungumzia kitu kinachofanana lakini zinatofautiana kimaudhui na kimantiki.

2.3.33 **Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Kanuni ifanyiwe marekebisho ili tafsiri inayotumika katika Sheria Mama itumike katika Sheria Ndogo kwa lengo la kukidhi matakwa ya Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.**

2.3.34 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwengine Kanuni ya 7 (1) inazungumzia mtoto kutoajiriwa katika mazingira hatarishi lakini wakati huo huo inaweka masharti kuwa mazingira hayo hayatochukuliwa kuwa ni hatarishi ikiwa mtoto amefikisha umri chini ya miaka 16 na anafanya kazi chini ya uangalizi. **Kamati inashauri kuwa, maneno “chini ya miaka kumi na sita” yafutwe ili dhana ya mtoto mwenye miaka kumi na sita kufanya kazi hizo iweze kujumuishwa.**

2.3.35 Kanuni ya 9 (3) inaweka masharti yanayotambua mazingira ambayo ni hatarishi kufanya kazi ikijumuisha maeneo na hali ambazo kimsingi zinakosa uhalisia, mfano joto, kuinama, kusimama au kukaa. **Kanuni hii ifanyiwe marekebisho ili kuendana na uhalisia wa mazingira ambayo mtoto anaweza kufanya kazi.**

2.3.36 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 4 inazungumzia umri wa chini wa kuajiriwa kuwa ni miaka kumi na nne (14). Hata hivyo Kanuni 4 (2) inaweka masharti ambapo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne anaweza kuajiriwa. **Kamati inashauri Kanuni hiyo iandikwe upya kuondoa maneno “chini ya” ili kuepuka mazingira ambayo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne (14) anaweza kuajiriwa.**

#### **KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2012 (GN Na.164 ya tarehe 13 Mei, 2016)**

---

2.3.37 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009 kwa lengo la kufafanua masharti kuhusu taratibu za uasili wa watoto. Masharti hayo ni pamoja na maombi ya kuasili, ridhaa ya kuasili, amri ya kuasili, rejestra ya kuasili, uasili wa wazi, kuasili kwa Mtanzania asiye mkazi na kuasili kwa wageni.

2.3.38 Katika Kanuni hizi, Kamati ilibaini dosari kadhaa ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwa mfano, Kanuni ya 10 (1) inaweka masharti kuhusu taarifa ya

kusikilizwa kwa shauri kwa mfumo ulioainishwa katika **Fomu Na. A. C6** katika majedwali. Kanuni hiyo inamtambua Afisa wa ustawi wa jamii lakini katika fomu inayotajwa hakuna sehemu inayotambua ushiriki wake.

2.3.39 Aidha, Katika Fomu Na. A.C7 aya ya 6.3 kuna maneno “**mtoto ana kilema**” yanaweza kutafsiriwa kuwa yana unyanyapaa. Maneno yanayoweza kutumika ni “**mtoto mwenye ulemavu**”. Kamati inashauri kuwa Kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho.

2.3.40 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 16 (5) inampa Kamishna jukumu la kufuatilia taarifa za mtoto aliyeasiliwa na wazazi wanaoishi nje ya Tanzania bila kuainisha taratibu za kuzingatiwa katika kufuatilia taarifa za mtoto huyo.

**Kwa madhumuni ya kulinda ustawi wa watoto wanoasiliwa nje ya nchi, Kamati inashauri Kanuni ziweke bayana taratibu ambazo taarifa za mtoto huyo zitafuatiliwa kwa kuhusisha pia balozi zetu.** Aidha, Kanuni ziweke bayana muda ambao ufuatiliaji huo utafanyika kama ilivyo katika kanuni ya 16 (1) inayohusu mtoto anayeasiliwa na wazazi wanaoishi Tanzania ambaye taarifa zake zitafuatilia miezi mitatu baada ya Amri ya kuasili kutolewa, ikihusisha kutembelea nyumba ambayo mtoto huyo anaishi.

2.3.42 **Mheshimiwa Spika**, maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa yana lengo la kuhakikisha kuwa katika kila Kanuni ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, maslahi ya mtoto yanakuwa ndiyo msingi wa kuzingatiwa katika masuala yote yanayohusiana na ustawi wa mtoto (*welfare of a child should always be a priority*).

**THE COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS (COPYRIGHTED WORKS - COMMUNICATION TO THE PUBLIC) REGULATIONS, 2016** (GN No. 29 ya tarehe 8 Januari, 2016)

---

2.3.43 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya Kifungu cha 45 cha Sheria ya Hakimiliki inayoitwa *The Copyright and Neighbouring Rights Act* (Cap. 218) ambayo, pamoja na mambo mengine, ina malengo ya kulinda maslahi ya wabunifu na wasanii yatokanayo na kazi au ubunifu wao kwa kuzitambua haki za kipekee (*exclusive rights*) za watu hao na kuweka masharti ya matumizi ya kazi hizo.<sup>18</sup>

---

<sup>18</sup> Kifungu cha 2 cha Sheria ya Hakimiliki (*The Copyright and Neighbouring Rights Act* , Cap. 218)

2.3.44 Sheria Ndogo hii inaweka masharti kuhusu namna za kuboresha mapato ya wasanii yatokanayo na kazi zao zinazotumika katika vyombo vya habari, makampuni ya simu, mitandao ya kijamii, tovuti na wavuti mbalimbali. Mapato hayo yanatokana na tozo ambazo Chama cha Hakimiliki cha Tanzania (COSOTA) kitatoza kwa watumiaji wa kazi za wasanii ambapo wasanii hao watapata mgao wa mrabaha (*royalty*) kulingana na matumizi ya kazi zao.

2.3.45 **Mheshimwa Spika**, katika Mkutano wa Kamati wa Kusikiliza Maoni ya Wadau (*Public Hearing*), baadhi ya wadau waliofika kutoa maoni yao walidai kuwa hawakushirikishwa katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo hii. Madai hayo yalitolewa na baadhi ya wawakilishi kutoka katika vyombo vya habari na baadhi ya wanamuziki walioshiriki. Hii ilikuwa hoja kubwa ambayo ilibua mjadala mpana mionganini mwa Wajumbe wa Kamati.

2.3.46 **Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masharti ya msingi katika mchakato wa utungaji wa Sheria yoyote ni ushirikishwaji wa wadau ili kupata maoni yao kuhusu maudhui ya Sheria husika. Hata hivyo, Sheria ya Tafsiri ya Sheria haijaweka bayana kuhusu utekelezaji wa masharti haya katika utungaji wa Sheria Ndogo.

2.3.47 Kwa utamaduni uliopo duniani katika utungaji wa Sheria Ndogo, suala la ushirikishwaji si kigezo kinachoweza kuzuia mchakato huo kukamilika na haibatilishi uhalali wa kutumika kwa Sheria Ndogo husika. Katika nchi ya Australia kwa mfano, Sheria inayoitwa *The Legislative Instruments Act, 2003* ambayo inasimamia masharti ya utungaji wa Sheria Ndogo, imeweka utaratibu katika Sehemu ya 3 wa kufanyika kwa ushirikishwaji katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

2.3.48 Hata hivyo, Kifungu cha 19 cha Sheria hiyo kinabainisha kuwa Sheria Ndogo isipozingatia ushirikishwaji wa wadau, haibatilishi uhalali wake. Hata hivyo, masharti ya ushirikishwaji yanaweza kuwa ni hoja ya msingi wakati Bunge linafanya uchambuzi wa Sheria Ndogo husika.

*"Part 3 of the LIA provides for rule-makers to consult with interested parties before making instruments. Section 19, however, provides that failure to consult does not affect the validity of an instrument. It likewise does not affect parliamentary control, although it may be an issue in parliamentary scrutiny."*<sup>19</sup>

---

<sup>19</sup> Odger's Australian Senate Practice, 13th Ed., Pg. 437

2.3.49 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hayo, pamoja na kwamba Sheria yetu ya Tafsiri ya Sheria haijaweka bayana masharti kuhusu umuhimu wa ushirikishaji katika utungaji wa Kanuni (*rules and regulations*), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo huwa haipuuzi wala kuacha kuzingatia umuhimu wa ushirikishwaji iwapo Sheria Ndogo inayozungumziwa kwa maslahi mapana ya utekelezaji wake. Kifungu cha 36 (3) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinafafanua kwamba, Sheria Ndogo yoyote inatarajiwa kuwa itakuwa imezingatia hatua zote za awali katika kutungwa kwake iwapo hakuna ushahidi wa jambo hilo kutofanyika. Kifungu hicho kinasema:-

*"36.- (3) It shall be presumed, in the absence of evidence to the contrary, that all conditions and preliminary steps precedent to the making of subsidiary legislation have been complied with and performed"*

2.3.50 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka ufanuzi kutoka Serikalini kuhusu ukweli wa madai kwamba wadau hawakushirikisha. Mhe. Charles Mwijage (MB), Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji alikanusha madai hayo kwa kusema kuwa, Wizara yake kwa kushirikiana na COSOTA iliwashirikisha wadau katika maandalizi ya Sheria Ndogo hii. COSOTA iliwasilisha nakala za vielelezo mbalimbali vinavyoonesha namna ambavyo Wizara ilishirikisha wadau.

2.3.51 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchunguzi wake ilibaini kuwa, mwitikio wa baadhi ya wadau kushiriki katika maandalizi ya Sheria Ndogo hii ulikuwa hafifu. Iwapo wadau wengine ambao wanalamika kutoshirikisha walipata barua za mwaliko lakini hawakushiriki kwa sababu yoyote, malalamiko yao hayatakuwa na msingi. Lakini iwapo taarifa hazikufika, wadau hao wana hoja ya msingi.

2.3.52 **Mheshimiwa Spika**, kwa namna yoyote, kwa kuwa malalamiko yapo na kwa kuzingatia kuwa, wadau wanaolalamika wana maslahi muhimu katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Kwa kuwa Sheria Ndogo hii imeanza kutumika kisheria baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa GN Na. 29 ya tarehe 8 Januari, 2016, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ifanye mikutano na makundi ya wadau wote wanaoathirika na Sheria Ndogo hii ili kuwapa elimu ya kutosha kuhusu maudhui yake. Aidha, mikutano hiyo itumike kama jukwaa la mjadala wa maudhui ya Sheria Ndogo hii ili Serikali ipate mawazo mapya ambayo yataiboresha na kurahisisha utekelezaji wake.

b) Wadau ambao wanaathirika na Sheria Ndogo hii, watumie fursa hii kuhamasishana kushiriki mikutano hiyo na kutoa maoni yatakayoboresha maudhui yake. Kwa mfano, vyombo vya habari kwa kutumia rasimilimali zake vitoe matangazo ili ushiriki wa wadau wote uwe na tija zaidi.

2.3.53 **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yana lengo la kuhakikisha kuwa, wasanii na wabunifu wanashiriki kikamilifu na wanafaidika na kazi zao kwa mapato yatokanayo na matumizi ya kazi hizo. Aidha, kwa kuzingatia jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John P. Magufuli katika kuhakikisha uchumi wa nchi unaendeshwa kwa viwanda, kazi za wasanii na wabunifu zinakuwa ni sehemu ya ongezeko la pato la nchi na kukuza uchumi.

2.3.54 **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano baina ya Kamati na wadau, baadhi ya walioshiriki walikuwa na maoni kuhusu utendaji wa COSOTA. Wapo wanaodhani kuwa chombo hiki muhimu kwa ustawi wa wasanii na wabunifu kingefaa kuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mapendekezo haya yalitolewa na washiriki katika vikao vya Kamati ambao wanadhani kuwa COSOTA haitekelezi majukumu yake ipasavyo ya kuwasaidia wasanii na wabunifu chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

2.3.55 Maoni haya pia yalitolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika taarifa yao kuhusu Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017<sup>20</sup> ambapo walisema:-

**“Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Chama cha Hakimiliki nchini (COSOTA) kinasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Hii imekuwa changamoto katika uratibu wa shughuli za wasanii na hivyo **Kamati inashauri COSOTA iwe chini ya Wizara ya Habari ili kurahisisha uratibu wa kazi za Wasanii na hata kuipa dhamana Wizara ya Habari kuisimamia ipasavyo.”**

2.3.56 **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inashauri kuwa, Serikali ifanye upembusi yakinifu na kufanya uamuzi kuwa chombo hiki muhimu kinapaswa kutekeleza majukumu yake chini ya Wizara gani kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa. Aidha, taarifa ya uamuzi huo iwasilishwe ndani ya Bunge hili ili Wabunge wapate mrejesho kuhusu maoni yao kwa Serikali.

---

<sup>20</sup> Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Uk. 15

**THE INSTITUTE OF JUDICIAL ADMINISTRATION LUSHOTO (STUDENTS' GENERAL WELFARE, CONDUCT AND DISCIPLINARY MATTERS) REGULATIONS, 2015 (GN No. 511 ya tarehe 6 Novemba, 2015)**

---

2.3.57 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya Kifungu cha 23 cha Sheria iliyotungwa na Bunge inayoitwa **The Institute Of Judicial Administration Lushoto (CAP 405)**. Sheria Ndogo hii inahusu masuala ya ustawi na nidhamu kwa wanafunzi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

2.3.58 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 13 (1) ya Sheria Ndogo hii inatoa adhabu ya mwanafunzi kusimamishwa masomo (suspension) endapo atashitakiwa kwa kosa la jinai. Aidha, Kanuni ya 13 (4) inaweka sharti kwamba muda wa kusimamishwa kwa mwanafunzi huyo ukizidi miaka miwili (2) mfululizo (two consecutive academic years) atakuwa amekoma kuwa mwanafunzi. Kanuni ya 13 ya Sheria Ndogo hii inasomeka kama ifuatavyo:-

"13.- (1) *The Institute shall suspend any student charged with any criminal offence in any court of law.*

(2) *Where a student is suspended under the provisions of sub-regulation (1) of this Regulation, he shall not be reinstated as a student until he produces the judgment of a court acquitting him.*

(3) *Any student who has been reinstated under sub-regulation (2) of this Regulation shall be re-suspended where an appeal has been preferred against him in the case he was facing and, such suspension shall continue until the final determination of the appeal.*

(4) *A student whose suspension period exceeds two consecutive academic years shall cease to be a student of the Institute.*

(5) *Any student who is convicted of any criminal offence shall cease immediately upon such a conviction to be a student of the Institute.*" Msisitizo ni wetu.

2.3.59 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti ya Kanuni hii yako kinyume na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara ya 13 (6) (b) inayosema:-

*"ni marufuku kwa mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo."*

2.3.60 Ibara hii inaweka masharti ya msingi ya haki za binadamu ya kutomchukulia mtu aliyeshitakiwa kuwa mkosaji mpaka pale mahakama itakapothibitisha kuwa ni mkosaji yaani “presumption of innocence”.

2.3.61 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliwasilisha hoja hiyo kwa Wizara ya Katiba na Sheria ili iweze kutoa ufanuzi. Kwa maelezo ya Wizara, Sheria Ndogo hii **ni lazima** isomwe pamoja na Sheria Ndogo inayoitwa **The Institute Of Judicial Administration Lushoto (Students' Performance Assessment) Regulations, 2015** (GN No. 510 ya tarehe 6 Novemba, 2015) inayohusu masuala ya masomo na mitihani ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

2.3.62 Kwa maelezo ya Wizara, Kanuni ya 19 ya Sheria Ndogo hiyo, inaweka sharti kwamba ili mwanafunzi afanye mitihani anapaswa kuwa amehudhuria vipindi vya darasani kwa asilimia themanini (80%). Kama hatahudhuria kwa muda huo hata kama hana kesi ya jinai, anaweza kuwa mgonjwa na hivyo chini ya Kanuni ya 37 ya Sheria Ndogo hiyo anaweza kuomba kuahirisha masomo kwa mwaka mmoja na akarudia baada ya mwaka mmoja kuendelea alipoishia ila ikizidi miaka miwili anapaswa kuomba upya kujeungu na kimsingi hawezi kukataliwa ila ni kwa ajili ya kuangalia muda ambao amekuwa nje ya masomo ni vigumu kuwa sambamba na wenzake.

2.3.63 **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Wizara hayakuridhisha Kamati kwa sababu, ukisoma Kanuni ya 13 (1) ya Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati, inasema bayana maneno yafuatayo “*The Institute shall suspend any student charged with any criminal offence in any court of law.*” Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, suspension ya mwanafunzi huyo itatokea mara tu **atakaposhitakiwa** (charged). Kitendo cha kumsimamisha mwanafunzi masomo (suspension) kinaweza kutafsiriwa kuwa ni kumpa adhabu mwanafunzi huyo kwa sababu tu ameshitakiwa katika mahakama fulani.

2.3.64 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kuifanya marekebisho Sheria Ndogo hiyo. Iwapo Kanuni za Sheria Ndogo kama zitabaki kubaki kama zilivyo, ni wazi kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendela kuvunjwa na watu kukosa haki zao za msingi.

## 2.4 MAJUKUMU MENGINE

### a) Mikutano na Wadau wa Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo

2.4.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa nyakati tofauti kati ya tarehe 15 – 18 Machi, 2016 Kamati ilikutana na taasisi zinazohusika na mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kupata elimu kuhusu hatua mbalimbali za utungaji wa Sheria Ndogo na kubaini changamoto zilizopo. Taasisi hizo ni zifuatazo:-

- i) Idara ya Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali;
- ii) Ofisi ya Rais TAMISEMI; na
- iii) Ofisi ya Mwandishi Mkoo wa Sheria wa Serikali.

2.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Sheria Ndogo ilitembelea Ofisi ya Mpiga Chapa Mkoo **wa** Serikali tarehe 15 Machi, 2016 ambapo wajumbe walipata fursa ya kujionea maeneo mbalimbali ambayo Sheria Ndogo hupitia katika hatua za uchapaji. Katika ziara hiyo Wajumbe walipata fursa pia ya kuuliza maswali kadhaa juu ya changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali katika hatua za uchapaji wa Sheria Ndogo.

2.4.3 **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali ni muhimu katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa kuwa huchapisha Sheria Ndogo zote nchini na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Idara hii isipotekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hawezu kuwasilisha kwa wakati Sheria Ndogo kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri, Sura ya 1.

2.4.4 Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Idara hii haiendeshwi kwa viwango vinavyokidhi mahitaji yaliyopo. Kwa mfano, katika vikao vya Kamati vilivyopita, Kamati haikupokea kwa wakati Sheria Ndogo mbalimbali kwa sababu hazikuwa zimechapishwa na Mpiga Chapa wa Serikali. Dosari hii inatokana na ukweli kwamba, Idara ya Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali inatekeleza majukumu yake chini ya kiwango kinachotakiwa kwa maendeleo ya teknolojia iliyopo.

2.4.5 Katika ziara hiyo, Wajumbe walijionea mitambo ambayo ni chakavu, majengo yaliyo chini ya kiwango pamoja na uhaba mkubwa wa vitendea kazi. Haya yote yalibainika huku Serikali nzima na vyombo vyake ikiitegemea Ofisi hii kuchapisha nyaraka mbalimbali muhimu zikiwemo Sheria Ndogo zote nchini.

2.4.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na maelezo ya Menejimenti ya Idara ya Mpigachapa Mkoo wa Serikali kuhusu uendeshaji na utendaji wa Idara hiyo. Kwa upande mwingine, Kamati haikuridhishwa na hatua ya Idara hiyo kutumia fedha za umma kununua mashine ya uchapaji kwa gharama kubwa na mashine hiyo kufanya kazi kwa muda mfupi. Kamati inashangaa kwa nini hadi wakati Kamati inafanya ziara hiyo, mashine hiyo ilikuwa haifanyi kazi.

2.4.7 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini pia kuwa kazi nyingi za Idara ya Mpigachapa wa Serikali zinafanywa nje ya Idara kwa sababu printa ya ofisi hiyo huzidiwa na kazi. Kwa kutoa kazi hizo nje, kazi kuchelewa na kutomalizika kwa wakati na hata kupoteza usiri wa kazi za Serikali na gharama pia huongezeka. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuiboresha Idara hii ili iachane na tabia ya kuchapisha nyaraka za Serikali nje ya Idara hiyo ambayo inahatarisha usalama wa nyaraka na kuongeza gharama kwa Serikali.

2.4.8 **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inaunga mkono maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria katika Taarifa yao kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu<sup>21</sup> ambapo walishauri kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu iboreshe mitambo na mazingira ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuiwezesha kufanya shughuli zake kibiashara zaidi.

2.4.9 **Kamati inashauri kwamba, menejimenti ya Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ifanyiwe mabadiliko kwa sababu kwa muda mrefu, Ofisi hii muhimu imekuwa haitekelezi majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi wa Ofisi hiyo yanapaswa kuboreshwa ili kuendana na shughuli wanazozifanya.**

2.4.10 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 18 Machi, 2016 Kamati iilikutana na Bi. Sara Barahomoka, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, kwa lengo la kufahamu taratibu juu za uandishi wa Sheria Ndogo. Katika kikao hicho, Bi. Barahomoka alitoa ufanuzi kuhusu masuala yafuatayo:-

- i) Nafasi na majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa mujibu wa Sheria
- ii) Hatua za msingi katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo
- iii) Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo

2.4.11 **Mheshimiwa Spika**, hatua hii ya Kamati kukukutana na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, iliwawezesha Wajumbe kupata ufhamu wa kutosha kuhusu masuala mbalimbali ya uandishi wa Sheria Ndogo, elimu ambayo imewasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

2.4.12 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na Kamati kufanya ziara na kukutana na Taasisi hizi, iliweza kupata taarifa ya kutosha ya rejea mbalimbali ambazo ziliisaidia Kamati kutekeleza kazi ya uchambuzi kwa ufanisi zaidi.

---

<sup>21</sup> Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2016, Uk. 21

## b) Mikutano na Wadau wa Mazao

2.4.13 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na wadau wa mazao mbalimbali katika jitihada za kuanza kuzishughulikia Sheria Ndogo zinazowagusa ili waweze kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo, changamoto wanazokabiliana nazo katika uzalishaji na uuzaji wa mazao hayo. Baadhi ya wadau waliofika mbele ya Kamati ni wafuatao:-

- i) Western Zone Tobacco Growers Cooperative Union Ltd.
- ii) Wakulima wa Tumbaku
- iii) Watafiti wa Zao la Pamba

2.4.14 **Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Kamati kuweka utaratibu wa vikao na wadau wa mazao una lengo la kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli katika kupunguza au kuondoa kero kwa wakulima wa mazao mbalimbali zitokanazo na tozo mbalimbali zinazowekwa na Sheria Ndogo tofauti.

2.4.15 **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Mhe. Dkt. John P. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja alinukuliwa akisema:-

*“Mheshimiwa Spika, wakulima wote wa kahawa wa Kagera wanataka kahawa yao wakaiuze Uganda lakini tulipouliza, wana kodi zaidi ya ishirini na sita. Kwa kuzingatia kuwa na kodi hizo zaidi ya ishirini na sita, bei wanayopewa wakulima wa kahawa kule Kagera na maeneo mengine inakuwa ndogo zaidi ukilinganisha na bei wanayopewa katika nchi jirani ya Uganda na ndiyo maana wananchi wanachukua risk hata ya kwenda kuzama kwenye maji lakini wawe wanasaferisha kahawa. Ndiyo maana nasema, kodi hizi za hovyo na ambazo ni kero kwa wakulima wetu katika mazao ya kahawa, mahindi, chai, pamba, korosho, mkonge, ngozi, nyama, maziwa na samaki tutahakikisha tutaziondoa kama si kuzipunguza kwa kiasi kikubwa sana.”*

2.4.16 **Mheshimiwa Spika**, kwa mfano katika kusikiliza maoni ya wadau hao, Kamati ilibaini kuwepo kwa mlolongo wa kodi na tozo katika zao la pamba. Kodi na tozo hizo ni pamoja na

- i) ushuru wa mazao
- ii) ushuru wa elimu
- iii) leseni ya biashara
- iv) leseni ya kituo cha manunuzi
- v) leseni ya uchambuzi

- vi) mchango wa mwenge
- vii) maombi ya leseni ya manunuzi
- viii) ada ya kikao cha halmashauri
- ix) faini ya uendeshaji na
- x) kodi ya mapato.

2.4.17 **Mheshimiwa Spika**, mlolongo wa kodi na tozo hizi unaleta mzigoto mkubwa kwa mkulima na hivyo kuathiri uzalishaji na kipato cha mkulima.

2.4.18 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, tozo ambazo zinazungumziwa zinatokana na Sheria Ndogo mbalimbali zikiwemo Sheria Ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) pamoja na Sheria Ndogo za Wizara (*Regulations*) katika mazao tofauti zikiwemo zifuatazo:-

- i) Kanuni zinazoratibu uzalishaji na soko la zao la pamba (*The Cotton Industry Regulations, 2011*)
- ii) Kanuni zinazohusu soko la zao la korosho (*The Cashewnut (Marketing) Regulations, 1998*)
- iii) Kanuni zinazohusu uzalishaji na soko la zao la kahawa (*The Coffee Industry Regulations, 2013*)
- iv) Kanuni za Mazao Mchanganyiko (*The Cereals and Other Produce Regulations, 2011*)

2.4.19 **Mheshimiwa Spika**, kwa kadri ya muda utakavyoruhusu na kwa kadri itakavyowezekana, Kamati itafanya uchambuzi wa kina wa Sheria Ndogo mbalimbali katika maeneo yafuatayo:-

- i) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula
- ii) Ufugaji
- iii) Uvuvi
- iv) Biashara za mama lishe
- v) Bodaboda

2.4.20 Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo na nyingine, unaweza kusaidia juhudini za Rais katika kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji, kupunguza kero kwa wananchi na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### 3.0 MAONI YA JUMLA

#### 3.1 UANDISHI WA SHERIA NDOGO

3.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, mamlaka zote zilizokasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zihakikishe kuwa zinazingatia misingi ya Katiba na haki za binadamu wakati wa uandishi. Aidha, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, masharti yanayopatikana katika Sheria Ndogo yaendane na masharti ya Sheria Mama zinazotoa madaraka.

3.1.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno (*copying and pasting*) bila kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili dosari za Sheria Ndogo hizo.

3.1.3 Kwa mfano, katika **Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita, 2015** na **Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, 2015** zote kwa pamoja zimeweka marufuku kupanda mimea mirefu maeneo ya mjini katika kifungu cha 6 cha kila Sheria Ndogo. Aidha katika kifungu cha 8 cha kila Sheria Ndogo za halmashauri hizo, imeweka wajibu kwa mmiliki wa nyumba kuweka "pavements" mbele ya nyumba yake. Sheria Ndogo hizo, kwa sehemu kubwa zinafanana neno kwa neno bila kuzingatia dosari zilizopo au utofauti wa mazingira ya halmashauri husika.

3.1.4 **Kamati inazishauri halmashauri zote kuhakikisha kuwa zinajiridhisha kikamilifu kabla ya kunakili Sheria Ndogo yoyote kutoka Halmashauri nyingine ili kutunga Sheria Ndogo kulingana na hali halisi ya Halmashauri husika.**

3.1.5 **Mheshimiwa Spika**, katika baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na makosa mengi ya kiuandishi na kiuchapaji kiasi cha masharti ya Sheria Ndogo hizo kupoteza maana. Aidha, baadhi ya rejea za vifungu katika majedwali zilikosewa kiasi cha kuleta mkanganyiko wa tafsiri. **Kamati inashauri kuwa mapitio ya Sheria Ndogo mbalimbali yafanyike ili kuondoa dosari hizo.**

3.1.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iandae programu ya mafunzo ya mara kwa mara kwa Wanasheria wa Wizara na Halmashauri zote nchini ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo ambazo zinakidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

### **3.2 MCHAKATO WA UTUNGAJI WA SHERIA NDOGO**

3.2.1 Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga sheria kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote.

3.2.2 Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ianze kutumia mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa upitishaji wa Sheria Ndogo katika hatua mbalimbali (*The By – Laws Database*) ili kuhakikisha kuwa Sheria Ndogo hizo zinakidhi vigezo vinavyotakiwa kabla ya hatua ya uchapishwaji katika magazeti ya Serikali na kuanza kutumika.

3.2.3 Serikali iongeza idadi ya Rasilimali watu katika Idara za Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa vitengo vinavyohusika na upitiaji wa Sheria Ndogo ili kuhakikisha makosa yanayojitokeza katika Sheria Ndogo yanafanyiwa kazi kabla ya Sheria hizo kuanza kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

3.2.4 Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka katika kuzifanya marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari na ambazo zinalalamikiwa kuwa zinawakandamiza wananchi. Baada ya marekebisheso hayo kufanyika, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria ili Kamati yangu ipate fursa ya kuzifanya uchambuzi wa kina. Hatua hii itaiwezesha Serikali kulifanya kazi tamko la Waziri Mkuu kuhusu kupunguza kodi katika mazao mbalimbali, kupunguza tozo zinazohusiana na masuala ya maliasili na utalii kama vile tozo za kitanda na Sheria Ndogo nyingine yoyote ambayo ni kero kwa wananchi.

3.2.5 Kwa kuzingatia masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Kamati inaishauri Serikali kijiwekea utaratibu wa kuwasilisha kwa wakati katika kila Mkutano wa Bunge, Sheria Ndogo zote zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita. Hatua hii italiwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikamilifu laini pia litaepusha mgogoro wa kiutendaji wa Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge linaweza kuazimia isitumike kwa kutowasilishwa Bungeni kwa wakati.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 SHUKURANI

4.1.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana.

4.1.2 Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa uratibu ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. George Simbachawane (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)
2. Mhe. William Lukuvi (Mb) –Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
3. Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (Mb) - Waziri wa Nishati na Madini
4. Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) –Waziri wa Katiba na Sheria
5. Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
6. Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) – Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi
7. Mhe. Charles Mwijage (Mb) - Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji
8. Mhe. Selemani Jafo (Mb) – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) – TAMISEMI
9. Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi
10. Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Mb) – Naibu Waziri wa Nishati na Madini
11. Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) – Naibu Waziri wa Fedha na Mipango

4.1.3 Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali. Vilevile niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao na wale wote ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi (*submissions*). Ushiriki wao katika vikao vya Kamati pamoja na maoni waliyowasilisha ni muhimu kwa Kamati katika utekelezaji bora wa shughuli zake.

4.1.4 **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano Tatu na Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

- |     |                                       |                   |
|-----|---------------------------------------|-------------------|
| 1.  | Mhe. Andrew John Chenge (Mb) -        | <b>Mwenyekiti</b> |
| 2.  | Mhe. William Mganga Ngeleja (Mb)      | M/Mwenyekiti      |
| 3.  | Mhe. Abdallah Ally Mtolea (Mb)        | Mjumbe            |
| 4.  | Mhe. Halima James Mdee (Mb)           | Mjumbe            |
| 5.  | Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu (Mb) | Mjumbe            |
| 6.  | Mhe. Daniel Edward Mtuka (Mb)         | Mjumbe            |
| 7.  | Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)         | Mjumbe            |
| 8.  | Mhe. Aida Joseph Khenani (Mb)         | Mjumbe            |
| 9.  | Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)    | Mjumbe            |
| 10. | Mhe. Esther Michael Mmasi (Mb)        | Mjumbe            |
| 11. | Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb)     | Mjumbe            |
| 12. | Mhe. Hassani Seleman Kaunje (Mb)      | Mjumbe            |
| 13. | Mhe. Sadifa Juma Khamis (Mb)          | Mjumbe            |
| 14. | Mhe. Khamis Mtumwa Ali (Mb)           | Mjumbe            |
| 15. | Mhe. Hassan Elias Massala (Mb)        | Mjumbe            |
| 16. | Mhe. Leonidas Tutubert Gama (Mb)      | Mjumbe            |
| 17. | Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)         | Mjumbe            |
| 18. | Mhe. Goodluck Asaph Milinga (Mb)      | Mjumbe            |
| 19. | Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma (Mb)       | Mjumbe            |
| 20. | Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)    | Mjumbe            |

4.1.5 **Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaopatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nimshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Nd. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi kwa usimamizi mzuri katika uratibu wa Shughuli za Kamati.

4.1.6 Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

## 4.2 HOJA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**  
NOVEMBA, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mjadala wa hoja hii utaanza kesho. Mheshimiwa Halima Mdee.

### HOJA YA KUUNDWA KAMATI TEULE

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia kanuni ya 120(1) na (2) (a)(b) naomba nizisome:-

120(1) inasema: "Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa." Pili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, tusaidie kidogo kwa sababu muda wetu ni finyu na tuna shughuli nyingine inayofuata baada ya hapa, naona wewe ujielekeze tu kwenye ile kanuni ambayo unataka kusimamia na siyo lazima utusomee ili tulimalize hili, twende kwenye linalofuata.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ninayotaka kusimamia ni 120(2)(a) ambayo inasema kwamba; baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa, kuamuliwa, Mbunge yeoyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya kanuni hii anaweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule.

Kwa hiyo, ndio maana nimesimama hapa na nilisimama mahali hapa wakati Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC alipokuwa akiwasilisha majumuisho yake na baada ya Bunge kuamua ili nitoe taarifa kwamba nataka nilete hoja ambayo italiomba Bunge liunde Kamati Teule ili lichunguze kwa kinagaubaga sakata la UDA kutohana na ukweli kwamba hata Kamati...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, nadhani kwa mujibu wa kanuni hii umeshaitendea haki, kwa sababu ni maneno tu unasema unakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule. Kwa hiyo, utapewa nafasi huko baadaye utaweza kutoa hayo maelezo mrefu. Tumeshaelewa kwamba unakusudia kuleta taarifa ya hilo jambo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sina haja ya kuelezea hiyo kanuni aliyo simamia Mheshimiwa Halima Mdee, kanuni iko wazi na nadhani wengi tutapata nafasi ya kuisoma. Isipokuwa kwa ushauri tu Mheshimiwa Halima Mdee, utakapokuwa unapeleka hoja hiyo kwa maandishi kwa mujibu wa kanuni zetu, ujaribu kuona Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa kwa sababu kuna eneo ambalo sikumbuki ukurasa vizuri, lakini nadhani ukurasa wa 30 mpaka 32 unazungumzia hilo suala la UDA na kwamba Kamati bado inalishughulikia. Kwa hiyo, jaribu kuangalia hayo yote mawili kama yanaweza kwenda pamoja. Huu ni ushauri tu, wala kikanuni haya maelezo hayakuzuii kufanya ulichopanga, lakini huu ni ushauri. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunayo shughuli moja mbele yetu. Kwa mujibu wa kanuni ya 28 kuhusu maelezo binafsi, sasa ukisoma Kanuni ya 28(12) na 28(8) na kanuni ya 50, Mheshimiwa Jesca David Kishoa anayo Maelezo Binafsi ambayo kwa mujibu wa kanuni zetu atayatoa kwa kufuata wakati amba umeamriwa na kanuni ya 28. Kwa hiyo, atapewa nafasi ya kutoa hayo maelezo binafsi.

Waheshimiwa Wabunge, nimeitaja kanuni ya 50 kwa sababu ndiyo inayotoa mwongozo wa muda utakaotumiwa na kanuni ya 50 inasema: "Maelezo binafsi yatatolewa kwa dakika 15 pekee. Mheshimiwa Jesca David Kishoa anatoa maelezo binafsi kuhusu mwenendo wa deni la Taifa. Mheshimiwa Jesca David Kishoa. (Makofi)

## MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Naomba sasa kutoa Maelezo yangu Binafsi chini ya Kanuni ya 28(12) na (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema ya kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Tano wa Bunge tukiwa salama. Aidha, naushukuru pia uongozi wangu wa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na Viongozi wote wa UKAWA kwa namna ambavyo wameendelea kusimama imara katika mapito magumu ya kutetea demokrasia ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu hususan mume wangu mpenzi David Kafulila na mtoto wetu mpewndwa Darwin, kwanza kwa upendo wao kwangu ulionipa utulivu wa ndani na hivyo kuniwezesha kuandaa maelezo nikiwa nimetulia; na pili, kwa kunivumilia wakati wote ninapokuwa mbali nao kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yangu ya Kibunge. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa mara ya kwanza kabisa kutoa maelezo yangu binafsi kuhusu deni la Taifa ambalo kwa maoni yangu, mwenendo wake inabidi utazamwe upya kwa mustakabali mwema wa uchumi wa nchi yetu. Nia yangu hasa ni kutaka Serikali pamoja na sisi Wabunge tufahamu na kutafakari athari za mwenendo wa deni la Taifa kwa uchumi wa nchi yetu na hatimaye tuishauri Serikali namna bora ya kulipa deni hilo bila kuathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika kutoa huduma za kijamii na kugharamia shughuli nydingine za maendeleo katika nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba ili nchi yoyote duniani iweze kuendelea, ni lazima ikope. Kwa mantiki hiyo, Mataifa karibu yote yenye maendeleo makubwa duniani yana madeni makubwa.

Mathalan, kwa mujibu wa *report* ya Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) ya 2015, uwiano wa deni la Taifa kwa pato la Taifa kwa baadhi ya nchi zenyé uchumi mkubwa duniani inaonyesha deni la Taifa la Marekani ni asilimia 76, Ujeruman ni asilimia 71.20, India ni asilimia 52.40, Ufaransa ni asilimia 96.20 na Uingereza ni asilimia 89.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu huo wa kukopa, bado wachumi wanasisitiza kwamba tusikope kwa kiasi ambacho kinaweza kuathiri mwenendo wa uchumi. Ndiyo maana Shirika la Fedha Duniani (IMF) limeshauri nchi zinazoendelea zisikope zaidi ya 50% ya pato lao la Taifa ili deni liweze kuhimilika. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi mwaka 2005 Serikali ilitoka kwenye kundi la nchi fukara zisizokopesheka duniani na kuingia katika kundi la nchi zinazokopesheka tukiwa na deni la kiasi cha trilioni kumi, deni ambalo lilikuwa himilivu kwa mujibu wa vigezo vya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kitabu cha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa mwaka 2017/2018, deni la Taifa kwa maana ya deni la ndani na la nje sasa hivi limefikia dola za Kimarekani milioni 18,614.93 sawa na ongezeko la 9.76% kufikia Juni, 2016. Deni la Taifa likijumuisha madai ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo yamekadiriwa kufika dola za Kimarekani milioni 1,649.3 pamoja na deni la nje la Sekta Binafsi, dola za Kimarekani milioni

2829.3 liliongezeka kufikia dola za Kimarekani milioni 2,393.3 sawa na shilingi za Kitanzania trillioni 50 kufikia Juni, 2016. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na deni dogo katika Serikali ya Awamu ya Tatu (Serikali ya Mkapa) inakumbukwa kuwa, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa alipoingia madarakani uwezo wa nchi wa kuagiza bidhaa na huduma za kigeni ulikuwa chini ya miezi miwili, lakini aliondoka madarakani akiwa ameiacha nchi ikiwa na akiba ya fedha za kigeni za kutosha kuagiza bidhaa za huduma kwa zaidi ya miezi saba. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo, wakati Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete anaondoka madarakani, aliiacha nchi ikiwa na akiba na fedha za kigeni yenyeye uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma za kigeni kwa miezi isiyozidi minne tu. Makusanyo ya kodi yalikuwa yamefikia 14% ya pato la Taifa mwaka 2005, yalishuka hadi kufikia 12% ya pato la Taifa mwaka 2015. Riba kwa Sekta Binafsi; mikopo ilikuwa na riba 36%, ilishuka mpaka 14% mwaka 2005 lakini ikapanda tena mpaka 24% mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nitoe picha ndogo hiyo ya uchumi ili kuonesha kuwa kama Taifa, tulipiga hatua mbele katika kusimamia uchumi mwaka 1995 mpaka mwaka 2005 na tukapiga hatua nyuma miaka kumi kuanzia 2005 mpaka 2015 katika kusimamia uchumi. Hivyo ni rai yangu kwa Serikali ya Awamu ya Tano isirudi nyuma zaidi kama ilivyofanya Awamu ya Nne na pengine isirudi nyuma zaidi kuliko hata Awamu ya Nne katika kusimamia uchumi hususan deni la Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kimekuwa kilio cha wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Bunge kwamba mwenendo wa deni la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2010 mpaka 2015 siyo salama sana kwa uchumi wetu ingawa majibu ya Serikali yamekuwa yale yale; "deni linaimarika, na kwamba tulikopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo" bila kutoa maelezo ya kina kuhusiana na usahihi wa hoja hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Society For International Development (SID) ya mwaka 2016, ilinukuliwa katika gazeti la *The East African* la tarehe 9 Agosti, 2016 kwamba Tanzania ndiyo nchi yenyeye hali mbaya ya deni la nje ukilinganisha na washindani wetu katika soko la Afrika Mashariki. Kwa mfano, uwiano wa deni la pato la Taifa kwa nchi ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa SID ni kama ifuatavyo:-

Uganda ni 28%, Rwanda ni 20%, Burundi ni 18% na Tanzania ni 40%. Aidha, uwiano wa kiasi cha bajeti kinachokwenda kulipa deni la Tanzania ni mbaya zaidi kuliko nchi washindani wake ndani ya Soko la Afrika Mashariki kwa maana ya Kenya na Uganda. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya S/D, kiasi cha deni la kulipwa kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 Tanzania ni 27%, Uganda ni 25% na Kenya ni 20%. Pamoja na ukweli wote huu, Serikali iliendelea kuhubiri kuwa deni la Taifa ni himilivu na kwamba bado halijawa tatizo kwa maendeleo. Hata hivyo, Waswahili wanasesma, mficha maradhi siku zote kifo humuumbua. Msemo huo umedhihirika, kwani tarehe 18 Oktoba, 2016, Serikali kuitia Makamu wa Rais ilisema kuwa hali ya uchumi siyo nzuri na kwamba utekelezaji wa bajeti hauendi sawa kutokana na kulemewa na deni kubwa la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyasema haya akiwa Dodoma kwenye kikao cha Waganga Wakuu wa Mikoa ambapo pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Makamu wa Rais alisema: "Tumekabidhiwa Serikali ikiwa na deni kubwa kiasi tunatakiwa kulipa shilingi bilioni 900 kila mwezi, wakati makusanyo, mapato ya kodi kwa mwezi hayazidi shilingi trillioni 1.3 huku mishahara ya watumishi ikiwa zaidi ya shilingi bilioni 530 kwa mwezi." Makamu wa Rais aliyasema hayo akiwasihii waganga wakuu wawe wavumilivu ktokana na uhaba wa dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ukubwa wa deni la Taifa na kiwango kikubwa cha fedha zinazotumiwa na Serikali kulipa deni hilo kumeathiri bajeti ya Serikali katika kutoa huduma za kijamii ikiwepo kushindwa kununua dawa za kutosha na hivyo kupelekea ukosefu wa dawa katika hospitali zetu na kushindwa kutekeleza miradi mingine ya maendeleo. Kwa mfano; kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya mwezi Agosti, 2016, Serikali katika utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017, ilikadiria kupata shilingi bilioni 230 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani lakini ikaishia kupata shilingi bilioni 67 sawa na 29% ya makusudio. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ripoti hiyo inaonesha kwamba Serikali...

**NAIBU SPIKA** Mheshimiwa Kishoa, kunywa kwanza maji kidogo hapo, usije ukaishiwa pumzi. (Makofi/Kicheko)

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ripoti ile inaonesha kwamba Serikali ilikadiria kupata shilingi bilioni 263 kutoka vyanzo vya nje, lakini ikaishia kupata shilingi bilioni 62 sawa na 23% na hivyo kufanya jumla ya makusudio ya Serikali ya kutumia shilingi bilioni 493 kuishia shilingi bilioni 130 tu sawa na 26% ya utekelezaji wa bajeti katika mwezi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe pia kwamba wakati bajeti hiyo ya mwaka 2016/2017, tulitegemea pesa za misaada zaidi kwa kiasi cha shilingi bilioni 3,600 ya wahisani kuliko bajeti ya 2015/2016. Tulitegemea shilingi bilioni 2,600 lakini mazingira ya mwaka huu ya mwenendo wa mambo kama inavyooneshwa kwenye ripoti ya Benki Kuu kuanzia na ile ripoti ya robo mwaka na hii ya mwaka 2016, ni wazi kwamba misaada kutoka nchi wahisani kwa ajili ya miradi ya maendeleo mpaka sasa inaonekana bado siyo zaidi ya 10% ya makadirio haya, ambapo hili halitoi taswira nzuri kwa utekelezaji wa bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi huu hafifu wa Serikali kumudu majukumu yake kutokana na kulemewa na mzigo mkubwa wa deni sio katika Sekta ya Afya tu, bali hata katika kusuasua katika mikopo ya elimu ya juu, kwa kiasi kikubwa inatokana na ukata Serikalini hali inayopelekea watoto wa maskini kuanza kukosa fursa ya elimu ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kwamba watumishi wa Serikali mwaka huu hawajapandishwa madaraja kwa sababu ya ukata Serikalini. Naamini hata ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji haijaanza kutekelezwa kwa sababu ya ukata kwani tunatarajia tu kuambiwa vijiji navyo bado vinafanyiwa uhakiki ili kubaini vijiji hewa kama ilivyozoleka, kwani hoja hiyo imekuwa sababu ya Serikali inapoona imeshindwa kutimiza ahadi yake kusema inafanya uhakiki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kwa ujumla inatuma ujumbe kwetu Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwamba bajeti tulioipitisha ya kutumia kiasi cha shilingi trilioni 29.53 ni wazi huenda isitekelezwe kwa zaidi ya 30% kwa mwenendo huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba miradi zaidi ya 70% haitatekelezwa katika bajeti ya 2016/2017. Pia kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kukosa nidhamu ya vipaumbele kwa sababu uhaba wa fedha ni mkubwa kiasi ni ngumu kusimamia vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hekima ya kawaida tu katika mazingira kama haya kwa Serikali kufanya ukaguzi wa deni la Taifa kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kujiridhisha na uhalisia wa deni hilo kwa kutafuta namna bora ya kulipa bila kuathiri uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi wa maelezo hayo na kwa kuzingatia umuhimu wa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wananchi wetu; nakuomba sana kwa mamlaka uliyonayo chini ya kanuni ya 28(11) uiagize Serikali mambo yafuatayo:-

Moja, kutoa kauli juu ya mwenendo wa deni la Taifa; na pili, kueleza hali ya kifedha na uwezo wa Serikali kulipa deni hilo bila kuathiri huduma za kijamii na shughuli nyingine za maendeleo ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maelezo haya muhimu kwa uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya wananchi wetu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca David Kishoa kwa Maelezo Binafsi kuhusu Mwenendo wa Deni la Taifa. Serikali iko hapa na imekusikia. Kama kuna jambo lolote ambalo wao wataliona linafaa humu, walifanyie kazi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu za leo. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.10 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 11 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)